

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Thelathini na Nne – Tarehe 22 Mei, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Waheshimiwa tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Moja, Kikao cha leo ni cha Thelathini na Nne, Katibu.

NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

SPIKA: Ahsante sana, Katibu.

NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Swali la kwanza tunaanza na Ofisi ya Mheshimiwa Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa linaulizwa na Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Buhigwe tafadhali.

Na. 287

**Serikali Kuwawezesha Kina Mama na
Vijana wa Jimbo la Buhigwe**

MHE. ALBERT O. NTABALIBA aliuliza:-

Akina mama na vijana wa Jimbo la Buhigwe wanajituma sana katika kilimo na uwekezaji.

(a) Je, ni lini Serikali itawasaidia kimtaji ili waweze kujikomboa?

(b) Je, ni kiasi gani kimetolewa kuwawezesha akina mama na vijana katika miaka ya 2010 hadi 2017?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Josephat Kandege.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Buhigwe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza viongozi wa Mkoa wa Kigoma kwa kuwashamasisha vijana wa Mkoa wa Kigoma kuanzisha vikundi vingi vya wajasiriamali ambavyo ni nyenzo

muhimu katika kuleta maendeleo ya wanawake, vijana na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwasaidia wanawake na vijana kwa kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Vijana. Mikopo hii imelenga kuwasaidia kupata mitaji ya kuendeleza shughuli zao za kiuchumi hivyo kujiongezea kipato na kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe imeanza kufanya kazi Januari, 2013 hivyo taarifa zilizopo ni kuanzia mwaka huo. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014 hadi 2016/2017 Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe ilitoa jumla ya shilingi 25,377,057 kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya wanawake na vijana. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 hadi kufikia Mei, 2018 jumla ya shilingi 10,500,000 zimetolewa katika vikundi vya wanawake na vijana. Aidha, kupitia Mfuko wa Jimbo Mheshimiwa Mbunge alitoa shilingi 10,500,000 kwa vikundi saba vya bodaboda na kikundi kimoja cha mafundi seremala.

Mheshimiwa Spika, jumla ya shilingi 20,200,000 zimetengwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya vikundi vya wanawake na vijana.

SPIKA: Mheshimiwa Ntabaliba, swali la nyongeza.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa vikundi vingi vimehamasika na wengi wanahitaji mkopo na uwezo wa Halmashauri yetu siyo mkubwa kiasi hicho na katika Wizara mbalimbali tunazo fedha kwa ajili ya maendeleo ya vijana katika mifuko mbalimbali.

Ni lini TAMISEMI itaunganisha nguvu na Wizara nyiningine ili sasa na sisi kule fedha hizo ziweze kuwafikia? (*Makof!*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kila siku tunasikia kwenye vitabu vya CAG na Wabunge wakilalamika kwamba hizi fedha haziendi kwa wananchi kutoka kwenye halmashauri. Nini kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba sheria hii ya asilimia kumi kwenda kwa akina mama, vijana na walemavu itatekelezwa kiufasaha?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la kwanza juu ya uwezo mdogo wa Halmashauri na kuitaka Serikali kuunganisha nguvu kupitia fursa tofauti tofauti, naomba nimhakikishie kama ambavyo amesema yeye mwenyewe kuna fursa kwa mikopo kwa vijana kupitia ofisi ya Waziri Mkuu, Sera na Uratibu ambayo iko chini ya Mheshimiwa Mhagama ni fursa ambayo ni vizuri wananchi wa Buhigwe wakaitumia katika kuweza ku-access mikopo.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili juu ya halmashauri kusuasua katika kutenga asilimia 10, anataka kauli ya Serikali. Kama ambavyo nimekuwa nikisema na leo narudia hata kama ingepatikana shilingi moja kinachotakiwa ni asilimia kumi ya shilingi moja hiyo itengwe. Kama ambavyo nilishawahidi kujibu hapa katika moja ya maswali wakati tunaenda kukamilisha *Finance Bill* kuna kipengele ambacho kitampa Waziri mwenye dhamana ili iwe ni takwa la kisheria na kama kuna Mkurugenzi yeoyote atashindwa kutenga fungu hilo hatua ziweze kuchukuliwa.

SPIKA: Waheshimiwa swali hili ni la vijana, wanatakiwa Wabunge vijana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Aida Khenani.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Lengo la kutenga pesa hii lilikuwa ni kuwainua vijana na wanawake jambo ambalo limekuwa ni kinyume

na lengo ambalo lilikusudiwa hasa pale zinapotolewa kipindi cha Mwenge. Serikali haioni kuna umuhimu wa kupeleka pesa hizi kulingana na mahitaji hasa kwa wale ambao wanajishughulisha na kilimo ikatolewa kipindi cha msimu wa kilimo? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo, majibu tafadhalii.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana kwa maswali yale ya awali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la dada yangu Mheshimiwa Aida, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumetoa maelekezo maalum kwa fedha hizi na niwasihii Waheshimiwa Wabunge, siku zote tunasema kwamba fedha hizi zinaishia katika halmashauri hata kule Hazina hazifiki. Ni jukumu la Kamati ya Fedha kila mwezi wanapofanya *collection* wahakikishe kama wamepata shilingi milioni 100, asilimia kumi ya shilingi milioni 100 maana yake ni shilingi milioni kumi zitolewe kwa wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni imani yangu kwamba Kamati za Fedha zote, dada yangu Mheshimiwa Aida nimepata *concern* yako, zihakikishe wanatenga fedha hizi. Ndiyo maana katika *Finance Bill* ya sasa hivi tunafanya mabadiliko ya sheria katika Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 ili kuhakikisha kwamba Waziri mwenye dhamana anasimamia vizuri eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba niwaambie wazi kwamba mtu yejote atakaye-temperna fedha hizi ambapo kwa mwaka huu wa fedha tumetenga zaidi ya shilingi bilioni 61, kwa kweli hatutakuwa na ajizi ya aina yoyote. Hata hivyo, niwasihii Wabunge tunapokaa katika Kamati ya Fedha tuweze kuzisimamia vizuri fedha hizi kwa sababu ni jukumu letu

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wananchi wetu hasa vijana na akina mama waweze kupata mikopo hii.

SPIKA: Bado tuko Wizara hii hii, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale uliza swali lako. Kwa niaba yake nimekuona Mheshimiwa Maige.

Na. 288

Kuboresha Maslahi ya Walimu na Ujenzi wa Madarasa

MHE. EZEKIEL M. MAIGE (K.n.y. MHE. HUSSEIN N. AMAR)
aliuliza:-

(a) Je, ni lini walimu wataboreshewa maslahi yao pamoja na nyumba za kuishi?

(b) Kwa juhudzi za Mbunge wa Jimbo la Nyang'hwale ameweza kujenga madarasa mawili katika Kata ya Izunya kwa lengo la kuanzishwa shule ya sekondari tangu mwaka 2014. Je, ni kwa nini shule hiyo hajifunguliwa hadi sasa ili kuwapa moyo wafadhili?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Josephat Kandege.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kwa dhati kuhakikisha walimu wa nchi hii wanabobereshewa maslahi yao ikiwemo ujenzi wa nyumba za walimu. Katika kuboresha maslahi ya walimu, Serikali kwa Sheria Na. 25 ya mwaka 2015 ilianzisha Tume ya Utumishi ya Walimu ili iweze kusimamia na kushughulikia masuala yote

yahusuyo maslahi ya walimu badala ya maslahi hayo kusimamiwa na chombo zaidi ya kimoja kama ilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi Juni, 2015 hadi Desemba 2017, Serikali imetumia kiasi cha shilingi bilioni 33.135 kwa ajili ya kulipa madeni ya walimu ambapo walimu 86,234 wamelipwa nchi nzima. Aidha, katika kuhakikisha maslahi ya walimu yanayoboreshwa na kero zao zinaondolewa, jumla ya walimu 52 wa shule za msingi na sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale walllipwa jumla ya shilingi 99,685,990 za madai mbalimbali na wengine 202 walipandishwa vyeo (madaraja) katika mwaka wa fedha 2014/2015 na 2015/2016.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Nyang'hwale, wananchi na uongozi wa Halmashauri ya Nyang'hwale kwa juhudini zao za kutaka kuiwezesha jamii kielimu wakiwemo wa Kata ya Izunya. Ili shule ya sekondari iweze kupewa kibali cha kufunguliwa wakati wa kuanzishwa inapaswa kwa kuanzia iwe na madarasa, kuwe na jengo la utawala, nyumba za walimu, vyoo vya walimu na wanafunzi, maktaba, viwanja vya michezo, samani pamoja na maabara kwa kuzingatia mwongozo uliowekwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa shule tarajiwa ya Izunya ina vyumba vya madarasa manne, vyoo matundu sita ya wasichana na wavulana matundu matano, jengo la utawala lenye vyoo vya walimu liko hatua za mwisho za umalizajaji na maabara zipo kwenye hatua ya jamvi. Hata hivyo, kwa kutambua jitihada za wadau mbalimbali wa elimu akiwepo Mheshimiwa Mbunge, Halmashauri imeazimia kutumia shilingi milioni 50 kutoka fedha za *EP4R* zilizopelekwa mwezi Februari, 2018 kwa ajili ya kukamilisha maabara zote. Ni matarajio yangu kwamba mara baada ya ujenzi wa maabara kukamilika taratibu za usajili wa shule hiyo zitakamilika. Aidha, naomba niitumie nafasi hii kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, wadau wetu wa maendeleo na wananchi kwa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

ujumla kuunganisha nguvu zetu pamoja ili kukamilisha miundombinu inayohitajika katika shule kuweza kufunguliwa ikiwemo ya Kata ya Izunya.

SPIKA: Sasa Waheshimiwa, huu ni mfano wa jibu refu, limekula muda kweli kweli jibu hili. Tunaendelea kuwaomba majibu yawe mafupi. Maana Mheshimiwa Mbunge alichouiliza tu ni lini walimu wataboreshewa maslahi na kwa nini shule hajafunguliwa, basi. Hapakuwa na haja ya mengine yote yale. Mheshimiwa Maige.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa maelekezo yako lakini kipekee nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri japo ni marefu kama ambavyo umesema.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu hayo mazuri, naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza, wananchi wa Halmashauri na Jimbo la Msalala kama walivyo ndugu zao wa Jimbo la Nyang'hwale na kwa kushirikiana na Mbunge wao hivyo hivyo nao wamefanya kazi kubwa sana ya kuanza kujenga shule mpya za sekondari, Shule za Mwazimba na Nundu ambazo miundombinu aliyoitaja Mheshimiwa Naibu Waziri karibia yote imekamilika, lakini shule hizi hazijapata kibali cha kufunguliwa.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kujua ni lini shule hizi mbili za Nundu na Mwazimba katika Halmashauri ya Wilaya ya Msalala zitafunguliwa kuanza kupokea wanafunzi?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Msalala kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo Msalala katika kipindi cha miaka minne iliyopita wamefanikiwa kujenga hosteli kwenye shule saba za sekondari za Kata, shule za Busangi, Baloha, Segese, Lubuya, Bulige, Ntobo...

SPIKA: Mheshimiwa Maige na wewe tena unachukua muda mrefu pia.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Samahani Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Waziri naye muda mrefu, yaani ni saa moja tu tunatakiwa tumalize. Kwa maswali haya mawili mnaona tumeşhatumia dakika 20, maswali mawili tu. Kwa namna hii hatuwezi kumaliza maswali.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, samahani, naomba nimalizie tu swali langu fupi kwamba shule hizi zina watoto lakini hazitambuliwi na Serikali na hazipati ruzuku ya uendeshaji wa hosteli. Ni lini shule hizi zitatambuliwa na Serikali ili ziwe zinapata ruzuku ya għarama za uendeshaji wa hosteli hizi?

SPIKA: Karibu Mheshimiwa Naibu Waziri ingawa pia na yeye mmemuonea, mnapotaja shule zenu halafu mnasema zinafunguliwa lini, sasa Waziri kweli atajua shule zote ambazo zinategemewa kufunguliwa? Mheshimiwa hebu jaribu, zile shule za Mheshimiwa utazifungua lini?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimsihi Mheshimiwa Mbunge taratibu zifuatwe ili hiso shule ziweze kufunguliwa. Kwa sababu ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba pale ambapo miundombinu ya shule imekamilika zinaweza kufunguliwa ili wananchi wetu wapate huduma kwa karibu.

Mheshimiwa Spika, katika hilo la pili amesema kwamba hosteli zimejengwa sasa anataka Serikali ianze kuhudumia hosteli.

Mheshimiwa Spika, sina uhakika kama msingi wa swalni ni juu ya kwamba hosteli ikishajengwa ianze kupata huduma, lakini kama nimemuelewa sawasawa kwamba anachomaanisha ni kwamba shule hiyo itambuliwe kwamba ni miongan mwa shule za *boarding*, naomba tu tufuate

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

taratibu ili wananchi na hasa vijana wetu ambao wana adha ya kutembea umbali mrefu hosteli pale inapokamilika huduma zilweze kutolewa.

SPIKA: Ahsante sana. Swali linalofuata Mheshimiwa Alfredina Apolinairy Kahigi.

Na. 289

Madarasa na Ofisi za Walimu – Kagera

MHE. ALFREDINA A. KAHIGI aliuliza:-

Madarasa na Ofisi za Walimu katika shule mbalimbali katika Mkoa wa Kagera ni mabovu.

Je, Serikali inawasaidiaje wanafunzi wa Kagera kupata mahali pazuri pa kusomea kadhalika na walimu wao wapate ofisi nzuri ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, bado tuko TAMISEMI, Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Alfredina Apolinairy Kahigi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kagera kuna mahitaji ya vyumba vyaa madarasa 14,275 kwa shule za msingi, vilivyopo ni 5,934 hivyo upungufu ni 8,341 sawa na asilimia 58. Aidha, mahitaji ya ofisi za walimu ni 1,780, zilizopo ni 925 na upungufu ni 855 sawa na asilimia 48. Kwa upande wa shule za sekondari kuna mahitaji ya vyumba vyaa madarasa 2,379, vilivyopo ni 1,582 upungufu ni 797 sawa na asilimia 34.

Majengo ya Utawala mahitaji ni 212, yaliyopo ni 67 upungufu ni 145 sawa na asilimia 67.

Mheshimiwa Spika, upungufu pia umejitokeza katika miundombinu mingine mfano nyumba za walimu, vyoo na maabara. Hali hii ya upungufu wa miundombinu inatokana na mwamko mkubwa wa wazazi wa kuwaandikisha watoto shule kufuatia Mpango wa Serikali wa Elimu ya Msingi Bila Malipo ambapo idadi ya wanafunzi imeongezeka katika shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Spika, Serikali itachukua hatua na mikakati mbalimbali za kuhakikisha kuwa wanafunzi na walimu katika Mkoa wa Kagera wanapata mahali pazuri pa kusomea na kufundishia ili kuinua taaluma katika Mkoa wa Kagera. Serikali inaendelea kutoa fedha za ujenzi na ukarabati kupitia mpango wa *EP4R* ambapo jumla ya shilingi 1,243,600,000 zimetolewa katika Mkoa wa Kagera katika kipindi cha mwaka 2017/2018 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa madarasa, mabweni, maabara, matundu ya vyoo katika shule za Kagemu na Rugambwa zilizoko kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba, Nyailigamba na Profesa Joyce Lazaro Ndalichako katika Halmashauri ya Muleba, Murusagamba katika Halmashauri ya Ngara na Omurwelwe iliyoko Halmashauri ya Karagwe.

SPIKA: Bado naendelea kuwaomba TAMISEMI majibu yenu kwa kweli yanapaswa kuwa mafupi. Mheshimiwa Kahigi, swalii la nyongeza kama lipo.

MHE. ALFREDINA A. KAHIGI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza, ni lini Serikali itawajengea nyumba walimu wale ambao hawana nyumba kabisa katika shule zao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, kwa kuwa mambo mazuri yanaigwa, je, Wakuu wa Mikoa hawaoni kama ni vizuri kumuiga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Makonda nao waweze kutafuta wafadhili wa kuweza kuwajengea walimu nyumba za kuishi na ofisi? Ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Jamani, ninyi hili swali si ni lenu, mbona hamshangilii.

MHE. NURU A. BAFADHILI: Tumeshangilia. (*Kicheko/Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la upungufu wa nyumba za walimu, naomba nimsihi Mheshimiwa Mbunge kwamba katika hizo pesa ambazo zimeletwa za *EP4R* ni wajibu wa halmashauri husika kuangalia kama hitaji kubwa ni nyumba za walimu, hakuna dhambi pesa hizo zikatumika pia katika kuhakikisha nyumba zinajengwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili, naamini ni wazo jema, naomba niwasihii Wakuu wa Mikoa mingine waige mfano mzuri kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge yeeye mwenyewe ameliona na anapongeza juhudii za Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. (*Makof*)

SPIKA: Tuendeleee na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Kawe, kwa niaba yake Mheshimiwa Mchungaji nimekuona.

Na. 290

Tatizo la Maji – Baadhi ya Maeneo ya Jimbo la Kawe

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA (K.n.y. MHE. HALIMA J. MDEE) aliuliza:-

Baadhi ya maeneo katika Jimbo la Kawe yanakabiliwa na changamoto za upatikanaji wa maji safi

na salama kwa kipindi kirefu. Maeneo kama Kata ya Mabwepande (Mtaa wa Mbojo, Mabwepande, Kinondo); Kata ya Makongo (Mtaa wa Changanyikeni na baadhi ya maeneo ya Mtaa wa Makongo Juu); Kata ya Wazo, Mbweni na Mbezi Juu na changamoto hii sugu ilitarajiwa kupungua na kumalizika kabisa baada ya mradi mkubwa wa maji wa Ruvu Chini kukamilika ambao kwa sasa tayari umeshakamilika.

(a) Je, mikakati ya usambazaji maji pamoja na mabomba katika maeneo ambayo hayana mtandao wa mabomba ikoje ili kutatua kero husika?

(b) Je, ni miradi gani inayotarajiwa kutekelezwa, muda wa utekelezaji, gharama za kila mradi na nani anayewajibika katika utekelezaji?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimwa Aweso, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Jimbo la Kawe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha wananchi wa Dar es Salaam hususan maeneo ambayo hayakuwa na mtandao wanaondokana na kero ya kutopata huduma ya maji, Serikali katika awamu ya kwanza kupitia DAWASA inakamilisha ujenzi wa matanki na mabomba makuu ya kupeleka maji katika maeneo ya miinuko ya Changanyikeni, Wazo na Salasala. Aidha, awamu hii pia itahusu ujenzi wa mtandao wa maji Kata ya Kiluvya na Mbezi Luisi. Mradi huu unatekelezwa chini ya ufadhili wa mkopo wa masharti nafuu kutoka India kwa gharama ya dola za Kimarekani milioni 32.772. Hadi sasa utekelezaji wa awamu ya kwanza umefikia asilimia 82 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2018. (Makof)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili ya utekelezaji itahusu ujenzi wa mabomba madogo madogo ya kusambaza maji na kuunganisha wateja katika maeneo yote kuanzia Changanyikeni, Bunju hadi Bagamoyo. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanzia mwezi Julai, 2018 na unatekelezwa chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia kwa gharama ya dola za Marekani milioni 45. Mradi huu utatekelezwa kwa miezi 15. Zabuni ya ujenzi wa mradi huo itatangazwa hivi karibuni baada ya kupata kibali kutoka Benki ya Dunia.

SPIKA: Mheshimiwa Msigwa, swalii la nyongeza.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri na kwamba kweli ujenzi wa matenki unaendelea, lakini kuna maeneo mengine ambayo ni korofii kama Mabwepande, Kijiji cha Mbopo na maeneo mbalimbali ya Kata ya Mbezi ikiwemo Mtaa wa Ndumbwanji. Ni lini sasa Serikali itatia mkazo kuhakikisha maeneo hayo yanapatiwa maji kwa haraka sana kwa sababu kumekuwa na shida?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, kwa kuwa Manispaa ya Iringa na Iringa kwa ujumla inategemewa kuwa ni kitovu kikubwa cha utalii wa Kusini na Manispaa ya Iringa imebakiza asilimia nne za upatikanaji wa maji. Je, ni lini sasa hizo asilimia nne zitaisha ili watalii watakafopika kule wasipate matatizo wanapokwenda katika maeneo yale? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Aweso, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya jitihada kubwa sana kuondoa tatizo la maji katika Mkao wa Dar es Salaam na mpaka sasa hali ya upatikanaji ipo katika asilimia 75 lakini yapo maeneo ambayo hayana maji. Serikali kwa kuona hilo sasa kuna mradi ambao unatekelezwa kutoka Mpiji – Tegeta - Bagamoyo lakini Mbezi mpaka kwa kaka yangu Mheshimiwa Mnyika katika kuhakikisha inatatua tatizo la maji.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Kwa hiyo, mpaka mkataba huu utakapokuwa umesainiwa na kupata kibali kutoka Benki ya Dunia tutatekeleza kwa wakati ili wananchi wa Dar es Salaam waweze kupata maji safi, salama na yenye kuwatosheleza.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kulishukuru Bunge lako Tukufu, katika bajeti yetu ya Wizara ya Maji tumepitishiwa kiasi cha shilingi 727,345,000,000. Katika fedha hizo tutauangalia Mji wa Iringa katika kuhakikisha tunaondoa tatizo la maji. Ahsante sana.

SPIKA: Swali linalofuata, Mheshimiwa Mbunge wa Mbogwe, Mheshimiwa Augustino Masele.

Na. 291

Miradi ya Uchimbaji Visima Virefu

MHE. AUGUSTINO M. MASELE aliuliza:-

Visima virefu vimechimbwa katika Vijiji ya Lugunga na Kabanga (Mkweni) na maji yakapatikana lakini shughuli za ulazaji mabomba na ukamilishaji imekwama. Je, Serikali iko tayari kutoa utaalam na fedha kukamilisha miradi hii?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mbogwe hadi sasa ina jumla ya watu 137,636 na asilimia 65 wanapata huduma ya maji safi na salama kuititia miradi ya maji minne ya skimu ya usambazaji maji, visima virefu 20, visima vifupi 460 na matanki 55 ya kuvuna maji ya mvua.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe inategemea kujenga miradi ya maji miwili katika Vijiji vitano ambavyo ni Lugunga, Luhala, Kabanga, Nhomolwa na Nyanhwiga. Mradi mmoja wa Kabanga – Nhomolwa na Nyanhwiga ni kutoka chanzo cha kisima kirefu cha Kabanga nan mradi wa pili ni Lugunga – Luhala ni kutoka chanzo cha kisima kirefu cha Lugunga na utahudumia Vijiji vya Luganga na Luhala.

Mheshimiwa Spika, usanifu wa Mradi wa Kabanga – Nhomolwa umekamilika na uko katika hatua ya manunuzi ili kumpata mkandarasi wa ujenzi wa mradi huu. Aidha, miradi wa Lugunga – Luhala bado upo kwenye Halmashauri ya Mbogwe na imetengewa shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya kuanzia ujenzi wa miundombinu ya miradi hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iko tayari kutoa wataalam ili kutatua changamoto za utekelezaji wa miradi hii kulingana na mahitaji.

SPIKA: Mheshimiwa Masele, swali la nyongeza.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba sasa nimuulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, tatizo kubwa hapa ni uhaba wa wataalam. Naomba kujua sasa Serikali itatupatia lini wataalam wa kuweza kutusaidia katika kurahisisha ukamilishaji wa hii miradi ya maji inayoendelea huko Mbogwe? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, naomba sasa kujua *time frame*, ni lini miradi hii itakamilishwa? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, ni lini?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza

Mheshimiwa Mbunge kwa namna anavyowatetea wananchi wake lakini kikubwa maji hayana mbadala na uhitaji wa maji ni mkubwa sana. Sisi kama Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo, kubwa nimwombe Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane ili tuwape watalaaam wetu wa Wizara waweze kumsaidia katika kuhakikisha wananchi wake wanapata maji safi, salama na yenye kuwatoshaleza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala zima la fedha na ni lini miradi hii itakamilika, kikubwa nimwombe sasa Mhandisi wa Maji katika Jimbo lake ahakikishe kwamba anatengeneza *certificate* ili sisi kama Wizara tutawalipa kwa wakati ili wananchi wake waweze kupata maji safi, salama na yenye kuwatoshaleza.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Edwin Sannda, swalifupi la nyongeza.

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kondoajini tulichimba visima kumi, tumepata usambazaji wa visima vitano, lakini bila ya ukarabati wa miundombinu ya maji pale mjini, hizi gharama zilizotumika kusambaza visima vitano ni sawa na bure.

Je, ni lini Serikali itatuletea fedha kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya maji mjini ambayo pia ni ahadi ya Waziri Mkuu? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya swalifupi la hilo, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Aweso, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, nikushukuru lakini kikubwa nataka nimpongeze kaka yangu Mheshimiwa Sannda kwa jitihada anazozifanya, sisi kama Wizara ya Maji lazima tumuunge mkono. Kikubwa nimuombe Mhandisi wa Halmashauri ya Kondoajini, fedha tumeshapitishiwa na Bunge a-rise *certificate* na sisi tutamlipa kwa wakati mkandarasi atakayetekeleza mradi huo katika kuhakikisha tunaondoa tatizo la maji.

SPIKA: Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi, uliza swali lako, bado tuko Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Na. 292

Kuanzisha Mradi wa Maji Kutoka Ziwa Tanganyika na Ziwa Rukwa

MHE. SILAFU J. MAUFI aliuliza:-

Kumekuwa na changamoto katika kuwapatia maji safi na salama wananchi wa Mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma pamoja na kuwa Ziwa Tanganyika na Ziwa Rukwa yako katika mikoa hiyo.

Je, Serikali sasa haioni umuhimu wa kuanzisha mradi wa maji kutoka kwenye vyanzo hivyo na kusambaza kwa wananchi wetu?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa lengo la kuboresha huduma ya maji kwa wananchi, Serikali imeanza kutekeleza miradi ya kutoa maji katika maziwa makuu nchini kupeleka kwa wananchi wanaozunguka maziwa hayo. Katika Mkoa wa Kigoma, Serikali inatekeleza mradi unaogharimu kiasi cha shilingi bilioni 42 kutoka Ziwa Tanganyika kwenda katika Manispaa ya Kigoma Ujiji ambapo utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2018.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na jitihada za kutumia vyanzo vya maji vya Ziwa Tanganyika na Ziwa Rukwa kwa ajili ya kuhudumia wananchi wa Mikoa ya Katavi, Rukwa

na Kigoma. Hivyo, Wizara imeziagiza Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira za mikoa husika kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi ya maji na uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya miradi ya maji itakayotumia vyanzo hivyo. Utekelezaji wa miradi hiyo ni kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji Awamu ya Pili (*WSDP II*).

SPIKA: Mheshimiwa Silafu, swali la nyongeza.

MHE. SILAFU J. MAUFI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili madogo ya kuiuliza Serikali yangu.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, mikoa hii ya pembezoni Serikali imekuwa inasuasua kuwapelekea huduma zinazohitajika kwa maendeleo ya jamii. Napenda kuiambia Serikali kwamba huu uzoefu waliloupata kutoka Ziwa Victoria kupeleka maji Shinyanga, Tabora, Simiyu na kadhalika naomba basi uzoefu huu wakaupeleke katika mikoa ya Katavi, Rukwa na Kigoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hii *speed* ya kupeleka maji katika Mji wa Ujiji ni ndogo sana, haina matunda mazuri kwa mikoa hii mitatu. Je, Serikali inasema nini katika kuhamisha uzoefu huu wa Ziwa Victoria na kuuweka katika mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Serikali haioni kwamba inatumia fedha nyingi za kuchimba visima virefu katika vyanzo ambavyo havina uhakika, inaonaje ikatumia vyanzo hivi ambavyo ni vya uhakika...

SPIKA: Mheshimiwa Silafu unatoa hotuba, uliza swali tafadhalii.

MHE. SILAFU J. MAUFI: Mheshimiwa Spika, ni katika kujenga hoja na kuweka mambo sawa. Napenda kufahamu ni lini hii awamu ya pili itaanza ili hivi vyanzo vya uhakika vya Ziwa Tanganyika na Ziwa Rukwa vifanyiwa kazi ili wananchi wa Rukwa wapate maji ya uhakika? (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, *Lake Rukwa* linakauka, mnataka tena mtoe maji *Lake Rukwa* jamanii? (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge na ukimuona mtu mzima analia ujue kuna jambo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, najua changamoto kubwa sana ya maji katika eneo lake. Sisi kama Wizara tupo tayari sasa kutoa ushirikiano na uzoefu wetu katika kuhakikisha wananchi wake wa maeneo ya Rukwa wanapata maji safi, salama na yenyewe kuwatosheleza.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe sisi ni Wizara ya Maji na siyo Wizara ya Ukame, tupo tayari kuwapatia maji wananchi wa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza jitihada, nipo tayari kufanya ziara maeneo ya Mheshimiwa Mbunge ili kuangalia namna ya kuweza kutatua tatizo hili kwa haraka. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Devotha nilikuona.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya tatizo la maji safi na salama kwa wananchi wa Manispaa ya Morogoro bado ni kizungumkuti. Bwawa la Mindu ambalo limekuwa likitegemewa na wananchi wa Manispaa kwa sasa halitoshelezi. Kwa kuwa Mkoa wa Morogoro una mito mingi, je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga bwawa lingine ili iwe mwarobaini kwa wananchi wa Manispaa ya Morogoro ambaao wanakosa maji kwa muda mrefu?

SPIKA: Majibu ya swali hilo fupi, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Spika, nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge dada yangu Devotha, ni kweli Morogoro kumekuwa na changamoto kubwa sana ya maji na tunajua kabisa tunaelekeea Tanzania ya Viwanda, lazima tuwe na mahitaji ya maji kwa maana ya maji yenye utoshelevu. Sisi kama Wizara ya Maji tumeliona hilo, tupo kwenye majadiliano ya dola milioni 70 katika kuhakikisha tunaondoa kabisa tatizo la maji safi na salama katika Mkoa wa Morogoro. (*Makofi*)

SPIKA: Swali linalofuata la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, tafadhali.

Na. 293

Ripoti za Sheria (*Law Reports*)

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA aliuliza:-

Je, Idara ya Mahakama iliandika Ripoti za Sheria (*Law Reports*) ngapi kwa mwaka 2017?

SPIKA: Majibu ya swali hilo la Kibunge, Waheshimiwa mnalionia swali hilo, Senatorhuyo, tafadhali Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania inatumia mfumo wa kisheria wa *Common Law* ambao maamuzi ya Mahakama za juu yana nguvu ya kisheria na yanazibana Mahakama nyingine za chini katika kufanya maamuzi ya kesi. Msingi huo wa kisheria unaofahamika *stare decisis* unazitaka Mahakama kutumia misingi ya tafsiri ya kisheria yaliyotolewa na Mahakama za juu na wakati mwingine zilizoamuliwa na Mahakama iliyo na mamlaka sawa endapo kesi zinafanana. Hata hivyo, Mahakama ya juu kabisa kama ilivyo Mahakama ya Rufani hapa Tanzania inaweza na ina mamlaka ya kubadilisha msingi au tafsiri ya sheria iliyotajwa huko nyuma inaposikiliza shauri jipya.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha msingi huo unafuatwa, uchapishaji wa mara kwa mara wa maamuzi ya Mahakama katika *Law Reports* ni muhimu ili wanasheria, Majaji na watu wote waweze kujua ni msingi gani na uamuzi upi wa sheria umewekwa na Mahakama katika kesi fulani iliyofo kishwa Mahakamani na kuamuliwa. Kwa kufuata utaratibu huo, tangu mwaka 1921 *Law Reports* zimekuwa zikichapishwa Tanzania. Hivyo basi, taarifa za sheria ni mfululizo wa vitabu ambavyo vina maoni ya Mahakama kutoka kwenye baadhi ya kesi zilizoamuliwa na Mahakama ambazo zinatakiwa kufuatwa na Mahakama nyingine.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2017 Mahakama ya Tanzania kupitia Bodi ya Uhariri ya Taarifa za Sheria za Tanzania (*Tanzania Law Reports Editorial Board*) imeandaa *Law Reports* zipatazo nne ambazo ni *Law Report* ya mwaka 2014, 2015, 2016 na 2017. Kwa sasa *Law Reports* hizo zipo katika hatua na taratibu za mwisho ikiwa ni pamoja na kufanyiwa uhakiki wa kina wa kiuhariri na taratibu zingine za ununuzi kwa ajili ya kumpata mzabuni wa kuchapisha *Law Reports* rasmi.

SPIKA: Mheshimiwa Mwambalaswa, swali la nyongeza.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Swali la kwanza, majibu ya Serikali yanaonyesha kwamba uchapishaji wa mara kwa mara wa ripoti hizi ni muhimu sana, kwanza kwa *best practice, openness na ease of reference*.

Ni kitu gani kimefanya ripoti hizi zisichapishwe kwa miaka minne mfululizo? La kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, naiunga mkono sana Serikali kwa juhudzi zake za kupunguza mlundikano wa kesi Mahakamani kwa ku-*appoint* Majaji wengi. Hata hivyo, kuna *practice* hii ya Majaji kwenda likizo mwezi Desemba na Januari ambayo ni ya historia tu. Je, Serikali haioni kwamba umefika wakati sasa wa kuwapangia Majaji likizo wakati

wowote wa mwaka (Januari mpaka Desemba) badala ya kuwaweka wote kazini na kwenda likizo Desemba mpaka Januari?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Waziri wa Katiba na Sheria.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya sababu iliyosababisha *Law Reports* kutotoka kwa wakati, kwanza ilikuwa ni mabadiliko makubwa sana ya *Editorial Board*. *Editorial Board* ya *Law Reports* hizi ni Shule Kuu ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na pamekuwa na mabadiliko makubwa pale ambayo yalifanya kazi ya uhariri wa hizo kesi ichukue muda kwa sababu siyo kuzihariri tu ni pamoja na kuzichambua na kuzihariri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tatizo hilo limeonekana na ndio maana tumeamua kuchapa ripoti zote nne kwa wakati mmoja na baada ya hapo Mahakama na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam tumekubaliana kwamba sasa tutaanza kutoa *annual reports*.

Napenda tu kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari katika huu mwaka wa 2018 tumekwishaandaa asilimia 42 ya mashauri yaliyoamuliwa. Kwa hiyo, ni mategemeo yetu mwisho wa mwaka tutatoa ripoti ya mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, kuhusu likizo ya Majaji mwezi Desemba mpaka Januari, nikubaliane na wewe kabisa kwamba ni utamaduni wa nchi za *Commonwealth* kwamba Desemba na Januari Majaji wote wanakwenda likizo kwa sababu huko kwa wenzetu Uingereza mwezi Desemba na Januari kila kitu kinasimama na miezi hiyo watu hawafungwi

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

ili wamalize Krisimasi ndiyo waende jela. Ni utamaduni tumeurithi, kwa hiyo, nitamshauri Mheshimiwa Jaji Mkuu tuuangalie kwa mukhtadha na mazingira ya Tanzania. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, ni kwa utamaduni huohuo pia Spika haitishi Bunge katika miezi hiyo hiyo, kwa sababu hizo hizo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Maryam Msabaha, nimekuona, karibu sana.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Na mimi naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, sambamba na Mahakama nydingi kuwa chakavu na wale wazee wa Mahakama maslahi yao ni duni, ni lini Serikali itakarabati Mahakama zote na kuboresha stahiki za wazee wale?

SPIKA: Mheshimiwa Maryam, mbona swali hilo haliendani kabisa na swali la msingi? Mheshimiwa Profesa Kabudi, tafadhalii tunaomba majibu kwa maswali hayo.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, moja, Mahakama inatekeleza mpango wa miaka kumi wa ukarabati na ujenzi wa Mahakama zote. Baada ya Bunge leo anione ili niweze kumpa mpango wote wa miaka kumi, lakini tuonane hapa hapa Bungeni. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, pili, wazee wa Mahakama, tutaangalia maslahi yao ili yazidi kuboreshwa.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri usiwe na wasiwasi, Mheshimiwa Maryam amefunga. (*Kicheko*)

Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda.

Ulipaji wa Fidia kwa Wananchi wa Vijiji vya Kyela

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA aliuliza:-

Wakati ujenzi wa barabara muhimu ya Ipinda – Matema ukiedeleta.

Je, ni lini wananchi, taasisi kama makanisa na ofisi za vijiji katika vijiji vya Matema, Katusyo, Mababu, Ngyekye, Katela na Ngeleka ambao hawajabomoa majengo yao kwa sababu hawajafidiwa fidia zao ambayo kimsingi ni haki yao na kupisha ujenzi unaoendelea wa barabara hii muhimu sana katika maendeleo na uchumi wa Wilaya ya Kyela Mkoani Mbeya zitalipwa fidia hizo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias Kwandikwa, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kikusya – Ipinda – Matema yenye urefu wa kilometra 39.2 ni barabara ya mkoa inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) ambapo ujenzi kwa kiwango cha lami unatekelezwa kwa sehemu ya Tenende hadi Matema (kilometra 34.7).

Mheshimiwa Spika, wakati wa utekelezaji wa mradi huu na kwa kuzingatia Sheria ya Barabara ya mwaka 2007 na Kanuni zake za mwaka 2009, uthamini wa mali za

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wananchi na taasisi zilizoathiriwa na ujenzi wa barabara hii ulifanywa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa uthamini huo ambao ulifanywa na Mthamini kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, malipo yalifanyika kwa waliostahili tarehe 17 Septemba, 2017 katika vijiji vya Masebe, Mpunguti, Mpanga, Ipinda, Ngamanga, Bwato, Mpegele, Ngeleka, Katela, Mababu, Kilombero, Kisyo na Matema. Hata hivyo, baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Ipinda walifungua mashtaka Mahakamani dhidi ya Serikali na hadi sasa hawajaondoa mali zao zilizo ndani ya eneo la hifadhi ya barabara.

SPIKA: Mheshimiwa Sophia, swalii la nyongeza.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, swalii langu la kwanza, pamoja na majibu yasiyoridhisha ya Mheshimiwa Naibu Waziri, atakubaliana nami kwamba imekuwa ni kawaida kwa Serikali kutokuwalipa waathirika wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwepo Wilaya hii ya Kyela? Barabara hii toka imejengwa hakuna aliyelipwa mpaka sasa na ndiyo maana wananchi wamefungua kesi Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, imekuwa ni kawaida ya Serikali kutokulipa wananchi wengi katika Taifa hili wanapowabomolea kwa kigezo cha ujenzi wa barabara, wakati huohuo mmewawekea umeme na maji. Kama mlitia wameingia kwenye hifadhi ya barabara kwa nini mlitoa huduma hizo za kijamii? Nataka majibu ya Serikali ni kwa nini wanafanya hivyo, wananchi hawapati haki zao wakati wamekaa kwa muda mrefu, zaidi ya miaka 50 katika eneo husika? (*Makofii*)

SPIKA: Kwa hiyo, Mheshimiwa Sophia, hamtaki barabara ya lami ninyi? (*Kicheko*)

Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, kwanza, namuomba sana Mheshimiwa Mbunge aridhike tu kwa hatua ambayo Serikali inachukua. Kwa sababu hivi navyozungumza shilingi bilioni 1.008 zililipwa kwa wananchi ambao walikuwa wanaathirika na ujenzi wa barabara. Hao wachache waliobakia kwa sababu wamepeleka kesi Mahakamani, ni haki yao wasikilizwe na Mahakama ili waweze kupata haki zao.

Mheshimiwa Spika, nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba sisi kama viongozi tunalo jukumu kubwa sana la ku-*influence* wananchi wetu. Kwa hiyo, labda nikuombe tu kwa sababu hii kesi iko Mahakamani tuonane ili angalau nikupe mbinu za kushawishi wananchi hawa ili waweze kuondoa kesi yao na ikiwezekana huduma ya barabara iweze kupita kwa sababu ni muhimu sana katika ujenzi wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, swalí la pili kwamba zimekwenda huduma kwa wananchi sehemu ambazo tunatekeleza miradi, inaweza kuwa kweli kwamba pale ambapo wakati mwininge ujenzi wa barabara haujaanza au hata kabla ya kuwa na mradi wa barabara, yaweza kuwa kulikuwa na huduma, lakini wakati sasa mradi wa ujenzi wa barabara unakuja ndipo sasa pale tunalazimika kufanya zoezi hili la kuweza kuwaondoa wananchi lakini na kuwapa haki zao kwa mujibu wa sheria.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nafikiri ukiliangalia kwa ukaribu unaweza ukagundua kwamba ni wakati gani huduma ilikwenda na wakati gani mradi huu wa barabara umekuja. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, nilikuona swalí la nyongeza.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi. Changamoto iliyopo Wilaya ya Kyela inafanana kabisa na Wilaya ya Mpanda katika barabara ya

Stalike – Misunkumilo, bado wananchi wanadai fidia na ni miaka mitano sasa.

Je, ni lini Serikali itawalpa fidia wananchi hawa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo kwa kifupi, ni lini, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbogo anafuatilia sana juu ya wananchi hawa ambao wanastahili kulipwa au wana madai yao na amenipa barua ambayo inahusiana na madai haya.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu kwamba sheria inaangalia pande zote; inaangalia upande wa wale wahusika ambao wana madai yao lakini pia inatazama kwa sisi Serikali wakati tunafanya malipo ya madai ya wananchi. Kwa maana hiyo, malipo yote yanafanyika kwa kufuata sheria.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Sheria ya Barabara Namba 13 ya 2007, hasa *section 16* inaonesha utaratibu unaotakiwa utumike kulipa fidia. Hii ni pamoja na kuitazama Sheria hii ya Utwaaji wa Ardhi (*Land Acquisition Act*), Sheria ya Ardhi yenye na Sheria ya Ardhi ya Vlijji pamoja na sheria nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo napenda kumwambia Mheshimiwa Mbunge avute subira wakati tunaendelea kutazama uhalali wa fidia hizo baada ya hapo wananchi hawa wataweza kupata haki zao. Kwa hiyo, nimtoe hofu lakini niwatoe hofu wananchi wa Nsimbo kwamba suala lao liko mikononi mwetu na tunaendelea kulishughulikia, haki za watazipata.

SPIKA: Bado tuko Wizara hiyo hiyo, swali la Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, Mbunge wa Chemba, uliza swali lako tafadhali.

Ujenzi wa Barabara ya Handeni – Singida

MHE. JUMA S. NKAMIA aliuliza:-

Je, ni lini barabara ya lami kutoka Handeni – Chemba – Kwamtoro hadi Puma Singida itaanza kujengwa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Kwandikwa, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, Mbunge wa Chemba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Handeni – Kiberashi – Kwamtoro – Singida yenye urefu wa kilometra 461 inayopita katika Mikoa ya Tanga, Manyara, Dodoma na Singida inaunganisha Ukanda wa Mashariki, Ukanda wa Kati na Ukanda wa Kaskazini Magharibi. Barabara hii inaunganisha mikoa ambayo mradi wa bomba la mafuta kutoka Hoima Uganda hadi Tanga unakopita. Mradi huu ni muhimu sana kwani utaweza kuinua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutumia fedha za ndani tayari imekamilisha upembuzi yakinifu wa kina wa barabara hii. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii utaanza katika mwaka wa fedha 2018/2019 ambapo shilingi bilioni moja zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya kazi ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na juhudii za kutafuta fedha za kutosha kukamilisha ujenzi wa barabara hii muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Juma Nkamia, nilikuona.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa maeneo ambayo barabara hii inapita sasa hivi ni miaka mitatu walishawekewa alama za X na hawajaambiwa nini kinaendelea kwa sababu wameshindwa kuendeleza hata maeneo yao. Naomba kauli ya Serikali, Mheshimiwa Waziri anaposema hapa mbele ya Bunge kwamba imetengwa shilingi bilioni moja sina uhakika kama amesoma vizuri hapo au amekosea? Nini kauli ya Serikali kuhusu wananchi hawa wa maeneo haya ambao wamewekewa alama za X?

SPIKA: Majibu ya swali hilo fupi na zuri, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, kwanza niseme tu alama hizi za barabarani ni muhimu sana zinavyowekwa kwa sababu alama hizi zinaleta mawasiliano, zinawajulisha wananchi kwa ujumla kwamba eneo hili litakuwa na mradi wa barabara. Kwa hiyo, tahadhari hii inasaidia kwenye mipango yetu ya wananchi na upande wa Serikali kwa ujumla ili wananchi hawa wasije wakaweka vitu vya thamani kama sheria inavyotaka. Kwa hiyo, niseme tu kwamba alama ni muhimu zinavyokuwepo zinatuweka kwenye *alert* ili tuweze kujua kwamba kuna mradi mkubwa wa maendeleo unakuja.

Mheshimiwa Spika, nini kauli ya Serikali, niseme kwamba ujenzi wa barabara hii umeshaanza. Nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Chemba na Watanzania kwa ujumla, barabara hii tumeainisha kati ya barabara ambazo zipo kwenye *integration* ya *East Africa* (mtandao wa barabara za Afrika Mashariki). Kwa hiyo, kuiweka katika mtandao wa barabara za Afrika Mashariki kunaonesha namna gani barabara hii tumeipa kipaumbele cha hali ya juu katika kuitafutia fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaambie tu wananchi kwamba alama hizi zimewekwa kwa ajili ya kuwatahadharisha wasiweke vitu vyatya thamani kubwa wakati tunafanya maandalizi ya kulipa *compensation* (fidia). Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira, ni mpango wa Serikali. Mimi niseme tu ukweli kwamba ujenzi wa barabara hii umeshaanza kwa sababu ujenzi tunaanza katika hatua tofauti; unaanza kwanza usanifu, michoro halafu sasa tunatafuta fedha na tumeuza mradi huu kwa wafadhili wanaofadhili Afrika Mashariki. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge uvute subira, mambo mazuri yanakuja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Martha Umbulla.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwanza mimi niishukuru Serikali kwa kujenga na kukamilisha barabara ya Dodoma hadi Babati kwa ufanisi na sasa inatumika vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha ni kwamba vyombo vyatya usafiri kutoka Dodoma, Singida, Babati wanatoza nauli kiasi cha shilingi 17,000 hadi shilingi 20,000 na wanatoza kiasi hichohicho kutoka Dodoma kupita Kondoa kwenda Babati, umbali ambao ni sawa na Dodoma kwenda Iringa kwa gharama ya shilingi 8,000 hadi shilingi 10,000 tu.

Je, Serikali iko tayari kurekebisha hitilafu hiyo ili wajasiriamali wetu sasa watoke Babati asubuhi kuja kufanya ujasiriamali katika Jiji la Dodoma kwa ufanisi na kwa nauli nafuu? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri Mheshimiwa Elias Kwandikwa, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia suala la nauli kwa wananchi kwa ujumla lakini pia kwa kufanya mchanganuo ambao nimemsikiliza hapa.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba pale nauli zinapopanda zinawiana na ubora au ubovu wa barabara. Kwa hiyo, yaweza kuwa labda watumiaji wa barabara hiyo walikuwa wamekariri nauli kubwa wakati barabara haikuwa nzuri.

Kwa hiyo, nizichukue pongezi zake lakini hili suala tutalifanya kazi, ziko mamlaka zinazoshughulika na masuala ya nauli ili waweze kuona stahili kamili ya nauli katika barabara hii Mheshimiwa Mbunge aliyoitaja ili tuweze kuchukua hatua zinazostahili. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Cecilia Parezzo na Mheshimiwa Martha. Tuanze na Mheshimiwa Cecilia.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Ujenzi inaelekeza kuunganisha mikoa na mikoa kwa kiwango cha lami na kumekuwa na kilio cha muda mrefu na ahadi ya muda mrefu ya ujenzi wa kiwango cha lami ya barabara ya kutoka Njiapanda – Karatu – Mang’ola - Lalago. Je, ni lini barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami?

SPIKA: Mheshimiwa Cecilia, umeleta barabara nyingine kabisa. Majibu Mheshimiwa Waziri kama unayo tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, ni kweli ni sera ya Serikali kuunganisha mikoa na mikoa. Kwa hiyo, tunaanza kuunganisha mikoa na mikoa, tunaungamisha mikoa pamoja na nchi za jirani na hizi harakati zinaendelea, zipo barabara chache sana ambazo zimebakia kuunganishwa kwa maana ya mikoa kwa mikoa.

Mheshimiwa Spika, kwa barabara kubwa ambazo zimebakia ni chache ikiwemo barabara hii ambayo Mheshimiwa Mbunge anaitaja ikiwa inatokea kule Simiyu –

Lalago – Sibiti – Mbulu – Karatu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba ukitoka Sibiti yako matawi mawili ya barabara, iko barabara ambayo inapita kandokando ya Mto Eyasi kwenda Karatu na hii barabara ambayo inapita Haydom – Dongobesh - Mbulu Mjini lakini itaunganika na barabara inayotoka Mbuyu wa Mjerumani - Mbulu Mjini - Karatu.

Kwa hiyo, hizi barabara zote ziko katika hatua mbalimbali. Barabara inayopita Eyasi tayari michoro yake imeshakamilika tunatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi na katika bajeti hii iliypitishwa na Bunge lako tumetenga fedha za kuanza ujenzi katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, lakini kizuri pia nimjulishe tu Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa maeneo ya Lalago kuja upande huu wa Manyara na Arusha kwamba pale Sibiti tulikuwa na tatizo kubwa sasa ujenzi wa lile daraja unakamilika, vile vyuma ambavyo tulivisubiri kwa muda mrefu vilishafika na baada ya mvua kupungua tutapandisha vile vyuma hata kabla ya harakati za kukamilisha lami basi wananchi wataweza kupita kutoka Lalago kuja katika mikoa hii pamoja na kuja Singida. Tutapunguza kilometra karibu 400 kwa mtu anayetoka Mwanza na Simiyu kwenda Karatu kama atapita pale Sibiti akipitia Eyasi kwenda Karatu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge vuta subira, sisi tumejipanga vizuri na Serikali inaendelea kutoa huduma na kuunganisha mikoa.

SPIKA: Mheshimiwa Martha Mlata, swali fupi la mwisho la nyongeza.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, ahsante na ubarikiwe kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, tunaposubiri ujenzi wa barabara kutoka Handeni - Singida na Waziri amezungumzia ubora wa barabara ile tukitambua kuna milima na mabonde. Nini kauli ya Serikali kuhusu ubora wa barabara ya kutoka Sekenke - Shelui ambayo imekuwa ikiua watu takribani kila mwezi? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, naona Wabunge wote wa Singida wamelishangilia. Mheshimiwa Naibu Waziri, Sekenke – Shelui.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, kwanza nikupongeze sana Mheshimiwa Martha Mlata kwa kufuatilia barabara za Singida na kila wakati tumezungumza ndani na nje ya Bunge, unafuatilia sana hizi barabara.

Mheshimiwa Spika, nimuahidi tu Mheshimiwa Martha na watumiaji wa barabara hii wakiwemo wananchi wa Singida kwamba tumeionna barabara hii. Barabara hii hatutaitazama upande wa Sekenke tu, tutaitazama kutoka Singida Mjini tunakwenda mpaka Misigiri tunashuka Sekenke. Tumetenga fedha ya kuweza kufanya usanifu wa barabara hii kwa sababu imekuwa ni ya muda mrefu na imechakaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Singida na Watanzania kwa ujumla kwamba sasa hivi tunakwenda na teknolojia mpya kwa barabara hiyo kama unavyoona kwa ile miteremko ile lami inakimbia. Kwa hiyo, tutaiangalia ili tuitengeneze kiasi kwamba ubora wake uwe mkubwa zaidi na watumiaji wa barabara watumie vizuri na pia kupunguza ajali ambazo zimekuwa zikitokea mara kwa mara. (*Makofii*)

SPIKA: Swali la mwisho kwa siku ya leo la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, litaulizwa na Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo, kwa niaba yake Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro.

Na. 296

Hitaji la Magari Katika Vituo vya Polisi – Ruvuma

MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO (K.n.y. MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO) aliuliza:-

Kuna upungufu wa magari katika Vituo vya Polisi Mkoa wa Ruvuma. Yaliyopo sasa ni mabovu kabisa na hayafanyiwi matengenezo kutokana na ukosefu wa fedha.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka magari kwenye vituo hivyo?

(b) Je, ni lini Serikali itapeleka pesa kwenye vituo hivyo kwa ajili ya matengenezo ya magari na mafuta ya magari hayo ili polisi waweze kufanya kazi zao kwa wakati?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo, Mbunge wa Viti Maalum, kama liliyoulizwa kwa niaba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Ruvuma una jumla ya magari 33 na kati ya hayo magari 24 ni mazima yanafanya kazi na magari tisa ndiyo mabovu. Aidha, Jeshi la Polisi hufanya mgao wa magari katika mikoa na vikosi kwa kuzingatia vigezo mbalimbali kama kiwango cha uhalifu katika eneo husika, hali ya jiografia, idadi ya watu na mahitaji ya kiutawala ambapo katika mwaka 2015 Mkoa wa Ruvuma ulipokea magari 11. Hivyo, mpango wa kupeleka magari katika Mkoa wa Ruvuma utategemea upatikanaji wa magari mapya na mahitaji kulingana na vigezo vilivyoainishwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitenga na kupeleka mgao wa fedha katika Jeshi la Polisi kila mwezi ambapo fedha hizi hugaiwa na kupelekwa mikoani kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya jeshi ikiwemo *operation*, matengenezo ya magari na mafuta kwenye vituo vya polisi. Aidha, utaratibu ulipo sasa kila Mkoa unapelekewa fedha kwa ajili ya matengenezo na mafuta kila mwezi kuititia kasima ya mikoa. Ni kweli kuwa magari mengi kwa sasa yamekuwa ni ya muda mrefu hivyo huhitaji matengenezo ya

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

mara kwa mara ambapo Jeshi la Polisi linahitaji kufanya matengezo kwa magari yanayoharibika kwa kutumia fedha zinazopelekwa na kuwashirika wadau wa ulinzi na usalama katika maeneo husika.

SPIKA: Swali la nyongeza kwa muuliza swali.

MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Mkoa wa Ruvuma unapakana na nchi za Msambiji na Malawi. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza idadi ya magari pamoja na boti kwa polisi ili kudhibiti uhalifu katika sehemu za mipakani?

SPIKA: Majibu ya swali hilo fupi la nyongeza, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, hata nilipotembelea Songea Mheshimiwa Mbunge pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma walileta hoja hiyo ya magari. Niseme tu kwamba Serikali tutazingatia maombi hayo punde tutakapopata magari. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Mbeya Mjini, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, karibu Bungeni, uliza swali lako.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, ahsante, *good to see you again. (Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na matatizo waliyokuwa nayo polisi kwenye masuala ya vyombo vya usafiri lakini nikuhakikishie Jeshi la Magereza lina hali mbaya sana, siyo tu magari mabovu ni kwamba hawana magari kiasi kwamba wanafikia kupeleka wafungwa amba wana kesi au rufaa wanawafunga pingu wanawapeleka Mahakamani kwa miguu. Sasa hii ni mbaya sana kwa usalama wao Askari Magereza, lakini pia kwa usalama wa wale watuhumiwa amba wamefungwa pingu na kutembezwa kwa miguu kwa sababu mathalani mtu anatuhumiwa kwa ujambazi

halafu anapita mitaani wale wanaomtuhumu wanamuona, wanaweza wakamvamia na kumshambulia na kuhatarisha maisha ya yule mfungwa. (*Makofi*)

SPIKA: Mfano mzuri sana huu, Mheshimiwa Sugu anatetea Jeshi la Magereza, Mheshimiwa Waziri unasemaje? (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Sugu kwa kuuliza swali kwa *experience* na niseme tu kwamba yeye ni mshauri mzuri tutazingatia hilo ili tuweze kuweka mgao upande Jeshi la Magereza ili kuweza kuepuka tahadhari hiyo aliyoisema. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la mwisho la nyongeza.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika Mkoa wetu wa Iringa kuna magari ambayo huwa yanaharibika tu kidogo yanawekwa katika vituo lakini tumekuta kuna mlundikano mkubwa sana wa magari mabovu. Ni kwa nini Serikali sasa aidha itengeneze au iyauze haraka sana ili yaweze kusaidia upungufu mkubwa ulipo katika Mkoa wetu wa Iringa?

SPIKA: Magari mabovu kwenye Vituo vya Polisi na pipipiki nyingi sana, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Ritta kwa wazo alilotoa. Niseme tu kama Serikali tunapokea ushauri huo, tutayatengeneza yale yanayotengenezeka na tutafanya utaratibu wa kuyauza yale yasiyoweza kutengenezeka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maoni yako upande wa pipipiki nilishatoa maelekezo kwamba vijana wa bodaboda

wanaokamatwa kwa makosa madogo madogo wafanyanyiwe utaratibu wa kuandikisha na kuruhusiwa waendelee na kazi zao ili wawewe kulipia kama kuna faini ambazo walitakiwa kulipa kuliko kuzirundika pikipiki hiso na zingine kuweza kuharibika wakati wangeweza kulipia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, juzi sikukuona pale Uwanja wa Taifa, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kwenda pale kwa sababu kwa kweli kwa matokeo yale kama Rais asingekuwepo viti visingebaki salama. (*Makof/ Kicheko*)

SPIKA: Kwa majibu haya ya Mheshimiwa Waziri basi kipindi cha maswali kimeisha, hatuendelei tena. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwatambulisse wageni, nikianza na wale walio kwenye Jukwaa la Spika ni wageni wangu, wageni 17 ambaao ni wanachuo 14 kutoka Chuo Kikuu cha Michigan, Marekani wakiongozwa na Mwalimu wa somo la Kiswahili katika Chuo hicho Profesa Nyambura Mpresa. Karibuni sana, hawa ni wanafunzi kutoka kule Mjini Michigan ambaao wanasoma somo la Kiswahili na Mwalimu wao Ndugu Nyambura Mpresa ambaao ni wageni wetu leo. Kwa hiyo, mnaona jinsi Kiswahili kinavyozidi kwenda mbali katika nchi mbalimbali. Karibuni sana wapendwa. (*Makof*)

Wageni hawa wameambatana na mwenyeji wao kutoka Chuo Kikuu cha St. John's ambaye ni Makamu Mkuu wa Chuo hicho Profesa Emmanuel Mbena, ahsante sana. Profesa Mbena ambaye ni Makamu Mkuu wa Chuo cha St. John's ni mpiga kura wa Kongwa na ni ndugu yangu. Karibuni sana, naomba mkae. (*Makof*)

Wageni wengine kwenye jukwaa hilo hilo ni mgeni wetu maalum kwa ajili ya ibada ya leo mchana na nitangaze moja kwa moja kutoka kwa Mwenyekiti wa Ibada *Chapel* ya Bunge, Mheshimiwa Anna Lupembe anasema kwamba leo saa 7.00 mchana kutakuwa na ibada eneo la wazi la

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

basement na ibada hiyo itakuwa na Mtumishi wa Mungu Mtume na Nabii Josephat Mwingira ambaye atahudumu katika ibada hiyo ikiwemo Kwaya ya Efatha na Kwaya ya Andrea Mtakatifu kutoka Msalato Dodoma. (Makofi)

Kwaya ya Andrea mpo leo hapa? Karibuni sana, hii kwaya ni maalum kabisa, inatoka Kanisa la Mtakatifu Andrea hapo Msalato na nyimbo zao ni mzuri sana, hongereni sana. (Makofi)

Kwa hiyo, Waheshimiwa mtakaoweza kushiriki kwenye ibada hiyo basi mfike muwaone vijana hawa wamebarikiwa sana. Natumaini mmekuja na cd zenu ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuzinunua pia, ahsante sana. Kwa hiyo, nimitambulisse sasa Mchungaji Mwingira kama yupo, kama hajafika basi tutamtambulisha baadaye atakapofika. (Makofi)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Jumaa Aweso, Naibu Waziri, Maji na Umwagiliaji anamtambulisha ndugu yake kutoka Iringa, Ndugu Eribariki Msengi, karibu popote pale ulipo. (Makofi)

Mheshimiwa Daniel Mtuka, Katibu Mkuu APNAC Tanzania anawakaribisha wafanyakazi wa TWAVEZA waliotoka Jijini Dar es Salaam na Kampala, Uganda wakiongozwa na Ndugu Emmanuel Arinaitwe, Mratibu wa APNAC nchini Uganda, karibuni sana. (Makofi)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ambaao ni familia yake, wakiongozwa na mke wake Ndugu Mary Hasunga, karibu sana shemeji yetu, karibu Bungeni. (Makofi)

Wageni 11 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambaao ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Mbozi, Mkoani Songwe, wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Mbozi, Ndugu Simon Mboya. Karibuni sana wageni wetu kutoka Mbozi, mbarikiwe sana. (Makofi)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Wageni wa Mheshimiwa Abbas Mwinyi ambaye ni Mwenyekiti wa CCM, Tawi la Mambosasa, Fuoni Zanzibar, Ndugu Ameir Haidar Mshenga, karibu sana Ameri. (*Makof*)

Wageni 78 wa Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu ambaa ni wananchi na Madiwani kutoka Hanang, Mkoani Manyara wakiongozwa na Ndugu Mathew Darema, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Hanang. Karibuni sana wageni wetu kutoka Hanang. Karibu sana Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya, pole kuna wakati nasikia ultaka kuswekwa ndani. (*Makof/ Kicheko*)

Wageni watano wa Mheshimiwa James Milly ambaa ni viongozi wa Taasisi ya *Pingos Forum* kutoka Mkoani Arusha, ndugu zangu wa *Pingos* karibuni sana, tumewa-miss kwa muda mrefu sana, karibuni sana hapa Bungeni. (*Makof*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Frank Mwakajoka ambaa ni viongozi wa BAVICHA, Mkoa wa Songwe. Ahsante sana. (*Makof*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Marwa Chacha ambaa ni marafiki zake kutoka Serengeti Mkoani Mara, wakiongozwa na Bi. Suzan Chacha ambaye ni mke wake. Bi. Suzan ndiyo yupi hapo sasa? Hebu nyoosha mkono Bi. Suzan, karibu shemeji yetu, yupo na mjukuu wangu pale. (*Makof*)

Wageni sita wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro ambaa ni Wanakikundi cha Ufugaji wa Samaki kutoka Songea, Mkoani Ruvuma wakiongozwa na Ndugu Grey Nyoni. Karibuni sana wafugaji wa samaki. (*Makof*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Fatma Toufiq ambaa ni Sekretalieti ya *Tanzania Paralegal Network (TAPANET)* kutoka Morogoro wakiongozwa na Ndugu Tolbert Mmassy, Mratibu wa *TAPANET*. Karibuni sana. (*Makof*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu ambaa ni Madiwani wa Halmashauri wa Wilaya ya Igunga

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Igunga, Mheshimiwa Lukas Moga. Hawa bado wako njani, wamepotea njia hawa, unajua Wanyamwezi wana matatizo wamepotea. (*Kicheko/Makofi*)

Wageni 38 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wanamaombi kutoka Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mchungaji Gonda, karibuni sana wanamaombi, mtuombee sana. (*Makofi*)

Wageni 150 wa Waheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mheshimiwa Rhoda Kunchela, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare ambao ni Wanakwaya wa Efatha ya Jijini Dodoma wakiongozwa na Ndugu Jacquline Manilakiza. Wanakwaya wa Efatha wa hapa Dodoma, karibuni sana. Hawa ni majirani zangu kabisa pale tunapokaa wote. (*Makofi*)

Wageni 50 wa Mheshimiwa Felister Bura ambao ni Wanakwaya wa Kwaya ya Mtakatifu Andrea ya Msalato ya Jijini Dodoma wakiongozwa na Padri Job Mwaluko. Kwa mara nyingine Mtakatifu Andrea simameni tena, ahsanteni sana. (*Makofi*)

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni wageni kumi ambao ni Wanaharakati wa Kutetea Haki za Wanyamapor Tanzania kutoka *Rafiki Wildlife Foundation* iliyoko Babati, Mkoa wa Manyara wakiongozwa na Mchungaji Clement Matigwa, Mkurugenzi Mkuu wa *Rafiki Wildlife Foundation*, karibuni sana, nilikuwa sijawahi kusikia hii organization. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nina orodha ya wachangiaji, tunataka twende moja kwa moja kwenye uchangiaji sasa kwa sababu muda wetu ni mdogo na tunachangia asubuhi hii tu ili jioni tuweze kuruhusu Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri waweze kujibu hoja zenu, kwa hiyo, naomba leo tusiwe na miongozo. Tutaanza na Mheshimiwa Magdalena Sakaya halafu nitakuja

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Heche, halafu tutakuja CCM Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa Amina Mollel. Mheshimiwa Sakaya.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru...

SPIKA: Ngoja kigodo tu, Katibu.

NDG. PAMELA PALLANGYO - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadilio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Wizara ya Maliasili na Utalii

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Lilikuwa jambo la utaratibu, Mheshimiwa Sakaya endelea.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye hotuba ya Maliasili na Utalii ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na matatizo mengi ndani ya nchi yetu na hasa migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji pamoja na maeneo ya hifadhi. Tumekuwa tunalalamika hapa Bungeni kwa muda mrefu sana na nashukuru kwamba Serikali iliunda Tume ya Wizara tano muhimu ambazo zinahusika na mambo ya Ardhi, TAMISEMI, Maliasili na wengine. Kwa taarifa zilizopo ni kwamba wataalam wa zile Wizara wamekamilisha taarifa ile na imekabidhiwa kwa Mheshimiwa Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, kwa kuwa bado migogoro inaendelea, hata hivi ninavyoongea migogoro inaendelea, ile taarifa ifanyiwe kazi haraka sana ili majibu yatolewe. Pia iwekwe wazi kwa Wabunge kwa sababu sisi

ndiyo tunaopiga kelele kila siku hapa Bungeni kuhusiana na matatizo ya hifadhi, wakulima na wafugaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini wakati ambapo pia ripoti hiyo haijawa wazi migogoro ya wakulima na wafugaji imeendelea lakini kwa namna ya pekee sana bado wafugaji wameendelea kuonekana ni tatizo ndani ya nchi hii. Hivi navyoongea kuna kitu kilifanyika ndani ya Wilaya ya Kaliua kinaumiza sana. Kuna mifugo 1,350 ilikamatwa ndani ya Wilaya ya Kaliua ambapo ilipelekwa Mahakamani na ikaamua kwamba mafugo ile iachiliwe kutokana na makosa yaliyokuwepo lakini watu wa Maliasili Kaliua walishikilia ile mifugo tangu Juni, 2017 mpaka Januari, 2018. Hata wale wenye mifugo yao walivyofuatilia Mahakamani kwa mara ya pili Mahakama ikatoa *stop order* kwamba isiuze. Siku waliyotangaza kuuza mifugo ile wale wenye mifugo wallkamatwa na watu wa maliasili wakaenda kuwateka, wakawaficha, wakapiga minada ng'ombe wale wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninavyoongea na wewe na Bunge hili wale watu wamekuwa maskini, watoto wao hawasomi, wamerudi nyumbani wakati hata Mahakama waliweza kuamua kwamba ile mifugo iondolewe. Hatuwezi kuwa na uhifadhi endelevu kama hamna ushirikishwaji, kiukweli inaumiza sana. Kwa sababu tunafuga kwa ajili ya nani, watu wa Maliasili wamekuwa hawana *humanity* (ubinadamu) wanafanya vitu vile kama vile wanaowafanya ni wanyama siyo binadamu wenzao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi navyoongea juzi na jana ndani ya Wilaya Kaliua walikuwa wanakata mipunga ambayo inavunwa, wanaikatia chini, wanaikanyaga na miguu kwenye maji ili isivunwe wakati iko tayari kuvunwa, chakula ambacho kimeshalimwa, kimeshakua ni kukivuna tu. Hata kama watu walikuwa ndani ya hifadhi ubinadamu na akili ya kawaida na bahati mbaya sana hata Mkuu wa Wilaya ameongoza zoezi hili kwenda kukata mahindi na mipunga ya watu.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, swali la kujiliza si ilikuwa ni busara tu kuwaambia vuneni mazao yenu ondokoni, lakini badala ya kuwaambia wavune wameamua kuikatakata ili iangamie na wabaki na njaa hata wakiondoka wakafe huko wanakokwenda. Huu siyo ubinadamu na siyo uhifadhi ambao tunauhitaji. Hii ni Tanzania ambayo tunahitaji amani lakini yanayofanywa ni ya kinyama. Kweli kama Wizara hii haitatumia weledi mkubwa kuhakikisha kwamba inashirikisha Watanzania kwenye uhifadhi itakuwa ni ndoto kuweza kuwa na hifadhi ambayo ni endelevu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na uhifadhi wa ushirikishi wa wanyamapori kwa maana *WMA* na nashukuru kwamba kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri imetamka vizuri ziko *WMA* 38, lakini zinazofanya vizuri ni kumi tu. Nashukuru kwamba tumeunda *TAWA* ambayo Mamlaka ya Kusimamia Mapori ya Akiba, *WMAS* pamoja na maeneo mengine. Naiomba *TAWA* itengete kitengo maalum cha shughulikia suala la *WMA* ili zote 38 ziweze kufanya kazi. Sasa hivi kumi tu ndiyo zinafanya kazi kwa ufanisi na nytingine zinasuasua.

Mheshimiwa Spika, lakini ipo *WMA* ya Wami Mbiki tukiwa tunaenda Dar es Salaam tunaiona. Mimi ni Mjumbi wa Kamati nilitoa ushauri pia kwenye Kamati, Mheshimiwa Waziri ametoa pendekozo kwamba iwe *game reserve*, bahati nzuri mimi nimefanya kazi pale, kwanza *location* yake ni nzuri na ina vivutio vizuri na ni jirani kutoka Dar es Salaam, napendekeza eneo hili liwe chini ya *TANAPA* kwa sababu...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kulia kwangu unapoongea na mwenzako ukasikia sauti imezidi unajaribu kupunguza ya kwako kidogo. Mheshimiwa endelea kuchangia.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Sasa hivi kwa taarifa za Mheshimiwa Waziri suala la utalii wa uwindaji umeanza kupungua. Hata ukiangalia

kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri mapato ya utalii yameanza kupungua, ukiangalia vitalu vingi vya utalii vimeanza kurudishwa na pia kuna mchakato unafanyika nchi za nje kuhakikisha kwamba wanazuia, kwa mfano sasa hivi kuna maeneo ambayo nyara za tembo zimezuiwa kuingia, nyara za simba zimezuiwa kuingia, kwa hiyo, lazima kujikita zaidi kwenye utalii wa picha ambao ndio utalii wenyе faida kubwa na endelevu. Ndani ya Wami Mbiki kuna Mto Wami unapita pale katikati, una samaki wa kila aina lakini kuna uwanda wa aina mbalimbali, kuna eneo unakuta tembo peke yake, unakuta twiga peke yake, unakuta swala pala (impala) na vitu vya aina hiyo. Kwa hiyo, ningependa sana kwa *location* ya eneo lile *WMA* hii iwe chini ya *TANAPA*.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tunasisitiza sana utalii wa ndani. Eneo la Wami Mbiki ni eneo ambalo mtu anaweza kutoka Dar es Salaam akafanya utalii, Mbunge anasafiri kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam ana-*spendsiku* moja pale anakwenda Dar es Salaam, eneo lile kwa *potentiality* yake nashauri Serikali ilifanye liwe chini ya *TANAPA* liweze ku-*utilize* vizuri rasilimali ambazo ziko pale ndani ya *WMA* ya Wami Mbiki.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni vitalu. Tulipitisha hapa sheria mwaka 2009, tulibadilisha Sheria ya Wanyamapori kwa sababu tasnia ya utalii wa uwindaji ilikuwa inamiliikiwa na wageni kwa asillimia 100. Tukasema haiwezekani tasnia hii iwe ndani ya mikono ya wageni peke yao na ili Watanzania waingie tukarekebisha sharia. Tukaishauri Serikali Watanzania wenzetu wavezeshwe kimitaji ili wavezeshwe kuingia kwenye tasnia hii. Pia kuwepo na masharti nafuu kwa Watanzania ili wavezeshwe kuingia kwenye tasnia hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, yote haya hayakufanyika, hakuna mitaji waliyopewa na bahati mbaya kwenye utalii wa uwindaji kuna *investment* kubwa sana, uwekezaji wake ni mkubwa bila kuwezeshe kimitaji hawawezi. Matokeo yake wamechukua vitalu, wameshindwa kuviedesha, vimerudi Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali bado tuna ulazima wa kuhakikisha kwamba Watanzania wanashiriki kwenye tasnia ya utalii. Nachoomba tuwawezeshe kimitaji na tuwape masharti nafuu. Bahati nzuri wale Watanzania wenzetu wakinufaika na utalii ule wanawekeza ndani ya nchi, wenzetu wale wa nje wanakwenda kuwekeza kwao. Kwa hiyo, suala la sekta ya utalii wa uwindaji tunaomba sana Serikali iingilie kati isaidie wazawa waweze kushiriki kikamilifu kwenye tasnia ya utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna Hifadhi ya Mikumi ambayo iko karibu sana hapa, barabara kubwa inayotoka Morogoro kwenda Kilosa na kwenda Kusini inapita pale, lakini wanyama wanauwawa sana kila mwaka. Kila siku tembo na twiga wanauuawa, ukipita barabara ile utaona huruma. Ninachoshangaa tulipendekeza angalau kuwepo na geti mwanzoni na mwishoni mwa ile barabara, nasikia *TANROADS* wamekataa hakuna kuweka geti, watu wanapita pale wanatalii bure bila kulipa chochote. Hata shilingi 1,000 kwenye basi moja kwa siku, tungeweza kupata fedha za kuendelea kutunza eneo lile lakini Serikali imekataa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tulipendekeza barabara ile ichepuke ipite mbele ya hifadhi lakini bado imeshindikana. Sasa rasilimali zetu wenyewe Watanzania ni za kutusaidia sisi wenyewe iweje tuwe na hifadhi ile katikati yetu hapo hapo Mikumi tunashindwa kuiwekea mazingira ya kuingiza zaidi kiasi kwamba mpaka sasa hivi inategemea hifadhi nyingine kwa ajili ya kuijidesha.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iangalie suala la barabara ile ambayo inaua sana, pale *speed* inatakiwa 50 wanapita kwa 120 au 140, matokeo yake wanaua wanyama hata wakilipishwa lakini bado wanaendelea kuua. Kwa hiyo, ili tuweze kunufaika na ile hifadhi, naiomba Serikali iweke utaratibu wa kuwa na geti mwanzoni na mwishoni. Mimi nimetembea mpaka nchi za nje, huwezi kupita katikati ya hifadhi bure, haiwezekani, ni hapa kwetu nashangaa. Hata ukienda Namibia barabara zote hata kama ni za udongo

maadamu inapita katikati ya hifadhi lazima kuna tozo fulani inayotozwa ili hifadhi ile iendelee kulindwa. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Magdalena Sakaya na nakushukuru sana. Mheshimiwa John Heche atafuatiwa na Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa Amina Mollel ajiandae. Mheshimiwa Heche.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii na namuomba sana Mungu leo aniwezeshe nisije nikalia humu kwa jinsi watu wa Tarime wanavyoteswa na Serikali hii.

Mheshimiwa Spika, watu wa Tarime wameteswa sana kwenye masuala ya madini, mpaka na sasa wanateswa sana kwenye suala la mbunga na mambo ya *TANAPA*.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Waziri wa Ardhi yuko humu atuambie ni nani hasa kati yake au kati ya Wizara yake na watu wa *TANAPA* au Wizara ya Utalii wanaohusika na masuala ya ardhi ya nchi hii? Kwa sababu leo tunavyozungumza na nataka niunge mkono taarifa ya Kamati iliyosema mambo yanayoitwa vagingi vinavyowekwa kwenye mijî ya watu na kwenye ardhi za watu yasitishwe mara moja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sijui kama nchi hii tunafikiria vizuri kwamba leo wafugaji wa nchi hii wakiamua hata kwa siku 10 peke yake kuzuia mifugo yao kuuzwa kwa ajili ya nyama mtatoa wapi nyama katika nchi hii? Sijui kama tumewahi kulfikiria hilo. Leo wafugaji ambao ni zaidi ya milioni 10 wamekuwa watumwa katika nchi hii, wanaishi kama watu ambao hawatakiwi katika nchi hii, Serikali yao wenyewe inawatesa watu hawa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, wiki moja iliyopita watu wa Tarime, Kata ya Kwhancha wameenda watu wa *TANAPA* na *DC* na *group* la watu wake anajua alipolitoa, wanakwenda kwenye vijiji, Mwenyekiti wa Kijiji hajui, Diwani hajui, wanavamia, wanaweka kitu kinaitwa *buffer zone*

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

mpaka ndani ya shule, zahanati, ndani ya miji ya watu, kwenye vungu za watu wanaingia wanachimba ndani wanaweka *buffer zone*, ndani kwenye mji wa mtu.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Gibaso kina kaya 120 zote ziko ndani, wanaambiwa watoke hapo, wameishi tangu mwaka 1975 na kijiji hicho kina usajili. Vijiji vya Karakatonga, Gibaso, Nyabirongo, kaya zaidi ya 200 zinaambiwa zihame. Ukienda Kata ya Gorong'a, Vijiji vya Kenyamosabi, Masanga, Nyanungu, Nyandage na Kegonga kaya zaidi ya 2,000 zingine zinaambiwa zihame. Hawa watu hawafuati utaratibu, hawafuati *GN*, hawafuati chochote. Ukienda pale kuna *GN* Na. 235 ya mwaka 1968 iliyosainiwa na Mwalimu Nyerere inaonesha mipaka yote kuanzia chini mpaka juu upande wa ile mbuga, *they just don't care. (Makof)*

Mheshimiwa Spika, wanakwenda pale, wanavamia, wanapiga watu, wanaswaga ng'ombe za watu wanaingiza mbugani. Mwanakijiji mmoja ng'ombe wake 250 wameswagwa wameingizwa mbungani, hii hapa risiti alioandikiwa ya shilingi milioni 25. Ng'ombe 250 wakiwemo ndama ambao hawana thamani ya shilingi 20,000 analipishwa shilingi milioni 25. Fikiria hata Mbunge mwenyewe ambaye anapata mshahara hapa aambiwe kutoa shilingi milioni 25!

Mheshimiwa Spika, ukichukua hizi karatasi, mwingine ana ng'ombe 54 analipishwa shilingi 540,000, mwingine ana ng'ombe 54 hao hao analipishwa shilingi 5,400,000, risiti *fake*. Watu wanalipishwa mpaka shilingi milioni 100. Hebu *imagine* katika nchi hii shilingi milioni 100 unamlipisha mfugaji? Ng'ombe zaidi ya 15,851 wamekamatwa na watu wa *TANAPA*. Kijana mmoja baba yake alikamatwa ...

SPIKA: Wamekamatwa kwenye *buffer zone* au ndani ya hifadhi?

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, nazungumzia masuala ya *buffer zone*. Kijana mmoja ng'ombe wao 400 wamekamatwa, baba yake akapata

mshtuko akafa, mama yake naye akafa anasoma Mzumbe wakarudi wakazika. Wamefanya kesi, wamefika mpaka *High Court, High Court*ime-rule kwamba wapatiwe ng'ombe wao 400 amekuta ng'ombe 25 peke yake. Huo ndiyo unyama ambao watu wa nchi hii wanafanyiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, watu wa Tarime wamepigwa risasi, Chacha Gasaya, Wang'enyi Muhere, Marwa Goyagwe, Chirawe Marwa Sira, hawa ni watu ambao wamepigwa risasi na wamekufa. Thobias Waitara, Chacha Gioto, Marwa Ryoba, Kebacho Kebacho, Mwera Muhere hawa ni watu ambao wameuawa kwenye mipaka hii ambayo ipo na watu wameishi hapo, vijiji vimesajiliwa tangu mwaka 1974. Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa bila aibu wanadanganya. Adam Malima ambaye juzi ametishiwa pale Dar es Salaam akapiga yowe dunia nzima ikasikia anakwenda kuwaambia watu wa Tarime kwamba atawashughullkia na Jeshi yaani kwamba Rais amempa mamlaka hayo ili akawashughulikie watu wa Tarime badala ya kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, naongea haya kwa uchungu mkubwa sana halafu wanasema uongo, wanasema watu wamewarushia mishale. Mimi nimemuuliza Waziri, pale Nyanungu kijiji kizima kina watu zaidi ya 5,000 warushe mishale kwa watu 14, mshale hata mmoja usimpate hata mtu mmoja mionganoni mwao. Wamerusha mawe hakuna hata gari moja lillolopatwa na jiwe yaani kijiji kizima hakina shabaha kiasi cha kushindwa kulenga hata kwenye kioo cha gari moja. Wamekamata watu 100, wamekaa nao siku nne Polisi, *DC* anawaimbisha nyimbo kwamba sisi ni wahalifu, akina mama, watoto wanaimba Kituo cha Polisi wanapiga makofi, sisi ni wahalifu, tunapaswa kufungwa, kwenye nchi hii. Mazao ya watu yanaharibiwa na ng'ombe wa watu wanataifishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa namuomba Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, msilete machafuko na chuki kubwa kwenye Taifa hili. Haya mambo yanaumiza kweli kweli, yanatia simanzi kweli kweli.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, watu wa Tarime tumelinda hiyo mbuga kwa miaka yote, haina faida yoyote na watu wa Tarime. Hajjawahi kutujengea darasa au batii moja. Naomba msiletie machafuko kati ya watu na mbuga. Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla nenda kaondoe zile *buffer zone* kaweke kule ambako *beacon zinaonesha* zinatakiwa kuwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri chukua *GNNa*. 235 ilioachwa na Mwalimu Nyerere fanyia kazi. Msitake kuua watu wa Tarime, tumechoka kuuawa, tumechoka kufanywa wanyama katika nchi hii, kila kitu kwetu ni hasara tu. Madini hayajasaidia watu wa Tarime, mbuga nayo imegeuka kuwa mauaji kwa watu wa Tarime. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mbuga hii hapa ya Selous leo Serikali imetoea kibali cha kwenda kukata zaidi ya miti milioni tatu, hamuoni hilo ni tatizo? Hamuoni kama ni uharibifu wa mazingira lakini ardhi yetu waliyoacha mababu zetu, tunaishi pale watu wamezikwa kuna makaburi wanakwenda kuchimba kwenye kaburi la mtu wanaweka kigingi, juu ya kaburi mtu anaweka kigingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, analeta *GPS*, *GPS* ilikuwa wapi mwaka 1968? Kulikuwa na *GPS* katika Taifa hili mwaka 1968? Watu wamepigwa hapa, kuna wazee wako hapa wa Kisukuma wanalia, wengine anatoka kwenye Jimbo la Mheshimiwa Doto na Majimbo mengine, watu wanateswa.

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ichukue hatua kwenye masuala haya yataleta machafuko mabaya sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Heche, japo sina uhakika sana na kinachoendelea huko, lakini mimi navijua Vijiji vya Gibaso na vile vingine vyote, huwezi kuweka *buffer*

zone kule kwa sababu ni *hard edge*. Mpaka ni huu na kijiji kiko hapa hapa na nyumba ziko hapa, sasa hiyo *buffer zone* utaipata wapi, haiwezekani. (*Makofii*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa Amina Mollel ajiandae.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru Mungu wangu kwa neema yake ya siku ya leo ya kuzungumza katika Bunge lako tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naamini kwamba Serikali inafanya kazi kubwa na Mheshimiwa Waziri Dkt. Kigwangalla pamoja na Mheshimiwa Hasunga mmezunguka nchi nzima kuangalia changamoto ambazo zinaleezwa na Waheshimiwa Wabunge. Najua utakaposimama kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge mtazungumzia changamoto hizo kwa sababu mnazija. Pia najua kwamba mmezikabidhi changamoto na kero hizi kwa wataalam wenu ili wazishughulikie na tunaamini sasa zitafanyiwa kazi. Tunakuamini Waziri na hukuzunguka bure na wataalam wako pia tayari kukusaidia na pale ambapo unaona hupati msaada najua utachukua hatua zinazostahiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukitaka mmea wako uzae matunda lazima uutunze, lakini lazima uweke mbolea na maji na upige dawa. Ukitaka mifugo yako upate mazao mazuri lazima uilishe, wapate chanjo na wapate maji na malisho mazuri. Wizara hii ya Maliasili na Utalii inafanya kazi kubwa, inachangia asilimia 17.6 ya pato la Taifa. Wizara hii ndiyo Wizara inayoingiza fedha nyingi za kigeni, Wizara hii ndiyo inayoingiza asilimia 25 ya fedha zote za kigeni na Wizara hii ndiyo inayoingiza fedha za kigeni dola bilioni 2.3 kwa mwaka. Kwa hiyo, lazima Wizara hii ipate fedha za kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia bajeti tunayomaliza Wizara hii ilipata asilimia 33.5 tu fedha za maendeleo, fedha ambazo haziwezi kuimarisha Wizara ya Maliasili na Utalii. Tunalalamika kwamba watalii hawaji kama

wanavyokwenda katika nchi jirani, hawawezi kuja kwa sababu fedha za maendeleo hatuna, hatuwezi kuimarishe barabara zetu, huduma zetu haziwezi kupendeza kama fedha hazipo za kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Utalii inafanya biashara na watu binafsi na bajeti iliyopita walismamisha biashara ya wanyama hai kusafirishwa nje ya nchi. Serikali ikaahidi kabisa kwamba hawa watu watalipwa fidia na tulitegemea kwamba mpaka leo bajeti nyingine imeingia, Wizara au Serikali itakuwa imekwishalipa fidia. Hawa watu walikopa fedha kwenye benki, hawa watu walitumia fedha zao lakini mpaka leo Serikali hajjalipa fidia kwa watu hawa.

Mheshimiwa Spika, nategemea Waziri utakaposimama utasema kitu kwamba hawa watu watalipwa fidia kipindi gani kwa sababu *interestinaendelea* kukua kule benki, lakini Serikali hajjawalipa fidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nirudi nyumbani, kule kwetu Mkungunero - Kondoa tumeshawapeleka zaidi ya Mawaziri watano. Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla ulikwenda, Mheshimiwa Hasunga alikwenda, tukaitisha m Kutano mkubwa, ukawahutubia wananchi, ukaenda na Mbunge wa pale Mheshimiwa Dkt. Ashatu, wananchi wakapata matumaini, lakini mpaka leo hakuna kinachoendelea kati ya wananchi wa vijiji vyake kule na hifadhi ya Mkungunero.

Mheshimiwa Spika, askari watatu waliwahi kuuawa kule, wananchi wanalima kule mazao yao yanafyekwa, ng'ombe wakiingia eneo lile la eka 50 tu wanachukuliwa, harudishwi kwa wenyewe na wenyewe wanatozwa faini, na ni mgogoro wa muda mrefu sana. Mheshimiwa Waziri ulipokwenda ultoa ahadi nzuri na wananchi wakapata imani na wewe, kijana ulipokwenda na *morale* walikupigia makofi, wakapata imani kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasikitika, natamani kulia kwa sababu kila ninaposimama katika Wizara hili nalizungumza suala la Mkungunero. Mheshimiwa Rais alipompa Mheshimiwa

Dkt. Ashatu nafasi ya Naibu Waziri, wananchi wa eneo lile la Mkungunero vijiji vile 12 walipata amani, kwamba sasa suala lao litaisha, lakini mpaka leo mwaka wa tatu sasa tumeanza, suala la Mkungunero bado liko pale pale. Ninakusihii hebu fanya kitu, ninakusihii wale wananchi shida yao sasa ikashughulikiwe.

Mheshimiwa Spika, lakini tena tuna suala la pori la Swagaswaga. Mpaka wa pori la Swagaswaga na Vijiji vya Handa na Lahoda ni tatizo kubwa. Mpaka upo lakini maafisa wako Mheshimiwa Waziri hawataki kufuata mpaka uliopo pale. Ninakusihii sasa ukashughulikie mipaka kwa sababu kila Mbunge anayesimama anazungumza suala la mipaka. Sisi Dodoma hatutaki migogoro na Serikali yetu, lakini kama migogoro haitatuliwi mapema wananchi hawawezi wakakubali, kama migogoro haishughulikiwi kwa wakati wananchi wataendelea kulalamika, Mheshimiwa Waziri naomba sasa suala hili likashughulikiwe haraka inavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie tena suala la tozo inayotozwa kwa TANAPA na Ngorogoro. Mashirika haya yanafanya kazi nzuri sana na hata fedha tunazopata yanatokana na mashirika haya. Na masharika haya nikubaliane na kamati kwamba wanatoa asilimia 15 ya mapato ghafi kwa Mfuko Mkuu wa Serikali. Halafu wanatoa asilimia tatu kwenda Mfuko wa Uendelezaji wa Utalii, na fedha hizi zinakwenda Serikalini.

Mheshimiwa Spika, lakini bado wanatakiwa kulipa VAT, na bado wanalipa kodi. Ninadhani tozo hizi na ghamara hizo ambazo mashirika haya yanaingia ndio maana unakuta ghamara zetu ni kubwa kuliko nchi ya Kenya, ghamara zetu ni kubwa kuliko nchi za jirani. Serikali inaona nini? Masharika haya ni Serikali, fedha zao hawatii mfukoni, fedha zao zinaingia Serikalini na fedha hizi ndizo zinazowasaaidia kutengeneza miundombinu na watalii wanapokuja wanakuta kwamba kuna miundombinu mizuri. Ninaomba sasa Serikali ione namna kuacha VATkwa fedha hizi ambazo kwa hakika zinakwenda Serikalini.

Mheshimiwa Spika, mashirika haya yamefanya vizuri kipindi chote, na hata tunapoongea asilimia 17.6 ya Pato la Taifa mashirika haya yanahuksika. Hata utalii wa picha kwenye mapori yetu yanahuksika, lakini bado wanatozwa kodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumze suala la ushikaji wa wanyama au ng'ombe au mifugo katika mapori yetu. Serikali inaweza ikaongea na hao wafugaji, wakaweka utaratibu, kwamba wanaposhika ng'ombe wakaandikishane kijiji ni wenye mifugo na Serikali iwe na *RB* kwamba nimeshika ng'ombe wa Mama Bura 400 na sasa kesi iendelee mahakamani ili huyu mtu aendelee kulima na aendeleze kufanya mambo ya maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa mifugo umechukua, halafu unakuja kumtoza faini shilingi milioni 50, anatoa wapi? Serikali yetu ni Serikali ya wanyonge, mkulima akishikiwa mifugo yake waandikishane kwa Mwenyekiti wa Kijiji *exhibit* itabaki kwa mwenye mifugo...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, inasikitisha na kuhuzunisha, lakini niishauri Serikali yangu, watafute utaratibu mzuri ila haya malalamiko yanayotokea kwa wafugaji yatoke, naunga mkono hoja. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Bura, ahsante sana, sana, bahati mbaya muda umekata, lakini *point* yako ilikuwa ya muhimu sana. Mheshimiwa Amina Mollel tafadhalii, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatuma Toufiq na Mheshimiwa Profesa Tibajuka ajiandae.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie. Sekta ya utalii ni muhimu sana katika nchi yetu na sekta hii ni mionganoni mwa sekta mojawapo ambayo inachangia kiasi kikubwa katika

pato la Taifa. Mwenyezi Mungu ametujalia nchi yetu ya Tanzania kuwa na hifadhi pamoja na vivutio vingi ambavyo endapo vivutio hivyo vitatatuliwa changamoto ndogo ndogo zilizopo, Tanzania tutafika mbali katika sekta hii ya utalii.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kabisa kwa kuipongeza Serikali, natambua jitihada wanazofanya na ninakupongeza sana Mheshimiwa Waziri tangu umeingia katika Wizara hii na tunamatarajio makubwa kwamba kutakuwa na mabadiliko katika sekta hii ya utalii.

Mheshimiwa Spika, mimi natoka Mkao wa Arusha na kwa bahati nzuri katika Mkao wetu wa Arusha ni Mkao namba moja ambao tunapozungumzia hifadhi, Kanda ya Kaskazini ndio inayoongoza. Tunafahamu kwamba Tanzania tuna hifadhi 16. Katika hifadhi hizi hifadhi namba moja inayoongoza kwa mapato makubwa ni *KINAPA* ambayo ipo chini ya Mlima Kilimanjaro na hifadhi nydingine zote za Kanda ya Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hifadhi hizi kufanya vizuri bado hizo hifadhi nydingine 11 hazifanyi vizuri kiasi kwamba haziweze kuongeza Pato la Taifa. Hifadhi hizi hazifanyi vizuri kwa sababu ya miundombinu. Kwa mfano *Ruaha National Park*. *Ruaha National Park* mbali ya ukubwa wa eneo hilli la Ruaha ambalo tukingalia kwa Afrika, *Kruger National Park* ya Afrika ya kusini inaoongoza kwa ukubwa na Ruaha inafutia kwa sababu ya eneo kubwa. Hata hivyo hii Ruaha bado haijafikia hifadhi zilizopo kaskazini ambazo kwa kiasi kikubwa zinachangia pato la Taifa hilli.

Mheshimiwa Spika, katika ziara yake Mheshimiwa Rais hivi karibuni akiwa Mkoani Iringa amesitisitiza umuhimu wa kuboresha uwanja wa ndege wa Nduli ili kuhakikisha kwamba watalii wanafika katika mkoa huu wa Iringa ili waweze kufika Ruaha. Pia si tu kwamba uwanja huu wa ndege wa Nduli, tuone pia ujenzi wa barabara ya kwenda *Ruaha National Park*, barabara hii pia ijengwe ili watalii waweze kufika kwa wingi katika Hifadhi hii ya Ruaha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizo ambazo, Wizara inapaswa kuhakikisha kwamba haya yanafanyiwa kazi, lakini bado hatujatangaza ipasavyo hifadhi zetu, vivutio vyetu, utalii wetu na kwa mfano ukienda Kigoma kuna Gombe na Mahale ambapo hapa Tanzania wanapatikana sokwe (*chimpanzee*), lakini miundombinu bado inakuwa ni tatizo. Kwa hiyo, Wizara tuone ni kwa kiasi gani tunaharakisha uboreshaji ili watalii wengi waweze kufika mpaka huko.

Mheshimiwa Spika, ukienda Katavi ambako nako pia kuna hifadhi na bahati nzuri sasa hivi asilimia kubwa barabara imefika, lakini je, huku Gombe na Mahale ambako hawa *chimpanzee* walioko kule ni kivutio tosha kabisa cha kuweza kutangaza utalii na watalii wengi wakafika huko.

Mheshimiwa Spika, si hilo tu, pia kuhakikisha kwamba Wizara inatenga fedha na kuhakikisha kwamba Bodi ya Utalii Tanzania ambayo ndio yenye jukumu la kutangaza utalii wetu, fedha wanazopewa ni kidogo, tunawawezeshaje kwa sababu unapotaka kitu kizuri lazima wewe mwenyewe ufanye jitihada, toa pesa upate pesa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tukiwawezesha Bodi ya Utalii kwa kuwapa fedha wakawenza kutumia nafasi ya kutangaza, *ku-brand* utalii wetu nina imani kabisa kwamba, Tanzania tutapanda juu na hifadhi hizi zitawenza kuingizia pato kubwa la Taifa.

Mheshimiwa Spika, ukienda katika uwanja wetu wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, hebu nenda pale, kwa mfano unapoingia katika barabara hii kubwa ya Mwalimu Nyerere, barabara hii mgeni anapoingia ni vivutio gani, matangazo yamewekwa ili kumuwezesha, mbali ya kile ambacho ye ye ametoka huko anataka kwenda kukitembelea, lakini je, kuna kitu gani kingine cha ziada ambacho kitamfanya ye ye aweze kutoka na kwenda kutembelea? Tuone umuhimu wa *ku-brand* hifadhi zetu, tuone umuhimu wa *ku-brand* utalii wetu pamoja na vivutio mbalimbali.

Mheshimiwa Spuka, tunazo mali kale nyingi, kwa mfano tu hapa katika Mkoa huu wa Dodoma ukienda hapo Kondoa kuna utalii upo, lakini haujatangazwa ipasavyo kuhakikisha kwamba watalii wanafika. Hivi sasa Dodoma ni Jiji, sasa kama Dodoma ni Jiji tunai-*brand* vipi Dodoma ili kuhakikisha kwamba vivutio vingi vinakuwepo?

Mheshimiwa Spika, katika matukio mengi nimeshuhudia, kwa mfano tu shughuli mbalimbali, ngoma zinazochezwa na wagogo, hizi ngoma zikitumika ipasavyo ni utalii tosha amba o utawawezesha watalii mbali ya kuona vivutio vingine hata hizi ngoma tu na kwa sasa kwa sababu Dodoma ni Jiji, tuone umuhimu wa kuwekeza katika mila, desturi na tamaduni zetu ili watalii wanapokuja wawe na vitu vingine vyaa ziada. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika hoteli zetu, kwa bahati nzuri sijatembea sana lakini nimefika nchi ya Nepal. Katika nchi ya Nepal unapokwenda katika sehemu yoyote ile na hasa wakati wa jioni katika hoteli zote wa kitalii kuna utaratibu wa ngoma, mila na tamaduni zao, ambapo wanashuhudia pale, na ni kivutio. Kwanza inawawezesha wale wananchi wanapata kipato, lakini pia Serikali inapata kipato. Kwa hiyo wakazi wanaoishi maeneo ya karibu na pale wanafaidika kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kule kwetu kwa mfano jamii ya Wamasai, Mmasai tu yeye mwenyewe ni kivutio, lakini je, tunawatumiaje hawa ndugu zetu Wamasai kuhakikisha kwamba ule utamaduni, mila na desturi zao zinawafaidisha hawa Wamasai lakini pia inakuwa ni njia mojawapo ya kuiongezea Serikali pato la Taifa?

Mheshimiwa Spika, nzungumzie pia katika mapori tengefu. Tunayo mapori mengi ninaiomba sasa Serikali kwa kuititia Sheria ya mwaka 2009/2010 ambayo inampa dhamana Waziri mwenye dhamana kuhakikisha kwamba anatenga maeneo kwa ajili ya wafugaji na wakulima ili kuepusha hii migogoro ambayo imekuwa ni shida. Ukisikia hawa wote wanaolalamika juu ya mifugo, mimi wakati na

kwenda *form one* mama yangu aliuza ng'ombe Kwa hiyo ninajua thamani ya ng'ombe.

Mheshimiwa Spika, leo hii mnavyowafilisi hawa na hasa kwa watendaji ambao si waaminifu inakuwa ni pigo na tunawaingiza kwenye umaskini hawa wafugaji. Tunahitaji wafugaji, tunahitaji hifadhi zetu kwa sababu tunaelewa umuhimu wa hifadhi zetu, tunaelewa umuhimu wa mifugo, lakini pia hata wakulima.

Mheshimiwa Spika, mimi nina imani kubwa na Waziri, tuone ni kwa jinsi gani hawa wafugaji hawaumii, wanakuwa ni sababu ya wao kuweza kulinda hizo hifadhi na wanyama lakini pia wakulima nao wanafaidika na haya maeneo yaliyopo. Tuone kwamba haya ni maeneo gani ambayo tutayatenga kwa ajili ya wafugaji na kwa ajili ya wakulima. Vile vile tuangalie jinsi ya kuisuluhisha migogoro hii yote kwa amani na utulivu ili kuepuka haya malalamiko ambayo yanawaumiza wananchi, na hasa wafugaji.

Mheshimiwa Spika, niipongeze pia Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro hasa kwa ujenzi wa maktaba mpya ya kisasa kabisa ambayo itasaidia na inasaidia kwa kiasi kikubwa kuhifadhi mali kale.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni...

SPIKA: Makumbusho, sio maktaba.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Makumbusho ambayo inasaidia kuhifadhi hizi mali kale. Kwa mfano hivi sasa tayari imegundulika kwamba mtu wa kwanza duniani aliishi Afrika; na kwa bahati nzuri huyo mtu wa kwanza imegundulika aliishi Tanzania...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA:Ahsante sana Mheshimiwa Amina.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, nikushukuru, naunga mkono hoja ahsante.

SPIKA: Muda haupo upande wako.

Sasa nimtambulisse Nabii Josephat Mwingira , naamini upo kwenye *gallery*yangu, naomba usimame kama upo. Ahsante sana karibu sana pamoja na timu yako uliofuatana nao, wasimame pia. Ahsanteni sana na karibuni sana. Saa saba ibada ile iliyopangwa itaendelea kama kawaida huko *basement*, karibuni sana. (*Makofii*)

Lakini pia niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge wale ambaao ni wanachama hai wa APNAC kwamba leo saa saba mchana baada tu ya kuhairisha shughuli hizi za hapa kutakuwa na semina ya masuala ya rushwa katika ukumbi wa Morena. Wanachama hai wa APNAC wakutane Morena Hotel saa saba mchana.

Mheshimiwa Fatma Toufiq atafuatiwa na Mheshimiwa James Mbatia.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa na mimi kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kazi kubwa wallyofanya ya kuandaa hotuba hii ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika na wengi tunaiyahamu kwamba sekta ya utalii imekuwa ikiingizia pato kubwa sana nchi yetu kwa asilimia 25 pesa ya kigeni. Lakini iwapo sekta hii itafanyiwa marekebisho na ukafanyika usimamizi madhubuti ninaamini kabisa pato hili linaweza likaongezeka zaidi.

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamezungumzia kwamba Tanzania ina eneo kubwa sana la fukwe, takribani kilometra 1000 ukianzia Tanga hadi Mtwara. Hata hivyo kwa masikitiko makubwa ni kwamba aina hii ya utalii katika nchi

yetu bado hajapewa kipaumbele cha kutosha, kwa hiyo tuna kila sababu ya kutumia tunu hizi.

Nilikuwa naomba niishauri Wizara wafanye utaratibu wa kuwapeleka watalaan wetu katika nchi za Seychelles, Egypt, Tunisia na zile ambazo zimefanikiwa katika utalii huu wa fukwe. Kwa sababu mimi naamini kabisa pia tukiongeza katika utalii wa fukwe pato letu linaweza likaongezeka mara dufu na hivyo sekta hii ikaingiza pesa zaidi.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 52 wa hotuba hii umezungumzia pia masuala ya *cultural tourism*. Napongeza sana juhudzi za Serikali kwa kuhamasisha hii *cultural tourism*. Hata hivyo, pamoja na juhudzi hizo bado kuna mambo makubwa sana ya kufanya, kwa sababu mengi sisi nchi yetu hajafanya. Nchi kwa mfano kama Kenya, wenzetu wako hatua kubwa sana, Morocco, Jordan, India pamoja na Uturuki. Katika hili pia nilikuwa natamani niishauri Serikali ifanye utaratibu wa kuona jinsi gani watalaamu wetu wanakwenda kujifunza na kuleta yale mema na sisi tuweze kufanya hii *cultural tourism*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia sambamba na hilo na wenzangu baadhi ya wenzangu wamelizungumza, tuna makabila mengi hapa nchini kwetu, nichukulie katika mkoa wa Dodoma. Mkoa wa Dodoma jamii ya Wagogo ni wachezaji wazuri wa ngoma, lakini pia wana utamaduni wao wa kuzungusha shingo ambayo naamini hakuna kabilia lingine lolote Tanzania hii wanaoweza kufanya.

Mheshimiwa Spika, sasa kama wakiendelezwa hawa wenyeji wa Mkoa wa Dodoma na wakawa ni kivutio cha utalii mimi naamini kabisa tunaweza tukapata pato kubwa sana. Si wa Dodoma tu, kuna makabila kama Wamakonde wanacheza vizuri sana, Wasukuma, Wanyamwezi, Wangoni, Wafipa, Waha na makabila mengine mengi. Kwa hiyo, iwapo kama utawekwa utaratibu makabila haya yakaonesha mila na desturi zao na tamaduni zao watalii watakuja kwa wingi, mimi naamini kabisa tukuzu jambo hili litatusaidia sana katika hii *cultural tourism*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie kuhusu vyuo vyetu vya utalii, ni vichache sana katika nchi hii. Sambamba na hilo mafunzo ambayo yanatolewa katika vyuo hivi hayaendani na ukuaji wa utalii katika dunia.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba niishauri Serikali kwamba wajaribu kuangalia upya ile mitaala ili kusudi iendane na hali ya sasa hivi. Kwa sababu ukiangalia katika sekta ya utalii Watanzania wengi wanafanya zile kazi za chini, zile kazi ambazo ni za juu hasa katika hoteli za kitalii zinafanya na wageni. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi naamini kabisa tumekuwa na tatizo kubwa sana la ajira, vijana wetu iwapo watapewa mafunzo ya kutosha mimi naamini kabisa hizi nafasi ambazo zinashikwa na wageni badala ya kushikwa na wageni zitachukuliwa na vijana wetu wa Kitanzania. Kwa hiyo, nilikuwa naomba nitoe shime kwa Wizara waone kwamba ili kupata ufumbuzi ni vizuri kurekebisha hili mitaala ili kusudi iendane na mahitaji ya kimataifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 17 wa hotuba hii Mheshimiwa Waziri amezungumzia kuhusu uwindaji wa kitalii. Ni kweli kabisa kuna baadhi ya vitalu vimetolewa, lakini Serikali imetoa wazo kwamba baada ya shughuli za uwindaji wa kitalii yaani ule msimu ukiisha ufanyike utalii wa picha.

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani hili ni wazo zuri sana, lakini pamoja na kuwa wazo zuri hebu sasa Serikali ione jinsi gani itarekebisha miundombinu katika maeneo haya kwa sababu tatizo la miundombinu ni kubwa. Mimi nimekuwa Mkuu wa Wilaya katika eneo la Manyoni na kule kuna *Rungwa, Kizigo, Mhesi Game Reserves*, lakini miundombinu yake ni mibaya sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia kuna zile *posts* ambazo ziko ndani katika haya mapori ya akiba, hebu Serikali ione ni jinsi gani ya kuzirekebisha ziwe katika hali nzuri zaidi ili kusudi wafanyakazi wetu waweze kukaa kule katika yale maeneo ya hizi *game reserves*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni jinsi ya kupata taarifa za jinsi watalii wanavyoingia nchini. Mimi nilikuwa napenda kushauri, kwamba ni vizuri kukawa kuna taarifa ambazo zitasaidia ni idadi ya watalii wangapi wameingia nchini, na watalii hawa wametoka katika nchi zifi. Hii itawasaidia baadhi ya wafanyabiashara ambao wanafanyabiashara za utalii wakajua hitaji la soko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wakitumia *social media*, tunafahamu kabisa kwamba watu wengi sasa hivi wanatumia *social media*, kwa hiyo, taarifa hizi zikiwekwa katika *social media* na watu mbalimbali wakasoma ina maana ya kwamba wale ambao katika nchi zao inaonekana kabisa kwamba utalii upo katika hali ya chini basi hata wafanyabiashara wanaweza wakafanya utaratibu maalumu wa kuona ni jinsi gani wakaweka mkakati kutafuta watalii katika maeneo yale ili sasa kupitia hiyo mitandao ya kijamii tuweze kupata watalii wengi zaidi katika nchi yetu. Sambasamba na hilo tukitumia hivyo inaweza ikatusaidia tukajua kwamba wapi tumejitangaza zaidi na wapi ambapo tunahitaji tujitangaze zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ambalo nilitaka kulizungumzia ni kuhusu *professionals* katika hizi Balozi zetu nje ya nchi. Nilikuwa napenda niishauri Serikali yangu kwamba kwa kuwa inavyoelekea kwamba utalii ndio unatangazwa lakini haujatangazwa kwa kiwango kile ni vizuri basi kule katika balozi zetu kukawa *attached* na baadhi ya wataalam ili waweze kusaidia kutangaza utalii. Kwa sababu ukienda maeneo kama Dubai kwa mfano wenzetu wamefanikiwa sana kwenye suala la utalii kwa sababu ya matangazo, wenzangu wengi wamelizungumzia. Kweli matangazo yapo lakini hata hivyo hapa kwetu matangazo hayatoshi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilikuwa nashauri ikiwezekana Serikali iweke utaratibu wa kupeleka *professionals* katika balozi zetu mbalimbali ili waweze kusaidia kutangaza utalii wa nchi yetu na hatimaye tuweze kupata...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Fatma Toufiq.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimekutaja Mheshimiwa Profesa Tibaijuka halafu atakuwa na Mheshimiwa James Mbatia, dakika kwa dakika kumi kila mmoja. Jaribuni kuwasha mlioko majirani ili itakayowaka, niokoe muda nina wachangiaji wengi

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Naomba nianze kabisa kwa kusema kwamba mimi hapa si kawalda yangu kukamata shilingi lakini katika hili ninaanza nalo kabisa.

Mheshimiwa Waziri Dkt. Kigwangalla anafanya kazi nzuri na kwa utaalam. Mimi najua kwamba yeche ni *Doctor of Medicine* daktari wa binadamu, sasa daktari wa binadamu napenda kuamini kwamba kitu muhimu kuliko vyote kwake itakuwa ni kuliunda maisha ya binadamu. Sasa hali halisi katika hifadhi zetu kwa kweli namuangusha Mheshimiwa Waziri huyu ambaye tuna matumanini naye makubwa Kwa sababu hali ya hifadhi haijaka vizuri.

Mheshimiwa Spika, tutakuwa tunajidanganya katika taifa hili ambalo kwa kweli linaongozwa na Mheshimiwa Rais anayesifika dunia nzima kwa kutetea wanyonge sasa watu/ majirani wa hifadhi si wanyonge? Maana yake ukweli ni kwamba hadi tunapozungumza sasa hivi kuna sintofahamu karibu na vijiji jiraniya hifadhi, mapori ya akiba na *game controlled areas* kwa kweli hali yao sio nzuri, na ni wajibu wa sisi Wabunge kuyasema mambo kama yalivyo kusudi Serikali mpate taarifa muweze kuyafanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwaka juzi Mheshimiwa Mama Samia Suluhu kwa mfano alisitisha zoezi la kutoa mifugo

kwenye hifadhi kusudi Serikali ijipange watafute maeneo ya wafugaji. Suala hili halikufanyika; kwa hiyo maafisa wanyamapori na ninazungumza jambo ambalo naliua kabisa, maana mimi katika jimbo langu Muleba Kusini tuna mapori ya Biharamulo, Buligi, Kimisi na kadhalika. Yanatokea kule kwa kweli wananchi hawawezi kutuelewa yasipofika katika Bunge hili na ninavyosikia taarifa za Tarime na kwingineko hali si nzuri; sasa tatizo ni nini na tufanye nini?

Mheshimiwa Spika, mimi ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba atambue kwamba dhana ya misitu ya akiba iliyo nyengi imepitwa na wakati kwa Mkoa wa Kagera, naomba kabisa Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa utueleze una programu gani ya kuendeleza utalii, misitu na hifadhi katika mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba kule achana na dhana ya Mapori ya Akiba ya Biharamulo na Kimisi na Buligi tangaza *national park*. Ukituletea programu ya kutangaza *national park* utakuwa na *comprehensive program* ya kufanya kazi na kuondokana na matatizo tuliyonayo sasa hivi, kwa sababu hizi shoroba ambazo nasikia mnaziweka hiyo ni kazi ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi. Tatizo linatokana na watu wa maliasili kujipimia ardhi, hamna mamlaka hayo, mimi najua na nilikuwa Waziri wa ardhi miaka mine, hayo mamlaka hamna. Tatizo linaanza kwa watu wa maliasili kuchukua kazi za *surveyor* ambaye yuko Wizara ya ardhi wanajipia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano, hapa Kisarawe kuna msitu wa Kazimzumbwe imekuwa ni mtafaruku mkubwa sana kwa sababu walikosea wale watu wa Maliasili, *wali-shift* mpaka na Gurumeti ni hayo hayo.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kusema kwamba kusudi tuende mbele, Mheshimiwa Waziri Kigwangala mimi nina imani naye lakini sasa hivi nimemkumbusha fani yake kwamba wajibu ni kuanza kulinda maisha ya binadamu. Sasa hatuwezi kukubalika tukionekana kwamba tunalindaje raia wetu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nishauri kwamba kwanza tu-*certify* mipaka na Waziri wa Ardhi amsaidie Waziri wa Maliasili ku-*certify* mipaka tujue hifadhi ni nini na wanyama hawa lazima wapate maji. Kwa mfano pale Serengeti kuna sehemu kwamba Serengeti haifikii Ziwa Victoria, shoroba za wanayama kufikia maji nazo ni muhimu. Nimesema kwa mfano kule Nyakabango kuna ushoroba katika ya Chato na Muleba kule kwangu tumeweka ushoroba wakati wa kiangazi lazima nyati waende kunywa maji kwenye ziwa.

Mheshimiwa Spika, sasa unaweza ukakuta njia kama hizo za wanyama zinawekwa, lakini ziwekwe kwa mujibu wa sheria na si kwa wanyamapori kupima mipaka kwa macho. Kwamba wanakaa hapo wanaamua kama mpaka unapitia hapa unapitia pale.

Mimi naomba kusema kwamba tuna hifadhi kusudi tupate mapato. Sisi kwa upande wa Kagera programu tunayohitaji sasa tunataka *national park* ili na sisi tuweze kupata watalii, maana sasa hivi wale maafisa wanyamapor wako mule wanachoma mkaa tu wala hakuna hifadhi yoyote utakayoweza kukamilisha. Unatoa mifugo, watu wanahangaika, lakini wale wanaendelea na biashara ya mkaa, kwa hiyo unakuta kwamba mazingira yanazidi kuharibika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka kusema kwamba jambo hili ninaposema natoa shilingi naamini kwamba tunaweza kupata sasa mkakati wa kuendeleza kwa mfano upande wa Kagera tuna mifugo mingi.

Mheshimiwa Spika, hii tabia mbaya kila mtu anaitwa Mnyaruanda, Mganda, Mnyamkole, Mkenya, Mloita kama ni Wamasai wanasema wewe ni Mloita, kwa hiyo, ukienda kule Loliondo wanasema huyu ni Mloita huyu, ukienda Tarime unakuwa Mkenya, ukija Kagera kama mimi ndio Mnyamlenge asili. Sasa mambo hayo hayawezি kujenga Taifa hili, Taifa hili ni makabila mbalimbali na si dhana ya viongozi wa nchi hii wala chama tawala ninavyokielewa mimi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilitaka kusema kwamba tuenda *scientifically*, twende na programu na nishauri kwamba tuachane na biashara ya operesheni, hizi operesheni hatuna maslahi nazo, ni mabo ya kushtukiza ni mambo ya haraka na unakuwa huna *proper program*. Kwa hiyo nimeona niyaseme haya yawe *on record*.

Mheshimiwa Spika, kengele ya kwanza ama ya pili hiyo?

SPIKA: Ya kwanza.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Ya kwanza, sawa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka kusema kwamba ninaposema tuwe na *development program* zitaondoa matatizo yote haya na wafugaji ambao kimsingi ndio *problem* kati ya hifadhi na wafugaji wapewe ardhi.

Mheshimiwa Spika, huwezi kuendeleza mifugo au utalii kama huna *proper land demarcations*. Sasa watalii kwa mfano wanapokuja kuangalia wanyama ndani ya hifadhi wanaona na watu wanachunga ng'ombe, hiyo nayo haitusaidii, inaweza ikafukuza watalii.

Mheshimiwa Spika, wanakuja kuangalia simba, nyati na faru, *that is granted*, lakini sasa hawa watu ambao wafugaji ardhi zao ambazo wametengewa ziko wapi? Tangu mwaka juzi, Serikali hii ya Awamu ya Tano naishukuru sana walitoa miezi kumi kwa Mawaziri kadhaa hapa kutafuta ardhi za ufugaji, hiyo kazi haikufanyika kilichotokea watu wakaja kuondolewa kwenye hifadhi kama *operation* na kwa kweli kwa mateso makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, niseme pia na niwe *on record*, ni utawala wa sheria. Kama mtu ameshinda mahakamani na unatakiwa arudishiwe mifugo yake ni lazima irudishwe, kama haipo lazima inunuliwe Serikali hapo ni lazima kuwajibika, ndiko kuwajibika kwenyewe huko, kuwajibika hakuwezi

kuwa sehemu tu ya wananchi na Serikali nayo ni lazima iwajibike pale ambapo kosa limefanywa na watendaji wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Muleba Kusini naomba nitaarifu kama tabia hii iko sehemu nyiningine, kwa upande wa Waziri wa Mambo ya Ndani lazima mtambue kwamba *OCD* maana yake ni *Officer Command District*, kwa hiyo officer wa Biharamulo *OCD* wa Biharamulo hawezi kuja kumkamata mtu wa Muleba bila *OCD* wa Muleba kujua kwa mfano. Kwa hiyo unakuta kwamba ni uvunjivu kunakuwa na ka-group la watu kanajandaa kula rushwa na kutesa wananchi. Sasa jambo hili kwa sababu wananchi wengi hawaelewi sheria hii vizuri unashangaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi kwangu wametoka Biharamulo kuja kuwakamata watu katika kata zangu za Nyakabango, Karambi, unasikia kwamba tumekamatwa na watu wa Biharamulo watu wa Biharamulo watawakamataje bila kufika kwa *OCD* wa Muleba? Kwa hiyo, ni matatizo kama hayo ambayo kwa kweli ni lazima niseme ukweli, na msema ukweli ni mpenzi wa Mungu jamani. Kwa mantiki hiyo nasema kwamba tusiharibiane utawala bora kwa sababu ya wale tulio raweka chini tunapokwenda sisi wanatupa taarifa nzuri. Mheshimiwa Waziri nakukaribisha uje Muleba ujionee mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, mtu anatoka Buharamulo kuja kumkamata mwananchi tena Diwani, anakamatwa anapelekwa mahakamani anasumbuliwa kabisa yaani huwezi kuamini. Mimi nikienda kama Mbunge wanaponismulia wakati mwingine hata na mimi nashindwa kuamini, kwamba hii haiwezi kutokea lakini ndivyo inavyotokea. Kwa hiyo, unakuta ni *network* ya watu kwa hiyo Mheshimiwa Waziri mimi suungi mkono hoja nangojea majibu ya Waziri, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Tibaijuka. Ni vizuri kwamba Mheshimiwa Lukuvi tunaye hapa, matatizo haya ya ardhi Mheshimiwa Waziri Lukuvi wanapokuja watu

wa hifadhi kutaka wachukue eneo fulani liwe ni sehemu ya hifadhi wanakuja na watu wa ardhi wanapima eneo na wanakijji wanaelewana, la kwanza, wakishaenda kule Dar es Salaam hawa wahifadhi wanafanya watu wa ardhi wale waongeze mpaka hiyo hatua ya kwanza. Mfano halisi ulikuwa kule wakati wa Luaha inaanizishwa, kule Ihefu huko waliongeza sana. Wasipoongeza mwanakijji anajua mpaka ni huu, baada ya miaka kumi wanawaaambia sasa kilometra tano kuanzia hapa ni *buffer zone* ambayo hawakusema wakati wanaanzisha. (*Makofii*)

Mwananchi anajua mpaka ni huu anakuja kuambiwa baadaye huko mbele wote tokeni kwa sababu hii ni *buffer zone*. Sasa hiyo ndiyo migogoro ambayo wanatakiwa waseme yote tangu mwanzo, watu wa hifadhi ni mimi mwenyewe muhifadhi sisi ni walafi mno wa ardhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa James Mbatia. (*Makofii*)

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwanza nianze kabisa kusema kwamba naunga mkono taarifa ya Kamati, hii taarifa ni nzuri sana na imewasilishwa kitaalamu kweli kweli, niwapongeze Wanakamati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, utalii atika Taifa letu, kwa miaka minne mfululizo kuanzia mwaka 2012 mpaka 2015/2016 utalii ulikuwa unakuwa kwa takribani asilimia 13.98 lakini mwaka 2016/2017 utalii umeshuka mpaka asilimia 3.3. Hii inatokana na kutokutekelezwa kwa sheria, matamko ya ajabu ajabu, kutokutabiliwa kwa kodi, sijui tunaenda wapi? Kwa sababu utalii 2013/2014 ulikuwa umekuwa kwa asilimia 17.5 na mwaka huu wanasema asilimia 17 lakini Serikali hii ilisema utalii ifikapo 2020 utakuwa umekuwa kwa asilimia 30 lakini badala yake umeshuka mpaka asilimia 3.3; kulikoni Serikali ya Awamu ya Tano? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mazingira rafiki ya utalii; nilishawahi kusema tena hapa na narudia, Tanzania tunahitaji dunia kuliko dunia inavyoihitaji Tanzania. Ukiangalia kodi katika sekta ya utalii ziko zaidi ya 57, lakini kodi hizi kila

kukicha kodi. Dubai juzi wametangaza ufutaji wa kodi kwenye sekta ya utalii na pia wanatoa viza kwa *foreigners* kwa zaidi ya miaka kumi katika ku-*invest seriously* kwenye utalii, lakini hapa kwetu kutoa kibali cha *foreigner* kwenye utalii ni dola 4,000 na ni kwa miaka miwili mpaka miaka minne. Sasa kupanga ni kuchagua, je vivutio nya utalii tunavifanyaje?

Mheshimiwa Spika, Mapato Yanayotokana na Utalii. Kati ya fedha zinazopatikana kutokana na utalii, na Waziri wa fedha alikuwa hapa; kwa mfano takribani dola za Kimarekani bilioni 10 utalii peke yake inachangia asilimia 25 takribani dola za Kimarekani bilioni 2.3, inafutiwa na bandari *transit goods* bilioni mbili, dhahabu bilioni 1.6. Kwa hivyo hawa *giant* watatu ni zaidi ya asilimia 61 ya mapato yote ya fedha za kigeni. Tanzania miaka miwili, mitatu iliyopita tulikuwa wa pili kwa vivutio nya utalii duniani kati ya nchi 133, lakini kwenye miundombinu ya utalii tunashika nafasi ya 110 kati ya nchi 133.

Mheshimiwa Spika, sasa utalii maana yake ni nini? Tutafikiaje watalii 8,000,000? Kwa mfano utafiti ulikuwa umefanya, lazima tuwekeze kwenye miundombinu ya utalii, lazima tuwekeze *seriously* na tuamue kwamba kwenye sekta hii ya utalii, kwa sababu kwa mfano *TANAPA* leo hii, Ngorongoro na wale wengine wote. Inakuwaje Serikali inachangia Mfuko Mkuu wa Serikali na Serikali hiyo hiyo inachukua *corporate tax* kwenye mashirika?

Mheshimiwa Spika, kwa mfano fedha ambazo zimepatikana *TANAPA* kwa mwaka 2017/2018 zilikuwa ni takribani shilingi bilioni 214, Ngorongoro yenewe ni shilingi bilioni 104. Mwaka huu tunategemea *TANAPA* yenewe wapatikane shilingi bilioni 292.8 Ngorongoro shilingi bilioni 156. Sasa lakini miundombinu ya utalii ipo hoi bin taabani.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia huwezi ukatangaza, Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake amesema wameweka mpango mkakati wa *TBC* kutangaza utalii. *TBC* itamtangazia nani duniani? Ningetaka nisikie kwamba katika

kutangaza huku, mashirika kama CNN, BBC, Voice of America, Aljazeera, India, China, Sky News na mengineyo mengi ndio wanaotangaza utalii. Utafiti umeonesha tukiwekeza vizuri kwenye utalii, kwa miaka mitatu/minne tutakuwa tunapata dola za Kimarekani bilioni 16.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa kiasi kikubwa kwa mfano TANAPA kati ya hifadhi 16 hifadhi tano zinatoka Serengeti, Mlima wa Kilimanjaro, Tarangire, Manyara, Arusha. Kwa miaka kumi mfululizo kwa mfano, Mlima wa Kilimanjaro peke yake uliliingizia taifa hili fedha shilingi bilioni 471.5; uendeshaji ulikuwa shilingi bilioni 67.5 miradi katika vijiji ambavyo vinazunguka mlima huo ambavyo vilikuwa 88 zilikuwa shilingi bilioni 8.2 ambayo chini ya asilimia 0.48 ilhali sera inasema ni asilimia 7.5. Tukiendelea namna hii ni kwamba tunaua utalii wetu sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, utalii Kaskazini kwa mfano, kuna tamko lililotolewa kwamba watu wa Kaskazini wasubiri kwanza, nilisema eeh Mwenyezi Mungu atujaalie, nilitumia Zaburi ya 141:3. Nilisema Mwenyezi Mungu awasadie viongozi wa Taifa hili walinde vinywa vyao na awe mngojezi pa midomo mwao kabla hawajatamka. Huwezi ukaligawa taifa kwa kiasi hiki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, fedha za kigeni asilimia 25 zinatoka Kaskazini au zaidi ya asilimia 98 zinatoka Kaskazini. Nakubali Ruaha na sekta nyingine zote lakini kwenye *classification theory* ya kawaida tu, aliye *class A* unaendelea ku-maintain kubaki *class A* wakati unamnyanya na huyu mwengine aweze kufika *class A*. Huwezi ukasema kwamba huyu wa *class A* unamwambia *stop*, unamshusha tuu aende chini, *thinking* ya wapi hii?

Mheshimiwa Spika, kweli nimeshangaa sana, Taifa hili ni moja na ndio maana Mathayo 5:9 wanasema heri wapatanishi wanakuwa wana wa Mungu. Tunakuwa ni kitu kimoja, roho ya umoja Baba wa Taifa uliyoijenga ndani ya Taifa hili, Taifa hili ni moja. Watu wengine wa kutoka Kaskazini sasa hivi wanaanza kuonekana kama si watu wa Tanzania,

hapana. Mama tibajuka ameongea vizuri, yaani tumeanza kugawana kwa misingi ya kikabila, ukanda, taifa letiu linakwenda wapi? Tanzania ni yetu sote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tusipoangalia tunakokwenda; nilisoma Kumbukumbu ya Yoshua bin Sira leo asubuhi, anasema kama huna macho yaani huna mboni ya jicho basi huwezi kuona na kama huna ufahamu huwezi kuwa na hekima. Wimbo wetu wa Taifa unazungumzia hekima, umoja na amani, ni rai yangu kwa viongozi wa taifa hili wazingatia wimbo wa taifa kwenye ile hekima, umoja na amani ili tuweze kukuza utalii vizuri ndani ya Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hoteli za Tanzania ziko hoi, nimeangalia hotuba ya mwaka jana inaonesha idadi ya hoteli tulizokuwa nazo na huduma za hoteli ziko 1,424 vitanda 35,000 ambapo ni sawa sawa tu na viliivyo mji wa Mombasa peke yake. Sasa tunasisitiza kukuza utalii hapa kwetu, lakini tunapoanza kusema angalia ufukwe wa Bahari ya Hindi una kilometra 1,424. Serengeti peke ake ina kilometra za mraba 14,750 Masai Mara ina 1,510 ambayo inaingia mara kumi ndani ya Serengeti, lakini Masai Mara inashindana na hizi 14,750, tunafikiriaje sisi? Lazima tufikiri *seriously*.

Mheshimiwa Spika, suala la vizingi, nilienda kule Ngarenanyuki na Momela. Hiyo bila hata ya ubishi wowote. Nimekwenda binafsi mpaka Makanisa ya KKKT yamefungiwa ndani, shule zimefungiwa ndani, watu wamepigwa makanisani, mambo gani haya? Nchi hii ya utawala wa sheria?

Mheshimiwa Spika, na mwaka huu tunatimiza miaka 70 ya tamko la ulimwengu na haki za binadamu ambalo lilianzishwa tarehe 10/12/1948 siku ya Ijumaa, lakini mpaka sasa miaka 70 tunapiga watu mpaka tunaingilia kwenye makanisa wanakosali Jumapili!

Mheshimiwa Spika, nilikwenda mwenyewe Momela mpaka wazee wanajificha ndani ya kanisa ndiko wanatupa chakula kule Ngarananyuki? *How? Why? This is not possible.*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani ndani ya nchi hii hili? Halafu Serikali iko kimya kwenye ukiukaji huu mkubwa? Ndiyo maana Tanzania leo hii tunashika nafasi ya 153 kati ya nchi 156 kwenye *happiness index*, yaani sisi tuko na Burundi, tuko na Yemeni tuko na wapi huku, si unajua, hata Somalia wametupita kwenye ukiukwaji wa haki za binadamu. How? Nchi gani? *With due respect* hapana hatuwezi tukakubali, Taifa hili tuwekeze akili zetu vizuri, tuangalie tunataka kufanya nini.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kwenye miundombinu kwa nini tuisiwakubalie ngugu zetu wa *TANAPA* na wengine wote, Ngorongoro na wengine, badala ya ule mfuko wa kuweka Serikali Kuu, japo ipo kwa mujibu wa sheria? Tuwekeze kwenye miundombinu ya utalii, miaka miwili, mitatu, minne, mitano, ijayo tayari tuna-*double* tunachopata au mara tatu; utafiti wa *World Bank* wamesema ni dola za Kimarekani bilioni 16 kama tukiwekeza vizuri.

Mheshimiwa Spika, mbuga nyininge za Ruaha, Katavi, kote huko tuzinyanyue lakini zinyanyuke kwa Serikali kukiri kuwekeza vizuri. Tukiwekeza kwenye utalii vizuri ndani ya Taifa hili litatoka, angalia hata kwenye ajira, utalii peke yake ni *direct* ni ajira zaidi ya 500,000 kati ya ajira 2,500,000.

Mheshimiwa Spika, sasa kila siku tunasuasua tunaongea lungha hii hii kwa nini hatufanyi maamuzi? Kwa nini hatukubari kwamba Tanzania yetu hii Mwenyezi Mungu alivyotujaalia Tanzania hii ilivyo nzuri, kwa mfano pale kwetu, ninakotokea, Jimbo la Vunjo, Iango kuu la kuingia Mlima Kilimanjaro, kwa miaka kumi yale mapato ambayo yamepatikana pale, ukiangalia vile vijiji viko hoi bin taabani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini kuna chuki imejengeka kati ya askari wa kulinda mbuga na raia. Kwa mfano vijiji vya Mshiri, Kijiji cha lyasongoro, vijiji vyote ambavyo vinazunguka, Kirie kote huku wanaonekana kama ni adui badala ya kuwa ni rafiki; na haya ni matatizo ya chuki tuu zinazojengwa. Sasa tujenge mahusiano yaliyo mema na yawe mema kweli.

Mheshimiwa Spika, tulikwenda huko na Naibu Waziri wa Utalii kabla hajabadiishwa akaona matukio ya utesaji wa hali ya juu. Sasa naamini *TANAPA*, General/ni mtu makini sana lakini nadhani kuna vurugu zinaingilia katikati ambazo si nzuri. Tutumie lugha iliyo nzuri ili tuhakikishe haya yote tuliyonayo ni kwa maslai mapana ya mama Tanzania ambayo ni yetu sote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kupanga ni kuchagua, wenzetu wa Kenya ukiangalia walivyowekeza, ukisoma hata kwenye website, nilikuwa nasoma leo asubuhi, kwa miaka mitano ijayo utaona wanataka wafikie wapi kwenye utalii utaona hapa kwetu tunasusua, ni blaa blaa tu tunafanya.

Mheshimiwa Spika, tuiwezeshe Wizara kwa mfano, Wizara imeomba bajeti hapa shilingi bilioni 115, lakini ukiangalia mapato tuu yanayotokana haya maduhuli yanayotiokana Wizara inayochangia ni shilingi bilioni 623.5.

Mheshimiwa Spika, sasa...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, ni ya pili.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, Mwenyezi Mungu akubariki sana.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Daniel Mtuka atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa na Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Nape ajiandae.

MHE. DANIEL E. MTUKA: Ahsante Mheshimiwa Spika na mimi kupata nafasi hii kuchangia Wizara ya Maliasili na Utalii.

Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii, kwa kutupa uhai, lakini pia naipongeza Serikali yangu ya Jamhuri ya Tanzania hasa Mheshimiwa Rais anavyofanya kazi, wote tunaiona.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze pia Wizara hii ndugu yangu Kigwangalla, shemeji yangu, kwa maana ya Naibu Waziri Hasunga, nawaona ni vijana wanachapa kazi, wanazunguka huku na huku ukimuona Mheshimiwa Kigwangalla shemeji yangu amepiga buti zile za kijeshi ananikumbusha mbali sana wakati nikiwa kambi za jeshi huko. Kwa kweli nawapongeza sana wanafanya kazi kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo ninayo maoni machache, mchango wangu mdogo na nikianzia, ukifungua kwenye kitabu chako ukurasa wa 19 nimekuta kuna ulinzi wa wananchi na mali zao dhidi ya wanyama pori wakali na waharibifu. Nimejaribu kupitia Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori (*Wildlife Conservation Act*) Namba 5 ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, kwenye sheria hiyo nimeenda nimeangalia zile *regulations* zake, kwenye *regulations* hizo za mwaka 2011 nimekuta kuna jedwali namba nne ambalo linaonesha viwango vya fidia wanazolipwa watu ambao wanauawa na wanyama, wanaopata ulemavu wa kudumu, wanaojeruhiwa pamoja na uharibifu wa mazao.

Mheshimiwa Spika, viwango hivi ni vidogo na vinasikitisha sana. Ukiangalia kwa mfano binaadamu anapouawa na mnyama, ukiangalia kwenye lile jedwali inasikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, binadamu anapouawa anasema fidia ni shilingi millioni moja lakini anapopata ulemavu wa kudumu, anapata shilingi 500,000 tu. Hapana, hiki kiwango ni kidogo sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naweza nikatoa mfano mdogo siwezi kulinganisha na mwanajeshi anapouawa anapokwenda kupigania kulinda amani, kwa mfano labda Darfur kwamba ameuawa kwa bahati mbaya. Tulijibiwa hapa na Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi kwamba fidia ya huyu mtu ni karibu milioni 150.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo hata wale waliouwawa kwenye vita vyatya Kagera wanalipwa pesa nyingi sana mamilioni ya fedha. Nimesema siwezi kulinganisha lakini angalau ukiangalia shilingi milioni moja dhidi ya milioni 150? Haya ni maisha wote wanakuwa wamepoteza maisha wanaacha familia zinahangaika lakini shilingi milioni moja ya fidia hii haitoshi hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara hii, shemeji yangu Kigwangalla naomba unisikilize, rudi, toeni mapendekezo, leteni hizi *regulations*, zibadilishwe viwango hivi viongezwe tafadhari; hiyo ni moja. Hata hivyo bei yake kwenye uharibifu wa mazao, nimejaribu kupekua sheria nimeangalia *regulations* na sheria zote zinazohusu wanyamapor kwenye fidia. Sasa hivi kwa mfano tumekuwa na shida sana manyoni sisi.

MHE. MUSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika Taarifa hapa Mussa Mbarouk.

MHE. DANIEL E. MTUKA: Mheshimiwa Spika, kumekuwa na shida sana, kwa mfano pale Manyoni. Manyoni tumepakana na Pori la...

TAARIFA

SPIKA: Mheshimiwa Mtuka, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mussa Mbarouk.

MHE. MUSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona.

Katika moja ya mambo ambayo tunaharibu ni pale tunapozungumza mambo *serious* halafu unataja shemeji, sijui mjukuu wangu, rafiki yangu, hebu tuyaoondoe, haya mambo ni mambo *serious* ya uchumi wa nchi, sasa haya maneno ya urafiki, shemeji, rafiki, mjukuu tuyaoondoe tuwe *serious* ndivyo wenzenetu wanavyofanikiwa. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mtuka.

MHE. DANIEL E. MTUKA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwenye mazungumzo ya kawaida binadamu mnapokutana huwezi kuongea umekunja uso tu, unaongea maneno magumu, lazima uchombeze kidogo, naomba niendelee. Nimesema hiyo ni bei yake fidia hiyo ni ndogo...

SPIKA: Endelea Mheshimiwa Mtuka, Mheshimiwa Mbarouk hana shemeji ndiyo shida yake, dada zake hawapendwi. (*Kicheko*)

MHE. DANIEL E. MTUKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nimesema fidia hiyo haitoshi, tafadhali sana leteni sheria zibadilishwe ili fidia hii iongezwe. Mnasema kifuta machozi, kwenye uhai sawa ni kifuta machozi, lakini familia inaachwa inaachwa hii. Shilingi milioni moja ndugu yangu ni kiwango kidogo sana hata hakiwezi kusemeka.

Mheshimiwa Spika, nimesema pia pili yake, mazao yanapoharibiwa ndani ya nyumba. Nimesema manyoni sisi kule unapakana na Mapori ya Mhesi na Kizigo, sasa wanyama wanahama, kiangazi mkulima amevuna mazao, ameweke ndani kwenye vihenge, amefungia ndani ya nyumba, tembo anatoka porini huko atokako anakuja anabomoa nyumba ananyanya lile tembe la nyumba, anatafuta kihenge kiko wapi anakula mahindi yote kabisa yanaisha.

Mheshimiwa Spika, lakini nimeangalia sheria hakuna fidia. Ni bora hata yawe yameliwa porini, hiyo naweza nikasema sawa angalau, lakini mtu ameyavuna ameyaweka ndani tembo anakuja atokako anakula mahindi halafu hakuna fidia. Naomba pia turudi kwenye sheria, naomba turekebishe kipengele hicho. Kama mnyama ameingia, ameumiza mtu, amekula mazao pia hicho kipengele cha fidia kiwepo.

Mheshimiwa Spika, nisemee tatizo la mipaka kwa ufupi sana. Sisi Manyoni tumepakana na mapori mawili ya Hifadhi ya Mhesi na Kizigo kama nilivyosema. Mwaka 1994 *Mhesi Game Reserve* ilianzishwa, ni moja ya *reserve* changa kabisa ambayo ina ukubwa wa kilometra za mraba 2000.

Ujio wa Mhesi imeleta kilio kikubwa sana kwa watu wa Manyoni kwa sababu kama ambavyo wenzangu wamelalamika, imeua vijiji na vitongoji vingi sana. Kwa mfano tulikuwa na vitongoji vya Chisola, Msisi, Ilowelo, Machochoroni, Mkindiria, chigugu, Ngongolelo, Chibwee na Iluma.

Mheshimiwa Spika, vijiji hivi tulikuwa tunavitumia kwa kilimo, machimbo ya dhahabu, kwa mfano Iluma pale. Ukichukua taarifa ya benki ya mwaka 1992 dhahabu inayotoka iluma ni dhahabu inayoitwa *alluvial* ambayo hajawahi kuchimbwa mahala popote duniani. Machimbo ya dhahabu tunajua huwa wanasa kwenye mawe, wanatumia madawa makali, zebaki lakini ile unachimba tu unapuliza puliza lile vumbi basi unauba imeshajiunda tayari imeshaji-mould tayari, angalieni tarifa za benki za mwaka 92. Wameweka mipaka, wamezuia yale machimbo, ilikuwa ni neema kwa watu wa Manyoni. Jamani, hii mipaka hii, tuangalie upya mipaka hii ndugu zangu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nizungumzie suala la uwekaji wa mipaka, wenzangu wamelalamika pia. Uwekaji wa mipaka tunaviziana, uwekaji wa mipaka si shirkishi kwa wananchi. Wanakuja huko watokako tunaona watu wanachimbia mambo wanaondoka, baadae inatolewa taarifa kwamba ninyi hapa mnatakiwa msiwepo maeneo haya. Jambo hili ni bayaa sana na limeleta mateso kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia pili, mipaka hii haionekani. Unaenda kuchunga ng'ombe hujui mpaka uko wapi, kumbe umeshavuka uko ndani ya hifadhi yao. Kipigo kinachofata hapo kwa wananchi wetu ni kikubwa mno ndugu zangu. Manyoni haisemwi sana sijui kwa nini, lakini Manyoni kuna watu wanateseka sana kwenye hii Mhesi na Kizigo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2016 nakumbuka ulikuja msafara wa wananchi kutoka Manyoni. Nina vijiji 12 vinavyogusana na mpaka wa Manyoni kule Mhesi na Kizigo,

nakumbuka sana, ilikuwa tarehe 25 Mei, na mimi mwenyewe niliwaongoza; walikutana na aliyekuwa Naibu Waziri kipindi kile Mheshimiwa Ramo Makani, kwenye Maliasili na Utalii. Vile vile walikutana na ndugu yangu Mheshimiwa William Tate Ole-Nasha akiwa Naibu Waziri wa Kilimo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, tuliongea kwa muda mrefu, tukapewa ahadi ndugu zangu mwaka 2016. Hata hivyo hata ile Kamati iliyoundwa kwenda kutatta migogoro ya kitaifa ile Manyoni hata hawakugusa, sjui ni dharau, sjui ni kitu gani? Watu wametekesa sana, wamekuja kwa utiifu wao, wamekutana na Mawaziri wametoa wito na wameahidiwa kwamba Wizara itakwenda. Kamati imeenda hata hawakupita Manyoni kwamba yaani wale hata hakuna kitu...

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Daniel Mtuka.

MHE. DANIEL E. MTUKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja lakini tafadhalii sana, naomba sana wananchi wangu wanapigwa sana kule Manyoni, njooji tutatue tatizo la mipaka. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge. Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa atafuatiwa na Mheshimiwa Nape Nnauye halafu tutahamia upinzani.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kutoa mchango wangu katika hoja hii iliyoko mezani ya hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Ninapenda kutanguliza shukurani zangu za dhati kwa kazi nzuri inayofanywa na Serikali hii ya Awamu ya Tano na hususan katika mambo mazuri pia yanayofanywa na hii Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengi mazuri yanayofanywa na pale mambo mazuri yanapofanywa hatuna budi kutambua na kuunga mkono na kupongeza.

Pia kuna madudu sehemu kadhaa, na hayo pia hayana budi kutolewa maelekezo ndani ya Bunge hili, sisi kutoa ushauri na tutegemee kwamba kuna marekebisho na mabadiliko yatakayofanywa.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote niruhusu pia nitoe shukurani kwa niaba ya watu wa Longido kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa sababu kwa miaka mingi tumekuwa na changamoto ya kutokuwa na gari la kusimamia uhifadhi wa wanyapori na maliasili katika Wilaya yetu. Idara yetu ya Maliasili ya Halmashauri ya Wilaya ya Longido ilikuwa na kilio cha muda mrefu cha kupewa gari la kusaidia doria. Hivi majuzi hata wiki mbili hazijaisha, ndipo gari hilo limepatikana na kwa niaba ya wananchi wa Longido naomba nifikishe shukrani zangu hapa kwa Wizara na kwa Serikali yetu sikivu.

Mheshimiwa Spika, nimepitia hotuba ya Waziri na pia nasimama kuunga mkono maoni yaliyopo katika taarifa ya Kamati kwa sababu nami ni mmojawapo wa wajumbe walioandaa, na maoni yetu tuliyoyatoa ninayasimamia, ninayaunga mkono mia kwa mia na ninaomba yafanyiwe utekelezaji. Bila kusahau lile suala la vizingi vilivyowekwa na TANAPA katika maeneo mbalimbali ya hifadhi za TANAPA ndani ya nchi yetu na yale yaliyogusa maeneo ambayo jamii imekuwa ikiishi kwa miaka mingi bila kuwashirikisha na bila kuwaandaa na kuwafanya watoe ridhaa. Hilo zoezi la kusitisha naomba litekelezwe.

Mheshimiwa Spika, pia nimeona katika hotuba ya Waziri kwamba anafanya *overhaul* ya vitu mbalimbali, sheria, kanuni na kuna rasimu zimeshaandaliwa. Kwa mfano katika mapitio ya Sera za Taifa kuna rasimu ya Sera ya Misitu na Utalii, anasema imeshaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, ningeomba atakapokuja kujumuisha hotuba yake atuambie ni lini itaonekana kwa sababu kuna mapitio mengi ambayo anayafanya na bila sisi kuona na kuridhia inaweza ikawa bado yale mambo ambayo tungependa yabadilishwe yakawa hayatafanyiwa kazi. Kwa mfano, amesema pia kwamba kuna mapitio ya

Sheria ya Misitu, kuna utunzi wa Sheria mpya ya Mali Kale, kuna sheria mpya ya uhifadhi wa wanyamapori zinazosimamiwa na *TANAPA*, Ngorongoro na taasisi mpya ya *TAWA*, kuna kanuni mpya za usimamizi wa shoroba na maeneo ya wazi yale ambayo wanyamapori wanatawanyikia ambayo kwa asili yake ni maeneo wanamoishi watu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya uhaba wa muda naomba basi nijikite zaidi katika maeneo matatu katika mchango wangu. Eneo la kwanza niongelee hili suala la *WMA's*, eneo la pili nigosie mambo yanayoendelea ya uhifadhi kupitia *TANAPA* na niptie pia maeneo yanayosimamiwa na *NCAA* maana yake ni *Ngorongoro Conservation Area Authority*, pamoja na taasisi yetu hii ya *TAWA*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hili la *WMA's*, *WMA's*ni sera nzuri ya Serikali iliyokuja kubaini kwamba uhifadhi wa wanyamapori nje ya maeneo yaliyohifadhiwa rasmi ni kitu cha muhimu na kisichowenza kuepukwa kwa sababu hatujaweka *fence* katika hifadhi zetu. Wanyama wanatoka, wanaingia katika maeneo ya jamii na wanapoingia humo maisha yao yanaweza yakawa hatarini, lakini pia wanaleta hatari katika maisha ya watu.

Mheshimiwa Spika, Sera ililenga kuwafanya wananchi wawajibike, kuwatunza hao wanyama na kuwafaidi pia hao wanyama na ndio maana *WMA's* zilianzishwa. Kwa wale ambao *WMA's* zinawaaletea kero na hazijawa baraka mimi nawapa pole kwa sababu inategemea mchakato wao waliufanyakaje kwa sababu ni mpango shirikishi wa jamii kutunga, kutenga, kupitisha na kuweka utaratibu wa kusimamia rasilimali ya maliasili iliyoko katika maeneo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, sisi kule Longido tuna *WMA* moja ya mfano, *WMA* ya Enduimet na *WMA* hii ilitungwa na jamii kwa kushirikiana na Wizara na wadau wa maendeleo ya uhifadhi (*African Wildlife Foundation*) mimi nilipokuwa Mkurugenzi kule na tuliweka kwamba ni matumizi jumuishi

ambayo yanaruhusu ufugaji na uhifadhi wa wanyamapori ndani ya eneo lile bila vikwazo kwa utaratibu wa mipango ya kanda ambayo imeshawekwa, inafanya kazi na hajifeli hata siku moja.

Mheshimiwa Spika, Ngorongoro iko hivyo hivyo, ule uhifadhi jumuishi ambao unawaruhusu wananchi na wanyama wabaki ndani ya lile eneo la hifadhi halijashindwa, limebaki na limekuwa sahihi na limekuwa salama kabisa kitu ambacho kinakera leo na labda hatujui kama dhana ni nini nafahamu kwamba kuna sensa ambayo imefanyika ya kuhesabu idadi ya watu halali na mifugo iliyoko ndani ya Ngorongoro na inawezekana pia hiyo ikawa ni chanzo cha kutafuta namna ya kuwasogeza watu ndani ya eneo lile.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niishauri Serikali kwamba ile dhana ya uhifadhi jumuishi kwa sababu wananchi walitolewa Serengeti wakaambiwa kwamba Ngorongoro wataishi pamoja na wanyamapiri na jamii yetu ya Wamasai kwa asili yao ni wahifadhi wakuu haijashindwa, kinachotakiwa ni mikakati thabiti ya jinsi ya kuendeleza uhifadhi shirikishi bila kuwabughudhi wananchi katika maeneo ambayo wanaishi kihalali na wanaishi sambamba na maliasili ya wanyamaporii iliyoko kule. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika nikitumia mfano wa *WMA* ya Makame ambayo pia ilianzishwa mimi nilipokuwa Mkurugenzi wa taasisi ya *African Wildlife Foundation* ilianzishwa na ikachukua yale maeneo ya muhimu ya wanyamaporii ambayo wamekuweko tangu enzi za kale wananchi wale wakiishi katika vile viji. Nikisikia leo kwamba kijiji cha Lekuishoibor wako hatarini kupoteza vitongoji vyao viwili, kitongoji cha Lombene na Enjulah kwa sababu *Mkungunero Game Reserve* inapanuliwa ije imege yale maeneo ninasikitishwa sana.

Mheshimiwa Spika, ninasikitishwa na kufanya nione kama inawezekana Watanzania tunapotea katika kuhifadhi maeneo yetu kwa kuanza kuhifadhi mpaka maeneo ambayo yalishahifadhiwa tayari na jamii kwa kufikiri kwa kuondoa

jamii ndiyo hifadi itafanikiwa. Tunaweza tukashindwa vibaya kwa sababu ya kuwafukuza wananchi katika maeneo waliyohifadhi kwa sababu wao wenyewe ni wahifadhi tayari na tunapowafukuza watapoteza urafiki na wale wanyama, na inawezekana wakawa maadui wa hifadhi badala ya kuwa marafiki wa hifadhi.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu haina haja ya kufukuza fukuza watu wanaoishi karibu na maeneo yaliyohifadhiwa, ina haja kubwa ya kutoa elimu, kuwashirikisha, kuwapa manufaa ya uhifadhi ili waweze kuwa wahifadhi sambamba na wale wa taasisi zinazohusika, hatuna uhaba wa maeneo. Naomba ninukuu kwamba kulingana na taarifa zilizopo za Wizara ya Maliasili na Utalii, Tanzania inasemekana imehifadhi asilimia 30 ya ardhi yake. Hata hivyo ukienda katika uhakiki wa kina zaidi, ni zaidi, *almost* asilimia 40.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, *TANAPA* wana hifadhi 40 zinazochukua asilimia nne za ardhi ya Tanzania. Ardhi mseto kama ile ya *NCAA* inachukua asilimia moja. Mapori ya akiba ambayo ziko 28 zinachukua asilimia 13, akiba ya misitu ambayo iko 570 inachukua asilimia 12, mapori tengefu ambayo yapo 44 yanachukua asilimia nane na hifadhi za bahari ambazo ziko nane zinachukua asilimia mbili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuna iddadi ya maeneo yaliyohifadhiwa 657 ambayo ni sawa na asilimia 40 ya eneo lote la ardhi ya nchi ya Tanzania. Sasa kama tuna hifadhi zote hizi ambazo nchi nyingi za Afrika hazina, kuna haja gani ya kujenga uadui na wananchi wanaoishi karibu na maeneo yaliyohifadhiwa kwa kuwafukuza fukuza na kuwabughudhi? Hakuna haja! (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna suala lingine ambalo naomba nishauri Serikali. Kuna hili suala la jinsi tunavyoweka *enforcement* ya kuzuia mifugo isiingie katika maeneo yaliyohifadhiwa. Ni kweli yanahitaji kuhifadhiwa na mifugo inaweza ikaharibu ile ardhi lakini hiyo *modality* ya kuwapiga *fine* na kuwakamatia ng'ombe ina kasoro kubwa sana na itazidisha uaduzi miongoni mwa jamii ambayo siku

zote wameishi kwa urafiki na wanyapori. Ninaomba na ninaishauri Serikali, wale ng'ombe wote ambao walishashikwa, kesi zikaendeshwa na zikamalizika, ng'ombe waachiwe mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili ninaomba Serikali ifikirie kuondoa hili suala la kupiga watu *fine* ya pesa kwa sababu kwanza imeleta mazingira mabaya sana ya ufisadi. Wale watekelezaji wa hizi sheria kule chini wengine wamekuwa mamillionea kwa sababu ya hili zoezi. Ninaomba ule utaratibu sasa utumike kwamba hawaruhusiwi kupokea pesa, hawaruhusiwi kutoza faini, ikiwezekana ng'ombe wanapokamatwa kwa sababu wameingia pale, utaratibu tu ufanyike wa kuwa-*identify* kwamba ni wa nani na wakaandikishwe na mwenye ng'ombe awajibishwe kulingana na sheria zilizopo. (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Dkt. Kiruswa.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja na ninaomba baadaye nipate maelezo kwamba ni kwanini *WMA* ya *Lake Natron* haijasajiliwa mpaka leo na wakati mchakato wote ulishamalizika, niko tayari kushika shilingi kama Waziri hataniambia kwa nini *WMA* ya *Lake Natron* haijapatikana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Sasa nawaomba wanaofuata wote tutumie dakika tano tano ili wengi tuweze kupata nafasi. Tutaanza na Mheshimiwa Nape Nnauye, watafuata Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Risala Kabongo na Mheshimiwa Zitto Kabwe.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie. Kama Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii nichukue nafasi hii kwa niaba ya Kamati kuwashukuru Waziri na Naibu

Waziri na Katibu Mkuu wake pamoja na watendaji wa taasisi zilizo chini ya Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa ambao walitupa wakati wa kutekeleza kazi zetu kama Kamati. Kwa kweli wametupa ushirikiano mkubwa, kwa hiyo, nimshukuru sana Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na watendaji chini ya Wizara hii kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Spika, nilisema nichangie jambo moja hapa kubwa. Wakati tunakamilisha Taarifa ya Kamati, tarehe 25 Aprili, 2018 *Tanzania Forest Services* walitangaza *tenderya* kukata miti kwenye Pori la Akiba la Hifadhi la Selous. *Tender* hii inahusisha ukataji wa miti zaidi ya *cubic meter* 3,495,362, na *point* fulani. Maelezo, ukisikiliza tafsiri ya idadi ya miti itakayokatwa wanasema ni karibia ukubwa wa Mkoa mzima wa Dar es Salaam na zaidi yake na wapo wengine wanasema ni ukubwa wa Unguja nzima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa eneo hili ni kubwa sana kukatwa ndani ya Hifadhi ya Taifa ambayo inaliletea heshima nchi yetu hifadhi hii, ni kubwa sana kiasi kwamba imenishtua sana.

Mheshimiwa Spika, lakini itakumbukwa Bunge hili lilitunga sheria mwaka 2004, Sheria Na. 20 ya mwaka 2004 ya Usimamizi wa Mazingira. Katika sheria ile sehemu ya saba ya sheria ile inazungumza tathmini ya mazingira kimkakati. Naomba niinukuu, inasema hivi:-

"Iwapo rasilimali ya madini au mafuta itagundulika kabla ya mpango wowote au kabla ya kuwa na mpango wa kujenga kituo cha nishati ya umeme wa maji haujafanyika Waziri mwenye dhamana ya masuala ya madini, nishati au maji atafanya tathmini ya mazingira ya kimkakati." (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunavyoongea, tathmini hii haijakamilika, tathmini hii bado inaendelea, *TFS* wametangaza *tender* ya kukata miti hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya sheria hii inasema hivi:-

"Tathmini ya mazingira kimkakati iliyotajwa chini ya kifungu cha kwanza itatathmini eneo lilitengwa kwa ajili ya shughuli husika pamoja na mambo yafuatayo; la kwanza; hali halisi ya mazingira na ya maliasili, utambuzi wa maeneo nyeti kiikolojia yanayolindwa, utambuzi na maelezo kuhusu jamii zinazolizunguka eneo husika, hali halisi ya kiuchumi, ya jamii iliyopo, shughuli za kiuchumi na miundombinu..."

Mheshimiwa Spika, na yako mengine muda hautoshi kusoma. (*Makofii*)

Sasa nataka nimuombe AG aisaidie Serikali kujenga utamaduni wa kuheshimu sheria zilizopitishwa na Bunge. Kwa unyenyekevu sana, Serikali naiomba isitishe zoezi hili, isubiri tathmini ya kimkakati ya mazingira ikamilike. Hifadhi hii ya Selous inahusisha mikoa mitano, Morogoro, Pwani, Lindi, Mtwara na Ruvuma. Haiwezekani tukapuuza maisha ya watu, wanyama, mimea na viumbwe mbalimbali katika mikoa mitano ya nchi, tunaamua kwenda kukata miti yote hii; napata taabu, inaingiaje akilini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi nilidhani tungesubiri tathmini hii ikafanyika, ikija hata kama tunataka kuendelea na mradi, tathmini itatuambia wapi tukanyage, wapi tusikanyage, tutaokoa maisha ya watu hawa. Maisha ya kwetu sisi kule baada ya gesi kuyumba ni korosho, ufuta, mbaazi na mazao mengine. Sheria hii...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Nape, dakika tano zimeisha. Nashukuru sana. (*Makofii*)

Huyu Mkurugenzi wa Misitu yeye anaingia mpaka kwa wenzake wa TAWA sijui kwa utaratibu gani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Lucy Owenya, atafuatiwa na Mheshimiwa Risala Kabongo halafu Mheshimiwa Zitto, dakika tano tano.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Spika, ahsante nashukuru. Utalii unachangia asilimia 17.5 kwenye Pato la Taifa, lakini utalii ungeweza kuchangia zaidi kama tungeweza kuwekeza katika kuiwezesha *TTB* iweze kutangaza utalii zaidi.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha *TTB* inapewa *2.4 billion* kwa ajili ya matangazo, watatangaza nini? Kutangaza *CNN* tangazo moja tu ni shilingi bilioni 1.2, wakienda kwenye maonesho/*exhibition*, mfano wameenda Ujerumanii *ITD, pavillion* moja ni zaidi ya shilingi milioni mia nne, sasa watatangazaje utalii wa Tanzania?

Mheshimiwa Spika, uki-*compare* na nchi za jirani, mfano nchi kama Kenya, imetenga shilingi bilioni ishirini na sita kwa ajili ya *Kenya Tourist Board, South Africa* imetenga shilingi bilioni 60, Namibia wametenga shilingi bilion 20, Uganda yenewe, nchi ndogo kama Uganda imetenga shilingi bilioni nane kwa ajili ya kutangaza utalii. Sasa hapa kwetu tutautangazaje utalii bila kuiwezesha *TTB*?... (*Makof*)

SPIKA: Sisi tumetenga ngapi?

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Spika, *2.8 billion only!*

Mheshimiwa Spika, tunazungumzia watalii kuwa wengi, Mheshimiwa Waziri amesema watalii wa Tanzania wamefika *1.3 million* ambao wamekuja kitembelea Tanzania. Lakini, Kenya pamoja na matatizo na waliiondoa VAT lakini watalii wa Kenya wamekuwa ni wengi kuliko Tanzania, walikuwa milioni milioni na laki nne.

Mheshimiwa Spika, sasa kama ni mambo yale unayosema ya *VAT haiku-affect* Tanzania naomba mkakae mfanye tathmini upya, muangalie kweli kama *VAT haiku-affect* utalii wa Tanzania kwa sababu ile *VAT* iliyoongezeka ukiangalia zile fedha za mwaka juzi hiyo *piece* iliyoongezeka ni ile *VAT 18%* iliyoongezeka, kwa hiyo mapato hayajaongezeka. Kwa hiyo, naomba miltathmini upya suala zima la *VAT* katika utalii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kingine kwenye masuala ya wafanyabiashara wa utalii ni hizi tozo, mlolongo wa tozo. Unakwenda kwenye ofisi ya mtu unakuta imepambwa na *certificate* nyingi tu, wafanyabiashara hawakatai kulipa kodi lakini tunaomba mfanye basi iwe dirisha moja, maana *time is money* huwezi kumchukua mfanyabiashara anatoka ofisi hii anaenda ofisi hii, mnampotezea muda. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ikiwa ni kwenye dirisha moja, watalipa hizo kodi. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri tunaomba sana mfanye iwe ni kwenye dirisha moja na wafanyabiashara watalipa hizo tozo kwenye dirisha moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna kitu nimekuwa nikizungumzia hapa mara nyngi kuhusu *volunteers*. Kuna hawa wanafunzi wanatoka nje, *they are just 16/14 years old*, wanakuja wazazi wao wanakusanya pesa kule kwenye nchi za nje wanakuja wanafanya *community work*, wanajenga mashule, wanajenga madarasa, mabwalo na kila kitu. Kazi ya hawa wanafunzi wanakuja kama wiki mbili, wanakuja wanapiga rangi, wanajenga madarasa lakini wanatumia mafundi watanzania wao wanataka tu ile *adventure*. Lakini unakuta Serikali naomba na Wizara ya Mambo ya Ndani mnawa-*charge* dola 500 za kufanya kazi pamoja na dola 50 za *tourist visa*, lakini wale watoto hawafanyi kazi wakija Tanzania wanafanya hiyo *community work* kwa siku saba lakini wanaenda kupanda Mlima Kilimanjaro, wanaenda Ngorongoro wanaenda Serengeti mpaka Zanzibar. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa hii, kazi hiyo wanaofanya ni *part of tourism* sasa badala ya kuwa-*encourage* kwamba waendelee na hiyo *part of tourism* ambayo tumeianzisha, sasa mnawafanya wanaacha wengine wamehamia Mombasa kwa sasa hivi. Kwa hiyo, Mombasa wamewapokea na wanafanya hizo *community work* kule, kule Moshi wamejenga shule nyngi tu lakini sasa hivi wame-*cancel* zile *booking* wanaenda Mombasa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba uliangalie hilo ili muweze kuwafanya hawa wafanyakazi warudi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipoongelea Mlima Kilimanjaro kila siku tunaonga hapa kuhusu Mlima Kilimanjaro. Mlima Kilimanjaro unaiingizia mapato Serikali mapato mengi sana, lakini bado tumeshauri mara nydingi ili kulinda mazingira kwa kuanzia tu, tunaomba ile njia ya *Machame route* mjenje mahema kwa ajili ya kulia *mess tents*, nataka nijue pamoja na vile vyoo kutoka Ujerumani vilikuwa vya majoribio *chemical toilets* vimefikia wapi.

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Lucy Owenya. Mheshimiwa Lucy Owenya ni Mdau katika maeneo hayo ya Utalii hasa kwenye Mlima Kilimanjaro. Mheshimiwa Risala Kabongo kwa dakika tano.

MHE. RISALA S. KABONGO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa dakika tano hizi ningependa kujikita kwenye makundi matatu yanayotoa huduma katika Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, kuna makundi matatu yanayotoa huduma katika Mlima Kilimanjaro, kuna waongoza watalii, wapagazi na wapishi. Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro ni hifadhi maarufu duniani lakini hifadhi hii ni moja ya maajabu saba ya dunia. Ni hifadhi yenyeye urefu wa mita 5,895. Vilevile hifadhi hii ina wageni wengi wanaotembelea kuliko Watanzania. Nikiangalia nina takwimu hapa mwaka 2013/2014 wageni wa nje walikuwa 35,682 na wa ndani walikuwa 2,021 lakini mwaka 2016/2017 walifika wageni 45,818 na wageni wa ndani walikuwa 2,723 tunaona tofauti ilivyo kubwa.

Mheshimiwa Spika, waongoza watalii, wapishi na wapagazi wamekuwa ndiyo *engine* ya kupandisha wageni katika Mlima Kilimanjaro na wapagazi hawa wanapandisha Mlima kwa mwaka wakiwa na idadi ya zaidi ya 30,000 lakini kwa muda mrefu waongoza watalii hawa wamekuwa

hawapati stahiki zao kama inavyopaswa. Watu hawa wamekuwa wakionekana kwamba hawana elimu wala hawana ujuzi wa kutosha, lakini ndio wanaofanya kazi kubwa sana, wakikosekana basi hakuna mgeni anayeweza kupanda Mlima Kilimanjaro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivyo basi ninaiomba Serikali itambue kuwa waongoza watalii ni kazi ya kitaalamu na ya kitaaluma inayostahili kuheshimiwa, kuthaminiwa ikiwa ni pamoja na kuwawekea mazingira mazuri ya kufanya kazi, pia watambulike kisheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitarejea barua moja hapa ya wakati Mama Shamsa Mwangunga alipokuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, hii ni pamoja na utekelezaji wa changamoto zinazowakabili waongoza watalii, pamoja na wapishi na wapagazi. Ilikuwa ni barua tarehe 15 Desemba, 2015 na tarehe 8 Aprili, 2016. Kulikuwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja ya namna ya kuwalipa wapagazi hawa, wapishi na watembeza watalii ambayo ilikuwa ni ya *GN* Na. 228 ya mwaka 2008. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kikao hicho walishiriki *Tanzania Association of Tour Operators, Kilimanjaro Association of Tour Operators, Kilimanjaro Guard Association, Tanzania Tour Guard Association, Tanzania Porters Organization* na kwa upande wa Serikali walishiriki Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Wizara ya Kazi, Ajira na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro. Kwa masikitiko makubwa kuna zaidi ya makampuni 400 yanayofanya shughuli za kupandisha Mlima Kilimanjaro lakini ni Makampuni 20 yanayowalipa stahiki hawa wapanda mlima, wapagazi na wapishi. Wengi wao wanawalipa shilingi 5,000/shilingi 8,000 mpaka shilingi 10,000 inasikitisha sana. Kwa sababu wapagazi hawa na wapishi na watembeza wageni wanafanya kazi ngumu, wengine wanafia kule mlimani, wengine wana familia, wana majukumu makubwa, hawana makato yoyote yanayowafanya baada ya kumaliza muda wao wa kazi hizi waweze kufaidika na kazi hii lakini bado wanalipwa kipato cha chini sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kingine kikubwa Watumishi hawa kwa kuwa hawapati mikataba kutoka kwa waajiri wao kama *Tour Operators* wanapoteza mapato mengi sana ya Serikali, kwa mfano hizi *withholding tax* hawawezi kulipa kwa sababu hawana mikataba na waajiri wao.

Kwa hiyo, ninaomba Serikali iangalie sana suala hii kwa mfano, Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Wizara ya kazi hawawezi kukwepa kukaa pamoja kuweza kushughulikia tatizo hili. Wamekuwa na kilio cha muda mrefu na hakuna msemaji wameunda vikundi vyao vya kuwasemea, lakini wanapofika kwa mwajiri wanakuwa hawana mtetezi kwenye Wizara ya Kazi, wakati mwingine kwenye mikoa kunakuwa na mwakilishi mmoja tu wa Wizara ya Kazi ambaye anakuwa na mambo mengi hawesi kuwasemea watu hao. Lakini vilevile wamekuwa wakipata mafunzo katika Chuo cha Taifa cha Mweka, kumekuwa na mafunzo ambayo yanatolewa ya muda mfupi wiki tatu wanalipa shilingi 800,000 ili waweze kupata *certificate*. Lakini nilikuwa naiomba Serikali...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Risala.

MHE. RISALA S. KABONGO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

SPIKA: Nakushukuru sana bahati mbaya dakika tano ni chache sana. Mheshimiwa Zitto Kabwe atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Getere na Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 21 wa Hotuba ya Waziri amezungumzia inaanizia ukurasa wa 20 kuhusu usimamizi wa Pori Tengefu la Kilombero na amesema

kwamba kuna miradi kadhaa inaendelea katika pori hili ikiwemo Mradi wa Umeme wa Maji Rufiji (*Rufiji Hydro Power Project*) na nihanukuu Waziri anasema; "Pamoja na umuhimu huo bonde hilo linakabiliwa na changamoto za uvamizi kwa ajili ya shughuli za kibinadamu." Moja ya shughuli ya kibinadamu zinazoendelea kule Mhifadhi Spika Job Ndugai ni pamoja na ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme megawati 2,100. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninapenda niwe *very clear*, hakuna mtu anayepinga nchi yetu kuongeza uwezo wa kuzalisha umeme. Lakini tunataka taratibu za kisheria, taratibu za utunzaji wa mazingira na kuhakikisha ya kwamba nchi haiathiriki kwa ujumla wake kutokana na mradi mmoja tu ambao tayari una mbadala mbalimbali kama jinsi ambavyo tukiwa tukielezwa hapa toka jana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Nape amezungumzia kwamba Selous inategemea watu takribani mikoa mitano na pamoja na kwamba ukikata miti ambayo inakatwa ambayo ni sawasawa na *size* ya Mkoa wa Dar es Salaam; Mkoa wa Dar es Salaam una *square kilometers* 1,360 na miti inayokwenda kukatwa ni *square kilometers* zaidi ya 1,400 kila Mbunge hapa afumbe macho aitazame Dar es Salaam yote, aione namna ambavyo ikiwa haina kitu kabisa jinsi ambavyo itakavyokuwa na mbaya zaidi eneo ambalo miti hii inakwenda kuondolea ndiyo eneo ambalo lina unyevunyevu ambao nyakati ambazo wanyama wanatafuta maji ndiko ambako wanakwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sitaki kuangalia hiyo *angle* ya maisha ya watu, nataka kuangalia *angle* ya uchumi. Kwa mujibu wa mikakati ya nchi tunataka itakapofika mwaka 2025 tuwe na watalii milioni nane kwa mwaka katika nchi yetu wanaoingiza dola za Kimarekani bilioni 16 kwa mwaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, watalii hawa hawatakuwa tena *Northern Circuit*, watalii hawa watakuwa ni *Southern* na *Western Circuit*, ukishaenda ukaiondoa Selous yote

ukaondoa, maana yake ni kwamba huwezi kufikia hii mikakati. Ni namna gani ambayo tunalinganisha mikakati yetu na mipango ambayo tunafanya, hasa ukizingatia tuna-alternative, tuna-alternative ya kuzalisha umeme, tuna-alternative ya bomba la gesi ambayo sasa hivi linatumia asilimia sita tu, na juzi hapa dada yangu Mbarouk amesema tusiite, dada yangu Mheshimiwa Subira alisema gharama ya kuzalisha umeme kwa maji ninafuu kuliko kwa gesi. Lakini ni lazima Serikali ikumbuke *capital injection the investment* unayokwenda kuifanya kwenye huo uzalishaji wa umeme kwa maji ni kubwa mno itakuchukua miaka 30 ku-recover mpaka urudi kuzalisha kwa senti mbili kwa dola kama jinsi ambavyo Serikali inasema. Kulikuwa kuna haja kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba ni kuombe, jambo hili la TFSkwenda kuangusha miti ile na kuuza yale magogo jambo hili lisamame kwa muda mpaka hiyo masuala ya *Environmental Impact Assessment* yatakapokuwa yamekamilika tuweze kuona *mitigation measures* ni zippi. Vinginevyo Serikali iangalie alternative ya uzalishaji wa umeme as upstream na kwenye power master plan ambayo tunayo inaonesha kuna orodha, Mheshimiwa Nassari ameitaja jana ya miradi mbalimbali ambayo imenorodheshwa ambayo itazalisha umeme sawasawa na huo ya *Stiegler's* bila kuiathiri *Stiegler's*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba jambo hili tuweze kilitazama kwa namna hiyo tunakwenda kupoteza maana kabisa ya kukuza utalii katika nchi. Kama tusipokuwa makini na namna ambavyo tunashughulika na suala la *Stiegler's Gorge*.

Mheshimiwa Spika wewe ulivyokuwa mwanafunzi, ulivyokuwa unafanyakazi wanyamapori, umekaa Selous, ulikuwa *game warden* Seloushebu itazame namna ambavyo tutaondoa hii miti na Selous itakavyokuwa imekufa na historia yako itakuwa imekufa kabisa, kwa hiyo lazima tulitazame jambo hili kwa mapana yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni hili ambalo limezungumzwa na Kamati suala zima la vitalu. Nilikuwa namuomba Mheshimiwa tu ndugu yangu Kigwangalla kwa kuwa tumeona kwamba kuna tatizo la kisheria ambalo limetokea na kwamba maagizo ambayo ameyatoa kwa nia njema kabisa, lakini ni maagizo ambayo yametolewa kinyume na Sheria turejee kwenye *status quo* na nilikuwa nakuomba uagize Serikali turejee *status quo* wakati marekebisho mengine yanafanyika ili tusafiri sekta hii. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri ataaeleza mwenyewe lakini ni ukweli *fact* ni kwamba unapojenga bwawa la kuzalisha umeme kama hili litakalojengwa ni lazima eneo lile utakalojenga bwawa litafurika maji, ni lazima uondoe miti yote kwa sababu ukiacha itakuja kuwa ni sehemu ya kuharibu zile *machines* utakazoziweka, yale magogo yataingia kule yatabomoa kila kitu. Kwa hiyo, hiyo ni *international* lazima ufanye. (*Makof*)

Lakini sasa cha ajabu ni huyu Mkurugenzi wa Misitu anaingiaje kule ndio watatueleza baadaye maana *fauna and flora* ya Selous ni ya mtu wa *TAWA*, huwezi kusema kwamba Mkurugenzi wa Misitu ana mti wake pale ile mimea na wanyama wake ni *TAWA*. (*Makof*)

Lakini pia *this is a joke* kwa Mkurugenzi wa Misitu ukishakata miti mingi namna hiyo lazima upate laana tu yaani huwezi kuishi salama, maana nao wale ni viumbwe wa Mungu. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Boniphance Getere atafatiwa na Goodluck Mlinga. (*Makof*)

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza

niwashukuru tu watendaji wa Wizara tukianza na Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii kasoro wale tu wanaodhulumu ng'ombe hao siwezi kuwashukuru hao ambao wanadhulumu ng'ombe.

Mheshimiwa Spika, nalionna jambo moja muhimu sana ambalo unawenza ukalifanya wewe kwa ujasiri wako. Wizara tulipokuja hapa Bunge hili tulikuwa tunataka kushughulikia masuala ya wafugaji na ardhi ya migogoro ya mipaka. Zikawekwa Wizara tano kushughulika matatizo hayo, zimeshindwa, zimeshindwa kushughulika matatizo ya wananchi katika mipaka na mapori. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa nakuomba wewe sasa ama uunde Kamati Maalum ya Bunge kushughulikia migogoro hiyo au ukiona hilo ni gumu utuachie Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii washughulikie hiyo migogoro. Kwa maana sasa watendaji wa Maliasili wanaoshughulika na mapori ya akiba na hifadhi wanachokifanya ni kile ambacho umekizungumza sasa hizi hapa wanakwenda na ramani, hata kama hiyo ramani mipaka yake ya asili ilikuwa Bahi, lakini ramani yao inaonesha wamekuja vizingi *UDOM*, watafika *UDOM* halafu wanamwambia mwanakijiji vizingi vyetu viro hapa kwa hiyo tuamue hapa. Haliwezi kuisha, hauwezi kuachia mgogoro wa mtu aliyeweka mwenye mali halafu aamue mgogoro wake, haiwezekani.

Kwa hiyo, tukubali sasa ile Wizara ya Ardhi na zile Tume zilizounda zimefeli. Sasa ni jukumu lako uunde Tume au uwaambie watu wa Kamati ya Ardhi Maliasili na Utalii waendelee ku-solve hiyo migogoro uwape mamlaka hayo, nilikuwa nafikiri kwamba hilo ni la maana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala la *Stiegler's Gorge* nilikuwa nalionna kwango kwa mawazo yangu, kwa sababu wafadhili hawawezi kujenga ule mradi, kama Serikali yetu ina uwezo wa kujenga huo mradi na wana fedha za kujenga huo Mradi wajenge na kama fedha hizo za mradi huo zitahujumu maeneo mengine ya miradi kwa mfano kwenye kilimo, ardhi,

viwanda kama fedha zetu hazitoshii kujenga *Stiegler's Gorge* kwa maana kwamba tuna mambo mengine yanagusa wananchi tuangalie upya juu ya mradi huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maana yake isije ikawa tukachukua fedha zote kama hatuna ufadhili tukazipeleka kwenye *Stiegler's Gorge* halafu maeneo mengine ya nchi yakaathirika na mradi huo. Lakini kama ni mazingira, mimi mwenyewe nimesoma mazingira, mazingira yapo kwa ajili ya binadamu na binadamu yupo kwa ajili ya mazingira. Habari ya kukata miti milioni ngapi hiyo sawa, lakini miti mingapi tunakata kwenye nchi hii? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuangalie kama tuna fedha ya kujenga hiyo ndo muhimu ili maeneo mengine haya tusije tukamalizia fedha. Kwa sababu wafadhili hawapo tayari kufanya ule mradi, nimeusoma muda mrefu wafadhili wamekuwa wakitukataza mambo mengi tu hata barabara ya Loliondo, hata maeneo ya kujenga viwanja vya ndege hata nini hawajengi viwanja hivyo. Kwa hiyo, suala ni moja tu tukubali tu Wabunge watuambie na Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ituambie ina fedha za kujenga? Je, fedha hizi hazitaathiri maeneo mengine ya uchumi wetu? Basi hilo ndiyo jambo muhimu la kufanya kwenye mambo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nazungumza kwenye maeneo yangu ya Bunda kwamba niwashukuru Wizara wamekuwa wanafanya maendeleo kwenye maeneo yanayozunguka vijiji vinavyozunguka mbuga za wanyama, niwashukuru Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kunijengea Kituo cha Afya Kunyali, wanafanya maendeleo, niwashukuru Wizara kwa kuleta barabara zile za kuvuka vijiji 15 vya kwangu havina uwezo wa kwenda porini kwenye eneo la Serengeti wamesema watafungua barabara ya kutoka Mgeta kwenda kule. Nimshukuru Mtu wa TANAPA, ndugu yangu Kijazi kwa kuona hili kwamba sasa mnaenda kufanya maendeleo kwenye maeneovijiji vinavyozunguka maeneo yanayotuzunguka hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niwashukuru kwa mpango wenu wa kupima vijiji vinavyozunguka maeneo haya ili vipate hati wawze kufanya biashara na mambo mengine na vijiji vyangu 15 mmsema vitakuwemo katika vijiji hivyo Unyali, Mgeta, Maliwanda, Kihumbu na maeneo mengine ambayo amezunguka maeneo haya. Niwashukuru sana kwa mpango huo ambaa mtaufanya kwenye maeneo hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna zile vitu vya *buffer zone*, sasa *buffer zone* nashangaa *buffer zone* za National Park au Hifadhi ya Taifa kwa maana Mapori ya Akiba, TAWA na TANAPA zinakwenda kuweka kwenye maeneo ya vijiji mpaka ambaa siyo wao, wao wanaweka mipaka kwa nini sasa? Kwa nini *buffer zone* isiende kwenye upande wako wewe? Nadhani kwa kuunda hiyo Kamati ambayo tumeisema tutashughulikia matatizo kama haya nadhani yanaenda kuisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla niseme jamani timu ya Wizara ya Maliasili na Utalii imejipanga vizuri. Kigangwalla wanaweza wakakutafsiri kwa maana umekaa kimya upo hivi, lakini una uwezo wa kufanya kazi, Naibu wako anauwezo wa kufanya kazi, Makatibu wana uwezo wa kufanya kazi kwa hiyo tuwashukuru waendelee kufanya kazi. (*Makof*)

(Hapa kengele ililia kushiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Bonipahce Getere ananikumbusha enzi zangu nilipokuwa nafanya kazi kwenye vijiji vyake kule Kihumbu, Maliwanda, Isenye kwenywewe hata Mgeta kule, mwenyeji sana mimi maeneo hayo yote ya pembeni ya Serengeti. Sisi tulikuwa tunafanya kazi kwa undugu mkubwa sana na wananchi, sasa hawa wahifadhi wa leo sijui wamekuwaje, yaani leo wana ugomvi na watu, sijui sera hii wameitoa wapi hawa jamaa? Na ilikuwa ni sera yao kuishi vizuri na watu, inabidi waiangalie tena kwenye kabati walikoitupa. (*Kicheko*)

Nilikutaja Mheshimiwa Goodluck Mlinga, tafadhalii.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba niende moja kwa moja Ulanga. Jimbo la Ulanga au Wilaya ya Ulanga kwa ujumla ina kilometra za mraba 11,000 na inakadiriwa kuwa na watu 200,000; lakini asilimia 47 ya eneo hilo ni hifadhi na eneo lililobaki ni milima mikali na mabonde makali na eneo lingine ni madini, kama unavyoijua Ulanga ilivyo, lakini hiyo sio shida. Maeneo ya hifadhi ambayo tumezungukwa, tumezungukwa na *Selous Game Reserve*, Bonde la Mto Kilombero na Hifadhi ya Ilumo na hifadhi ndogo ndogo 14.

Mheshimiwa Spika, shida inakuja kwenye mipaka, upande ambao tumepekana na *Selous Game Reserve* kuna Kata tatu, Ilonga, Ketaketa na Mbuga, lakini kama kawaida ilivyo ya watu wa maliasili wameongeza mipaka kinyemela katika hizi kata tatu. Kuongeza mipaka sio shida, watu hao maeneo ya kijiji watu ambao walikuwa wanalima wakikanya hayo maeneo wanakamatwa na kuachiwa wanatozwa faini ya shilingi 500,000 hadi shilingi 1,000,000.

Mheshimiwa Spika, nilikuja kwa Waziri, Waziri akafanya mawasiliano watu wa Selous wakamthibitishia hilo eneo sio la Selous na wakasema pia, sio eneo la kijiji. Waziri akawauliza mamlaka ya kuwakamata watu na kuwatesa mnayatoa wapi? Wakashindwa kumjibu na Waziri ameniahidi ataenda, ili kutatua mgogoro huu kuangalia nini kilichopo, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, upande mwengine tumepekana na Bonde la Mto Kilombero ambayo ni Kata ya Ilagua, Lupilo, Minepa pamoja na Milola. Mwaka 2012 Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Halmashauri waliweka mipaka, lakini leo hii Wizara wamekuja wanaondoa watu katika yale maeneo ya ile mipaka ambayo iliwekwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali leo tunafanya hivi kwesho tunaamka na hili, hii mpaka lini? Kwa hiyo, naomba Waziri Kigwangalla, najua wewe ni mahiri sana, naomba ulifuatilie hili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, la pili ni *operation* ya tokomeza. *Operation* ya tokomeza iliumiza watu wengi sana katika Jimbo langu la Ulanga, lakini mpaka leo hii kuna watu ambaao walihakikiwa kwa ajili ya kulipwa hawakulipwa, hasa katika Kata ya Iputi nina wananchi wangu sita ambaao mpaka leo hii hawajalipwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jimbo langu la Ulanga kama nilivyosema limebarikiwa kuwa na hifadhi nyingi. Kuna vijiji ambavyo vimefuata taratibu zote kwa ajili ya uvunaji wa mbao, lakini tatizo kubwa Wizara mpaka leo hii hawataki kutupa nyundo. Mkurugenzi wangu leo hii yuko hapa na anasema ikifika Jumatatu kama hamjatupa nyundo nitaita Madiwani wote pamoja na wananchi wangu wa Ulanga tutakaa tutaweka kambi katika Wizara mpaka mtupe hiyo nyundo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la mkaa, nchi yetu, kama tunavyojua maisha yetu ya vijijini sio watu wote wenye uwezo wa kutumia gesi, lakini Wizara wakimkamata mtu ana debe moja la mkaa wanamtoza faini shilingi 500,000. Sasa kama mnaona hawa wauza mikaa wanafaidi si Wizara ya Maliasili nawashauri mchome ninyi mikaa muweke *ma-agent* watu wawe wanaenda kununua huko kwenu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ni suala la utalii, ulitutuma China, tulienda tukaangalia pamoja na fursa za utalii, China wana mnyama mmoja tu anaitwa panda, lakini wanapata mamilioni ya pesa kwa ajili ya huyo mnyama.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tuna wanyama wa kila aina, lakini hatutangazi na nikabaini hata sisi wenyewe ni fursa kwa utalii, tulienda na Mheshimiwa Kanyasu, Mbunge wa Geita, kwa urefu wake Wachina walikuwa wanamshangaa na mimi nikapiga chapuo hapo hapo nikawaambia kuwa huyu ni mfupi Tanzania wako warefu kuliko huyo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maliasili urekodi, kivutio kimojawapo hicho cha utalii. Mheshimiwa Omary Mgumba, atafuatiwa na Mheshimiwa James Millya na Mheshimiwa Susan Kiwanga kwa dakika tano, tano. (*Kicheko*)

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu ambayo iko kwa ajili ya maslahi ya Taifa letu. Tunafahamu kazi moja ya Bunge ni kutunga sheria, pamoja na kazi nyingine, lakini nikuombe ili Bunge lako liingie kwenye historia. Wakati mwingine tusiwe tunatunga sheria tu, wakati mwingine jje sheria tuzifute zile sheria ambazo zinakinzana na maslahi ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu misingi ya sheria iko mitatu, kuna sheria ya katazo, kuna sheria wezeshi, kuna sheria ongozi. Sheria katazo zile sheria zinakataza katakata usifanye jambo hilo, lakini sheria wezeshi ni zile ambazo tunazitunga kwa ajili ya kutuwezesha kupata kitu fulani kwa faida ya watu wetu na sheria ongozi ni zile ambazo tunazitunga kwa ajili ya kutuongoza kutimiza jambo fulani, lakini kwenye kutimiza majambo hayo inawezekana tukakumbana na mambo mengi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo nataka nichangie jambo moja tu kwa sababu sasa hivi Bunge zima pande zote tunakubaliana, kila mtu anakubali kwamba kuna umuhimu mkubwa sana wa mradi mkubwa huu aliouanzisha Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli wa *Stiegler's* kwenda kuutekeleza ili kutatua changamoto za umeme zilizoko nchini kwetu. Tuko kwenye Wizara ya Utalii, tunaambiwa, tuliambiwa miaka mitatu nyuma nchi hii Tanzania kwa vivutio duniani ni ya pili, lakini leo hii sio ya pili ni ya nane. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hizi sio taarifa zangu, ni ya nane, sababu kubwa ni sababu mionganoni mwa huduma zetu ni mbovu, miundombinu ni mibovu, umeme sio wa uhakika, ndege hakuna, mambo mengi ambayo yapo tumeshuka mpaka wa nane kwa kuwa na vivutio vya utalii. Kwa hiyo,

niseme tu nitazungumza hapa kwa sababu, kuna upotoshaji mkubwa sana kama vile huu ukataji miti ambao unaenda kuiharibu Tanzania nzima. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wewe mwenyeji wa Dodoma, hata *UDOM* lilikuwa pori, lakini kwa maslahi ya umma tuliamua tujenge Chuo Kikuu na ndio maana mpaka leo unaona tembo kila ikifika msimu wake wanapita pale ziliikuwa njia za tembo. Hata wale wazee wa zamani wanajua Dar es Salaam iilikuwa pori pia, lakini leo Dar es Salaam imejaaj maghorofa, tumeharibu mazingira. Alisema ndugu yangu Mheshimiwa Getere hapa, kati ya mazingira na binadamu nini ni muhimu? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi naumia sababu Wabunge wa Tanzania tunazozitoa ndio sababu zilezile wakoloni wetu walizitumia kutukwamisha kutengeneza miradi hii wakati wa Mwalimu Nyerere. Kama kuna Mtanzania anahisi kama walioendelea, nchi zilizoendelea zinafurahia siku moja nayo Tanzania waione imeendelea anajidanganya. Wanatamani sisi tuendelee kuwa hivi hivi maskini na wao waendelee kuwa matajiri. Ndio maana kwenye miradi yote mikubwa inayotaka kutuhakikishia kwenye kuongeza uzalishaji nchini kwetu na kujikwamua kwenye umaskini hawataki kuisikia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, leo ingekuwa mradi ule kutekeleza *condom* ungesikia hela zinamiminika. Ingekuwa suala la vyandarua vya mbu hela zinamiminika, lakini mradi ule tunakwenda kuzalisha umeme zaidi ya megawati 2,100 ni umeme mwingi tutaupata ndani ya miaka mitatu ambayo tuna miaka 57 ya uhuru mpaka leo nchi hii tuna megawati 1,400 tu, leo mtu anakuja kukejeli pale, nashangaa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nashauri somo la uzalendo lianze kuanzishwa haraka sana kuanzia chekechea ili watu waijue nchi yao, waweze kuitetea nchi yao, pale tunapokandamizwa. Hivi kuna uharibifu unaofanywa kama mataifa yaliyoendelea? Iraql iili kuwa vile? Ule uharibifu

uliofanyika Iraq, Libya, unafanana na uharibifu ule wa pale?
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Asante sana.
(Makofi)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Mgumba. Nikwambie neno moja tu, ukitaka kujenga *hydroelectric power plant* popote pale duniani, jiandae sana kutetea mradi wako kwa sababu yaani upinzani *is natural.* *(Makofi)*

Mheshimiwa James Millya na Mheshimiwa Susan Kiwanga.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Ninyi mnatandikwa halafu mnashangilia, hamjamuelewa Spika?

MHE. JAMES K. MILLYA: Mheshimiwa Spika, hili la *Stieglers' Gorge* halihitaji wala akili nyingi, ukifananisha eneo la *UDOM* na Dar es Salaam kwamba kulikuwa na wanyama pori na kwenyewe na hili eneo la *Stieglers' Gorge* ambalo ni Selous, haihitaji kusoma hata kidogo kujua kwamba kule hakuna wanyamapor. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini wafugaji wa nchi hii kwa muda mrefu wameonewa sana. Mwaka 1968 Mwalimu Nyerere alipokuwa Rais wa nchi yetu, alipotembelea eneo la Indumiet kule Longido, ambayo kwa sasa ni Siha aliwaambia Serikali kwamba wafugaji watengewe ekari 5,500 kwa ajili ya kufuga, mwaka 1968. Mwaka 1973 Bunge hili likatunga sheria na kuiagiza Serikali mwezi wa tatu, mwaka 1973 kwamba wafugaji wapewe eneo hilo. Serikali kupitia *GN Na. 59* mwaka huohuo wakatenga ekari 5,500 kwa ajili ya wafugaji, lakini *TANAPA* kwa kukaidi maagizo ya Mheshimiwa Rais Nyerere, Marehemu, Baba wa Taifa, waliwanyang'anya wananchi wale ile ardhi wakairudisha *Kilimanjaro National Park.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mwaka 1998 Mahakama ya Rufani chini ya aliyekuwa Jaji Mkuu Nyalali iliagiza Serikali ya

Tanzania kuwapatia wafugaji wa Mkomazi eneo lingine mbadala la kufugia. Mpaka leo miaka 20 tayari kamili wafugaji wale wanahangaika wako pale juu, wanahangaika hawana eneo la kufugia.

Mheshimiwa Spika, lakini kama haitoshi, juzi mwezi Februari, 2018 Mheshimiwa Kigwangalla alienda Wilayani Simanjiro, Kijiji cha Kimotorop, najua unafahamu kwa sababu, ulitembelea muda mrefu sana, Kijiji cha Kimotorop. Amekuta vizingi wanyama pori wamepiga kuanzia pale zahanati, shule ya msingi na kuchukua kaya 3,000 akatoa tamko kama Waziri kwamba wafugaji wale wote wafukuzwe na waondoke. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ifike mahali sasa mnajiliza kwa nini Tanzania tunashika nafasi ya 110 duniani kati ya nchi 133 kiutalii, mnajiliza ni kwa nini pamoja na vivutio vikubwa ambavyo tunavyo. Jibu ni dogo, laana na vilio vya wafugaji nchi hii na wananchi wanaolia kwa sababu ya kuonewa kwa muda mrefu sasa. Ifike mahali wananchi hawa wasikilizwe, watu wanaumia kwelikweli, naomba Mheshimiwa Waziri wa Ardhi saidiana na Wizara hii maana mliambiwa, Bunge lilitoa tamko la Wizara tano mkae kwa ajili ya kusaidia wananchi, mpaka leo hamjakaa, mmeweke vizingi wenyewe, wananchi waaonewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini lingine, kuna dada yangu kutoka Arusha aliongelea kuhusu Loliondo, mgogoro wa Loliondo miaka 26 leo halina majibu Bunge, Serikali haina majibu, Loliondo wananchi wanaumia sana. Ifike mahali niungane na Mheshimiwa Mbunge aliyesema unda kamati malum kama ambavyo umeunda ia *Tanzanite*, ya madini mengine, ili tusaidie nchi hii kuwanusuru wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pale juu kuna mfugaji mmoja anaitwa Julius Tisho amepoteza ng'ombe 240 ambaو wameswagwa na wahifadhi kwenye Mbuga ya Selous, wakalipia risiti, hizi hapa kwa ajili ya faini, lakini mwisho wa siku pamoja na kulipa risiti hizo ng'ombe wale walipigwa risasi na wahifadhi, *CD* ninayo hapa nitakukabidhi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, najua Wasukuma wameonewa, najua Wagogo wameonewa ambao ni wafugaji, Wamasai wameonewa ambao ni wafugaji, Wabarbaig, lakini wengine na Wakurya, itafika mahali tutaweka tamko na ninyi Chama cha Wafugaji mko hapa ndani, tufike mahali tuseme kwa sababu utalii unaathiri maisha yetu tufike huko Ulaya na Marekani, twendeni China na mahali popote duniani tuwambie kwamba tunawaombeni msije Tanzania kwa sababu mnapokuja Tanzania maisha yetu yanaathirika, tutaweza. Tukaeni pamoja, tuunganishe pamoja na sisi Wabunge tuko tayari kuitangaza Tanzania kwamba utalii huu unaathiri maisha yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, bado hatujafikia hapo, lakini tutafikia mahali fulani tunaumia sana, inauma sana. Naombeni Serikali hii isikie kwa mara ya kwanza. Bahati mbaya kule Lolliondo ambako 2015 ndilo Jimbo pekee Arusha ambalo mmechagua CCM watu wanaumia sana. Wafugaji nchi hii naomba sasa ifike mahali wasikilizwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nashukuru. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Susan Kiwanga atafuatiwa na Mheshimiwa Raphael Chegeni na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu ahsante sana kwa kunipa dakika tano, ili nipate kuchangia. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kwenye hii hotuba ya Waziri wa Maliasili nimeenda kwenye ukurasa wa 62, aya ya 5.4.5.2, kuhusu Idara ya Wanyamapori, akasema kwamba mradi na usimamizi endelevu wa ikolojia ya ardhi oevu ya Bonde la Mto Kilombero na Mto Rufiji.

Sasa nimesimama hapa na kwa kkuumba sana ili kuzungumzia hilo suala kidogo ambapo kwenye kitabu chake ameongea kitu kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri nimealikwa kwenye vikao mbalimbali vyatishati na madini kwenda na wataalam wanaoshughulikia suala la *Stieglers' Gorge* kule Rufiji, kuhusu kutuelimisha namna tutakavyopata umeme. Lakini wakiwa wametujumuisha watu wa Mkoa wa Morogoro, hususan Bonde la Kilombero kwa sababu wanasesma kuna asilimia karibu 60 na zaidi za maji zinategemewa kutoka Kilombero kwenda kwenye lile bwawa la umeme. Pamoja na mpango huo, lakini Wizara hii pamoja na Wizara ya Nishati haizungumzii athari za wananchi zitakazotokana na uwekezaji huo mkubwa ndani ya nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nitiririke sasa moja kwa moja, mradi huu ndani ya Jimbo la Mlimba kuna kata zipatazo nane na vijiji vipatavyo 18 vinaenda kuathirika moja kwa moja na mradi huu, lakini mradi huu hauzungumzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, leo katika hiso kata na hivyo vijiji vipatavyo 18 kuna kilometra 359 inachukuliwa kwenye Kijiji cha Ngombo, chote kinaondolewa kwa ajili ya kutunza maji ili yaende Rufiji, Kata za Mlimba hiso. Katika Kata ya Mofu, Kijiji cha Idandu wanachukua ekari moja na Mwawala Kata wanachukua kilometra moja, Kata ya Idete wanachukua kilometra tatu Kijiji cha Miwangani, Kata ya Mofu wanachukua Kijiji cha Miomboni kilometra 13, Kata ya Kalenga Kijiji cha Mofu wanachukua kilometra 23, Kata ya Mofu wanachukua kilometra 31, Kata ya Ikwambi, Kijiji cha Ikwambi wanachukua kilometra moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Kata ya Mchombe, Kijiji cha Lukolongo wanachukua kilometra mbili, Kata ya Mngeta wanachukua kilometra moja, Kata ya Chita, Chita JKT, wanachukua kilometra 74, Kata ya Melela wanachukua kilometra 27, Kata ya Kalenga Kero wanachukua kilometra 19, Kata ya Ching'anda Kijiji cha Udagaji wanachukua kilometra 37, Kata ya Chisano wanachukua kilometra sita, jumla ni Jimbo la Mlimba, ni kilometra 37. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kule wanakochukua huko ndio tunakotegemea kulima, ndio tunakotegemea wafugaji

wameingia wengi, wanafuga huko, tutakwenda wapi? Hawatuambii hawa watu wanakwenda wapi? Hiyo ni hatari ndani ya Jimbo la Mlimba, ni maumivu makubwa. Mradi huu hauzungumzii chochote kuhusu athari ya maeneo haya, hawa watu takribani karibuni 30,000 wanakwenda wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba majibu ya Serikali, hiyo ni hatari, eti kwa sababu tu kwa *Stieglers' Gorge*, jamani hata mradi mzuri angalieni athari za wananchi wanazopata. Hiyo nimesema Jimbo moja tu, kuna Jimbo la Kilombero lenyewe, kuna Jimbo la Ulanga na Jimbo la Malinyi kote wanaenda kuathirika, si kazi yangu kusemea, watasema Wabunge wao.

Mheshimiwa Spika, hiyo ni hatari. Watuambie Serikali sisi wanatupeleka wapi? Wafugaji wamejaa kule mnawapeleka wapi? Wakulima watalima wapi? Tutaishi viyi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hakuna mbinu mbadala ya kutusaidia sisi, naongea hivi kwa machungu makubwa, yaani sipati jibu, hali ni hatari, sijui tutaenda wapi sisi wananchi wa Mlimba? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siwezi kusema sana kwa sababu moyoni naumia sana pamoja mnacheka lakini sisi tunaenda kuathirika na sisi ni Watanzania hatuna barabara, umeme wenyewe hatuna, maji hatuna, hivi mnatufanyia nini sisi, tumewakosea nini nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hali ni mbaya ndani ya Jimbo la Mlimba, Serikali hebu hamieni kule mkaone watu wanavyoenda kuathirika na huo mradi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Asante sana Mheshimiwa Susan Kiwanga. Nilishakutaja Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab tano, tano dakika.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi niweze kuchangia katika hoja hii. Kwanza napenda niunge mkono hoja hii na nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kuandaa bajeti ambayo ni nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kupanga ni kuchagua Watanzania tumefika mahali tukipanga hiki tunalalamika tunasema kibaya, tukianza hiki tunasema hiki ni kibaya, lakini yote Watanzania tufike mahali tunapopanga tuchague wenyewe. Siamini leo hii kwa Tanzania hii tuweze kulalamika sana. Ukichukua mfano kama Tanzania uki-comprena Kenya Uganda nchi zinazotuzunguka hapa hivi. Ni nchi gani ambayo ina rasilimali nydingi na kila neema kama Tanzania. Lakini tuko nyuma kwa sababu tukipanga kitu tunaanza kupinga tena tunakataa. Unataka uchumi wa viwanda unasema hutaki *stiegler's Gorge*, tunataka umeme sijui wa aina gani na kadhalika. Tunakwenda wapi? Tunatoka wapi? Kama nchi lazima tuwe *national agenda* ya pamoja lakini tunakuja hapa tunaanza kuchukua mawazo ambayo hayatusaidii kama nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimesikiliza mijadala yote hapa lakini nasema Watanzania lazima tubadilike kama tunapenda nchi hii lazima tukubali na kwenye mabadiliko lazima wengine waumie. Huwezi kuwa na mabadiliko katika nchi yoyote ile watu wasiumie haiwezekani. Nchi zote ambazo zimeendela watu waliumia sana, sana. Naomba Watanzania na hasa Wabunge sisi Wabunge humu ndani tusiwe ndumila kuwili. Kama tumekubali ajenda ya uchumi wa viwanda twende nayo tutoke nayo. Mnataka baada ya miaka mitano au kumi tufeli tuanze na ajenda gani nydingine tena. *Let be serious.* (*Makofii*)

TAARIFA

SPIKA: Mheshimiwa Msongosi nilikuona.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, nataka tu nimpe taarifa mzungumzaji anayezungumza sasa

kwamba eneo la Selous ni kubwa sana, *square meter* zake za mraba ni *square meter* 54,600, eneo ambalo limetengwa kwa ajili ya mradi huu ni *square meter* 1,400 tu. Kwa hiyo ni vizuri Serikali yetu kama Wabunge tukasimama tukatetea huu mradi ili uweze kujengwa. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Taarifa hiyo Mheshimiwa Chegeni unapewa endelea dakika zako zinamalizika.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Spika, amelenga penyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee, kama tunataka utalii katika nchi hii lazima Bodi ya Utalii tuiwezeshe. Haiwezekani tukawa tunaongea ngonjera, utalii, utalii bila kuwezesha Bodi ya Utalii haiwezekani. Lazima kuwe na *synergy* ya mambo ambayo yanafanyika kama Taifa. Ningombaa sana kwa sababu ya muda sijui nitaongeaje sasa hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo tunataka utalii huu uchochee uchumi wa nchi hii, lakini pamoja na haya lazima tuangalie kuna vitu ambavyo naomba sana Mheshimiwa Waziri uangalie sana hili. Nchi yoyote katika uchumi uweze kuwa *vibrant* lazima kuwe na biashara zinazofanyika. Watalii waingie hapa kwa gharama ndogo lakini wanakuja ku-*spendzaidi* hapa wanaingiza uchumi wetu hapa hivi.

Leo hii ukienda Dar es Salaam kwa mfano mahotelii yako tupu, ukienda Mwanza mahotelii yako tupu, ukienda Arusha mahotelii yako tupu. Sasa unasema watalii wanaongezeka, tunajiuliza swali kubwa sana kwamba tunafanyajae. Tuwe na mkakati wa Taifa tuondoe gharama ambazo zinakwaza watalii wasiingie hapa, tuchochewe ili watalii waweze kuingia na tuitangaze nchi yetu kwa urahisi zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia gharama za mtu kuingia hapa nchini na kufanya kazi ni kubwa mno, dola

3050 ni hela nyingi sana za Kimarekani kama milioni saba za Tanzania. Hivi kweli biashara gani zinaweza ku-support mambo kama haya. Naomba mambo kama haya Waziri wa Fedha na wadau wengine wote tuongee kama nchi. Tusiongee kama mtu au kama Wizara kwa Wizara *in isolation* tufanye kazi kwa mtiririko ambao unaunganisha mambo. Lengo la nchi hii bila kuwa na uchumi hatuwezi kusonga mbele, bila kuwa na mapato ya kutosha hatuwezi kusonga mbele na bila utalii ambao ndiyo moja ya kigezo cha kutengeneza mapato katika nchi hii kuongezeka hatuwezi kupata mapato ya kutosha. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Raphael Chegeni. Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab tafadhalii kwa dakika tano, utafuatiwa na Mheshimiwa Gibson Ole Meiseyeki.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii kuchangia hoja hii ya Maliasili na Utalii ambayo ni muhimu sana. Kwa sababu ya muda nitakwenda moja kwa moja kwa utalii na vivutio vya utalii ambavyo viko jimboni kwangu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwanza Mawaziri wote Mheshimiwa Waziri na Naibu wake wameweza kuja katika Jimbo la Muheza na kuweza kuona vivutio vya utalii ambavyo viko maeneo ya Amani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kule Amani kama walivyoona ni kwamba kuna mambo mengi sana ya vivutio vya utalii, acha pamoja na mambo ya kuwa na miti mirefu hapa duniani, pamoja na kuwa na majoka makubwa hapa duniani na mambo mengine mengi, lakini kitu kimoja ambacho Mawaziri hawa wameweza kukiona kule ni namna ya wananchi wa Fanusi maeneo ya Amani ambapo wanachuma/wanavuna vipepeo. Vipepeo ambavyo vinawaletea hela nyingi na kukuza uchumi sio Muheza tu na hata Mkoa mzima wa Tanga. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sasa tatizo ambalo lilitokea kwenye uvunaji wa hawa vipepeo ni kwamba waliingia kwenye kundi la kuzuiwa kusafirisha vipepeo hivi nje ya nchi. Ni kwamba Serikali ilipiga marufuku kusafirisha wanyama pori hai nje ya nchi basi wakachukua na vipepeo. Lakini sidhani kama lengo la Serikali lilikuwa ni kuzuia vipepeo hawa kuzuia vipepeo hawa kusafirisha nje ya nchi. Naamini kabisa Serikali ilikuwa na nia ya kuzuia wanyama wakubwa faru na wanyama wengine kwenda nchi za nje, lakini sio vipepeo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wote wawili mliahidi mtalishughulikia suala hili, lakini siku zinavyozidi kwenda na wale wavunaji na wenyewe wanakata tamaa. Naomba suala hili Mheshimiwa Waziri utakapokuja ku-*wind up* jioni ultolee maelekezo kwa sababu ni suala muhimo sana katika maendelezo ya uchumi pale Muheza, kwa sababu linaingiza fedha nyingi sana na pia uliahidi kuboresha yale maeneo kuwaboreshea wale wavunaji yale maeneo bado suala hilo bado Wakala wa Misitu hajalishughulika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo ni mgogoro wa muda mrefu pale Derema. Kuna wakulima ambao walikuwa kwenye hifadhi karibu 1,028 mgogoro huu ni wa muda mrefu tangu miaka kumi umeukuta na wote mlipokuja mliwaona wale wananchi walivyokuwa wanalamika. Sasa hivi Muheza tumeanza kuwagawia viwanja kuwatoa pale wameshaondoka lakini tunawagaia viwanja eneo la Kibaranga ili waweze kuondoka vizuri. Lakini kuna fidia ambazo mapungufu ambayo wanadai na ni muda mrefu sana, sasa naomba suala hili pia Mheshimiwa Waziri utakapokuja ku-*wind up* jioni naomba ulishughulikie ili ulilezee/ultolee tamko kwa sababu hata wiki iliyopita tu walikuwa hapa Dodoma hawakupata nafasi tu ya kuwaona. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ni suala la tiki, sisi tunalima tiki, tunalima tiki katika Afrika tunaongoza, tiki yetu iliyoko pale ni *the best in Africa*. Sasa suala hili Serikali inaelewa

kabisa, kulikuwa na mpango ambao ulikuwepo ambao wakulima wa tiki ilikuwa inagaiwa kwenye vitalu. Sasa vitalu ilikuwa inawawezesha wafanyabiashara ya Muheza au kutoka nje kununua vile vitalu na kuweka viwanda pale Muheza. Sasa baadae mmeanzisha mtindo wa mnada, mnada ambao anakuja tajiri mmoja ananunua vitalu vyote kiasi kwamba ilisababisha viwanda karibu 10/12 vyote vya wilaya ya Muheza kufungwa.

Sasa mlipokuja mliwaona na Mheshimiwa Waziri uliahidi kabisa kwamba suala hilo unalirekebisha na wananchi wa Muheza watafaidika sasa kuanza kununua vile vitalu. Naomba hiyo ahadi yako itekelezwe ili tuweze kuweka viwanda ambavyo ni viwanda vingi kwa ajili ya uchumi wa Muheza.

Mheshimiwa Spika, na mwisho ni suala la Maafisa Misitu. Maafisa Misitu kupewa madaraka ya kukata au kutoa vibali vya misitu katika hizi Halmashauri. Suala hili limetokea hapa juzi Muheza ambapo Afisa Misitu wa Muheza ameamuru karibu misitu mia na ushee kukatwa. Sasa suala hili ni kubwa sana ambalo Baraza la Madiwani liliamua kabisa kupendekeza hawa watu wasimamishwe kazi.

Sasa ni vizuri hawa Maafisa Misitu ili kuweza ku-*protect* misiti yetu na wenyewe wawe *answerable* moja kwa moja kwa Katibu Mkuu. Kama vile Rais alivyoamuru maafisa/wahandisi wa maji na watu wa ardhi wote waripoti moja kwa moja kwa Waziri Mkuu nafikiri Mheshimiwa Rais amesahau hii kitengo cha misitu na wao waende moja kwa moja wawajibike ili waweze kushughulikiwa kwa haraka pale panapotokea matatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa sababu muda ni mdogo ningombaa kuunga mkono hoja na nakushukuru sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab. Mheshimiwa Gibson Ole Meiseyeki atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mchafu.

MHE. GIBSON B. MEISEYEKI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, labda ni-*declare interest* kwamba ni mfanyabiashara wa utalii takribani miaka 20 sasa.

Mheshimiwa Spika, sitatofautiana na wengi ambao wamenitangulia kwa maeneo mengi niseme wameni-*pre-empt some how*. Lakini niseme idadi ya watalii tunayoipata nchi hii ni ya kusikitisha sana. Ni watalii wachache sana ukilinganisha na uzuri na *natural gift* ambayo tumeijaliwa kama Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema ni wachache kwa sababu kuna nchi kama Thailand ambayo haina kabisa vivutio ambao naweza kusema wana robo tu ya tulichonacho sisi. Wao wanapata watalii milioni 35 kwa mwaka na wanaongezeko la watalii milioni moja na nusu kila mwaka. Sisi ongezeko letu ni tena kwa namba ya kuchakachua maana yake Mheshimiwa Dkt. Chegeni hapa amenigusa mahali. Kila siku tunaambiwa hapa tunaambiwa hapa imeongezeka lakini kiukweli mahotelii yetu yanalala bila wageni. Sasa tunashindwa kuelewa hawa wageni wanaongezeka huwa wanakwenda kulala wapi. Sasa wanaongezeka angalau kwa namba hizi za kuchakachukua 100,000 kwa mwaka. Kwa hiyo, ili tuweze kufika watalii milioni tatu kwa mwaka tunahitaji miaka *at least* 15. Thailand kila mwaka wanaongezeko la watalii milioni moja na nusu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ulinifurahisha sana juzi uliposema kwamba hatuwezi kuwa na Mawaziri ambao wanakaa tu humu bila kwenda nje kujifunza. Basi kama kuna mmoja ambaye anatakiwa ahamie huko ili akajifunze kweli kweli sio kutalii kwenda kujifunza kweli kweli ili tujue kwa nini Thailand wao kwa miaka kumi wameongeza watalii zaidi ya milioni 15. Sisi tunahitaji miaka 15 ili kuongeza watalii milioni moja na nusu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kiukweli tuwapigie chepuo hawa wakajifunze, Thailand wanafanyaje mpaka wapata watalii kiasi hicho. Sisi na uzuri wote huu tumezidi

kulia lia tu na hii nchi tumekuwa wa ajabu sana kila mahali tunalia, kila sekta tunalia, wakulima wanalia, wavuvi wanalia kama watu walivyosema hapa na sisi humu Bungeni tunalia. Sasa mpaka wakati mwingine tunashindwa.

Mheshimiwa Spika tusaidie kama kuna kitu tunaweza kufanya ili hivi vilio vipungue kwenye nchi hii basi tufanyeni kama Wabunge kwa sababu kulia kumezidi. Unda, wamesema watu hapa hizi sekta zote ambazo zinamatatizo ambaao Wabunge wengi tumekubaliana humu ndani ikiwezekana unda tume mbalimbali ili tufanye kazi yetu kama Wabunge tuunde tume mbalimbali kwa kila Idara ambayo tumeona kwamba tumekubaliana humu ndani ili ukafanyike upembuzi yakinifu na tuje hapa na maamuzi ya Kibunge ili kulia lia kuishe humu ndani ya hii nyumba, tunalia tu toka mwaka juzi. Kwenye Wizara hii ya Maliasili kwa miaka mitatu mfululizo tumekuwa tukilia hivi hivi na inaelekea tutaendelea kulia mpaka mwisho wa maisha yetu ni kulia tu humu ndani. Ifike mahali tuchore mstari, maamuzi yafanyike ili tuone kama yanawenza kuleta mabadiliko yoyote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Kigwangalla na wenzake pengine na Wabunge humu ndani iundwe tume tukaifanyie *ovehau/hii* idara ya Utalii ili tuweze kufaidika maanake utalii huu unaweza kutumalizia shida nyingi sana katika Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda nimwombe Mheshimiwa Waziri sasa nilishamwomba Waziri aliyekuweko hapo kabla kwamba mwaka jana mwanzoni mliweza kuwapiga watu wangu watano risasi mkawaua na wengine zaidi ya nane kujeruhwa na mmojawapo ni mtoto ambaye amepata ulemavu wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, watu hawa toka wameuawa baada ya msaada wa mazishi hamjaenda kwenda tena kuwaona wala hakuna kifuta machozi. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri ukawaone watu wale na uwafute machozi ikiwezekana tukio hilo lisirudie tena kwa sababu kwa kweli hali ilikuwa ni tete wakati ule. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache nashukuru sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ole Meiseyeki. Mheshimiwa Hawa Mchafu tufungie pazia.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote nipende kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake wanafanya kazi vizuri sana na nipende kusema Waziri na Naibu wake ni wasikivu na wanyenyekuvu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kukuomba Mheshimiwa Waziri ile *speed* uliyoanza nayo wakati unateuliwa naamini umejipumzisha kidogo mara baada ya kutoka hapa ukaendelee nayo ile ile dhidi ya haya malalamiko yanayotolewa hapa ya askari wako kuuwa watu na kuliza watu, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho nataka kusema tunapozungumzia utalii ni *international business* ni biashara ya kimataifa. Tuna vivutio vingi tunachangamoto ya miundombinu. Niliuliza swali *last week* linalohusiana na urithi wa malikale kule Kilwa Kisiwani hapaendeki hakuna kivuko cha uhakika hakuna miundombinu ya kueleweka. Kwa hiyo, niombe sana hii changamoto ya ufinyu wa bajeti ama huku kupunguzwa kwa bajeti kwa asilimia 22 ni tatizo, tuwaongezee bajeti kwa bahati nzuri tunapozungumzia Wizara ya Maliasili na Utalii kuna mashirika ya kimataifa ambayo *yana-support* wizara hii au sekta hii lakini pia tuiombe Serikali suala zima la miundombinu ya maeneo husika liko kwenye mikono yenu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine nilichotaka kusema kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wake wa tano alisema malengo ya Wizara yanaendeshwa kupitia sheria, kanuni, taratibu na mikakati. Baadhi ya sheria kwenye wizara hii zimepitwa na wakati. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri uangalie namna bora ya kwenda kuzifanyia marekebisho

Sheria ya Malikale lakini pia Sheria ya Masuala mazima ya Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine sambamba na hilo ni kuhusiana na suala zima la Sera. Sera ya utalii ya mwaka 1999, Sera ya Malikale na Sera ya Utamaduni hebu tuziangalie hizi sera tuone kama tunaenda nazo vile ambavyo zilivyoandikwa. Sera zinasema katika kila Mkoa na kila Wilaya tuwe na *cultural centre*, lakini katika uhalisia hivyo vitu havipo. Kwa hiyo tuangalie matakwa ya sera hii kama bado tunaenda nayo na kama yako vinginevyo basi tuende tukazifanye kuzipitia upya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kingine Serikali imehamia Dodoma. Dodoma sasa hizi ni Jiji na hatuna *museum* hapa Dodoma na tutapokea wageni wengi sana kutoka mataifa mbalimbali na wenzetu kati ya vitu ambavyo wanavipendelea mara baada ya kazi ni kujifunza tamaduni mbalimbali ama kujifunza historia ya eneo husika. Kwa hiyo, niishauri Serikali ione umuhimu wa kuanzisha *museum* hapa Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine twende Pwani kidogo, Mheshimiwa Dau jana alizungumza kwa masikitiko ya hali ya juu kuhusiana na viboko wanaouwa watu. Lakini pia kule Kisarawe kuna mamba wanaokula watu. Niombe sana Wizara ya Maliasili na Utalii muende mkavune mamba wale, muende mkavune viboko wale kwa sababu itakuwa ni wazuri kwa masuala ya utalii. Kule waliko Kisarawe Mafidhi na kule waliko Mafia wanababisha madhara makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda naomba tumalizie na maporomoko ya Mto Njombe. Maporomoko ya Mto Njombe...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Hawa.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana, dakika zimeisha, dakika tano ni chache. Waheshimiwa wengi tu mmeikosa nafasi msisikitike ni hali halisi ya mambo ya uendeshaji wa hapa Mezani na kwa kweli wenye *interest* ya kuchangia kwenye Wizara hii waliokuwa wengi sana, kwa hiyo imetupa taabu kidogo.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. LUCY S. MAGERELI: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maelezo mafupi juu ya masuala mawili ambayo ni kero katika utendaji wa watumishi wa Wizara ya Maliasili na Utalii. Moja ni hili la Wizara kuongeza maeneo ya hifadhi kwa kutwaa ardhi ya wananchi bila kufuata utaratibu. Binafsi suala hilli nalliona ni suala la kiuonevu sana kwa wananchi wa vijijini. Inasikitisha sana kuona sasa wanyamapori wanapewa kipaumbele na thamani kubwa kuliko wanadamu/raia wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, ni mahusiano mabaya baina ya wahifadhi, wananchi na wafugaji wanaoishi jirani na mbuga. Sote ni mashahidi kuwa hali ya malisho ya mifugo ni changamoto kubwa kwa wafugaji wa Tanzania na Wizara ya Mifugo hajafanya jitihada kidhi kusaidia wafugaji kuzalisha malisho ya kutosha.

Suala la askari wanyamapori kukamata, kuswaga na kushikilia mifugo ya wafugaji katika hifadhi, kuwapiga risasi na kuwaua ng'ombe wanaowashikilia ni suala la kifedhuli na dhuluma. Askari wenu hufikia maamuzi hayo ya kukamata ng'ombe kwa misingi ya rushwa kuliko uhalisia. Mifugo ni maisha ya wafugaji. Unaposwaga na kushikilia mifugo ya wafugaji, kuiua na kuitelekeza bila huruma ni kuwalilishi na kuwatia umaskini wafugaji. Naomba Serikali itazame upya mambo haya ili kupunguza kero kwa wananchi na kuboresha mahusiano baina ya uhifadhi na wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Spika, nianze na suala la migogoro isiyokwisha kati ya Hifadhi ya Mikumi na Vijiji vinavyopakana na hifadhi.

Mheshimiwa Spika, jana tu kumetokea mauaji ya vijana wawili katika Kijiji cha Ilakala kilichopo kwenye Kata ya Jimbo la Mikumi. Huu ni muendelezo tu wa mauaji ya watu wetu wengi katika Jimbo la Mikumi. Tunaiomba sana Serikali iweze kuingilia kati na kutoa adhabu kwa wahusika ambaao wanasababisha mahusiano mabaya kati ya hifadhi zetu na Vijiji vinavyopakana na kusababisha migogoro ya muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, tembo wamekuwa kero sana katika Vijiji vya Kilangali, Mhenda, Mululu na kadhalika na kusababisha uharibifu mkubwa sana wa mazao, mali na hata watu kupoteza malsha. Njia hii inayotumiwa na Serikali ya Awamu ya Pili imeshindwa kabisa kwa kiasi kikubwa kusaidia kudhibiti tembo hao. Tunaiomba sana Serikali ianzishe vituo vyenye askari katika maeneo haya muhimu ili waweze kusaidia kudhibiti tembo hawa ambaao wanaleta madhara makubwa sana kwa wananchi wetu.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Spika, vivutio vya utalii visivytambuliwa na hivyo kutangazwa; kuna vivutio vingi sana katika visiwa vya Ukerewe ambavyo vikitambuliwa na kutangazwa vinaweza kuingizia Taifa pesa nyingi sana, miongoni mwa vivutio hivi ni:-

- (a) Jiwe linalocheza Kisiwani Ukara katika Wilaya ya Ukerewe;
- (b) Mapango ya Handebezyo;
- (c) Makazi/Majengo ya Chifu Lukumbuzya; na
- (d) Fukwe za kipekee maeneo ya Rubya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hivyo Wizara ione umuhimu wa kutambua vivutio hivi, kuvijengea mazingira mazuri na kuvitangaza ili viweze kuliingizia Taifa mapato.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa

Maliasili kwa juhudini kubwa ambazo Wizara yako imezichukua katika kuhakikisha kuwa tembo wa nchi hii wanalindwa na kubaki salama. Ombi langu kwako tafadhalini naomba juhudini hizo za kupambana na ujangili zisiendeshwe kwa kukiuka haki za binadamu na dhuluma dhidi ya mali za wananchi kama vile ng'ombe.

Mheshimiwa Spika, nimesikitishwa sana na kitendo cha kuacha hata kulitambua na kutaja mabaki ya mijusi yaliyopo Ujerumani ambayo yalichukuliwa jimboni kwangu. Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 6, 7, 8, 9, 10 na 11 wa kitabu chako, umezungumzia namna ya uendelezaji wa Mali Kale. Mheshimiwa Waziri imekuwaje uache hata kutambua tu kwamba kuna hayo mabaki yalichukuliwa na kupelekwa katika makumbusho ya Mali Kale kule Ujerumani. Kutokana na hali hiyo nimejiuliza maswali matano yafuatayo ambayo nimekosa majibu hivyo naomba majibu kutoka kwako:-

- (a) Je, suala la mijusi huyo haulitambui?
- (b) Serikali imeshindwa kabisa kulipatia muafaka suala hili?
- (c) Serikali haina utashi wa kisiasa kurudisha na kutunza rasilimali hiyo ya kale?
- (d) Majibu ambayo Serikali imekuwa ikiyatoa hapa Bungeni mara kwa mara kuhusu mijusi yote ni ya uongo?
- (e) Serikali haitaki kuliendeleza eneo lile ambalo taarifa zinaonesha kuwa yapo mabaki mengine chini ya ardhi?

Mheshimiwa Spika, kama kuna suala ambalo Serikali ya CCM inaonesha udhaifu mkubwa katika kuliinda rasilimali na maliasili ya nchi zetu ni huku kufeli kwenu kwa kushindwa kurudisha nchini mabaki yale, kushindwa kuliendeleza suala lile na au hata namna ambavyo nchi haipati kitu chochote kutokana na mabaki yale ya mijusi. Jambo hili linafedhehesha sana na kukianika Chama cha Mapinduzi kwani ni dhaifu

katika kulinda, kutetea na kuhifadhi rasilimnali na maliasili za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nakuomba basi uutangazie umma wa Tanzania kwamba Serikali imeshindwa kulipigania suala hili. Mnashindwa hata kuchonga barabara inayokwenda katika lile bonde ambalo watalii wamekuwa wakienda mara kwa mara kila mwaka. *Shame to you guys.*

Mheshimiwa Spika, kutokana na longo longo ya Serikali katika jambo hili, wananchi wa Mchingga tunaona ni dhana ile ile ya vitendo vya makusudi ya Serikali kudharau, kutothamini na kutojali vitu vya thamani vilivyopo Kusini hususan Mkoa wa Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, ninaandika haya kwa uchungu mkubwa nikliwiwa na namna ambavyo Serikali inaacha kutumia mali kale hii katika ku-promote eneo husika, kukosa pesa za kigeni lakini pia kushindwa kujivunia rasilimali hii muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Ahsante.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukrani zangu kwa Serikali kwa kusaidia kukarabati miundombinu ya maji katika Jimbo la Same Mashariki, Kata ya Maore ambapo wanyama pori waliharibu miundombinu ya maji. *TANAPA* walitoa fedha kwa hiyo tatizo hili limetatuliwa.

Pili, pia nitoe shukrani zangu kwa *TANAPA* kwa ushirikiano mzuri walio nao kwa wakazi wanaopakana na Hifadhi ya Mkomazi. Baada ya kusema hayo naomba nitoe changamoto zinazowakabili wananchi waishio karibu na hifadhi hii ya Mkomazi, nazo ni hizi:-

(i) Kutokana na kwamba Hifadhi ya Mkomazi haina maji ya kutosheleza kwa ajili ya hawa wanyamapori, wanyama hawa bado wanatoka kwenye hifadhi na kwenda kufuata maji kwa wanavijiji. Kwa maana hiyo miundombinu hiyo iliyokarabatiwa hivi karibuni iko hatarini kuharibiwa tena.

Mheshimiwa Spika, kwamba *TANAPA* watenge fedha ili wachukue maji ya mtiririko (*gravity water*) kutoka chanzo cha Mto Hingilili amba una maji mengi na hayajawahi kukauka tangu kuumbwa kwa dunia hii, chanzo hiki cha Mto Hingilili alisha kwenda kukiona Mkurugenzi Mkuu wa *TANAPA Mr. Kijazi* na kuahidi kutenga fedha kwa ajili ya mradi huu.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba Serikali inapoteza fedha nyngi kuchimba mabwawa ambayo baada ya muda mfupi maji yake hukauka na hivyo kusababisha wanyama pori kuvamia makazi ya watu. Wakati wanyamapori hawa wakienda kutafuta maji, huleta madhara makubwa kwa kula mazao ya wakulima pamoja na kujeruhi watu.

Mheshimiwa Spika, kutohana na kwamba mpaka wa Hifadhi hii ya Mkomazi umesogezwa karibu sana na makazi ya watu hasa wafugaji, kumetokea mlgogoro mikubwa katika ya *TANAPA* na wakulima na wafugaji. Tatizo ni kwamba wananchi hawakushirikishwa wakati wa kuweka mipaka. Matokeo yake ni kwamba wananchi wameachwa na ardhi kidogo wakati *TANAPA* wamechukua ardhi kubwa zaidi. Wananchi wanaona Serikali yao inathamini wanyama pori zaidi kuliko inavyothamini binadamu. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Same Mashariki wanaoishi karibu na Hifadhi ya Mkomazi, tunaomba mipaka iangaliwe upya ili wananchi watengewe eneo kubwa la malisho pamoja na eneo la kulima.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba barabara ya Same - Kiswani - Mkomazi ambayo inapita kando kando ya Hifadhi ya Mkomazi, ni mbaya sana kiasi kwamba hata watalii hawawezi kuvutiwa kwenda kuona wanyama kwenye hifadhi hii. Itakumbukwa kwamba faru mweusi kutoka Czech alipelekwa kwenye Hifadhi hii ya Mkomazi. Hivyo basi *TANAPA* wana kila sababu kutafuta namna ya kuongea na Wizara ya Ujenzi ili barabara hii itengenezwe kwa kiwango cha lami ili kuweka mazingira mazuri ya kuvutia watalii kutembelea hifadhi hii. Ni wazi kwamba utalii ni sekta ambayo inaweza kuongeza pato la Taifa kwa kiwango kikubwa sana. Nchi zinazowekeza kwenye utalii uchumi wake ni mkubwa sana.

Hivyo sekta hii ni muhimu sana kwa ukuaji wa uchumi wa Tanzania ili tufikie azma ya kufikia uchumi wa kati, kati ya miaka ya 2025 – 2030. Hifadhi ya Mkomazi ina wanyama wa kila aina wakiwepo tembo, nyati, twiga na kadhalika. Hivyo naamini Wizara hii ya Maliasili na Utalii itaiangalia Hifadhi ya Mkomazi kwa jicho la tatu.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Spika, umiliki wa vitalu vya uwindaji, tamko la Serikali la tarehe 23 Januari, 2017 kuwafutia wamiliki wa vitalu vya kuwindia biashara kutoka miaka mitano hadi miwili kumesababisha biashara hii kuyumba. Biashara ya utalii wa uwindaji huwa inaandaliwa kwa muda mrefu sana na uwekezaji wake ni wa gharama ya juu inayohusu kukarabati miundombinu mbalimbali. Aina hii ya utalii ni ya bei ya juu, sasa ni karibia dola 60,000 mpaka dola 80,000 kwa mtalii kuja kwenye utalii huu. Hivyo watalii wanataka wawe na uhakika wa *deposit* zao watakazotoa. Pamekuwa hakuna utulivu tena katika tasnia hii. Wawekezaji hawana uhakika na biashara zao hadi kupelekea wengine kuvirudisha vitalu hivyo.

Mheshimiwa Spika, ushauri, kama Serikali inataka kuuza kwa mnada hivyo vitalu kwa nini visiuze na vile vilivyo wazi kama jaribio kulikoni kuvuruga wawekezaji ambao tayari wameshatumia fedha nyingi kuendeleza vitalu vyao?

Mheshimiwa Spika, sekta ya utalii inachangia katika pato la Taifa asilimia 17.5 na inaweza kuchangia vizuri zaidi kama tukiweza kuendeleza *Southern Circuit*, utalii wa utamaduni na michezo kwa mfano *Kilimanjaro International Marathon* inakuwa ni kivutio kikubwa sana mbali na riadha, watu wakimaliza kukimbia huenda kupanda Mlima Kilimanjaro na kutembelea mbuga zetu lakini wengi wanarudi zaidi ya mara moja. Lakini safari ya kwenda Selous lakini *tour* ya kwenda huko ni ghali sana, hakuna hoteli za kutosha na zilizopo ni za ghali sana.

Mheshimiwa Spika, katika sekta hii kumekuwepo na tozo nyingi sana takribani tozo 36 tofauti. Wafanyabiashara hawakatai kulipa kodi lakini kwa nini zisiunganishwe zikalipwa sehemu moja ili kuondoa usumbufu hata dakika moja tu ya mfanyabiashara ni fedha. Unakuta ofisi ya mtu (*tours operation*) imezungukwa na leseni nyingi kama mapambo.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi bado Serikali haijaaelekeza ipasavyo katika utalii wa picha, mfano kuna baadhi ya watalii wanataka wafanye utalii wa kupiga picha wakati wakipanda mlima, lakini huu ukiritimba uliopo mpaka apate kibali cha kupiga picha ni shughuli, havitoki kwa wakati mpaka mtalii huwa ana-*conce/safari* yake.

Mheshimiwa Spika, Mlima Kilimanjaro; Serikali kwa kushirikiana na nchi ya Ujerumani walikuwa waweke *clinical toilet* katika njia za kupanda Mlima Machame, *Umbwe route*, Lemosho, Landorosi lakini mpaka leo Serikali haijaweza kuviveka vyoo hivyo. Je, ule mchakato umeishia wapi? Hii inasaidia sana kutunza mazingira (usafi) sababu kule *crater* kunatia aibu ni kuchafu sana.

Suala lingine mara nyingi nimekuwa nikishauri kwa kuanzia ile njia ya Machame *KINAPA* wajenge majiko ya kupikia na sehemu za kulia (*dinning tent*), hii itasaidia sana kuanza tu *uniformity*na kuzuia kila kampuni kuchimba sehemu tofauti kuweka mahali pa kulia na kupikia na hii itavutia sana watalii kwa kuona *park fee* wanazolipa zimetumika kwa kuendeleza *park* hiyo ukizingatia ilikusanywa zaidi ya bilioni 20 hizi ni Mlima Kilimanjaro tu.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kilimanjaro, Jimbo la Moshi Vijijini, Kata ya Mbokomu wenyeji waligundua mti mrefu sana na unakisiwa una ziadi ya miaka 500 mpaka leo sijaona juhudzi zozote za Serikali kwenda kuhifadhi sehemu ile kuweka uzio ili watalii waanze kuutembelea *officially* na Serikali wanapeleka watalii pale anatoza asilimia ngapi kutokana na mti huu?

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, ukuaji na uingiaji wa watalii ulikuwa asilimia 12.9 mwaka 2015/2016; mwaka 2016/2017 mwaka wa kwanza wa Awamu ya Tano kasi imeshuka mpaka asilimia 3.5 tu. Hifadhi ya Ruaha inayopakana na wananchi maeneo ya Mbarali wapo katika wakati mgumu wa kufukuzwa kwenye makazi yao na mpaka sasa hakuna hata waliopata fidia yoyote mpaka sasa hawana cha kufanya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukataji wa miti kilometra za mraba 1,430 sawa na zaidi ya ukubwa mkoaa mzima wa Dar es Salaam huu mradi si wa Watanzania kwa maana ya kuwasaidia. Tunaomba Serikali ichunguze na kuamua kwa faida ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Guanzhuo ni mji wa kibiashara lakini hatuna Balozi Mdogo na timu ya kutangaza bishara hasa watalii kuja nchini kwetu kwani Kenya ina timu inayofanya matangazo ya nchi yao. Hakuna pesa za kutangaza utalii kwa nchi yetu na kutegemea makampuni binafsi ambayo hata wao hawaweki mkazo juu ya utalii huu. Vifaa vya kutendea kazi kwa wafanyakazi mbugani kama magari, tochi, bunduki hata boti sehemu zenye kuhitaji mabomu. Tunaomba Serikali iongeze bidii katika kuwezesha fedha za utendaji.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Rungwe kuna vivutio vingi sana lakini hakuna uwekezaji wa kutosha ili kuvuta watalii maeneo hayo ni Daraja la Mungu, *Lake Ngozi* na Kijungu. Haya maeneo ni ya muhimu sana kwa uchumi wa Wilaya ya Rungwe tunaomba Serikali iwekeze maeneo hayo.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara, Mheshimiwa Waziri kwa utendaji na usimamizi mzuri katika kuhakikisha mali na rasilimali zetu za asili zinatunzwa na pia kukuza na kuinua sekta ya utalii nchini.

Mheshimiwa Spika, ushauri, katika kutekeleza nia njema ya Serikali kwa kuweka Mfuko wa Misitu, huoni vyema Wizara ikafuatilia kwa karibu zaidi juu ya wanufaika wa

mfuko huo kama wanakidhi vigezo husika kwa lengo liliokusudiwa ili kuepuka wajanja kuitumia fursa hiyo na wale walengwa husika kukosa fursa ya kupata (*fund*) hizo kwa lengo la kutekeleza azma ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali iendelee kuelimisha juu ya kulinda na kuhifadhi uoto wa asili. Mali Kale zitunzwe, zifanyiwe ukarabati na zilindwe ili ziweze kubaki kuwa ni urithi wetu wa Taifa kwa lengo la kuhifadhi historia na kuongeza vivutio nya utalii. Kuangalia namna ya kupata nishati mbadala yenye gharama nafuu kwa wananchi ili kuepusha ukataji wa miti kwa madhumuni ya kutengeneza nishati ya kuni na mkaa. Upatikanaji wa miti upewe mkazo wa pekee kunusuru nchi kuwa jangwa. Baada ya kupandwa kuwe na ufuatiliaji wa karibu kuhakikisha miti hiyo inakuwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, ahsante naunga mkono hoja endeleeni kuchapa kazi kwa manufaa ya Watanzania.

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA: Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie uwezekano wa kuboresha maeneo ya mwambao wa Ziwa Nyasa inayozunguka na milima mizuri ya Livingstone. Maeneo haya yanafaa sana kwa utalii kwa sababu ya *beach* nzuri zilizopo mwambao wa Ziwa Nyasa. Katika eneo la Kata ya Lumbila, Tarafa ya Mwambao palijengwa boma la Mjerumani ambalo limezama ndani ya Ziwa Nyasa na Wajerumani kuhamisha boma hilo kule Tukuyu. Boma la Mjerumani la Tukuyu asili yake ni Lumbila. Kwa hiyo, Serikali ione uwezekano wa kuweka kumbukumbu kihistoria kwani historia hiyo haifahamiki. Maeneo haya yakipewa usimamizi na kushirikiana na wananchi tutapata maeneo mazuri na mengi ya kihistoria. Maeneo haya bado yana picha nydingi za kihistoria ambazo zimehifadhiwa hasa katika makanisa ya Katoliki, kuna historia nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, eneo kubwa la Wilaya ya Ludewa ina vijito nya maji vinavyotiririka toka Milima ya Livingstone kuelekea Ziwa Nyasa. Vijito hivi baadhi vinatoka umbali wa kilometra 200. Hivyo kufanya maeneo mengi kuwa kijani (*greenish*) muda wote wa mwaka na kufanya mandhari nzuri

ya maliasili ya nchi hii. Ifike wakati Serikali iwe na mkakati wa makusudi wa kutenga fedha za uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya Wizara hii ya Maliasili na Utalii kushirikiana na Wizara nyingine kama miundombinu na ulinzi ili kufanikisha utalii kuweza kufanyika katika maeneo ya kando kando ya Ziwa Nyasa. Kuna wageni wengi toka nchi mbalimbali hasa za Ulaya kutembelea maeneo haya hasa yaliyokaliwa na wageni Wamisionari. Wageni hawa wanapokuja wanakumbana na mazingira magumu hasa miundombinu ya barabara na mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, tamaduni zetu hasa ngoma za asili zimeendelea kufifia mwaka hadi mwaka kutohana na kutopewa kipaumbele kikubwa. Kufifia kwa tamaduni hizi kumepelekea kumomonyoka kwa kiasi kikubwa kwa maadili ya vijana na watoto wetu. Lazima kuwe na mkakati wa moja kwa moja wa kuhamasisha watu kupenda tamaduni za makabila yetu. Viwepo vipindi maalum vingi vya ngoma zetu na pia kuwe na muda maalum hasa kuanzia baada ya shughuli za kilimo katika maeneo ya vijjjini. Ni vizuri walau kwa mwaka mara moja katika vijiji vyetu. Ngoma hizi zinazohusha akina baba, akina mama na watoto kujenga mahusiano baina yao toka katika maeneo mbalimbali, hamasa iende maeneo mbalimbali hasa mashulen sherehe na mengineyo.

MHE. ZAINAB M. AMIR: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Dkt. Hamisi A. Kigwangalla (Mb) pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga (Mb) kwa kazi nzuri mnayoifanya katika Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ijenje uzio wa senyenge katika hifadhi za mbuga zetu ambazo zinapakana na makazi ya wananchi ili kuepusha wanyamapori kutoingia katika makazi ya raia na kusababisha maafa hadi kupelekeea kifo kwa wananchi. Pili, Serikali itafute matumizi ya mkaa mbadala ili kuepusha ukamataji wa mkaa unaotokana na misitu. Pia mkaa huo mbadala utaepusha wananchi

kutokata miti hovyo na kuharibu misitu yetu na kupelekea ukame.

Tatu, naishauri Serikali iongeze vyuo ambavyo vitasaidia nchi kuweza kupata wataalam wa kutosha ili kusimamia maliasili yetu pamoja na kukuza utalii wetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali iboreshe kiwanja cha ndege kilichopo katika Mkoa wa Morogoro Mjini ili kuweza kutumika nyakati zote za usiku na mchana ili kuwasaidia watalii ambao watakuja kutembelea mbuga ya wanyama ya *Mikumi National Park* kufika kwa urahisi. Pia Serikali iboreshe miundombinu iliyopo ndani ya mbuga zetu za wanyama na ili kuweza kurahisisha watalii kufika maeneo mbalimbali ndani ya mbuga kwa urahisi katika vipindi vyote vya msimu.

Mheshimiwa Spika, Serikali iongeze magari ya kisasa ambayo yatatumika ndani ya mbuga zetu mara tu watalii wanapotaka kwenda kuwaona wanyama na vivutio mbalimbali. Pia nashauri kuutangaza mlima wetu wa Kilimanjaro kama kivutio cha watalii hususan kwa watalii wa nje ya nchi. Ili kuepuka nchi ya Kenya kutangaza mlima Kilimanjaro kuwa upo nchini mwao.

Mheshimiwa Spika, mwisho namuomba Mwenyenzi Mungu awape afya njema na umri mrefu ili kuweza kuwatumikia Watanzania.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Spika, misitu; (kwa nini ni muhimu kuwa na Chuo cha Misitu Mufindi) Pamoja na mchango huu, naomba kuwasilisha nakala ya kwa nini tuwe na Chuo kama Tawi la Chuo cha Misitu cha Olmotonyi. Nakala yangu imejieleza vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, mgao wa malighafi, ninashukuru Wakala wa Misitu kwa kuitikia kilio changu cha kukutana na wadau wa mazao ya misitu kabla ya msimu kuanza. Hata hivyo kama sehemu ya maoni ya wadau tulipokea tarehe 30 Aprili, 2018 mgao uzingatie pia kiwango cha uwekezaji na

hivyo kwa waliowekeza mitaji mikubwa wepewe mikataba ya malighafi, mfano watu kama kina *CF* (Makambako), *Hongwei International* just mention some few ukiacha *MPM* na *Sao Hill* (ambao kiasi fulani wameyumba) kuna watu wanapewa kwa mkataba wakati wao hawavuni, hawana viwanda isipokuwa wanauzu malighafi zao kwa wenzao, sio haki kabisa.

Ninashauri timu inayopita kukagua, itende haki na itoe maoni ya wanaostahili kupewa mikataba ya malighafi. Ikiwa mtu anatoa ajira *direct employment* ya watu 200 na kuendelea kwa nini asipewe mkataba? Mgao wa *cubic meter* 90,000 za *Sao Hill* ambao wameyumba mngefanya review ili walau *one third* ya mgao huo uende kwa wavunaji wadogo waliowekeza.

Mheshimiwa Spika, ushauri, ili kupunguza malumbano na mivutano isyo na sababu Wizara itoe maelekezo kuwa na chama kimoja tu ambacho kitafanya kazi na Serikali pasipo mivutano maana mwisho wa siku wote ni wadau hivyo kuwa na chama kimoja ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, napongeza uongozi wa shamba la *Sao Hill* kwa ushirikiano na *Mafinga Town Council*.

Mheshimiwa Spika, *why a need for a forestry college in the Southern Highlands of Tanzania and preferably in Mufindi District?*

Mheshimiwa Spika, historia/*background*, Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania imejaaliwa kuwa na hali ya hewa nzuri na udongo wenye rutuba, vyote kwa pamoja ni muhimu kwa kilimo cha miti ya misindano na mikaratusi. Wananchi wanaoishi katika mikoa ya Iringa, Njombe, Ruvuma, Rukwa na Katavi wanajishughulisha kwa kiasi kikubwa na upandaji miti. Wilaya ya Mufindi iliyoyo katika Mkoa wa Iringa inaongoza kwa upandaji miti kitaifa. Wilaya hii pia ni nyumbani (*is a home of*) misitu ya *Sao-Hill*, msitu mkubwa wa pili Barani Afrika na wa kwanza nchini Tanzania. Ukubwa wa msitu huu ni zaidi ya nusu ya misitu yote

inayomilikiwa na Serikali ya Tanzania iliyopo sehemu mbalimbali kama Arusha, Tanga, Kilimanjaro, Tabora, Mbeya na kwingineko. Msitu una eneo lenye ukubwa wa zaidi ya hekta 135,903. Msitu huu umesambaa katika tarafa nne kati ya tano za Wilaya ya Mufindi. Umesambaa katika tarafa za Kibengu, Ifwagi, Kasanga na Malangali.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1937 Waingereza walianzisha Chuo cha Misitu Mkoani Arusha kiitwacho Olmotonyi. Chuo hiki kililenga kuzalisha wataalam wa misitu katika fani mbalimbali. Wakati Chuo cha Olmotonyi kikifunguliwa msitu wa *Sao-Hill* ulikuwa katika hatua ya majaribio. Kuanzishwa chuo mikoa ya Kaskazini ilikuwa ni muhimu kwa sababu tayari kulikuwa na misitu kadhaa iliyokuwa imepandwa na Wajerumani na Waingereza kwa nyakati tofauti. Chuo hiki kiliwapa fursa Watanzania toka sehemu mbalimbali ya nchi kupata elimu ya misitu na hivyo kuajiriwa katika mashamba mbalimbali ya Serikali na katika Wizara ya Maliasili. Hata hivyo, kwa kuwa Serikali ya kikoloni ilikuwa inaona shida kuwaghamaria watu wa mbali usafiri, kipaumbele kikubwa ilikuwa ni kuwasomesha watu wa Kaskazini ambao walikuwa karibu na chuo. Hivyo, tangu kipindi cha ukoloni Watanzania wengi wanaoishi mbali na Chuo cha Olmotonyi walikosa fursa ya kupata elimu ya misitu.

Mheshimiwa Spika, baada ya uhuru Serikali ilirithi chuo hicho na kukiendeleza ikiwa ni pamoja na kuanzisha elimu ya misitu *Sokoine University of Agriculture (SUA)*. Baada ya Serikali kupanua shughuli za upandaji miti katika msitu wa *Sao-Hill* baada ya uhuru ilitambua kwamba haikuwa na maafisa misitu wa kutosha hasa wazawa.

Mheshimiwa Spika, miaka ya 1980 ikaanzisha chuo cha kutoa mafunzo ya elimu ya misitu ya muda mfupi katika makao makuu ya *Sao-Hill* (majengo bado yapo hadi leo) (*Sao-Hill Forestry College*). Kwa sababu ambazo hata hazifahamiki chuo kilihudumu kwa muda wa miaka saba tu hivyo hakikuendelea kutoa tena mafunzo. Kutoendelea kwa chuo hicho kimewanyima wananchi wengi wa maeneo yanayozunguka misitu na Mkoa ya jirani ya nyanda za juu

kujipatia elimu ya misitu na hivyo kuwafanya wategemezi kwa *NGOs* chache zinazotoa huduma hiyo. Pia vijana wengi wa nyanda za juu wamekosa *exposure* ya elimu ya misitu na hivyo kuishia kufanya *unskilled jobs* ambaao zinawafanya kulipwa ujira mdogo sana.

Mheshimiwa Spika, kwa nini tuwe na Chuo cha Misitu Mufindi (*Mufindi/Sao-Hill Forestry College, a Constituent College of Olmotonyi Forestry College*). Tayari kuna majengo (madarasa, ofisi za walimu na mabweni) pale makao makuu ya *Sao-Hill* ambayo yalijengwa tangu miaka ya 1980 hivyo haitatumika gharama kubwa ya kuanzisha chuo kwa kuwa majengo ya kuanzia yapo. Kwa sasa majengo hayo wanaishi wafanyakazi na mengine wanafugia tu kuku na kuhifadhi mahindi.

Natambua jitihada za Serikali katika kuyafufua majengo hayo kwa msaada wa watu wa Finland ili yatumike kutoa mafunzo kwa wakulima wa miti wadogo wadogo. Hata hivyo, hii haizui majengo hayo kutumika kama chuo kishiriki cha Chuo cha Misitu cha Olmotonyi kwa sababu wananchi wanaopata mafunzo yatakuwa yanatolewa kwa muda mfupi tu (kwa uelewa wangu). Hivyo, kuwa na chuo kitakuwa ni msaada mkubwa hasa kwa vijana wengi wanaotoka maeneo yanayozunguka misitu na hata nyanda za juu katika mikoa tajwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mufindi tarafa zake nne kati ya tano zimezungukwa na misitu na hivyo hii ndio shughuli yao kubwa ya kiuchumi kwa sasa. Kuwa na chuo kitavutia vijana wengi kusoma ili kupata elimu ya misitu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mufindi ina wawekezaji wengi wakubwa kwa wadogo waliowekeza katika kilimo cha miti. Wawekezaji hawa wanatakiwa kuajiri watu wenye weledi katika mashamba yao. Pia wanahitaji wavunaji wenye elimu ya kuvuna misitu kitaalamu zaidi. Kuwa na chuo Mufindi kutafungua fursa mpya za ajira kwa vijana wengi ambaao watapata mafunzo kwa ngazi mbalimbali za cheti na diploma.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mufindi ndio mwenyeji wa msitu mkubwa zaidi nchini na wa pili Afrika. Eneo kubwa la ardhi ya wananchi lilichukuliwa ili kupisha uwekezaji huu. Kuwa na chuo Mufindi ni njia mojawapo ya Serikali kutoa fadhila na kudumisha mahusiano mema kati ya wananchi wa Mufundi na *Sao-Hill*/Serikali kwa kuwa vijana wao watapata elimu ya misitu inatakayoinufaisha jamii nzima inayozunguka mradi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, vijana wengi wa Mufindi hawaajiriki katika mashamba ya miti na viwanda vyakupasua mbao. Wengi wao wanaajiriwa katika kazi ambazo sio za kutumia utaalam kama kusukuma magogo, kuzima moto, kupanda miti na kusafisha mashamba. Hii imejenga matabaka kati ya wenyiji wengine na hivyo kujiona kama hawathaminiwi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, ni moja ya ahadi zilizowahi kuahidiwa tangu kipindi cha mkoloni wa kiingereza na kurudiwa tena na Serikali yetu baada ya uhuru. Wakati wanawashawishi wananchi kuhama ili kupisha mradi wa *Sao-Hill*/wananchi waliahidiwa vitu vingi ikiwa ni pamoja na ajira, chuo cha misitu na mengine. Ahadi hiyo ilianza kutekelezwa miaka ya 1980 baada ya kuanzisha chuo pale *Sao-Hill* lakini hakikudumu hadi leo hii yamebaki majengo tu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mufindi ina eneo la kutosha na hali ya hewa nzuri. Vilevile uwepo wa msitu mkubwa, viwanda vyakuchakata magogo vikubwa na vidogo pamoja na kiwanda cha karatasi vinaifanya Wilaya kuwa sehemu nzuri hasa kwa mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, *relevance* ya kuwa na chuo eneo tofauti na Mufindi kama ilivyo sasa Arusha kwa sasa haipo kwa kuwa hakuna viwanda vyakaratasi, wala viwanda vyakutosha kwa mafunzo ya vitendo na pia eneo hilo sio rafiki kwa kilimo cha miti kwa sasa kwa kuwa hawana ardhi ya kutosha hivyo manufaa yake kwa jamii inayokizunguka chuo ni ndogo ukilinganisha na manufaa ambayo wanaweza

kuyapata wakulima wa miti wa Mufindi pamoja na wa Nyanda za Juu kwa ujumla ambao ndio wadau wakubwa wa misitu kwa sasa.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Spika, nasikitika kuona vyanzo vya utalii vilivyopo Wilaya ya Mbozi zimesahauliwa kuwekwa kwenye kumbukumbu ya Wizara, pia havijatangazwa mfano katika Kata ya Nanyara Wilaya ya Mbozi kuna vivutio vya utalii vya maji moto na mapango ya popo. Vyanzo hivi havitajwi popote pale wala havipo kwenye kumbukumbu za Wizara. Wizara ichukue hatua thabiti za kuvitambua vyazo hivi na kuvitangaza ili kuongeza mapato ya Halmashauri ya Mbozi na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, pia askari wa wanyama pori waepukane na mauaji ya raia wanaoingia kwenye maeneo ya hifadhi badala yake wachuke hatua za kisheria na siyo kuua. Mfano wapo wananchi wasiokuwa na hatia waliuawa mwaka jana Arumeru, Arusha na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA: Mheshimiwa Spika, naomba kufanya mabadiliko ya usajili wa kijiji cha Sibwesa kwenye karatasi yangu niliyochangia kwa maandishi badala ya kusajiliwa mwaka 1967 sahihi ni kuwa Kijiji cha Sibwesa kilisajiliwa mwaka 1975 na hati ya usajili wa kijiji hicho kusainiwa tarehe 20/5/1976 hivyo mgogoro huu una zaidi ya miaka 31.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri, nawapongeza watendaji wote wa Wizara hii naunga mkono hoja. Pia nampongeza Waziri na Naibu Waziri wake kwa jinsi wanavyoweza kushuka na kupokea ushauri na maoni wanayopewa na wadau wa maliasili na utalii mfano kundi la uhamasishaji wa utalii wa ndani uitwao Utalii 255.

Mheshimiwa Spika, Waziri na Naibu Waziri kwa wakati mbalimbali walipata fursa ya kuzungumza na wadau hao.

Katika suala zima la uwindaji, nashauri muda wa kuwinda unapofika taarifa itolewe kwa uwazi kuitia vyombo mbalimbali vya habari. Taarifa hiyo ileze muda wa kuwinda, gharama zinazotakiwa kulipwa, aina ya silaha zinazoruhusiwa kutumika na kadhalika. Kwa sasa taarifa hizo hazipo wazi kwa wananchi ambao wangependa kupata kitoweo chenye ladha tofauti kinachopatikana nchini.

Mheshimiwa Spika, katika nchi jirani ya Kenya kuna ukumbi wa burudani mjini Nairobi unajulikana kwa jina la Carnival, kuna aina tofauti za nyama choma kutoka mbugani mfano nyati, nyumbu, swala, mbuni na kadhalika. Huku kwetu jambo hilo halipo hivyo Tanzania tunafanya utalii na kuwatunza lakini wenzetu wanatafuna!

Mheshimiwa Spika, suala la maeneo ya hifadhi na changamoto zake, kazi za ulinzi katika maeneo hayo inafanyika vizuri sana. Naomba ubinadamu ufanyike, kuna tofauti kubwa ya majangili na wananchi wanaoingia katika hifadhi kupata dawa, kupata miti ya kuni au kutengeneza mipini ya majembe na mashoka. Ukweli wananchi hao wanapokutwa huko adhabu wanayoipata ni kubwa kuliko kosa walilolifanya. Wengine wamepata vilema hata kupoteza maisha. Naomba elimu itolewe zaidi kwa wananchi ili kuwaepushia na adhabu hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uanzishwaji wa vituo vya utalii wa ndani katika mikoa mbalimbali nchini, vituo hivyo vitasaidia kuleta hamasa na ushindani baina ya Mkoa na Mkoa, utasaidia wananchi kusafiri umbali mdogo ili kufikia vituo. Kama malipo yatawekwa kidogo itasaidia wananchi wengi kutembea na kuingiza mapato kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika uhamasishaji wa utalii wa ndani, kuwe na utaratibu wa kuwazoeshaa watoto na wanafunzi kutembelea vivutio mbalimbali na kuelezewa umuhimu wa kutunza tunu zetu na kuwa wazalendo, watoto hao na wanafunzi wataendeleza tabia nzuri ambayo itasaidia kuondoa au kupunguza mambo ya ujangili na uvunjaji wa sheria na kuisadia katika kulinda tunu zenu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara hii kwa kuitangaza nchi yetu ndani na nje ya nchi. Naipongeza kwa kuingizia Serikali mapato kupitia vivutio mbalimbali, nampongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante.

MHE. ESTER A. MAHAWE: Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kutoa maoni yangu kwa Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Utalii unachangia pato la Taifa kwa asilimia 17.5 lakini changamoto za Wizara hii kutokuza pato hilo kama zilivyo nchi jirani kazi zinazotuzunguka ni nyingi mno, kati ya hizo naomba nitaje zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, bado hatujatenga bajeti inayotosheleza Wizara hii kufanya (*marketing*) matangazo ya kutosha kwa ajili ya ufinyu wa bajeti. Tanzania ni nchi pekee katika Ukanda wa Afrika Mashariki yenye vivutio vingi na visivyopatikana maeneo mengine lakini nchi hizo kama Kenya, Uganda, Rwanda na na kadhalika kutenga bajeti kubwa ya matangazo ya hifadhi na maliasili zao na hivyo kupata fedha nyingi zinazochangia chumi zao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri Serikali yangu iweze kuongeza bajeti ya Wizara hii ili tuweze kupata watalii wengi na tupate kuongeza fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, nitoe masikitiko yangu kuhusu suala la *single entry* katika hifadhi hasa Ngorongoro na Serengeti. Huko nyuma wageni waliingia katika hifadhi na kutoka kwenda kwenye vijiji vya jirani kwa ajili ya kula, kunywa na pengine kuleta hali iliyofanya vijiji vya jirani kupata mapato ikiwa pamoja na kuongeza pato la mtu mmoja mmoja. Leo hii wakazi wengi wamebakia kuwa maskini na wengine wamekuwa vibaka. Kwa kukosa ajira walizokuwa wakizipata kupitia watalii hao.

Mheshimiwa Spika, ni ajabu sana na utashangaa kuacha *system* ya zamani na kuanzisha *single entry* eti ni kwa sababu tu mgeni anaweza kutoka na *permit* yake ikatumika

na mtu mwagine, sababu hii inasikitisha kama nchi ina wataalam na wanaishi katika dunia yenye teknolijia kubwa kiasi hiki wanashindwa kujuu yupi kaingia na yupi katoka, ndioo mtalii yule yule? Ni ajabu sana.

Mheshimiwa Spika, kuna tozo na kodi lukuki ambazo zinazokatisha tamaa watalii wengine kutokuja Tanzania. Kodi hizi pia zimekuwa kero kwa wafanyabiashara wa utalii hasa *tour operators* na watu wa mahoteli. Naomba nishauri Serikali ikae na wadau wa utalii na ione ni kwa jinsi gani wanaweza kuondokana na kero ambazo si za lazima zinazokatisha tamaa wawekezaji hawa.

Mheshimiwa Spika, kwa nini tusiige kutoka kwa nchi kama Dubai na nyinginezo ambazo unakuta wanachajji viza ya dola za Marekani 150 tu ili kuvutia watalii wengi kuja huku kwetu? Watalii hawa wakija wanalala, wanakula, wanatembelea mbuga na kadhalika na kwa vyovyote vile lazima watuachie fedha nyingi za kigeni, kwani tunawakatisha tamaa kwa kuwawekea tozo nyingi zisizo na maana.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara hii ikae na wataalam na ione mbinu mbadala kwa kuongeza idadi ya watalii kutoka idadi ya watalii milioni 1.3 haidhuru mpaka milioni tatu. Mimi najua tunaweza na ninawaombee Mawaziri wetu, wataalam na watendaji wa Wizara hii kwa Mwenyenzi Mungu ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga hoja mkono.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Spika, tumekuwa na matatizo mengi hasa baina ya wakulima na wafugaji. Tatizo hili limekuwa sugu sana hasa kwa wafugaji kuwa na mifugo ndani ya nchi hii imekuwa ni shida sana. Wafugaji wanahangaika sana na mifugo, kila wanapoelekea wanafukuzwa na wakati mwagine mifugo yao inakamatwa na kupigwa mnada, wanalipishwa fedha nyingi sana ambazo hata uwezo wa kuikomboa mifugo yao hawa wanabakia na umaskini mkubwa, wengine wanapata msituko wa

moyo wanakufa. Serikali ilione tatizo hili kuwa ni kubwa na ipo haja ya kuingilia kati ili tuweze kuishi kwa amani na hawa wenzetu ambao ni wafugaji wajisikie kuwa na wao wanathaminiwa ndani ya nchi yao.

Mheshimiwa Spika, pia najielekeza kwa wakulima wetu wanapata shida sana wanapolima wakati mwingine wanabanwa wamelima kwenye hifadhi ya akiba. Hivyo basi Serikali yetu iwatengee eneo wananchi wetu waweze kulima isiwe kila eneo ambalo ni zuri kwa kilimo linawekwa kuwa ni kwa ajili ya hifadhi tu. Tuwasaidie wakulima wetu na wao wahisi kuwa wanathaminiwa na kupewa nafasi ya kuweza kujidoreshea maisha yao. Serikali itenye maeneo maalum kwa ajili ya kilimo.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ninachangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Nkasi Kusini kuna Vijiji vya Kusapa, King'ombe, Mlambo, Kilambo, Ng'undwe, Namansi, Kizumbi na Mlalambo, vilevile Kijiji cha China na Kijiji cha Nkata mipaka ya vijiji vyao na hifadhi havieleweki na vijiji vingine viko ndani ya pori na kuwa pori lilituka vijiji hivyo na kuvizingira, kwa hiyo hawana ardhi ya kutumia kwa ajili ya kuendeleza maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali kuititia Kamati ya Wizara mbalimbali itoe matokeo ili kusuluhisha jambo hili. Naomba matokeo yawe wazi na wananchi wajue hatma ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Kasapa kwa mfano, kimezingirwa na maeneo ya hifadhi mawili pori la *TFS* na *Lwanfi Game Reserve* ambapo Wizara ilitembelea kwa juhudhi yangu. Waziri mstaifu Mheshimiwa Maghembe aliweza kuona jinsi wananchi walivyokosa eneo la kulima maana mipaka iko mita zisizozidi 300 pande zote nne yaani Mashariki, Magharibi, Kusini na Kaskazini. Wizara ilete mapendekezo ni namna gani Wizara imejipanga kuwasaidia wananchi baada ya kutembelea kila kijiji wamekaa kimya, *why?*

Mheshimiwa Spika, matatizo ya wanyama (tembo) wanasumbua wakulima wa Vijiji vya King'ombe, Mlalambo, Ng'undwe na Mlalambo na Vijiji vya Kisumbaka na Kasanga Wilayani Kalambo, tembo wameuwa watu zaidi ya watatu kwa miaka miwili mfululizo. Wananchi wa eneo hilo wanasema hawana mtumishi hata mmoja wa kuzuia tembo wasilete maafa hayo. Tunaiomba Serikali ipeleke watumishi wa Maliasili Kisumba kuzuia maafa haya. Naiomba Serikali itusaidie kupunguza ukubwa wa pori hili ili wananchi wa vijiji nilivyovitaja wapate ardhi ya kulima ili waendeleze maisha yao hapa duniani.

Mheshimiwa Spika, Mlalambo, Ng'undwe wananchi wanapekuliwa hovyo hovyo, hawawezi kujenga nyumba eti mbao kutoa wapi? Wananchi wanachapwa viboko, Mlalambo na Ng'undwe si sawa eti huo ubao wa mlango katoa wapi? Haya ni malalamiko nilliyopewa nillipoenda kwenye ziara, naomba tuliangalie jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kuna ardhi ya wananchi ya Kakumbu inatumika chini ya kiwango iko wapi Kamati ya Wizara tano ambayo tumeipatia migogoro ya watu wa Sintali, Nkama na Nkomanchindo.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Spika, kuna mkakati gani uliowekwa na Serikali kuhakikisha kuwa miji mikongwe inatangazwa na kukarabatiwa ili iwe kivutio cha utalii kwa mfano Mji wa Mikindani katika Manispaa ya Mtwara, Mikindani umetekelizwa, mchafu, miundombinu mibovu na kadhalika. Naamini mji ule ukiendelezwa na kutangazwa vizuri utawavutia watalii hivyo kuongeza pato la Manispaa na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina makakati gani wa kuhakikisha inautangaza na kuuendeleza utalii wa bahari na fukwe zake. Wananchi wanaoishi maeneo yenye bahari mfano Mtwara, tulitarajia kuwa Serikali ingefanya uwekezaji mkubwa katika fukwe za bahari kwa kushirikiana na wawekezaji wengine ili kuwezesha uchumi kukua maeneo

husika. Kinyume chake fukwe hizi zimeachwa chafu bila uwekezaji wowote. Je, Serikali inaridhika na hali hii?

Mheshimiwa Spika, naomba kujua msimamo wa Wizara hii juu ya kutoa elimu mbalimbali zinazohusu uhifadhi wa watu na wanyama pori ambavyo vimekuwa vikitekelezwa na watu mbalimbali ikiwemo Serikali mfano kibali cha kukata miti mingi sana katika mbuga ya Selous.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, na mimi naunga mkono hoja hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Pamoja na kuunga mkono, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya Rais kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuhakikisha anasimamia vizuri sekta hii ya maliasili na utalii na hata kuleta tija nzuri katika Taifa.

Mheshimiwa Spika, Waziri alipata nafasi ya kutembelea mbuga na hifadhi zetu katika Halmashauri ya Chalinze na Wilaya ya Bagamoyo. Katika ziara hiyo amejionea mengi ikiwemo migogoro baina ya wananchi na hifadhi. Lakini pamoja na maelekezo, hakuna liliofanyika hadi leo. Wananchi wameendelea kupata shida na Serikali Kuu imekuwa kimya.

Mheshimiwa Spika, ni masikitiko yangu kuwa mbuga ya hifadhi au Pori la Hifadhi la Uzigua na Wami Mbiki limekuwa sehemu nzuri kwa ajili ya mapitio ya wanyama. Lakini ujangili umekuwa shida, pamoja na juhudhi kubwa zinazofanywa na Serikali sijajua mna mipango gani kuhusu usimamizi wa *WMA* hii.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia juu ya uangalizi wa maeneo ya malikale. Pamoja na mipango mizuri, lakini ukweli ni kwamba Mji wa Bagamoyo ambao ndani yake kuna *Caravan Serai* na Mapango ya Kaole umesahaulika. Mji huu una mambo mengi ya kihistoria na majengo mengi ya kale. Kwa kifupi matarajio yangu ni Serikali kuwa na mkakati juu ya mji na historia wa Bagamoyo. Inakumbukwa katika maeneo mengi kuanzia ujio wa Wareno, Wajerumani, Waarabu na

shughuli za utumwa, bandari ya kwanza Tanzania na mengineyo mengi lakini Bagamoyo mmeisahau.

Mheshimiwa Spika, Waziri atakapokuja atusaidie sisi wana wa Bagamoyo kufahamu nini kinafanyika au mpango gani uliopo juu ya Mji wa Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maliasili na utalii kuweka mipaka ya hifadhi ya uwanda iliyowekwa toka mwaka 1959, eneo lililotolewa na wakulima, lakini kwa sasa ramani hiyo imekiukwa na kuingilia makazi ya wananchi katika mipaka ya Vijiji vya Kilangawana, Maleza, Kilyama, Tundu, Legeza, Kapenta, Mkusi Iwelya Mvua na Nankanga. Nataka Mheshimiwa Waziri anipatie majibu kwa hoja zifuatazo:-

(a) Hifadhi ya Uwanda, je, ni mali ya Maafisa Misitu wa Mkoa wa Rukwa?

(b) Kwa nini hifadhi hiyo imejaa mifugo mingi hata uthamani wa hifadhi haupo tena?

(c) Kwa nini wanaingiza mifugo (ng'ombe) kwa kuwatoza pesa kwa manufaa binafsi?

(d) Kwa nini wanaruhusu wakulima ndani ya hifadhi hiyo baada ya mpunga kukomaa wanavuna wao kwa kutumia ukatili wa kinyama kabisa? Naomba nipatiwe majibu katika hoja hizi vinginevyo sitaunga mkono hoja na nitashika shilingi ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili.

MHE. DKT. HADJI H. MPONDA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na maoni ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwamba kumekuwa na ushirikishwaji mdogo sana na wananchi katika uwekaji wa vagingi vya mipaka ya hifadhi/vijiji.

Mheshimiwa Spika, zoezi la utambuzi wa mipaka katika Wilaya ya Malinyi katika Pori Tengefu la Kilombero limekamilika lakini limeacha changamoto/lawama kwa Serikali kwamba wananchi hawakushirikishwa kwa mapana. Matokeo ya zoezi hili limesababisha wananchi kukosa mashamba na baadhi ya vitongoji kuwa katika miliki ya pori tengefu. Hii imeleta tataruki kubwa kwa wananchi kukosa ardhi kwa maendeleo ya kilimo na kiujumla ustawi wao.

Mheshimiwa Spika, katika kampeni zake Mheshimiwa Rais mwaka 2015 aliwaahidi wananchi wa Malinyi kuongezea ardhi kutoka katika Kingo (*buffer zone*) ya Pori la Kilombero. Kingo hii bado ni pana sana (kilometra 5 -12) hivyo kuwaongeza wananchi angalau kilometra tatu tu hakutoathiri kwa vyovyyote ustawi au uendelevu wa Pori Tengefu la Kilombero. Hali hii kwa ukosefu wa mashamba kwa wananchi wengi wa Malinyi kutakuwa na athari kubwa kimaendeleo, ustawi wa uhai kiujumla kwa wananchi wa Malinyi.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Wizara ya Maliasili na Utalii iridhie maoni/ushauri wa Kamati hususan kurejea upya mipaka ya Pori Tengefu la Kilombero kunusuru mashamba na baadhi ya vitongoji na kuondoa migogoro katika maeneo hayo. Ahsante.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu migogoro ya mipaka, kumekuwa na migogoro ya mipaka kati ya *TANAPA* na wananchi wa Kijiji cha Luduga katika Wilaya ya Wanging'ombe, Mkoa wa Njombe. Pia huko Kituro, Wilaya ya Makete, Mkoa wa Njombe wananchi wamekuwa wakisumbuliwa na *TANAPA*, kutokana na kuweka *beacon* kwenye maeneo yao ambayo hapo awali hayakuwa kwenye eneo la hifadhi lakini Serikali imeongoza. Hii imesababisha kuwavurugu wananchi wanaoishi maeneo ya mipaka ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali isitishe zoezi hili la kuweka mipaka hadi wawashirikishe wananchi katika maamuzi ya Serikali yanayohusu kuongezeka kwa maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, kutopeleka fedha kwa wakati naomba kujuu ni kwa nini fedha hazipelekwi kwa wakati. Lakini pia kutopelekwa fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge, lakini kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tozo nyngi kwenye sekta ya utalii, matokeo yake kumesababisha kupunguza watalii wanaokuja nchini kwetu. Naiomba Serikali ipunguze tozo zisizo za muhimu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Spika, hoteli za kitalii na uhudumiaji wageni, ningependa kushauri Serikali kuanzisha vyuo maalum kwa ajili ya vyuo vya kuelimisha wahudumu wa kuhudumia watalii. Imekuwa watalii wengi wakilalamikia huduma zinazotolewa hapa nchini kuwa ni za chini sana.

Mheshimiwa Spika, hata waongozaji wa watalii ni kwamba hawana mafunzo maalum hivyo kuwa shida kwa watalii wetu. Gharama za juu kwa watalii hivyo kupunguza ujio wa watalii, mfano watalii kulipia huduma moja mara mbili kuliko ilivyo sasa ambapo mtalii analipia hoteli, analipia usafiri halafu anapofika kwenye eneo la mbuga anakutana na tozo ya kuingiza chombo hicho kwenye mbuga hii inakatisha tamaa kwa watalii.

Mheshimiwa Spika, nishauri gharama zinazolipwa wenyе mahotelі hata kama watalii hawajalala hivyo kukatisha tamaa kwa wamiliki wa mahotelі ya kitalii.

Mheshimiwa Spika, vitalu vya uwindaji; nashauri Serikali kugawa vitalu kwa kuzingatia wazawa pia ugawaji wa vitalu uende kwa wakati. Pia nashauri kuwawekea

mazingira mazuri ya uwekezaji katika utalii. Pia niishauri Serikali kuangalia upya juu ya mipaka ya kuhifadhi maliasili na mbuga kwa ujumla. Pia Serikali ihakikishe maeneo hayo ili yale ambayo hayatumiki yarudi kwa wananchi na yabadilishwe matumizi.

Mheshimiwa Spika, niishauri Serikali kuhakikisha inaongeza fidia kwa wananchi wanaopata madhara ya kuvamiwa na wanyama hivyo kuleta hasara kwa wananchi. Vikundi vyta wanawake, wanawake wachonga vinyago mfano pale Mwenge. Niishauri Serikali kuyaangalia makundi haya ya wanawake wanaojishughulisha na vinyago wanawauzia watalii wetu wapewe mikopo ya kuwawezesha kutoka maliasili kuwasaida. Pia Serikali isaidie masoko ya vinyago.

MHE. NURU A. BAFADHILI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kupata muda wa kutoa mawazo yangu kwa faida ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa kwanza nitajikita katika suala zima la utalii. Utalii ni sekta ambayo inalipatia faida Taifa letu. Mbuga nyingi zinazotangazwa ni Mikumi, Serengeti, Ngorongoro, Manyara na Selous. Mbuga hizi ndizo ambazo kila leo utasikia zikitangazwa katika vyombo vyetu mbalimbali vyta habari. Kuna mbuga ya Saadani katika Wilaya ya Pangani, mbuga hii imepakana na ufukwe wa bahari. Katika maajabu ya mbuga hii utakuta simba na tembo na wanyama wengine wanacheza pamoja katika ufukwe wa bahari hivyo nayo ni maajabu.

Mheshimiwa Spika, ukiacha huo utalii wa wanyama pia kuna eneo katika Wilaya ya Tanga ambapo kuna maji moto yenye *sulphur* ambayo wenye matatizo ya ugonjwa wa upele huenda kuogelea hapo. Sehemu hiyo huitwa Amboni, Kata ya Mzizima Wilaya ya Tanga, eneo hilo ni maarufu kwa jina la *Amboni Sulphur Baths*.

Mheshimiwa Spika, katika vivutio vyta utalii pia kuna sehemu katika Bandari ya Jiji la Tanga kuna eneo linaitwa

Jambe, eneo hili kuna magofu ya mahandaki ambayo zamani watu walioishi hapo walitumia kujificha na pia kuna visima vilivyo chimbwa na wenyeji walioishi wakati huo.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, mipaka inayozunguka hifadhi ipitiwe upya. Kulingana na idadi ya watu kuongezeka nchini kumekuwa na muingiliano mkubwa sana kati ya wananchi na wanyama na kupelekeea mahusiano mabaya kati ya wananchi wanaozunguka hifadhi na watumishi wanaohusika na kuhifadhi wanyamapori. Nashauri Serikali kuititia upya mipaka yake ili kuondoa migogoro isiyokuwa ya lazima.

Mheshimiwa Spika, sheria ya fidia ibadilishwe, suala hili limekuwa na malalamiko makubwa kwa wananchi pale inapotokea mtu au watu kuuawa, kujeruhiwa au mazao, makazi ya wananchi kuharibiwa, fidia au kifuta jasho haviendani na adhabu inayotolewa kwa mtu au watu wanapokamatwa wakiwa wameua mnyama au wanyama.

Mheshimiwa Spika, kuwekwe mazingira rafiki kwa wawekezaji, kumekuwa na changamoto za wawekezaji waliopo na wanaotaka kuja kuwekeza nchini kwetu. Kwa kuwa Taifa letu tunategemea utalii kukusanya na kupata pesa za kigeni ni vema kama Wizara kukawekwa mkakati wa makusudi utakaokuwa rafiki kwa wawekezaji wanaotaka kuwekeza kuja.

Mheshimiwa Spika, tozo na malipo kwa watalii ziangaliwe upya ili kuleta tija kwa Taifa letu kwa kuangalia tozo zote zenye kero ambazo zinaweza kufanya watalii wetu wakaweza kushindwa kuja kutalii na kusababisha Taifa letu kukosa mapato na kupeleka nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, suala la ugawaji vitalu, kumekuwa na malalamiko mengi kwa wananchi wanapokuwa wanataka kumiliki vitalu kwa kufuata taratibu na sheria tulizo jivekeea, kumekuwa na ukiritimba mkubwa na kupelekeea mianya ya rushwa na kufanya waone kuwa wageni wanapewa nafasi kubwa kuliko wageni wenyeji.

Mheshimiwa Spika, huduma za kijamii ziboreshewe kwa vijiji vinavyozunguka au karibu na hifadhi. Kumekuwa na changamoto kwa wananchi wanazunguka hifadhi ili kulinda wanyama hasa pale ambapo wananchi wanafuata huduma za maji na vitoweo mbali. Nashauri Wizara kuweka utaratibu mbadala wanapoonaa kuna umuhimu wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara itoe elimu kwa maeneo yanayokuwa karibu na hifadhi ili kujua umuhimu wa uhifadhi na wao wananchi wajue kuwa wao ni walinzi wa kwanza kuliko ilivyo sasa wanavyojiona kama wanyonge.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi, Wizara ya Mazingira na Wizara ya Maliasili na Utalii kuna umuhimu wa kukaa pamoja ili kupitia suala la mipaka na shughuli za binadamu, kwa kuwa Serikali ni moja endapo kama mtakaa pamoja mtamaliza tatizo hilo kwa umakini.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kubadilisha kutangaza vivutio vyetu ubadilishwe kwani utaratibu unaotumika kwa sasa haujaleta matokeo makubwa na ya haraka kwa Taifa letu kulingana na faida wanazozipata nchi nyingine zinazotuzunguka.

MHE. ENG. GERSON H. LWENGE: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja kwa sababu naamini malalamiko ya wananchi wa Wilaya ya Wanging'ombi yaliyo na Pori la Akiba la Mpanga – Kipengere litafanyiwa kazi na Waziri.

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba ya Waziri ukurasa 69 imeelezwa kuwa Wizara inaweka *beacons* upya kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, TAMISEMI na wananchi.

Mheshimiwa Spika, ushirikishwaji wa kazi hiyo haupo kwenye Pori la Akiba la Mpanga – Kipengere na taarifa hii nimemwambia Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii lakini hakuna hatua iliyochukuliwa *TANAPA*, bado *TANAPA*

wameendelea kuweka *beacons* ndani ya vijiji vilivyoandikishwa kisheria. Jambo hili limeleta adha kubwa kwa wananchi hasa vijiji vya Iyayi, Igandu Hanganani, Ludwega, Mpanga, Malangali, Wangamaho, Masage na kadhalika. Naomba zoezi hili lisimamishwe ili ushirikishwaji wa kutambua mipaka ya awali iweze kutambuliwa ili kuondoa hofu kwa wananchi kwenye Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, iliwahi kutolewa kauli ya Serikali katika kuondoa migogoro ya mipaka kuwa kuna Kamati ya Wizara ya Ardhi, Maliasili na TAMISEMII inayopitia kila hifadhi au Pori la Akiba zote nchini ili kutatua matatizo ya mipaka na vijiji vilivyoandikishwa na kuwekewa *GN*. Kazi hiyo sasa ni miaka mitatu sijawaona wakipita katika pori hili la Mpunga – Kipengere na hivyo kusababisha mgogoro huu kuwa mkubwa zaidi na kufanya wananchi wa jimbo langu kurudi nyuma katika kufanya kazi za maendeleo kwenye maeneo yao kwa kujenga mashule, zahanati na kilimo.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara hii iangalie upya haja ya kuwa na Mapori ya Akiba kwenye maeneo wananchi wameongezeka sana na itafika muda wananchi watakosa ardhi ya kuishi.

MHE. JOYCE B. SOKOMBI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii na mimi niweze kuchangia Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nitaanza na ukamataji hovyo wa wauza mikaa. Naomba utambue kuwa mkaa ni kimbilio la wananchi kwa 95% mfano mwananchi wa Kaburabura, Bugoji, Salagana, Kangetutya umwambie atumie gesi ni kichekesho cha hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, kwanza vile usafirishaji wa gesi kutoka Mjini Musoma hadi ifike kusambazwa kwa wananchi huko vijiji ambako bado wanaamini kupika kwa kutumia kuni na mkaa, leo hii wananchi hao wananyanyasika kutokana na upatikanaji wa kupatikana (upatikanaji wa kuni) kwa kuni na mkaa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatakiwa iwasaidie wananchi wake na siyo kuwanyanyasa kwa sababu leo hii mtu akikamatwa hata na gunia moja la mkaa ni shida na linaweza kumfunga. Serikali inazuia ukataji miti hovyo sasa kama mnawazuia wananchi hata kupata kuni mnategemea mwananchi wa kijiji atapika kwa kutumia nini? Kwani wale watendaji wenu wananyanyasa wananchi kule vijiji kwani hata mwananchi akikamatwa na mzigo wa kuni au gogo lililoanguka lenyewe anashtakiwa na viongozi wa eneo husika eti kwa nini hajachukua kibali.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali irekebishe kanuni zinazosimamia matumizi ya nishati ya mkaa kwani wananchi wengi wa vijiji hawajapata nishati mbadala ya kutumia kuni na mkaa.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Msitu wa Kyanyari uko chini ya *TFS*, mpaka sasa katika Kijiji cha Nyamikoma, Mwibagi Kata ya Kyanyari, Butiama kuna wananchi walifukuzwa ili kupisha eneo la msitu lakini toka walivyofukuzwa hadi leo wananchi hao bado wananyanyasika kwani hawana makazi maalum na mashamba.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kyanyari wanateseka sana kwa kukosa maeneo ya kulima, niishauri Serikali kabla ya kufanya uhamisho kwa wananchi ili wapishe hifadhi ni vizuri iwaandalie maeneo kabla ya kuwahamisha ili wananchi wanapofurushwa wawe na eneo la kuweka makazi ya kudumu ya uhakika na sehemu ya mashamba ambapo wananchi watakuwa na uhakika wa kulima na kupata mazao ya chakula na biashara ili kuweza kukidhi mahitaji ya wananchi ya kila siku.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Spika, makosa ya matumizi ya takwimu, ukurasa 73 aya 164; Wizara inasema mapato yatokanayo na utalii yameongezeka kutoka dola milioni 2. mpaka dola bilioni 2.25 mwaka 2016 – 2017. Kamati pia katika taarifa yake ukurasa 11 imerudia kusema; mapato yatokanayo na utalii mwaka 2016/2017 yameongezeka hadi dola bilioni 2.3; hili ni kosa. Dola bilioni 2.3 sio mapato ya

sekta bali ni *forex* (fedha za kigeni zinazoingia kwenye *reserve* kutoka utalii). Tusichanganye *forex* na *revenues*. Matumizi ya takwimu hizi ni muhimu kutiliwa maanani. Tutumie mapato ya fedha za kigeni ili kuwa sahihi. Pia utalii unachangia 25% ya *forex* na sio 25% ya *GDP*.

Mheshimiwa Spika, mradi wa umeme Rufiji katika ukurasa 71 wakati wa mjadala wa makadirio ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Serikali ilitoa *commitment* kuwa kabla ya mradi kuanza itafanyika *ESIA*. Hata hivyo *TFS* wametangaza zabuni ya kuvuna miti milioni mbili katika eneo lenye ukubwa sawa na Mkao wa Dar es Salaam. Ni kweli kuwa hili eneo ni 3% tu ya Selous, lakini eneo husika ni eneo la mazalia ya wanyama. Kwa nini Serikali isisubiri *ESIA* iishe ili waanze utekelezaji? Kwa nini Serikali inafanya haraka hii?

Mheshimiwa Spika, narudia kusisitiza kuwa tutazame miradi mbadala iliyoainishwa kwenye *Power System Master Plan (2016 update)* ili kuepuka madhara ya mazingira katika *Selous Game Reserve*. Ni muhimu jambo hili tulitazame kitaifa ili kulinda maliasili zetu.

Mheshimiwa Spika, ni sahihi kuwa na uwezo mkubwa wa kuzalisha umeme lakini sio kwa kuharibu ekolojia. Kwa nini hatutumii bomba la gesi kikamilifu? Asilimia 25 ya bomba la gesi inazalisha umeme wote *Stiegler's*. Kwa nini tuendelee na mradi huu?

Mheshimiwa Spika, nashauri *ATCL* wanahisa wake wawe *TANAPA* na *NCAA*. Hii ni kwa sababu wao ndio wafaidika wakuu wa Shirika la Ndege. Asilimia 15 ya makato yanayokwenda Hazina zitumike kama mtaji kwa *ATCL*.

Mheshimiwa Spika, suala la Loliondo lipate suluhisho ya kudumu kwani wananchi wanaumia sana. Mwaka 2017 boma 250 zilibomolewa na wananchi kupigwa sana. Waziri aliahidi kuwa *OBC* itanyang'anywa leseni ifikapo Januari, 2018. Hata hivyo mpaka leo *OBC* bado wapo. Kwa nini tusifuate sheria na kuiacha Loliondo kama *village land*?

Mheshimiwa Spika, *CAG*, ametoa hoja ya ukaguzi kuwa *TANAPA* na *NCAA* hukatwa mchango kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina asilimia 15 na wakati huo huo kukatwa kodi asilimia 30 bila kuondoa makato yanayotambuliwa (*allowance expense*). Suala hili ni kinyume kabisa na *principles* za kodi kwani hiyo asilimia 15 ilipaswa kuondolewa kabla ya kutoza kodi. Ni muhimu sana Serikali ifuate ushauri wa *CAG* wa kurekebisha sheria ili kuwezesha makato yanayokwenda mfuko wa Hazina (Rejea *CAG Pg. 98 – 99*).

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii kutoa mchango katika Wizara hii. Aidha, napenda kumpongeza Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kuandika na kuiwasilisha hotuba hii kwa ufasaha mkubwa. Katika kuchangia hotuba hii ya maliasili na Utalii, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nianze na vivutio cha utalii, napenda kuipongeza Serikali pamoja na Wizara hii kwa kuendelea kutilia mkazo namna ya kuboresha vivutio hivi vya utalii. Mazingira ya vivutio vyetu vinaonekana kuimarika na kuvutia watalii. Ushauri wangu katika suala hili kwa Serikali ni Wizara kwa jumla ni kuongeza vivutio hivyo na kuviveka katika hali ya kisasa zaidi. Aidha, ni vyema kuwe na vivutio vya namna tofauti katika maeneo yetu ya vivutio kwa mfano, ikiwa kivutio kingine kiwe na wanyama wa aina nyingine ili kuweka *variety* ya vivutio. Kutatua migogoro ya mipaka ya Hifadhi za Utalii.

Mheshimiwa Spika, hali ya migogoro katika nchi yetu imezidi kila siku. Naipongeza sana Wizara hii kwa kuchukua juhudzi za kulishughulikia suala hili. Utaratibu wa kuwashirikisha wananchi walio katika maeneo husika ni jambo jema sana. Ushauri wangu katika suala hili ni kuzingatia kuwapa kipaumbele wakulima wa maeneo hayo ili kuendeleza kilimo ambacho ni uti wa mgongo wa uchumi wetu hasa tunakoelekea kwenye siasa ya kujenga viwanda. Viwanda vinategemea sana kilimo kama rasilimali kubwa. Hivyo ni vyema Wizara ikazingatia suala la wakulima. Aidha,

wananchi wa maeneo husika wewe wanapewa uhuru wa kuzungumza na kutoa maoni yao badala ya kushirikishwa kwenye mahudhurio tu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kuendelea na shughuli za Bunge letu. Nawatachia Waislam wote heri ya mwezi Mtukufu wa Ramadhanii.

Mheshimiwa Spika, *operation tokomeza* na wafugaji/wakulima. Kama kuna wakati Serikali ilikosea ilikuwa ni katika kipindi cha *operation tokomeza*, kwa kuwa ulifanyika ukatili na unyama wa kutisha kwani wanyama katika hifadhi walikuwa na thamani zaidi ya binadamu na mapori tengefu nayo pia yalkuwa na thamani kuliko mifugo na binadamu katika maeneo yaliyo karibu na mapori hayo. Cha kushangaza, hawa wananchi walikuwa toka enzi za kabla na baada ya ukoloni ndio waliokuwa walinzi na rafiki wa wanyama, kwa mfano, Wamasai, Wahadzabe na Wasandawe.

Mheshimiwa Spika, Serikali badala ya kuwaelimisha ili wajue faida zipatikanazo na utalii, Serikali inawatumia askari wa wanyamapor (game rangers) kuwapiga, kuwatesa na hata kuwaua kwa risasi kwa kisingizio cha uvamizi wa hifadhi na mapori tengefu, lakini pia wawindaji haramu. Hii si sawa na ni kinyume cha haki za binadamu. Ni vyema Serikali ikatoa elimu na kuwashirikisha wananchi wa maeneo yaliyo karibu na hifadhi, mapori tengefu na mbuga zetu ili wajue kwamba mbuga za Serikali ni mali yao na wajulishwe faida zinazopatikana kutokana na utalii.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi katika mbuga/ hifadhi na wakulima; migogoro haitaisha katika mbuga na hifadhi kwa kuwa watu wetu (wakulima na wafugaji) hawapangiwi mipango shirikishi ambayo ingeweza kugawa maeneo machache ya kulisha mifugo na maeneo mengine yabaki kuwa ya hifadhi. Ukipatikana ushirikiano wa pamoja

ungeleta mafanikio kwani hifadhi/mbuga na mapori tengefu ni mali ya Watanzania, ni mali yetu. Tabia ya kuwanyang'anya ng'ombe iachwe.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali; watu huongezeka, ardhi haikui; Serikali ijue wazi wananchi wakiamua kugoma watalii wasipite katika miji yao, wakiamua kufanya hujuma dhidi ya utalii, hakutakuwa na utalii. Hivyo ni vyema Serikali ikawapa elimu na ushirikiano na iache kuwafanya ukatili wakulima na wafugaji ili Wizara hii iendelee kuwa chanzo cha mapato ya Serikali ambayo ni 17.6% Pato la Taifa (*GDP*) = *USD 2.3 billion per year*.

Mheshimiwa Spika, unyang'anyi unaofanywa na *game rangers* katika utalii kwa Watanzania (wakulima/ wafugaji) kuwapiga ng'ombe mnada kisha fedha inayopatikana ni shillingi ngapi, iko wapi na inafanya nini? Je, hii ndiyo Serikali ya wanyonge au ni Serikali ya kuwaonea wanyonge?

Mheshimiwa Spika, wosia wangu kwa Serikali, rasilimali tulizonazo tumezipata kwa mapenzi yake Mwenyezi Mungu, lakini badala ya kuwaneemesha Watanzania imekuwa ni NAKAMA, hivyo Serikali iijitathmini, ishirikishe wananchi zaidi, badala ya wageni.

Mheshimiwa Spika, utalii kimataifa (*cultural tourism*) (Sukuma, Makonde, Ngoni, Bondei, Digo). Zipo kabilo katika nchi yetu, ni utalii kwa kutumia mavazi yao (Wamasai), ngoma mbalimbali, taarab (Zanzibar) pamoja na picha za kuchora. Vyote hivi wanapokuja watalii wa nje huzinunua na kuzifurahia, lakini tuijulize makabilo haya yananufaika vipi kutokana na utalii? Hawanufaiki zaidi ya mifugo yao na wao wenyewe kupigwa na kufungwa magerezani.

Mheshimiwa Spika, matangazo kimataifa; yapo matangazo katika ligi ya Uingereza (*England Premier League*) peke yake ambayo hayakidhi haja, ni vyema tungkuwa na matangazo katika Bundesliga (German) Laliga (Spain), *Series A (Italy)*, *French-League* na kadhalika. Pia *CNN, BBC, Sky News*,

Reuters, DW – Deutsche Welle, Aljazeera, kote tutangaze nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hata katika *World Weather Condition* Tanzania majiji yetu hayaonekani, tunaona tu Cape Town, Johannesburg, Cairo, Kampala, Kigali, Nairobi, Bujumbura lakini huoni Dar es Salaam, Arusha, Tanga, Mbeya na Mwanza, kwa nini?

Mheshimiwa Spika, utalii wa bahari (*ocean tourism*), Tanzania tumejaaliwa ufukwe wa bahari wenye urefu wa kilometa 1,425 kutoka Jasini – Mkinga (Tanga) hadi Msimbati (Mtwara) lakini tunapata mapato kidogo ukilinganisha na mapato ya Kenya ambao ufukwe wao hauzidi kilometa 180 kutoka Mombasa – Vanga (Kenya). Tujiulize tunakwamia wapi?

Mheshimiwa Spika, *fishing tourism & surfing*; upo utalii wa kuvua samaki wakubwa na kuogelea kwa vidani pamoja na mashindano ya ngalawa (*boat*). Mashindano haya yanafanyika katika nchi za Dubai, Mozambique, Kenya, South Africa, kwa nini Tanzania tusifanye ambapo watalii wanapokuja wanakaa kwenye *hotels* na wanatumia huduma mbalimbali zinazotolewa na wenyeji, hii ni ajira, lakini tunashindwa kuweka vivutio (*attractions*).

Mheshimiwa Spika, VAT na tozo nyingi katika utalii Tanzania; Tanzania tumejaliwa mbuga, mapori, mito, maziwa, vijito na bahari; vyote hivi vipo na Mwenyezi Mungu ametaka tuvitunze na tuvitumie vizuri, vinahitajika vitupatie pia manufaa kwa Serikali na wananchi. Katika nchi sita za Afrika Mashariki, Tanzania ni ya kwanza kwa kuwa na vivutio vingi vya kitalii, lakini kimapato, kimipango, kitaratibu na mazingira tunashindwa na nchi jirani zetu. Hata kwa watalii wengi kuja katika mbuga tunashindwa. Tunazo mbuga ambazo ni *unique*. Kwa mfano mbuga ya Saadani (*Saadani National Park*) ni mbuga pekee inayopakana na bahari na watalii wanapenda kuja kuitembelea lakini kodi zimezidi mno. Kwa mfano VAT, Kenya imeondolewa hali ambayo imekuwa ni kivutio kwa watalii kwenda Kenya zaidi kwa

kuwa gharama ni nafuu. Hivyo na Tanzania tuondoe VAT/ kodi lukuki

Mheshimiwa Spika, maliasili za misitu, katika nchi zote za SADC ni Tanzania pekee ndiyo pembezoni mwa barabara kumekuwa na magunia ya mkaa na kuni ambayo ni biashara iliyoshamiri.

Mheshimiwa Spika, kwa nini biashara hii imeshamiri? Ni kwa sababu Tanzania ndiyo nchi ambayo umeme na gesi ni bei ghali kuliko nchi zote duniani. Kama tunavyojuza asilimia 75 ya Watanzania ni wakazi wa vijiji (wakulima na wafugaji). Je, hivi wakulima na wafugaji wanawenza kumudu kununua umeme wa luku na gesi kwa ajili ya kupikia?

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali ipunguze bei ya umeme, iondoe VAT na pia londoe utitiri wa kodi, kuokoa muda na kuvutia watalii na pia kuwanufaisha Watanzania katika maisha yao ya kila siku.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Spika, ni kwa muda mrefu sasa Mikindani Mtwara kuna majengo mengi ya kale ambayo yangeweza kuvutia sana utalii Mtwara na Kusini kwa ujumla wake. Mtwara kwa kushirikiana na *Trade Aid - Shirika la Charity* kutoka Uingereza tuliweka Siku ya Mikindani ili kuutangaza rasmi Mji wa Mikindani kuwa ni mji wa utalii Tanzania na hasa katika sekta ya mali kale.

Mheshimiwa Spika, tulipanga kila kituo lakini Wizara kwa nini inasuasua kulifanya hili kwa maendeleo ya Mtwara, Kusini na nchi kwa ujumla wake? Naomba Wizara ituambie Wana Mtwara Mikindani lini watazindua Siku ya Mikindani ili kuutangaza utalii?

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha za *Regrow*; kuna fedha zaidi ya shilingi bilioni mbili za kuendeleza utalii kusini. Fedha hizi zimepelekwa Morogoro, Iringa ambako sio Kusini, Kusini kijirografia na kiutawala ni Mtwara na Lindi pamoja na Ruvuma. Mikoa hii imesahaulika sana pamoja na kuwa

vivutio vingi nya kiutalii kwa nini fedha za *Regrow Kusini* zipelekwe maeneo mengine badala ya Kusini halisi?

Mheshimiwa Spika, kwa nini kila kinachopangwa Kusini kinahamishwa? Tatizo ni nini? Fedha za *Regrow* ziletwe Kusini Mtwara na Lindi ili ziendeleze Mikindani, Fukwe na Kilwa pamoja na Mbuga ya Selous upande wa Kusini.

Mheshimiwa Spika, *Olduvai Gorge* irudishiwe mali zake, hii ni mara yangu ya tatu naongelea hili. Eneo hili la mali kale lilikuwa linaingiza fedha sana kabla halijahamishwa kwa maslahi binafsi na kupelekwa Hifadhi ya Ngorongoro ambalo ni Shirika la Umma. Hivi sasa *Olduvai Gorge* inaingiza fedha ndogo sana kuliko wakati ikiwa mambo kale. Kama lengo ni kuongeza mapato, basi *Olduvai Gorge* irudishwe kwenye Idara ya Mambo Kale na si Ngorongoro.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, leo naomba mchango kwenye Wizara hii kwa kujadili namna ya migogoro ya mipaka kati ya hifadhi na vijiji vinavyozunguka hifadhi zetu kwani migogoro hii imedumu kwa muda mrefu na kurudisha nyuma hali ya mahusiano ya wahifadhi na wananchi pia hata na Serikali kwa ujumla. Kwa mfano katika Wilaya ya Liwale kuna mgogoro mkubwa na wa muda mrefu kati ya Hifadhi ya Selous na Kijiji cha Kikulyungu. Hadi sasa mgogoro huu umegharimu maisha ya watu wake katika kijiji hicho. Ni muda mrefu sasa mgogoro huu haujapewa kipaumbele licha ya kugharimu maisha ya watu.

Mheshimiwa Spika, unapozungumza juu ya malikale utakuwa unafanya dhambi kama ukiacha kumbukumbu zilizoachwa wakati wa Vita ya Maji Maji na utawala wa Wajerumani hapa nchini. Wizara bado ina kazi ngumu na muhimu sana ya kutambua majengo na alama mbalimbali za malikale kwa faida ya utalii na urithi wa nchi yetu kwa majengo mengi nchini yamesahauliwa hivyo kupoteza historia ya nchi yetu. Kwa mfano katika Wilaya ya Liwale kuna Boma la Mjerumani, boma hili lina kumbukumbu nzuri na nyingi sana hasa ya Vita ya Maji Maji. Mawe ya kujengea

jengo hili yametoka Wilayani Kilwa, zaidi ya kilometra 250 kutoka Liwale, mawe hayo yalibebwa na watumwa.

Mheshimiwa Spika, kuna mabaki na picha za mashujaa na watawala wa Kijerumani waliotawala Ukanda wa Kusini. Kama haitoshi vilevile kuna kumbukumbu ya Mfaransa inayojulikana kama Mikukuyumbu, hapa ndipo mzungu wa kwanza kuingia Liwale aliuawa na mtu ajulikanaye kama Mchimae. Huyu ni mzungu ajulikanaye kama (Mfaransa). Kumbukumbu zote hizo zimesahauliwa sana.

Mheshimiwa Spika, Pori la Akiba la Selous kwa upande wa Ukanda wa Kusini hauna lango la utalii wa picha kwani kuna utalii wa uwindaji tu, jambo hili linakosesha mapato katika ukanda huo na watu wa ukanda huo kukosa kuona falda ya kuwepo kwa Selous Ukanda wa Liwale. Tunahitaji lango la utalii wa picha ili kuongeza ajira na mapato ya Halmashauri yetu ya Liwale.

Mheshimiwa Spika, hadi leo Liwale zaidi ya kushambuliwa na tembo na wanyama wakali hakuna faida ya moja kwa moja kwa wananchi kwa kukosa lango la utalii wa picha. Hivyo, kukosa wawekezaji wa mahoteli na miundombinu mingine ya kiutalii.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zinazopakana na hifadhi zinatakiwa kupata asilimia 25 ya mapato ya hifadhi husika. Naomba Wizara kuititia upya sheria hii kwani kiasi hiki ni kidogo sana kwa sasa, ni bora kiasi hiki kikaongezwa kufikia asilimia 30. Vilevile fedha hizi zinachelewa sana kufika kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu malipo ya kifuta machozi na fidia ya uharibifu wa wanyama pori, fedha hizi licha ya kuwa ni kiasi kidogo lakini hata utaratibu wa upatikanaji wake bado hauko wazi, haueleweki kwa watu wetu jambo linalofanya watu wetu kutopata fidia yoyote licha ya wengine kupata vilema na mashamba yao kuliwa na wanyama kama tembo, nyati na kadhalika. Malipo ya kifuta machozi ni kama

danganya toto kwani walio wengi hawapati. Kwa mfano Halmashauri ya Liwale ina muda mrefu sasa watu hawajawahi kupata malipo haya licha ya kuwa na madai ya muda mrefu zaidi ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ipitie upya sheria ya *TFS* kwani wakala huyu anavuna mazao ya misitu ya vijiji hata ile ya *open area* kiasi kinachokibaki kwenye Halmashauri ni kidogo sana. Misitu inakwisha lakini Halmashauri inakosa mapato ya moja kwa moja kutoka *TFS* jambo linaloleta mahusiano ya mabaya katika *TFS* na wananchi wa kawaida kwani hakuna faida ya moja kwa moja kutokana na uvunaji huu wa *TFS*. Kwa mfano katika Wilaya ya Liwale mahusiano ya *TFS* na wananchi si mazuri kutokana na watu wetu kutoona manufaa ya moja kwa moja kutoka kwenye taasisi hii.

MHE. USSI SALUM PONDEZA AMJADI: Mheshimiwa Spika, kwanza naanza kwa kumshukuru Mungu kutujalia uhai na afya njema na hivyo kuweza kuhudhuria vikao vinavyoendelea vya Bunge letu hili.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayofanya yeye na mtaalam wake, kwa jinsi wanavyofanya vizuri kwa muda aliokaa, kuna mambo mengi mazuri ambayo ameyafanya.

Mheshimiwa Spika, nampongeza kwa kanuni mpya alizozitunga kwa Wizara, zimeifanya Wizara yake ioneckane jinsi gani inafanya kazi kwa maslahi mapana ya wanyonge. Nampongeza pia Mheshimiwa Waziri kwa kuanzisha (*Tourism One Stop Centre*) ambalo limejengwa jengo la mamlaka katika Mji wa Arusha.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa programu ya ujirani mwema kwa kuchangia miradi ya vijiji zaidi ya 30 vinavyozunguka hifadhi kwa kuwachimbia visima, zahanati, vyumba vya madarasa na mambo mengine. Changamoto pia haziko kuhusu mifugo inayoingia kwenye hifadhi, adhabu zake ni kweli zinahitaji kuboreshwa zaidi kwani utaratibu uliopo haukidhi kwani haijaka vyema.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, wanyama wanaoingia utaratibu ungekuwa Wizara kutoa mwongozo wa kuwa wale ambao mifugo yao imeingia kwenye hifadhi basi wao ndio wapewe kipaumbele ili kuondoa dhana ya rushwa kwenye zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, mwisho nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wao jinsi wanavyofanya kazi vizuri.

MHE. SILAFU J. MAUFI: Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza kwa kazi nzito waifanyao Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na baadhi ya wataalam wafanyao kazi kwa weledi na kwa maslahi kwa nchi yetu. Wizara hii inatoa pato au inachangia kwa asilimia ya kutosha kwenye pato la Taifa. Kama miundombinu yake ikiboreshewa ipasavyo na kwa kukubali maoni, ushauri wa Wabunge na Kamati husika ni dhahiri pato la Taifa litaongezeka hadi asilimia 10 -15.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imekuwa na upungufu wa watumishi wenyе mafundisho sahihi kwa kada mbalimbali za kutoa huduma kwa watalii na wabunifu wa shughuli kadhaa za kuwavutia watalii kwenye maeneo yetu kuzingatia mazingira yetu. Vyuo vya Utalii kuongezeka kwa idadi ya usaili na miundombinu ya kuikabili hali na mahitaji ya wataalam. Mitaala iendane na mahitaji ya kuwa na utalii endelevu uendao na wakati wa maendeleo ya utalii ulimwenguni.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kwamba eneo kubwa la utalii linahitajika ulinzi na usalama kwa wageni na nchi kwa ujumla wake, ni vyema usaili wa watumishi wa Wizara hii watokane na vijana wa JKT pia.

Mheshimiwa Spika, bado Serikali haijasambaza nishati mbadala kwa matumizi ya wananchi wetu kwa huduma mbadala ya nishati ya kuni na mkaa. Ni vema Wizara ikajikita katika kuhakikisha tunapata umeme wa kutosha na gesi na kupelekeea gharama yake kuwa rafiki kwetu na wananchi

kuelimika na kuikubali hali ya matumizi hayo kutapunguza uharibifu wa misitu yetu.

Mheshimiwa Spika, wakati huu tunalazimika pia kuangalia tozo zitolewazo kwa wajasiriamali wa uuzaaji wa mkaa mpaka afikishapo mjini kutoka vijijini ni kubwa ukichanganya na changamoto azipatazo katika kuupata mkaa na kuusafirisha.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya watumshi wakusanyao maduhuli ya misitu vijijini si waaminifu, ni bora uwepo utaratibu wa kutumia mashine za kieletroniki, kudhibiti makusanyo hayo kwa kuwapa malengo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tumekubaliana kuendeleza utalii Nyanda za Juu Kusini, tunaomba Wizara kuwa na utaratibu wa awali kabisa kuimarisha miundombinu (barabara) inayoelekea kwenye maeneo ya vivutio vilivyobainishwa kwenye maeneo yetu, naomba ushauri kuzingatiwa. Kwa mfano barabara inayoelekea *Kalambo Falls* – Rukwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Waziri pamoja na timu yake kwa kazi kubwa wanayoifanya. Suala zima la upandaji miti katika maeneo yetu yaliyo wazi pamoja na maeneo yaliyoungua. Niishauri Serikali yangu kuwa na mpango mkakati wa kuhakikisha miti inapandwa kwa wingi na si kupanda tu pamoja na kuitunza mpaka ikue pamoja na kuwapa miche bure. Pia kuna misitu iliyoungua katika maeneo mbalimbali ya nchi ikiwemo Lushoto.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali ikapande miti katika maeneo hayo hasa Lushoto katika Misitu ya Magamba, Shume, Gara, Irente; maeneo yote yameungua tangu mwaka 2004 mpaka sasa kumeota tu majani bila miti. Kwa hiyo maeneo haya ni muhimu sana yarudishiwe miti ya asili ili kurudisha mandhari na uoto wa asili uliopotea. Wananchi

wa Lushoto wapo tayari kupanda miti isipokuwa hawana uwezo wa kununua miche hiyo. Hivyo basi niiombe Serikali itenye mafungu ya kununua miche ya miti ili kuwapa wananchi hao.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la kuungua kwa misitu hii inatokea kila wakati lakini uzimaji wa moto unategemea wananchi. Kwa hiyo, niiombe Serikali inunue ma-*grader* ili yakachimbe barabara maeneo ya msituni ili janga la moto linapotokea iwe rahisi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, katika zao la misitu kuna tozo zaidi ya 32. Tozo hizi zimewaathiri sana wafanyabiashara kiasi kwamba mpaka sasa mgao wanaopewa umesimama kwa sababu gharama zenyewe zimepanda, ambapo kwa *square meter* 100 ni shilingi 10,000,000 tofauti na mwaka 2016 – 2017 illikuwa *square meter* shilingi 6,000,000 ukichanganya na hizo tozo gharama inakuwa kubwa sana ambayo haiendani na bei ya soko.

Mheshimiwa Spika, niishauri Serikali, zao la misitu ni sawa na mazao mengine, kwa hiyo tozo hizi zipungue kama mazao mengine ya kahawa, pamba, korosho na tumbaku kwa sababu hii imesababisha wafanyabiashara hao kununua miti kwa watu binafsi kwani huko bei ni nzuri. Changamoto yake ni kwamba wanaauza miti ambayo haijakomaa na hii itasababisha nyumba zetu hatimaye kwenda na upemo maana mbaao zilizoezekea si imara.

Mheshimiwa Spika, niishukuru Serikali kwa kuziacha hizi mashine ndogo za kuchania mbaao ziendelee mpaka hapo zitakapoisha zenyewe. Hivyo basi nikuombe Waziri wetu utakaposimama na kujibu hoja naomba hili ulisemee kwani kuna watu wengine wamezisimamisha na kazi zao kusimama. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri naomba tamko juu ya hili. Mashine hizo zinaitwa Dindon.

Mheshimiwa Spika, pia wafanyabiashara hao wana *group* lao la *LMDA*, hili linatoa pesa kwa ajili ya kupanda miti lakini cha kushangaza mchango huu hautambuliwi.

Wadau hawa ni watu muhimu na wanastahili kupunguziwa pamoja na kuwaangalia kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, niunge mkono ushauri wa Kamati kuhusu kuweka miundombinu ya barabara katika mapori ya Biharamulo, Burigi na Kimisi pamoja na vifaa vyakazi, magari, wafanyakazi pamoja na nyumba za wafanyakazi bila kusahau kuweka mazingira mazuri kwa ujumla ili kuweza kuvutia watalii wetu watakaokuja. Hivyo basi niishauri Serikali iharakishe kazi hii ili Serikali iweze kuongeza pato la Taifa kuititia mapori hayo. Pia imekuwa ni jambo la furaha sana na la kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kujenga Uwanja wa Ndege wa Chato, uwanja huu utakuwa umepandisha hadhi mapori haya matatu, Mwenyezi Mungu ambariki sana Rais wetu kwani kazi anayoifanya ya kuwatumikia Watanzania inaonekana dhahiri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Mungu ibariki Tanzania, Mungu mbariki Rais wetu pamoja na Watanzania wote. Amen

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, uhifadhi wa Ziwa Manyara; ziwa hili ni mionganini mwa maeneo ya utalii hapa nchini kwa watalii wengi kutembelea. Hata hivyo, ziwa hili lipo kwenye hatari ya kupotea/kutoweka kutokana na tope lililojaaa ziwani kunakosababishwa na shughuli za kilimo katika maeneo yanayozunguka ziwa. Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka kuokoa Ziwa Manyara ambalo ni kivutio cha utalii hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, kuhusu tozo nydingi katika hoteli za kitalii; tunapohitaji sekta ya utalii iendelee kukua na kuongeza pato la Taifa ni muhimu na ni lazima kuhakikisha kunakuwa na mazingira mazuri na rafiki kwa wawekezaji katika sekta hii ya utalii. Hoteli za kitalii zimekuwa zikilipa tozo nydingi sana hivyo kufanya hoteli hizi kuwa na mazingira magumu kuendesha biashara.

Ushauri, Serikali itazame kwa upya tozo hizi ili kuendelea kuwajengea mazingira mazuri wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, *TALA* ni leseni inayotolewa kwa makampuni ili waweze kuendesha shughuli za utalii. Hata hivyo leseni hii imekuwa ikilipwa na/au kutolewa kwa mtu akiwa na magari matatu kwa kulipa dola 2,000. Hata hivyo, mtu akiwa na magari zaidi ya matatu analazimika kulipa sawa na mwenye magari matatu (kwa kuwa ni takwa la kisheria). Hivyo basi, mtu akiwa na magari 50 au 100 atalipa sawa na mwenye magari matatu. Hapa hakuna usawa na ni unyonyaji kwa watu na kuendelea kuweka mazingira magumu kwa vijana wanaotaka kujajiri.

Mheshimiwa Spika, ushauri, Serikali itoze leseni hii kwa kila gari, kwa kufanya hivi Serikali itaongeza mapato na kutawapa vijana nafasi/fursa ya kuingia katika sekta ya utalii na kujajiri.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ningependa kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa kazi kubwa mnayoifanya hususan katika sekta ya utalii. Nashauri mtumie vizuri ndege hizi ambazo zinakuja/zilizonunuliwa na Serikali kuongeza idadi ya watalii. Aidha, utumiaji wa *Tour Operators* zilizopo (ama zianzishwe) nje ya nchi ni muhimu zitumike.

Mheshimiwa Spika, eneo la Amani – Muheza ambalo Waheshimiwa Mawaziri wote mmefika ni eneo zuri ambalo linaweza kuwa kivutio kizuri kwa watalii. Naomba uliboreshe, kuna miti mirefu kuliko sehemu nyngi duniani, majoka makubwa, maua na kadhalika, kuna vipepeo ambao ni vivutio na pia ni biashara kwa wanakijiji wa Fanusi – Amani, ambao wanapeleka vipepeo hao nje kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo tangu Serikali ipige marufuku usafrishaji wa wanyama hai nje ya nchi wananchi wa Fanusi wameathirika. Mheshimiwa Waziri uliahidi kuboresha mazingara ya utunzaji wa vipepeo hao lakini bado wakala wa misitu amesahau naomba kukumbushia.

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa watu 1,028 wa Derema bado haujamalizika. Tumeanza kuwapatia maeneo kwa kushirikiana na Wakala wa Misitu lakini bado kuna suala la upungufu wa fidia zao. Tumeongea jana na Naibu Waziri na Katibu Mkuu na naomba ulishughulikie.

Mheshimiwa Spika, miti ya tiki ambayo inalimwa Lunguza – Muheza bado tatizo la kuruhusu wakazi wa Muheza au wanunuvi kuwa na uwezo wa kushindana nadhani halijatatuliwa. Tunaomba utaratibu wa zamani (kwa maboresho kidogo) mgao wa wananchi urudishwe na waweze kupatiwa fursa ya kufunga viwanda vidogo vidogo hapo hapo Muheza badala ya matajiri wachache kununua vitalu vyote na kutoa miti hiyo nje ya Muheza.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo lingine kubwa dhidi ya Maafisa Misitu la utoaji wa vibali vya kukata miti hovyo. Kwa mfano Afisa Misitu wa Muheza juzi Baraza la Madiwani limearifiwa kukatwa mivule 100 nje ya utaratibu. Sasa pamoja na wazo la kuanzishwa Mamlaka ya Misitu lakini Maafisa Misitu pia wangehamishiwa chini ya Katibu Mkuu wa Wizara.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikupongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa unayoifanya ya kulinda maliasili ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie juu ya utalii wa Ukanda wa Magharabi, Mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma. Eneo hili la ukanda huu Serikali haijawekeza kabisa ambaa una vivutio vingi vya utalii. Mkoaa wa Rukwa kuna maporomoko ya Kalambo na Ziwa Rukwa na misitu mizuri ya kuvutia. Mkoaa wa Katavi una mbuga nzuri ya *Katavi National Park*, mbuga ambayo ina wanyama wakubwa wenye afya njema na ndiyo mbuga pekee yenye twiga mweupe anayepatikana Katavi peke yake.

Mheshimiwa Spika, tunaomba mbuga hii muitangaze sambamba na kuweka miundombinu ya maji ili kunusuru wanyama wanokufa kwa kukosa maji wakati wa kiangazi Mto Katuma unapokauka.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kigoma kuna mbuga ya Mahale jirani na Mkoa wa Katavi na Hifadhi ya Gombe. Mheshimiwa Waziri tunaomba ukanda huu utengwe kwa ajili ya utalii. Sambamba na hilo kuna fukwe nzuri ya Ziwa Tanganyika ambako watalii wengi wa kutoka nchi ya Israel wangependa sana kufanya utalii wa boti ndani ya Ziwa Tanganyika. Tatizo kubwa bado miundombinu ya kuvutia watalii haijawekwa. Tunaomba Wizara yako muweke mikakati ya kuwekeza katika kuweka miundombinu zikiwemo ununuzi wa boti ya kisasa na kushawishi wawekezaji wa kujenga hoteli za kisasa.

Mheshimiwa Spika, nitoe shukrani za dhati kwako wewe Mheshimiwa Waziri kwa kuidhinisha Pori la Tongwe Magharibi kumilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika. Mheshimiwa Waziri Wana Tanganyika wanakuombea kwa Mwenyezi Mungu akuongoze vyema katika majukumu yako ya Wizara. Pia nakupongeza na kukushukuru sana kwa kutupatia gari ya doria Wilaya ya Tanganyika. Tunaahidi tutalifanya kazi na kulitunza kwa ajili ya uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ZAINABU N. MWAMWINDI: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingu wa rehema aliye niwezesha kusimama na kuweza kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Maliasili na Utalii, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Naunga mkono maoni na ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, ili tuwe na utalii endelevu lazima tutunze vivutio vyetu. Mkoa wa Iringa ndio kitovu cha utalii katika Nyanda za Juu Kusini. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuendeleza utalii kwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Spika, ninatambua mchango mkubwa wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kwa nchi yetu. Hifadhi ya Ruaha inayopakana na vijiji 21 vinavyofaidika na uhifadhi kuititia Mbomipa. Pamoja na hayo kuna vijiji ambavyo bado ni maskini sana na ndivyo vinavyotumika kwenye ujangili wa wanyamaporii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Rais amekubali kutujengea barabara kwa kiwango cha lami itokayo Iringa kwenda Hifadhi ya Taifa ya Ruaha yenye urefu wa kilometra 130, ninaomba kuishauri Serikali kuititia Wizara hii wawe wanatoa elimu ya ujirani mwema, wasaidie kutoa elimu ya ujasiriamali kama ilivyo Hifadhi za Manyara na Ngorongoro ili kuweza kutengeneza soko la bidhaa za asili kwa kuwatengea eneo ili wageni wanapopita kuelekea hifadhi waweze kusimama na kununua bidhaa na wananchi hawa watafaidika moja kwa moja na kuwapunguzia umasikini.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie makumbusho ya Chifu Mkwawa ambayo yameachwa kwa muda mrefu na hivyo kuendelea kupoteza mapato ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kuona umuhimu wa kutembelea makumbusho ya Chifu Mkwawa. Ninaomba yaweze kuendelezwa ili wageni wanaopata nafasi ya kupumzika Iringa Mjini wapate fursa ya kutembelea makumbusho yetu na kuongeza kipato kwa Taifa na pia kuwanufaisha wananchi wa Kalenga.

Mheshimiwa Spika, naomba pia Serikali imalize mgogoro uliopo kati ya familia ya Mkwawa kuhodhi Makumbusho haya ya Taifa.

Mheshimiwa Spika nashukuru, naunga mkono hoja, naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Spika, takribani asilimia 90 ya Watanzania hutumia nishati ya kuni

na mkaa kwa matumizi ya nyumbani, hali hii huleta uharibifu mkubwa wa misitu nchini. Inasemekana kwa wastani hekta 400,000 hupotea kila mwaka. Ni kwa nini Wizara hii isishirikiane na Wizara ya Nishati ili kuja na mikakati mahsusni ya kutumia nishati mbadala nje ya mazao ya misitu?

Mheshimiwa Spika, *TFS* imekuwa ikitoa leseni za kuvuna bidhaa za misitu ya kwenye ardhi ya kijiji bila kushauriana na mamlaka husika ya kijiji. *TFS* imekuwa ikikusanya tozo (*collecting revenues*) kwenye bidhaa za misitu zilizovunwa kinyume cha sheria, ikiwa ni pamoja na mkaa na mbao na kujiongezea mapato. Pia kuna malalamiko kuwa *TFS* haina ushirikiano mzuri na jamii zinazojishughulisha na hifadhi za misitu (*community forestry management*) na kuwachukulia kama washindani, hali hii pia hujitokeza kwa kukwamisha harakati za *CSOs* na *NGOs*.

Mheshimiwa Spika, ripoti ya *NARFOMA* inaonesha kuna jumla ya hekta milioni 48 za misitu wakati idadi ya watu ni trakribani milioni 50. Kwa hiyo bila usimamizi sahihi wa misitu tutaangamia. Kuna haja ya kuwa na mipango sahihi ya kuangalia, kwa mfano matumizi ya *biomass energy*, mikaa bado ni changamoto. Mashaka haya yanabidi kushughulikiwa ikiambatana na marekebisho ya Sera ya Taifa ya Uwekezaji katika misitu inapaswa kukuzwa kwa kuzingatia vigezo vya utunzaji/uvunaji endelevu (*sustainable harvesting*) ili ku-address economic, environmental and social issues.

Mheshimiwa Spika, kuna *alternatives* nydingi nchini za vyanzo vya umeme ambavyo havina madhara makubwa sana katika ekolojia ya maeneo husika pamoja na jamii inayoitegemea, sasa basi, ni kwa nini Serikali inang'ang'ania kutumia *Stiegler's Gauge* ilhalii itasababisha madhara makubwa kwa rasilimali maji, maliasili na shughuli za kiuchumi? *Rufiji Basin Hydropower Master Plan* imeainisha maeneo mengine yenye uwezo wa kutoa umeme kama Kihansi, Ruhudji, Mnyera na Kilombero.

Mheshimiwa Spika, ukataji wa miti zaidi ya $1,430 \text{ km}^2$ ni janga kubwa kwa Taifa, hasa kwa maeneo ya Kusini

(Selous), Rufiji Delta na kadhalika katika maandalizi ya mradi huu wa *Stieglers*.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana endapo itazingatia ushauri wa Kamati, hususani katika suala la kutatua migogoro iliyopo kati ya wananchi na Hifadhi za Taifa (mipaka).

Mheshimiwa Spika, ni lini mtakuja Katavi kufuatilia na kutatua migogoro iliyowaathiri Wana Katavi hususani katika Kata za Isengule, Ikola, Kapala Msenga kijiji cha Lyamgoloka Jimbo la Mpanda Vijijini (Ikuba). Wananchi walipigwa na askari wa wanyamapori tangu 2004 mpaka sasa wananchi wanaishi kwa hofu, wanauawa kwa kupigwa risasi. Hivi karibuni kuna vijana wameuawa kwa kupigwa risasi.

Mheshimiwa Spika, akina mama wanabakwa, wananyang'anya mali zao, je, Mheshimiwa Waziri ni sheria ipi inayoruhusu unyanyasaji huu kuendelea kutokea na Serikali hii inakaa kimya? Je, Serikali inasemaje kuhusu ukatili huu? Ni utaratibu gani unatumika kupima mipaka? Je, wananchi wanaingia ndani ya hifadhi au hifadhi inaongeza maeneo kwa kuwanyang'anya maeneo yao? Ni lini mtawalipa fidia kwa kuchukua maeneo yao bila utaratibu wa sheria?

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa mpaka kati ya Stalike na hifadhi mpaka sasa wananchi hawa ni lini watarudishiwa maeneo yao? Wananchi wa kata hii wameshindwa kufanya shughuli za kiuchumi kulima na kutumia maji ya mito inayowazunguka. Je, ni lini jambo hili litaisha ili wananchi wafanye shughuli zao za kiuchumi?

Mheshimiwa Spika, kupigwa risasi ng'ombe/wafugaji; wafugaji wengi hawana elimu ya mipaka, makazi na hifadhi ni kwa nini elimu haitolewi kwa vijiji/vitongoji? Serikali ina kazi gani? Serikali kushindwa kuweka mipaka kumepelekeea wafugaji kuendelea kunyanyasika katika Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, sheria inasemaje kuhusu mauaji ya wafugaji na ng'ombe kupigwa risasi hovyo katika Kata

za Ikuba, Majimoto, Luhagwe? Je, Serikali inasaidiaje tatizo hili la kitendo cha *TANAPA* kuvunja sheria kwa kuweka mipaka iliyo kinyume na *GN*.

Mheshimiwa Spika, suala la wafugaji kulipishwa faini na watendaji/askari wa wanyama pori ng'ombe mmoja inalipishwa shilingi milioni moja ikiingia hifadhi au mfugaji kupigwa risasi, Je, sheria ya haki za binadamu Wizara hii mbona iko kimya kuhusu unyama huu?

Mheshimiwa Spika, risiti *fake wanazolipishwa* wafugaji wetu je, Wizara inachukua hatua gani kuhusu tatizo hili? Ajira kupitia wawezeshaji hoteli zilizopo ndani ya hifadhi, Mkoa wa Katavi haunufaiki kwa wazawa kupata ajira mbugani, je, Serikali haioni ni tatizo?

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja kwa njia ya maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la *GN* kutokutambulika katika hifadhi nyingi nchini inaongeza migogoro isiyo ya lazima kati ya wananchi na hifadhi, utatuzi wa haraka unahitajika. Wahifadhi/askari wanyamapori wanatumia *GN* kama fursa ya kuwaumiza wananchi kwa kigezo kwamba wameingia kwenye hifadhi na kuwalipisha faini zilizo onevu.

Mheshimiwa Spika, bado Wizara haijaweka dhamira ya dhati kwa kuimarisha utalii wa fukwe hapa nchini kama ilivyo nchi za Mauritania/Morocco na nchi nyingine. Hapa nchini fukwe zetu kama *Coco Beach* ambazo zinatumika kuuza mihogo kwa nini Wizara isiziboreshe kwa kujenga hoteli za kitalii, *beach* za kisasa, hasa watalii wanapotua Dar es Salaam wakati wakisubiri kwenda kwenye hifadhi wakapumzika *beach*, wakaongeza mapato badala ya ilivyo sasa kwamba wanabaki hotelini wakisoma vitabu huku wakisubiri kwenda kwenye hifadhi?

Mheshimiwa Spika, malipo kwa wananchi wanaouawa na tembo au wanyama wengine ni kidogo,

ipo haja Sheria ya Fidia kuletwa Bungeni ibadilishwe. Kwa sasa kifuta jasho ni kati ya shilingi 100,000 ni kidogo ikilinganishwa na thamani ya utu/mwanadamu. Tembo akigongwa na gari faini ya *USD 1500* zaidi ya shilingi milioni 30 kwa tembo mmoja, lakini ukilinganisha mtu akiuawa na tembo eti kifuta jasho shilingi 100,000 sio sawa kabisa.

Mheshimiwa Spika, Wami Mbiki ni *potential* kwa hifadhi, wanyama wapo wa kutosha, Sweden imewahi kusaidia hifadhi ile na Mwenyekiti wake ni Rais Mstaafu Mheshimiwa Jakaya Kikwete. Kwa nini Wizara isiendeleze hifadhi hii ambayo ina rasimali za wanyama za kutosheleza? Sasa hivi wananchi wameingia kwenye hifadhi wanalima, wanawinda wanyama na wanakata miti, sasa badala ya hifadhi imegeuka mashamba. Wanyama wanavamia makazi ya wananchi kula mazao kwa sababu hifadhi inakosa sifa. Tunaltaka Serikali kurudisha hifadhi hii kwenye hadhi yake ili kuongeza kipato kwa wananchi wanaozunguka hifadhi hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika Hifadhi ya Mikumi wanyama wanaendelea kuuawa kwa kugongwa na magari. Ulikuwepo mpango wa barabara ya Morogoro – Mikumi ku-*divert* Kilosa mpaka Mji wa Mikumi. Kwa nini mpango huu hautekelezeki?

Mheshimiwa Spika, kuzibwa kwa shoroba; Hifadhi ya Saadani kuitia Wami Mbiki kwenda Mikumi hadi Selous kuna wanyama wanatembea kwa mfano tembo wanatoka Saadani hadi Selous, lakini shoroba zimezibwa. Mbaya zaidi Serikali imejenga majengo ya Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, wameziba shoroba. Vilevile Serikali hiyo imevunja nyumba za wananchi Mtaa wa CCT Mkundi kwa madai kuziba shoroba wakati majengo ya Serikali Wilaya ya Mvomero yapo, hayajavunjwa.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wa Wizara kwa jithada nzuri za kusimamia sekta ya utalii na shughuli zote za Wizara.

Mheshimiwa Spika, ushauri, takwimu za mchango wa sekta kwenye pato la Taifa (17%) na *rate* ya ukuaji ya *number of arrivals* kwa mwaka (3.3%) haziridhishi. Tanzania ina *unique comparative advantage* za kijiografia ambazo bado lazima ziwe *optimized* ipasavyo. Vikwazo ninaviona ni viwili.

Mheshimiwa Spika, kwanza *Benchmark Tax Region* ya sekta ya utalii *against* nchi washindani wetu. *Findings* za *benchmarking* zisaidie Wizara kukaa na Wizara nyingine zinazohusika (mfano Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Ofisi ya Makamu wa Rais) na kujadili kwa pamoja ulazima wa kuboresha *tax region* ya sekta kuongezeka *competitiveness*.

Mheshimiwa Spika, *strategy*, Wizara iache mazoea ya kutegemea *TTB* pekee kufanya *promotion marketing*. Angalia nchi nyingine zilizofanikiwa wametumia *modality* zipi kufanya *promotion and marketing*.

Mheshimiwa Spika, naomba vizingi vilivyowekwa kwenye vijiji vya Mgoruka, Rweizinga zoezi lirudiwe upya na kushirikisha wananchi pamoja na mimi Mbunge ili kuleta ustawi mzuri na ujirani mwema kati ya wananchi wangu na mapori akiba ya Kimisi na Burigi.

Mheshimiwa Spika, kaeni na Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji muangalie namna ya kushirikiana ili kutumia teknolojia ya majiko jadidifu kama mbadala wa utumiaji wa mkaa. Kutumia mabavu kukataza utumiaji mkaa si *sustainable* na ni ishara ya kukosa *innovation* na mikakati ndani ya Serikali.

MHE. YOSEPHER F. KOMBA: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mungu kwa siku hii na nafasi ya kuchangia Wizara hii kwa maslahi ya Watanzania na wananchi wa Tanga. Katika Wilaya ya Muheza, Tarafa ya Amani kuna vivutio vizuri na vya asili vya utalii kama misitu mikubwa, maporomoko ya maji, vipepeo adimu duniani, kima na sokwe wa kipekee lakini pia katika Kata ya Magoroto kuna kivutio kikubwa cha mito na michikichi. Pamoja na vivutio

vyote hivyo bado hakuna jitihada za makusudi kuvitangaza vivutio hivyo ili kuongeza watalii na pato la Taifa. Je, Wizara ina mkakati gani katika kufufua na kuvitangaza vivutio hivyo?

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Tanga na mikoa mingine ya Pwani imekuwa maarufu kwa mchezo wa bao ambaeo ni mchezo wa kipekee kwa jinsi unavyochezwa, na ni mchezo unaounganisha pamoja tamaduni za pwani kwa maana ya mavazi, ustaarabu wa dini hasa Waislamu. Naishauri Wizara iandae mkakati wa kuufanya mchezo huu unaoenzi tamaduni za watu wa Pwani ili uwe kivutio cha watalii wanapotembelea maeneo haya ya Pwani hasa fukwe na mapango kama ya Amboni.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Mamba, Jimbo la Bumbuli viro vijiji vilivyo karibu na Mbuga ya Mkomazi ambaeo wamekuwa wakisumbuliwa na wahifadhi wa *Mkomazi Park* na wamekataliwa kufanya shughuli za maendeleo katika makazi yao ambayo wameishi kwa miaka mingi tangu mababu zao. Je, Wizara ina mkakati gani wa kumaliza tatizo hili la mipaka ili wananchi waweze kuishi kwa amani katika maeneo yao na hifadhi ziendelee kuwa na faida kwa wananchi wanaozunguka hifadhi hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba kupatiwa ufanuzi. Ahsante na nawasilisha.

MHE. PROSPER J. MBENA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa jitihada kubwa anazofanya za kutuletea maendeleo nchini.

Mheshimiwa Spika, sekta ya maliasili na utalii ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu. Ni vyema Serikali ikaweka mipango yake vyema ili kuhakikisha wananchi wote wananaufaika kutohana na maliasili zilizopo nchini.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Morogoro Kusini lina mchango mkubwa katika kulinda na uhifadhi wa maliasili kama vile misitu ya asili, wanyamapori, hifadhi za taifa

hususani *Selous Game Reserve* upande wa Kata ya Kisaki, mito ya maji na kadhalika. Yapo malalamiko makubwa ya baadhi ya wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini ambao kwa masikitiko makubwa mimea yao ya mpunga waliyolima kwenye maeneo ambayo baadae yametambulika kuwa ni ya hifadhi ya Taifa iliharibiwa kwa makusudi. Wananchi hawa waliomba waachiwe ili waweze kuvuna mpunga wao na baada ya hapo wasingelima tena maeneo hayo ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, wakati mwininge wananchi waelekezwe na kuwasaidia wanapokosea. Pia yapo malalamiko ya mifugo ya ng'ombe kuteketezwa na askari wa hifadhi. Yupo mwananchi anayedai ng'ombe wake zaidi ya 200 kuteketezwa. Barua yake ya kukumbushia malalamiko hayo ya tukio lililodaiwa kutokea mwezi Aprili, 2015 nimeletewa nakala yake ambayo nimeikabidhi kwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii hapa Bungeni jana tarehe 21 Mei, 2018. Naomba Mheshimiwa Waziri aweze kushughulikia malalamiko hayo na muhusika ajibiwe ipasavyo, kuendelea kukaa kimya si sahihi.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Morogoro Kusini lina maeneo mengi ya vivutio ambavyo vinaweza kutumika kuvutia watalii. Jiwe lenye umbo la matiti makubwa ya mama kwa lugha ya Kiluguru tunaita Matombo, jiwe hilo ndilo lililopelekea Tarafa nzima iitwe Matombo. Jiwe lile lipo, ninasikia ziwa lake moja limekatwa na mgeni mmoja aliyekuwa anakata mawe. Hii ni sehemu ya utamaduni na utalii, tuhakikishe historia kama hii inatunzwa na kutumika kuvutia watalii.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Bwakila Juu ipo nyumba alioishi chifu wa zamani wa Waluguru. Nyumba ile ingeweza kuwaleta watalii na wenyе kufuatilia historia kuja na kuandika zaidi kuhusu taarifa za maisha ya chifu huyo. Barabara kutoka Bigwa hadi Kisaki ndiyo hiyo inayotumika na watalii kwenda kwenye Hifadhi ya Selous kupitia Morogoro. Miundombinu ya barabara hii si mizuri. Lazima tutambue umuhimu wa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, *TANAPA* ni shirika muhimu katika kukuza na kuendeleza sekta hii ya maliasili na utalii. Misaada ya *TANAPA* kwa Jimbo la Morogoro Kusini bado inahitajika na kwa kweli bado hajjaonekana kwa kiwango cha juu. Eneo lote la Kisaki, Sesenga na kadhalika *TANAPA* ingeweza kusaidia miradi yao ya maendeleo, maji, shule, barabara na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mahusiano kati ya wananchi na askari wa hifadhi sharti yawe mazuri kwa ustawi mzuri wa nchi yetu. Naomba Serikali isimamie ili kuhakikisha wananchi wanatendewa haki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru Mungu kwa kunifikisha mahali hapa salama ili na mimi nichangie hotuba hii muhimu ya Wizara ya Maliasili na Utalii ya mwaka wa fedha 2018/2019. Ninaipongeza Wizara pamoja na wataalam wake kwa kuandaa bajeti nzuri. Bajeti hii inakwenda kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi katika kuleta mapinduzi makubwa katika sekta ya maliasili na utalii.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kwa kuanza kuipongeza Serikali hii ya Awamu ya Tano kwa jitihada zake za dhati kabisa katika kukuza utalii na kuhakikisha sekta hiyo inaimarika na kuliingizia Taifa pato. Tanzania ni nchi ya pili duniani kwa kuwa na vivutio vyya kihistoria, nafasi hiyo ni muhimu sana kwa Taifa na hatuna budi kuitumia ipasavyo kuandaa mikakati mbalimbali ya kimapinduzi katika sekta hii ya utalii ili ilete matokeo chanya.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tumebarikiwa kuwa na vivutio hivyo ambavyo havipatikani mahali pengine popote duniani ila ni hapa nchini kwetu. Mikakakati ya kuvitangaza kwa kutumia njia mbalimbali ndiyo njia pekee itakayotusaidia kusikika duniani kote na kupata wageni watakaokuja kutembelea vivutio vyetu na kuliingizia Taifa letu fedha za kigeni pamoja na kutoa ajira kwa watu wetu ambao

watahudumu kwa wageni hao. Serikali imejitahidi sana kuliangalia hilo, lakini tukiwa kama sehemu ya Serikali hatuna budi kuishauri pale tunapoona changamoto zinajitokeza hasa ambazo zinarudisha juhudi hizi muhimu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri Serikali kuzidisha matangazo mbalimbali katika maeneo mbalimbali duniani hasa kuvitangaza vivutio vyetu ipasavyo. Tukiwatumia mabalozi wetu katika mataifa mbalimbali wanayotuwakilisha itatusaidia sana kuvitangaza vivutio hivyo na kupata watalii wengi. Aidha, Serikali ije na mkakati wa kuvitangaza vivutio vyote vilivyosahaaulika kwani tuna vivutio vyta kitalii katika maeneo mbalimbali nchini. Vivutio vyta kihistoria ambavyo vimesahaaulika sasa ni wakati muafaka kwa Serikali kuvitangaza ili tuweze kupata wageni wa kuvitembelea.

Mheshimiwa Spika, aidha, ninaipongeza Serikali kwa juhudi kubwa ilizoweka na kufanikisha ongezeko la watalii kuja nchini kwetu kwa mwaka 2017 ambapo idadi imefikia milioni 1.33 ikilinganishwa na watalii milioni 1.28 mwaka 2016. Hii imepelekea mapato kuongezeka na kufika dola za Marekani bilioni 2.19 mwaka 2017 ikilinganishwa na dola za Marekani bilioni 2.13 kwa mwaka 2016. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia sita, ni hatua muhimu na zinaonesha kuwa sekta hii ya utalii ikijengewa mikakati madhubuti basi italiingizia Taifa letu pato kubwa na kuwezesha maendeleo kuja kwa haraka na hivyo uchumi kukua.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imebarikiwa kwa kuwa na misitu pamoja na maliasili mbalimbali na Serikali imekuwa ikifanya juhudi kubwa kuyalinda maeneo hayo ya misitu, wanyamapor, malikale, uvuvi, ufugaji nyuki, pamoja na kuhakikisha kwamba rasilimali hizo zinanufaisha vizazi vyta sasa na vyta baadae.

Napenda kuipongeza Serikali kwa kuchukua hatua za kuimarisha mifumo ya kukusanya mapato katika sekta hizo, kupambana na ujangiri, kuzuia upotevu wa mazao yatokanayo na misitu na kutatua migogoro ya mipaka kati

ya hifadhi na vijiji. Hizi ni hatua nzuri na za kupongezwa zinazoendelea kufanywa na Serikali yetu katika mikakati endelevu.

Mheshimiwa Spika, lakini bado kuna changamoto katika maeneo mbalimbali ya uchomwaji wa misitu, uvunaji wa magogo kiholela na kutokutolewa kwa elimu ya kutosha kwa wananchi juu ya upandaji miti.

Mheshimiwa Spika, tukianzia suala zima la uchomajii wa misitu kiholela limepungua kwa kiasi kikubwa, lakini kuna baadhi ya maeneo changamoto bado inajitokeza. Wizara ichukue hatua mbalimbali za kukomesha majanga haya yanapotokea kwani huharibu mazingira hasa kwa baadhi ya maeneo ambayo yana viumbe hai na kwamba hupelekeea viumbe hao kuhama.

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa Serikali na taasisi zake za kichunguzi zinazohusika na masuala mbalimbali yanayohusiana na Wizara hii, kuchukua hatua za haraka. Pale kwenye taarifa ama namna yoyote itakayoonesha au kudhihirisha kuna watu wanahujumu sekta yetu hii basi wachukuliwe hatua kali za kisheria na si kuachwa, watu hawa wakiachwa watalipeleka taifa letu katika mgogoro wa kimataifa ama kwa kuharibu mazingira, kuua wanyama wa mwituni na mengineyo yanayofanana na hayo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Spika, na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kutoa pongezi lakini kuna tatizo kubwa la *TFS* na Jeshi la Wanyamapor. Wilaya ya Uvinza ina Hifadhi za Ilunde, Mahale pamoja na Ipuguru. Vilevile ina Msitu wa Pakunda Pachambi na Msitu wa Masanza.

Mheshimiwa Spika, nianze na Hifadhi ya Mahale, hifadhi hii imepakana na vijiji viwili, Kijiji cha Simbwesa na Kijiji cha Kalilani. Kijiji cha Kalilani kilisajiliwa tangu mwaka 1995 kwa Namba 244 na Kijiji cha Simbwesa kimesajiliwa kisheria tangu mwaka 1967.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na tatizo kubwa na *DC* wa Uvinza kwa kushirikiana na mhifadhi pamoja na watumishi wa Hifadhi ya Mahale. Mheshimiwa *DC* alienda Kalilani na kuwafokea wazee kama watoto wadogo. Naye Mheshimiwa *DC* wa Kigoma Mjini Ndugu Hanga alikwenda Kijiji cha Simbwesa akawatukana wanakijiji na kuwatishia kuwa Serikali hii ya Awamu ya Tano haitaki mchezo na mtu na kutoa amri kwa askari na askari wa hifadhi kuwa waweka vingi ndani ya Kijiji cha Simbwesa na kuwatishia kuwaweka Serikali ya kijiji ndani.

Mheshimiwa Spika, ninavyoona mimi kama mwakilishi wa wananchi hawa wa Vijihi vya Kalilani na Simbwesa sina mahusiano kabisa na Hifadhi ya Mahale kwa kuwa hata wakiwa na suala na vijiji hivi wanatakiwa kunishirikisha mimi, mimi kama mwakilishi wa wananchi badala yake wanatoa hongo kwa viongozi wa Wilaya. Niwe wazi Mheshimiwa *DC* Mwanamvua Mlindoko ni kero, kero, kero kubwa kwénye suala la utatuzi wa migogoro.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vijiji hivi viwili vya Kalilani na Simbwesa vimesajiliwa kwa mujibu wa sheria, kwa nini hifadhi walazimishe kuweka vingi ndani ya eneo la vijiji? Nimuombe Mheshimiwa Waziri watoe vingi ndani ya vijiji hivi ili wananchi waweze kupata maeneo ya kulima na kufanya shughuli zao za kimaendeleo. Kwa kuwa kuna Kamati ya Waziri Mkuu hivi vijiji vya Kalilani na Simbwesa vimo niombe basi kauli ya Serikali itolewe kuwaachia wananchi maeneo yao. Mgogoro huu una zaidi ya miaka 46.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Msitu wa Masito, tunao msitu huu ambao umekwisha kabisa na hauna wanyama wala miti. Tulipata fedha za ujenzi wa barabara ya Basanza – Lugofu Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza.

Tangu tupewe fedha za ujenzi wa barabara hii inayopita ndani ya Msitu wa Masito ni miezi 12 sasa tunashindwa kujenga barabara hii kwa kigezo cha kuzuiliwa na Mkuu wa TFS wa Uvinza.

Mheshimiwa Spika, ni barabara ngapi zinapita ndani ya hifadhi za Selous, Ngorongoro Serengeti na kadhalika? Kwa nini sisi Uvinza tusiruhusiwe kujenga hii barabara ambayo ni muhimu sana kwa wananchi wa Kata ya Basanza? Niombe Mheshimiwa Waziri tupewe kibali kabla pesa hazijarudi Hazina.

Mheshimiwa Spika, Msitu wa Pakunda Pachambi, msitu huu uko chini ya Halmashauri ya Wilaya, lakini changamoto tuliyonayo ni watu wa maliasili kuweka vizingi hadi kwenye vyoo vya wananchi na kusababisha wananchi wa Kata ya Nguruka, Kitongoji cha Humula na Kitongoji cha Reli Mpya kukosa maeneo ya kulima, kujenga zahanati pamoja na kujenga taasisi muhimu za Serikali. Tuombe pia kibali cha kugaiwa ekari kadhaa kwa vitongoji hivi pamoja na Vijiji vya Chagu, Mganza nan Nyangabo ili wapate maeneo ya kulima na kujenga mahitaji yao muhimu.

Mheshimiwa Spika, tuiombe Serikali itupe pesa za kujenga barabara ya kutoka Rukoma hadi Kalilani ili kukuza utalii. Watalii wanapata shida sana ya kutumia boti wakati wa upemo mkali. Tuna vita Rukuga, ni lazima barabara hii ijengwe na TANAPA. Tunaishukuru TANAPA kwa kujenga madaraja mawili, lakini madaraja haya hayana tija kama barabara haitojengwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Waziri kwa kutupa Msitu wa Masito – Ugala kwani kwa kupata msitu huu Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza itaongeza mapato. Pia niombe Mheshimiwa Waziri atusaidie gari kwa ajili ya Idara ya Maliasili kwa ajili ya kujengea ufanisi idara hii. Baada ya kuchangia haya niendelee kumpongeza Waziri na Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya nishati ya mkaa na kuni kwa taasisi, nimesoma ushauri wa Waziri kwa taasisi kutumia nishati mbadala. Ushauri huu hauonekani kuwa ni msisitizo wa kuokoa misitu. Naishauri Serikali kuleta sheria ambayo itazilazimisha taasisi kuweka mkakati wa matumizi ya gesi badala ya kuni au mkaa. Pamoja na sheria hiyo Serikali itoe punguzo la kodi maalum kwa vifaa nya gesi yenye kwa taasisi zilizo tayari ambazo zitatambuliwa. Jambo hili iwapo litafanyika litasaidia kupunguza matumizi ya kuni na mkaa kwa sehemu kubwa.

Mheshimiwa Spika, suala la mipaka mipyä ya hifadhi, naunga mkono maoni ya Kamati juu ya kuondoa kabisa mipaka mipyä ya mbuga na hifadhi kwenye vijiji na nchi nzima kwa ujumla. Mipaka hii imeleta tafrani kubwa na imekiuka kabisa mipaka ya asili iliyowekwa kwa mujibu wa *GN* na sheria za nchi hii. Mipaka mipyä isimame mpaka ushirikishwaji utakapofanyika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kesi za mifugo inayokamatwa, baadhi ya mifugo imekuwa ikikamatwa ndani ya hifadhi au mbuga za wanyama na Serikali kuzishikilia kwa muda mrefu. Kwa kuwa askari wa wanyamapori hawana utaalam wa mifugo, mifugo mingi huwa inakufa na Serikali na wananchi kupata hasara kubwa. Kwa mfano mwaka 2014/2015 huko Ngara Tanzania mifugo (ng'ombe) 887 ilikamatwa ndani ya hifadhi, mifugo 700 ilikufa kabla ya maamuzi ya Mahakama na hata waliobaki walikosa bei ya soko kwani walikuwa wamekonda sana.

Naishauri Serikali kubadilisha utaratibu wa kushikilia mifugo, badala yake iachwe kwa mtuhumiwa kwa uangalizi maalum mpaka kesi ya msingi itakapoamuliwa.

MHE. DANIEL E. MTUKA: Mheshimiwa Spika, nianze kuhusu migogoro ya mipaka baina ya hifadhi za wanyamapori/misitu na wananchi. Katika ya Jimbo la Manyoni Mashariki jumla ya vijiji 12 vimepakana na Hifadhi za Kizigo na Muhesi. Vijiji hivi ni Chikola, Chikombo, Mpola,

Iteka Azimio, Nkonko, Chidamsulu, Iseke, Mpapa, Simbanguru, Sasilo, Chisnjisa na Imalampaka.

Mheshimiwa Spika, wananchi katika vijiji tajwa hapo juu wanalamikia uhaba wa ardhi kwa ajili ya kilimo, malisho ya mifugo, uchimbaji wa madini pamoja na ufugaji wa nyuki. Aidha, wanalamikia kitendo cha kuzuiwa kutumia maji ya mto uliopo mpakani kati ya hifadhi na vijiji. Uhaba wa ardhi umejitokeza baada ya ardhi yao kuchukuliwa na Serikali ulipofanyika upanuzi wa mipaka ya hifadhi za misitu tajwa mwaka 1994.

Mheshimiwa Spika, *Muhesi Game Reserve* imanzishwa rasmi kupitia GN Na. 531 ya tarehe 04/11/1991 na kusainiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 09/03/1994. Muhesi ni hifadhi changa yenye kilometra za mraba 2000 na kwa hiyo imesababisha machungu makubwa kwa wananchi katika maeneo haya. Tangazo la kuipandisha Muhesi kuwa *game reserve* mipaka yake mipya imeleta madhara makubwa kiuchumi kwani imechukua maeneo muhimu kama eneo muhimu la kilimo cha mahindi liitwalo Chiumbo na eneo la machimbo ya dhahabu aina ya *alluvial* yaliyogunduliwa mwaka 1991. Hii ni dhahabu bora ambayo haijawahi kuonekana na kuchimbwa mahali pengine katika nchi hii (Ref: Taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania, 1992).

Mheshimiwa Spika, maeneo au vitongoji vingine vilivyochochukuliwa ni pamoja na Chosola, Msisi, Illelo, Machocholoni, Mkindilya, Chigugu, Ngongolelo pamoja na Chibwee. Aidha, maeneo haya yaliyochukuliwa yalitegemewa sana katika malisho ya mifugo, ufugaji wa nyuki na vyanzo vya maji safi ya kunywa binadamu na mifugo katika Mito ya Muhesi na Kizigo. Malalamiko mengine ni unyanyasaji utesaji na udhalilishaji vinavyofanywa na askari wa *game reserve* dhidi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, naambatisha na taarifa ya malalamiko ya wananchi yenye kichwa cha habari; "Yah: Malalamiko ya Wananchi Kuhusu Migogoro ya Mipaka Bainam

ya Viji 12 na Hifadhi za Muhesi na Kizigo; na Manyanyaso ya Askari wa Hifadhi Dhidi ya Wananchi."

Mheshimiwa Spika, malalamiko haya yaliwasilishwa na wananchi 18 kutoka Jimbo la Manyoni Mashariki wakiongozwa na Mbunge wao Daniel Mtuka walipokutana kwa mazungumzo ya ana kwa ana ofisini kwao (Dodoma) Naibu Mawaziri wawili; kwa wakati huo walikuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii *Engineer* Ramo Makani, tarehe 27/05/2016 (mchana) na Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa William Tate Ole Nasha tarehe 27/05/2016 (mchana).

Mheshimiwa Spika, tunasikitika, hadi leo hatujibowi (mwaka mzima)

Mheshimiwa Spika, ombi, wananchi wangu bado wanasubiri majibu.

MHE. MUSSA R. SIMA: Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake pamoja na watendaji wote. Narejea ukurasa wa 37 wa hotuba ya Waziri kuhusu matumizi ya mkaa. Nampongeza kwa kutambua umuhimu wa matumizi ya mkaa na kuja na mkakati mzuri. *In short* ingependeza zaidi kama elimu hii ya matumizi ya mkaa ingehusisha viongozi wote wa ngazi ya chini kama watendaji (*VEOs/WEOs*) ambao wana jukumu la kutoa elimu hiyo na ujumbe kufika kwa haraka. Kwa kuwa teknolojia hiyo ya gesi bado wananchi hawana uwezo wa *ku-afford* kununua gesi ni vizuri Serikali ikaendelea kuruhusu matumizi ya mkaa.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Maafisa Maliasili na Utalii kwenye Halmashauri zetu ikiwemo Manispaa ya Singida kuwa na mpango kazi wa kuboresha eneo hili. Kwa mfano Singida tunavyo vyanzo vya utalii vingi ikiwa na fukwe. Niombe Serikali itoe maelekezo ya kila Halmashauri kuititia mikoa yao waandae na kuleta taarifa ya maliasili na utalii. Hii itasaidia kubaini maeneo hayo na kuongeza wigo wa utalii.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, nianze na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Dkt. Hamisi Kigwangalla (Mb), Naibu Waziri Mheshimiwa Hasunga na watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha hotuba yao ya bajeti ili tuweze kujadili. Nimpongeze Waziri kwa kuongeza pato la Taifa kwa zaidi ya asilimia tano, hongera sana.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa ujenzi wa viwanja vyta ndege nchini kikiwamo Kiwanja cha Ndege cha Nduli, Mkoa wa Iringa. Pia ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami inakwenda katika Hifadhi ya Ruaha. Tunaamini kabisa miundombinu itakapokamilika Mkoa wa Iringa utakuwa kitovu cha utalii, pia Nyanda za Juu Kusini kutafunguka kiutalii na pato la mkoa na nchi litaongezeka.

Mheshimiwa Spika, kuvibaini vivutio zaidi vyta utalii viliwyoko nchini na kuviendeze, nilikuwa naomba Serikali itueleze mpango maalum walioupanga kwa ajili ya kuvibaini vivutio viliwyopo katika nchi yetu kwa ajili ya kuviendeze na kuvitangaza ili viwe na tija na visaidie kuongeza pato la Taifa. Katika Mkoa wetu wa Iringa kuna vivutio vingi sana vyta utalii ambavyo bado havijapewa kipaumbele katika kuvitangaza kama vile Fuvu la Kichwa cha Mkwawa, Jiwe la Hangilongo (jiwe lililokuwa linaongea), sehemu waliyokuwa wananyongwa watumwa (vitani), sehemu waliyopigania uhuru alipokuwa anaishi Mandela, Lugalo sehemu lilipo kaburi la Nyundo na vingine vingi sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu ya utalii, nilikuwa pia nataka kujua mpango mkakakti wa kuwapatia elimu wananchi wa Mkoa wa Iringa. Tunaipongeza Serikali kwa uzinduzi wa utalii katika mkoa wetu kama kitovu cha utalii wa Nyanda za Juu Kusini. Ni imani yangu kabisa kupitia utalii wananchi wetu watajajiri. Kama wataandalowiwa katika utalii kuna ajira nydingi sana.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa ununuzi wa ndege ambazo nina imani utaongeza utalii katika mikoa yetu na nchi yetu. Tulikuwa tunaomba huu mradi wa *Regrow* unaokuja kukuza utalii Nyanda za Juu Kusini uendelee

kusaidia utangazaji wa vivutio vya utalii vilivyopo katika mikoa hii ya Kusini. Mradi huu uendelee ku-support maonesho haya yaliyozinduliwa Iringa ya Karibu Kusini ambapo imefanyika kwa miaka miwili kwa Mikoa ya Iringa, Mbeya, Njombe, Songwe, Katavi, Ruvuma na Rulewa.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru mradi huu utajenga jengo kama Kituo cha Utalii eneo la uliokuwa Msitu wa Kiheza, Kilolo Iringa. Nilikuwa naomba watakapojibu watujulisho makao makuu ya mradi huu ni wapi? Kwa kuwa mradi wa Spanest unaishia mwezi wa sita, je, utaongezewa muda tena? Kwa kuwa sasa mkoa wetu utakuwa kitovu cha utalii, je, Serikali imejiandaaje kutoa elimu na mafunzo kwa wananchi ili waweze kujiajiri kupitia utalii?

Mheshimiwa Spika, Mkoa wetu wa Iringa una eneo la uwekezaji lillopo katika Msitu wa Kiheza, Kilolo ekari 640 za eneo zima, lakini ekari 230 Halmashauri ya Manispaa ya Iringa ilipatiwa kuendeleza katika utalii. Tunaomba Serikali ilete rasilimali fedha na rasilimali watu ili kusaidia kuutunza msitu huo kwa eneo lillobaki.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkoa wa Iringa katika Halmashauri zote kuna vivutio vya utalii, pamoja na kuwa Afisa Wanyapori, Dada Hawa Mwechaga anafanya kazi nzuri sana za utalii pia Mkuu wetu wa Mkoa Mheshimiwa Amina Masenza anahamasisha sana utalii, tunaomba Wizara ya Maliasili na Utalii ishirikiane na Wizara ya TAMISEMI ili kuhakikisha Halmashauri inakuwa na Afisa Utalii ili vivutio vilivyomo katika Halmashauri zetu vitumike kama vyanzo vya mapato. Niendelee kumpongeza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mito yenye mamba, niendelee kumpongeza, naomba kujua Serikali inasaidiaje mito yenye mamba hasa katika Mkoa wa Iringa? Wanasaidiwe kuvuta maji ili wananchi wasiendelee kuuawa na kupata ulemavu?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya utalii nchini. Sote tunatambua kuwa masuala ya sekta ya utalii si masuala ya Muungano, hivyo kujumuisha idadi ya watalii wanaoingia Zanzibar kama sehemu ya Muungano kwa mujibu wa randama ndiko kunakozua mtanziko. Serikali ituambie ni lini hasa imeamua mambo ya utalii kuwa sehemu ya Muungano kama ambavyo Serikali imekuwa ikijinasibu na idadi ya watalii inayojumuisha Tanzania Bara na Tanzania Visiwani?

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Serikali ikaweka wazi dhamira yake ya kujumuisha idadi ya watalii ikiwemo ya Zanzibar. Vilevile pamoja na mazingira mazuri ya kibashara na faida zake, sekta hii ya utalii inaweza kukua pale ambapo nchi inakuwa katika hali ya amani na utulivu. Amani na utulivu huja pale ambao mamlaka zinazingatia haki za kira la.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uwindaji, ni nini hasa kinachosababisha kushuka kwa mapato katika sekta hii tofauti na miaka ya nyuma? Pia Serikali imeshindwa kudhibiti uwindaji haramu na ujangili. Biashara ya uwindaji inaonekana kutafsiriwa tofauti mionganoni mwa wananchi walio wengi. Serikali imeshindwa kutoa ajira za kutosha kwa walini wa wanyamapori, kushindwa kulinda mazalia ya wanyamapori, kushindwa kufanya tafiti za mara kwa mara juu ya ongezeko na upungufu wa wanyama na viumbe hai, wananchi kutoshirikishwa juu ya kulinda wanyama wetu na badala yake wananchi wanaoishi kando kando ya hifadhi wamechukuliwa kama maadui au wanyama. Hii yote ni kutokana na kutowapa elimu na mafunzo ya ulinzi shirikishi katika suala zima la kulinda rasilimali hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kudhoofika kwa biashara ya uwindaji na athari zake, tukumbuke kuwa biashara ya uwindaji ndiyo biashara inayoingizia Serikali fedha nyingi zaidi za kigeni kwenye sekta hii ya utalii ni jambo la kushangaza Serikali imefuta vibali kinyume cha Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 2009 ambayo inaeleza wazi taratibu na makosa ambayo yanaweza kusababisha kampuni kufutiwa vibali.

Ikiwa ni pamoja na kushindwa kutimiza masharti ya leseni, endapo kampuni imepatikana na hatia au kushindwa kulipa ada na tozo mbalimbali na si kufuta vibali kwa ghafla pasipo kufuata sheria na taratibu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikikiuka utaratibu mara kadhaa jambo ambalo linaathiri mazingira ya kibiashara na hivyo kusababisha hasara kubwa kwa wawekezaji wa ndani na wale wa kigeni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushuru wa maendeleo ya utalii, kutokeupeleka fedha katika akaunti ya tozo ya maendeleo ya utalii ina athari za moja kwa moja katika utendaji kazi ndani ya Wizara. Mpaka sasa Wizara hii imekuwa ikitegemea zaidi wahisani na hivyo kuendelea kukwamisha jitihada za Wizara. Kutokuhamisha fedha kwa wakati maana yake ni kuifanya Wizara kushindwa kutekeleza majukumu yake. Pia ndiko hasa kunaporuhusu matumizi mabaya ya fedha kuanza kujipenyeza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu migogoro sugu baina ya Serikali na wananchi wanaoishi kando ya hifadhi za wanyamapori, kumekuwa na tatizo sugu la migogoro baina ya Serikali na wananchi wanaoishi kando kando ya hifadhi ya wanyama pori kwa muda mrefu sasa. Pamoja na jitihada mbalimbali za kuizungumzia na kushauri hatua stahiki za kuitatua bado hali inaonesha migogoro hii imekuwa na nguvu kubwa kuliko uwezo wa Serikali wa kuitatua.

Mheshimiwa Spika, vilevile migogoro hii imedumu kwa muda mrefu ambapo imegharimu maisha ya wananchi wengi. Tumepoteza wanyama ambao ndio fahari yetu na chanzo cha mapato. Migogoro hii imesababisha kuenea kwa magonjwa yanayosababishwa na wanyama pori, mifugo na hivyo kuathiri afya za wanyama wa kufugwa na wanyama wa porini. Kwa baadhi ya maeneo migogoro imekuwa ni ya muda mrefu kutokeupeleka na tuhuma kuwa kuna baadhi ya mapori ya akiba na hifadhi kupanua mipaka yake bila kuwashirikisha wananchi wa maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Idara ya Misitu na Nyuki, sekta ya ufugaji wa nyuki imekuwa haifanyi vizuri kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo kutopewa kipaumbele ipasavyo. Miradi mingi inayoanzishwa na Serikali imekuwa haifanyi vizuri na mingi imeshindwa kuendelea kutokana na kutokutunza vizuri na kukosa ufuutiliaji wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uharibifu wa mazingira katika hifadhi za misitu, suala la utunzaji wa mazingira ni muhimu sana kwa ikolojia ya misitu, bahari pamoja na mbuga zetu kwani uwepo wa maji, hali nzuri ya hewa na udongo vinapelekeea mimea na wanyama kuzaliana na kuwa katika hali bora zaidi. Sote tunatambua umuhimu wa kutunza ikolojia na madhara makubwa yanayojitokeza nchini kwa sasa kutokana na kuharibu wa ikolojia na madhara makubwa ya mabadiliko ya tabia ya nchi. Pia kukauka kwa vyanzo vya maji, kuharibika kwa ardhi, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua madhara haya makubwa kwa binadamu na mimea Serikali iliamua kuridhia mikataba mbalimbali ya Kimataifa ya kulinda mazingira. Pamoja na kuweka sheria na sera za kulinda mazingira nchini ni vyema Serikali ikaamua kufanya mkakati wa tathmini ya mazingira kwa miaka mingi ijayo. Bado nchi yetu ina namna nydingi ya kuzalisha umeme katika maeneo mengi ambayo athari zake za mazingira si kubwa kama itavyotokea kwenye chanzo cha Mto Rufiji. Vilevile Pori la Akiba la Selous limekuwa chanzo kikubwa cha mapato ya wananchi na ajira. Mpaka sasa pori hili limeorodheshwa katika maliasili zilizo, hatarini kupotea. Kwa mujibu wa Mkataba wa Kimataifa wa Urithi wa Dunia kutokana na kuongezeka kwa mauaji ya tembo na kuharibika kwa mapitio ya wanyama. Vilevile kuna maeneo mengi ambayo wananchi wamefukuzwa na wengine kuhamishwa kutokana na kulinda ikolojia ya maeneo hayo.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya wataalam wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa hotuba nzuri ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Serikali kuwekeza katika maliasili zetu bado kuna changamoto nydingi za migogoro ya mipaka kati ya hifadhi za wananchi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Wilaya ya Mbeya wamekuwa wadau wakubwa wa hifadhi zetu ikiwemo Hifadhi ya Kitulo na Hifadhi ya Misitu ya Kata ya Inyala. Kuna mgogoro wa muda mrefu kati ya *TANAPA* (Hifadhi ya Kitulo) na wananchi wa Kata za Ilungu, Igoma na Ulenje. Pamoja na juhudzi za Serikali za kutatua mgogoro huu, pia Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliahidi kumaliza mgogoro huu kwa kuwafidia wananchi zaidi ya 600 waliopisha maeneo yao kwa ajili hifadhi.

Mheshimiwa Spika, inaelekea *TANAPA* kwa kushirikiana na Serikali ya Mkoa wa Mbeya badala ya kumaliza mgogoro wameanza kuchochea chuki na wananchi pasipo kushirikisha uongozi wa chini ikiwemo vijiji na Halmashauri. Wameanza kuchukua hatua za kutaka kuhamisha wananchi wa Kijiji cha Kikondo na kukipeleka kwenye Hifadhi ya Misitu wa Kijiji cha Ilungu ambacho ni chanzo kikubwa cha maji na kimekuwepo kisheria kabla ya uhuru. Bila kushirikisha Serikali Kijiji cna Baraza la Madiwani *TANAPA* wameenda kupima hekta 800 kwa ajili ya kuhamisha wananchi wa Kijiji cha Kikondo ambacho kipo kisheria.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanajuliza ni kwa nini kuhamishia wananchi kwenye hifadhi ambayo ni chanzo muhimu cha maji? Hata hivyo, wadai ni zaidi ya 600 ambaao walihakikiwa tangu awali, miaka zaidi ya mitano iliyopita na si 20 wanaokusudiwa kupata fidia.

Mheshimiwa Spika, hatua zinazoshawishiwa na *TANAPA* zinachochea migogoro isiyokuwa ya lazima, ukichukulia hawa wananchi ndio wanaotegemewa na Serikali katika kulinda hifadhi hizi. Hifadhi ya kituo na misitu ya Kata ya Ilungu ni muhimu sana kwa ajili ya vyanzo vya maji ikiwemo Mto Ruaha. Pamoja na mgogoro wa hifadhi ya Kitulo, wananchi wa vijiji vya Kata ya Inyala wameporwa

maeneo yao na *TFS*. Naomba Serikali kuchukua hatua za kutatua mgogoro huu ambao eneo lilidochukuliwa kinyemela ni dogo sana ukilinganisha na athari za mgogoro.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kijiji cha Mjele, Kitongoji cha Mtakuja, wanapata usumbufu mkubwa kutoka *TFS* na mara kwa mara wamekuwa wanapata usumbufu wa kuchomewa nyumba zao na kuharibu mazao yao kwa mazingira ya uonevu. Serikali irekebishe hii mipaka ambayo wananchi wapo hapo kabla ya mwaka 1940.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Spika, migogoro kati ya hifadhi za wanyama na vijiji vinavyozunguka hifadhi hizo ni ya muda mrefu na inaumiza sana. Mgogoro kati ya Vijiji vya Losilette, *Upper Kitete*, Slahamo, Makuromba na Endamaghang Wilayani Karatu na Hifadhi ya Ngongoro ni ya muda mrefu. Pia mgogoro kati ya *TANAPA* (*Lake Manyara National Park*) na wananchi wa kata ya Buger umekosa wa kusuluhisha.

Mheshimiwa Spika, askari wa wanyamapori wamekuwa na ubabe wa kuwanyanyasa na kuwapiga wananchi. Mipaka ya hifadhi hizi imewekwa siku nyingi tangu ukoloni na bila kumung'unya maneno mipaka halisi inafahamika, inaonekana na ni ubabe tu wa hifadhi kuyaongezea maeneo ya wananchi. Serikali iachane na tabia ya kuvamia maeneo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, wanyama wamekuwa chanzo cha kutia umaskini wananchi wetu. Tembo na mbogo wamekuwa wakitoka hifadhini na kwenda vijijini kuharibu mashamba ya wananchi na hata kusababisha vifo. Uongozi wa hifadhi hizi hauko makini kuwazuia wanyama hao. Niishauri Serikali kuhakikisha timu za doria zinaongezwa na kupewa zana za kuwadhibiti wanyama hao.

Mheshimiwa Spika, sheria ya kutoa kifuta jasho na pole kwa uharibifu na mauaji yanayofanywa na wanyama hao imepitwa na wakati na inahitaji marekebisho makubwa. Pole ya shilingi 1,000,000 haitoshi kabisa hivyo inafaa iongezwe.

Utaratibu wa kukamata na kutaifisha mifugo ya wafugaji pale inaposemekana wameingia hifadhini haufai kabisa na ni unyanyaswaji wa wananchi. Ng'ombe wamekuwa wakitaifishwa kwa uonevu mkubwa. Utaratibu huu ubadilishwe, haufai kabisa.

MHE. CATHERINE N. RUGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ningependa kuchangia mambo machache katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Jambo la kwanza ni kuhusu mtiririko wa bajeti katika Wizara hii. Mwaka 2016/2017 Bunge liliidhinisha fedha za miradi ya maendeleo kiasi cha shilingi 17,746,682,000; hata hivyo, kiasi kilichotolewa ni shilingi 2,199,870,358 ambacho ni sawa na asilimia 12 ya fedha zote zilizotengwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2017/2018 jumla ya shilingi 51,803,204,000 zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo mpaka kufikia mwezi Februari, 2018 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 27,946,781,302 ni ambayo ni sawa na asilimia 54 ya fedha zilizoidhinishwa. Makadirio ya bajeti ya mwaka 2018/2019 ni shilingi 29,978,082,000 hii inaonesha anguko la bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, mtiririko wa bajeti wa Wizara hii unaonesha bajeti ya maendeleo imekuwa ikitegemea fedha za nje. Mfano kwa mwaka 2017/2018 fedha za ndani zilizotolewa zilikuwa shilingi 11,353,250,489 na fedha za nje ni shilingi 16,593,530,813. Mwaka wa fedha 2018/2019 fedha za maendeleo zinakadirwa kwa shilingi 29,978,082,000 kati ya hizo fedha za ndani ni shilingi 3,000,000,000 tu.

Mheshimiwa Spika, hili ni tishio kubwa kwa Wizara kwani kuzidi kutegemea misaada kutoka kwa wahisani hakuwezi kamwe kunyanya sekta hii. Kumekuwa na matamko mbalimbali ya Mheshimiwa Rais, hatutategemea wahisani, ila hali halisi ni kuwa bajeti yetu imekuwa tegemezi kwa zaidi ya asilimia 50. Hii inaonesha kuwa bado Serikali hajakubali kuwekeza ipasavyo kwenye sekta ya maliasili na utalii.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu ukuaji wa sekta ya utalii nchini. Mwaka 2012/2016 wastani wa ukuaji wa sekta ya utalii ilikuwa asilimia 13.7 mwaka 2017 sekta ya utalii imekuwa kwa asilimia 3.3 kwa sababu ya maamuzi holela ya Wizara hii, *unstable policy decisions* katika sekta ya uwindaji ambayo imesababisha kushuka sana kwa ukuaji wa sekta ya utalii.

SPIKA: Tunategemea tukakapokutana saa kumi basi Waheshimiwa Mawaziri wataanza kujaribu kupitia hoja. Lakini niwaambie tu wahifadhi kwa kweli mnamwangusha sana Mheshimiwa Waziri wetu. Hii maneno inayosemwa endapo ni kweli ku-*shoot shoot* watu, hii kupiga risasi ng'ombe, kama mambo hayo yapo kwa kweli hebu mkaache huu ukatili unatoka wapi huo. (*Makofi*)

Lakini pia hili la sijui ni sheria zetu nadhani hili la kuuza ng'ombe wote Mwanasheria Mkuu wa Serikali aah, hili hata kama sheria hiyo ipo hebu tuiangalie jamani. Unajua Mheshimiwa Ole Nasha anaweza akanielewa vizuri sana, yaani mtu mwenye mifugo yake 100; sijui 150; sijui ngapi ile mifugo ni mapokea wakati mwingine imetoka kwa babu, baba na yeze na familia yake. Kwa sababu tu wamekanyaaga hifadhi inatoka hukumu wanauzwa wote. Yaani kwa sisi tunaotoka kwenye ufugaji huo kwa lugha rahisi wanasema *it is difficult even to imagine*. Yaani yule mzee anarudije kwenye familia yake ana fimbo tu hana chochote yaani kwa sababu *is a lively hood. You deprive somebody of a lively hood*. Anarudi nyumbani anakutwa vile vindama vinalia mama zao wameuzwa, vindama vingine vimezaliwa wiki iliyopita vingine vinalia pale hakuna namna ya kufanya vile vindama lazima vife. Utavifanyaje vile mama zao wameuzwa wote aaah! *No, no hatuwezi kufanya hivyo Tanzania jamani!* Hapana hapana. (*Makofi*)

Hata mkichukua nusu si adhabu tosha yaani mpaka wote wote? Yaani huyu mtu anakuwa maskini yaani ni kama wewe una nyumba zako na magari yako yamechukuliwa yote yaani yote halafu umebakvi *zero*, utajinyonga, utaishi, utafanyaje yaani ndiyo mambo haya wafugaji wana-face.

Mheshimiwa Waziri wa Mifugo pole bwana lakini kwa kweli hili hili hapana hili linakera kama linafanyika kweli, endapo linafanyika. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, kuna matangazo kidogo tu machache, Mheshimiwa Mbunge wa Mbarali ambaye yeye ni mkulima wa mpunga kule Mbarali Mheshimiwa Haroon Pirmohamed, Mbunge mwenzetu wa Mbarali ametoa sadaka ya mchele, ametuletea lori moja hapo nje Waheshimiwa kila mhitaji anaweza akapata hadi kilo 50. (*Makof*)

Kwa hiyo, kwa niaba yenu nimshukuru sana Mheshimiwa kwa kutuletea sadaka hiyo na wengine mnalima, mnafuga muwe mnatuletea kidogo sadaka eeeh hasa wakati huu wa mwezi mtukufu. Tunawashukuru sana Mheshimiwa Mbunge wa Mbarali kwa niaba ya Wabunge wote kwa sadaka hiyo, lakini pia watumishi wa Bunge pia na ninyi mnahesabiwa kule kwa hiyo baadae baadae, kuanzia leo mchana huna haja ya kufanya haraka mchele upo taratibu taratibu tu kuanzia leo mchana jioni mpaka kesho tutapata. (*Makof*)

Waziri wa Viwanda na Biashara Mheshimiwa Mwijage anatutaarifu kwamba jana Maofisa wake watatu wa kutoka Kituo cha Uwekezaji walipata ajali eneo la Msoga, ajali mbaya ambayo maafisa watatu walifariki hapo hapo Ndugu Saidi Amir Moshi ambaye alikuwa Kaimu Mkurugenzi Idara ya utafiti, Ndugu Zacharia Nihula Kingu ambaye alikuwa Kaimu Mkurugenzi Idara ya *Cooperative Affairsna* Ndugu Martin Lawrence Masalu ambaye alikuwa Meneja wa Utafiti. Walikuwa njiani kuja Dodoma kwa ajili ya kikao cha wataalam wa Kamati ya Taifa ya Uwekezaji (*National Investment Steering Committee*) na kwa ajali hiyo watumishi wawili wapo Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili Ndugu Godfrey Kilolo, Meneja wa Sheria na Ndugu Prisicas Chuwa ambaye alikuwa dereva wa gari. Taratibu za mazishi zinaendelea kuratibiwa na Wizara husika. Tunawaombea marehemu Mwenyezi Mungu azipokee roho zao na aziweke mahali pema peponi, lakini pia tunawatakia hao ambao wako hospitali waendelee kupata nafuu.

Waheshimiwa Wabunge basi kama nilivyosema tatarudi hapa saa 10.00 tutaanza na Mwanasheria Mkuu wa Serikali halafu atafuata Waziri wa Katiba na Sheria dakika saba, saba, Naibu Waziri dakika 20 na mtoa hoja dakika 30. Basi nisitishe shughuli za leo hadi saa 10.00 jioni ya leo.

(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilitrudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu!

NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadilio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Wizara ya Maliasili na Utalii

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu yanayohitajia Bunge likubali kupilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha ujao. Kama nilivyokuwa nimeeleza pale mapema tutaanza na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa dakika saba, atafuata Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria. Mheshimiwa AG tafadhali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa wasaa wa kuanza kuwa mchangiaji wa kwanza upande wa Serikali. Nitajielekeza moja kwa moja kwa hoja iliyoibuliwa na Mheshimiwa Nsanzugwanko (Mbunge), lakini pia alikuwa ananukuu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii katika ukurasa wa 16 na 17 ambayo inahusu zoezi la kuhuisha vibali vya uwindaji ambapo Mheshimiwa alizungumza na iko hivyo katika taarifa kwamba Mheshimiwa Waziri alihuisha vibali hivyo mwezi Januari, 2017 lakini mwezi Oktoba akatoa tangazo la kuvifuta. Mwezi Disemba akatoa

tena tangazo au maelekezo ya kuongeza kipindi cha miaka miwili kwa vibali hivyo. Kwa hiyo, maoni ya Kamati pamoja na Mheshimiwa Mbunge ni kwamba Mheshimiwa Waziri alivunja sheria, na kwa hiyo, akaomba mahsusni Mwanasheria Mkuu wa Serikali atoe *position*.

Mheshimiwa Spika, *position*ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika suala hili ni kwamba Mheshimiwa Waziri hakuvunja sheria. Mheshimiwa Waziri alipochukua hatua hizi na imeelezwa vizuri katika ile barua ya kwanza ya kuongeza muda ya mwezi Januari lakini pia na kwenye hayo mawasiliano mengine ya mwezi Oktoba na mwezi Disemba kwamba alikuwa anachukua hatua hizo kwa ajili ya kuweka mfumo mzuri zaidi wa uendeshaji wa vitalu kwa namna ambayo Taifa litaweza kufaidika zaidi kuliko hali ilivyo sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa napenda kukuthibitishia na kukuhakikishia na kumhakikishia Mheshimiwa Mjumbe pamoja na Kamati kwamba Mheshimiwa Waziri alipofanya hivyo alikuwa pia anatekeleza sheria.

Mheshimiwa Spika, swali litakuja ni sheria gani hii ambayo Mheshimiwa Waziri alikuwa anaitekeleza. Sasa nitaomba nilikumbushe Bunge lako tukufu kwamba mnamo mwaka jana mwezi wa saba Bunge hili lilitunga sheria na hii sheria inaitwa *The Natural Wealth and Resources Permanent Sovereignty Act.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lengo kubwa la hiyo sheria ilipotungwa mwaka jana na Wabunge wote ni mashahidi nafikiri mijadala ilikuwa mikali na kadhalika, lakini ilikuwa zaidi kuhuisha Ibara za 9 na 27 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sehemu hii ya Katiba katika sheria tunasema inahitaji *enabling law* uweze kuitekeleza. Sasa nadhani ni vema nikarejea kwa ufupi na kwa haraka kabisa Ibara za 9 na 27 za Katiba zinasemaje. Nitakwenda Ibara

ndogo (c) na Ibara ndogo (i) lakini nitakwenda zaidi (c) inatosha; kwamba shughuli za Serikali zinatekelezwa kwa njia ambazo zitahakikisha kwamba utajiri wa Taifa unaendelezwa, unahifadhiwa na unatumiwa kwa manufaa ya wananchi wote kwa jumla na pia kumzuia mtu mwingine kumnyonya mtu mwingine. Hiyo ni Ibara ya 9. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 27 inasema; watu wote watatakiwa na sheria kutunza vizuri mali ya mamlaka ya nchi na ya pamoja na kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhirifu na kuendesha uchumi wa Taifa kwa makini kama watu ambao ndio waamuzi wa hali ya baadae ya Taifa lao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishesema palikuwa na matatizo katika suala zima la hivi vibali vyu uwindaji na kwa hiyo Mheshimiwa Waziri akachukua hatua hizo kulingana na hii sheria mpya. Nafikiri niende pia kwenye hiyo sheria mpya ya *The Natural Wealth and Resources Permanent Sovereignty* inatuambia nini. Naomba niende kifungu cha 6(1) na ninaomba niirejee hapa kinasema; “*It shall be unlawfully to make any arrangement or agreement for the extraction, exploitation or acquisition and use of natural wealth and resources except where the interest of the people of the United Republic are fully secured.*” (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri aliongozwa na kifungu hicho, lakini kipo kifungu chenye nguvu zaidi ambacho *actually* kinampa maelekezo Waziri na hana jinsi nyiningine. Kifungu cha 6(3) na chenyewe naomba nikisome; “*It shall be the duty and responsibility of the Government. all organs and persons or authorities exercising executive, legislative or judicial functions to take cognizance of, observe and apply the provisions of this Act.*”

Mheshimiwa Spika, kifungu hicho kinamfunga Waziri kwamba ni lazima ajue kwamba sheria hiyo ipo na kwa hiyo ni lazima chochote anachofanya kuanzia sheria ilipotungwa aongozwe na sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, sasa ninaelewa baada ya kusema hayo swali linaibuka je, kuna mgongano wa sheria. *Position* ya Mwanasheria Mkoo tena hapa katika swali hili ni kwamba hakuna mgongano wa sheria kwa sababu hii ni sheria msingi na umsingi wake unapatikana kwenye kifungu hicho nilichosema cha 6(3) kwa hiyo ina nguvu kuliko sheria nyingine. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, muda umekwisha nakushukuru sana. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali. Sasa naomba nimuite Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria Profesa Palamagamba Kabudi tafadhalii.

WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA: Mheshimiwa Spika, na mimi nataka niungane na wale wote ambao wamewapongeza Waziri na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kuwasilisha bajeti yao. Pia niendeleze machache ya yale aliyojasema Mheshimiwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, panapokuwa na sheria msingi na sheria ya zamani panakuwa na kipindi cha mpito na ni imani yangu kwamba haya yaliyotokea ni ya kipindi cha mpito. Katika kipindi cha mpito zipo changamoto za utekelezaji wa sheria na panapokuwa na changamoto kazi kubwa ya mamlaka za Serikali ni kuona ni jinsi gani kipindi hicho cha mpito kinatekelezwa na kama kuna changamoto zozote zinatatuliwa kiutawala. Kwa hiyo, nisingeenda kusema kwamba Waziri amevunja sheria, ninachoweza kusema ni kwamba kipindi cha mpito kina changamoto kati ya sheria iliyouwepo na sheria msingi iliyoukuja ili kusaidia kupata utaratibu ambao mwisho wa siku una tija kubwa.

Mheshimiwa Spika, maadam Mwanasheria Mkoo wa Serikali amesema na kwa mujibu wa Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali kifungu cha 21 ushauri wake *is binding*. Kwa hiyo, nikiwa Waziri ushauri wa Mwanasheria Mkoo wa Serikali *is binding* mpaka a-overcatch na maadam haja-overcatch basi huo ndio msingi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala hili ambalo linatugusa sisi wote nalo ni suala la mifugo inayokamatwa katika maeneo ya hifadhi. Hili kama nilivyosema ni suala nyeti, ni suala zito, ni suala ambalo huwezi kulipuuza ni lazima nikitumia lugha yako ufungue masikio mawili. Nini maana ya kufungua masikio mawili, uko upande wa sheria na uko upande wa utekelezaji wa sheria. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa kwa upande wa sheria na wewe unaifahamu hii sheria vizuri kabisa, hii sheria ni miongoni mwa sheria iliyochukua zaidi ya miaka nane kutungwa. Ilikuwa na majadiliano mengi na miongoni mwa maeneo ambayo yalizungumzwa yalikuwa eneo hili hili tunalolizungumza leo la mifugo kuingia katika maeneo ya hifadhi na kulishwa na hatua gani zichukuliwe na limeendelea kuwa hivyo. Ni kweli kabisa kifungu cha 18 cha sheria kinazuia mifugo kwenda kulishwa ndani ya maeneo ya hifadhi na kinaeleza kabisa mifugo ikitamatwa ndani ya hifadhi suala zima la kutaifishwa.

Mheshimiwa Spika, Sheria hiyo hiyo kama unakumbuka ilijadiliwa sana kwamba ziko nyakati na yako majira ambayo kweli kabisa kunakuwa na ukame uliopitiliza, malisho hayapatikani na inawezekana kabisa bila kuchukua hatua mifugo mingi ikafa. Ndio maana kwa busara ya Bunge wakati ule kwenye kifungu cha 21 kilisema; *"Any person shall not serve with the written permission of the director previously solved and obtained graze any livestock in any game controlled area."* (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa mara nyingi jambo hili limekuwa pia halijaangaliwa kwa hiyo yako mazingira kwa sababu amesema kuna maeneo watu wanaruhusiwa kuingia, kuna maeneo watu wanazuiwa. Si ajabu huko walikoruhusiwa kuingia haikuwa suala la rushwa au *arbitrariness* lilikuwa uwezekano mkubwa sisemi ni hivyo kwamba walipata ruhusa katika kufanya jambo hilo na ikitokea hivyo watu hao basi wametekeleza matakwa ya sheria. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mifugo inayokamatwa kwenye kifungu cha 111 cha Sheria kinaruhusu utaifishaji wa mifugo na nisikisome kimeeleza kwa kirefu sana. Kifungu hicho hicho cha 111(4) kinaeleza wazi mifugo hii ikikamatwa inachukuliwa kuwa ni mali ya Serikali na baada ya hapo ukienda kifungu cha 114(2) kinahusu suala zima la uuzaji wa hiyo mifugo na kinasema wazi; *"The value of a livestock shall be calculated on the basis of the normal price of the livestock on a sale in open market between a buyer and a seller independent of each other."*

Mheshimiwa Spika, lazima tukiri, eneo hili ni mionganini mwa maeneo ambayo yametatiza sana na yamewakera watu wengi kwamba mifugo imekamatwa, lakini kwenye mnada kumekuwa na mazingira yanayoonesha ama bei ilipangwa au imeuzwa kwa bei ya chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kulizingatia hilo nipende kulieleza Bunge hili kwamba Serikali jambo hili imelisikia na imelizingatia. Kesi nyingi hizi ziko tayari kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ambaye kwa mujibu wa Katiba ana mamlaka ya mwisho kuhusu uendeshaji wa kesi hizi, lakini alipokea malalamiko na bango kitita ninalo la kesi moja moja. Baada ya kuzichambua kesi zote amechukua hatua zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, hatua ya kwanza kama nilivyoeleza kwenye bajeti ya uvuvi, ameachia jumla ya ng'ombe 553 wanaomilikiwa na wafugaji wanne na mifugo hiyo imekwisharejeshwa, na hizo kesi nne baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka kuzipitia ameamua kutokukata rufaa. Hakuona kama kuna sababu ya kukata rufaa na mara moja mifugo hiyo imeachiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna jumla ya kesi tano zina rufaa katika Mahakama ya Rufani ambapo Mkurugenzi wa Mashtaka amekata rufaa kupinga uamuzi wa Mahakama Kuu na nimemuomba Mkurugenzi wa Mashtaka nielewe ni kwa nini katika hizi kesi tano amekata rufaa/amekwenda Mahakama ya Rufani. Tatizo hapa siyo suala la ng'ombe, ni suala la tafsiri ya sheria iliyotolewa na Mahakama Kuu ambayo

Mkurugenzi wa Mashtaka anaamini ikibaki ilivyo inaweza kuwa na madhara makubwa baadae kwa uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, pia ziko kesi nne ambazo washtakiwa wenyewe wamekata rufaa Mahakama Kuu kupinga uamuzi wa Mahakama ya Wilaya kuwatia hatiani na kutaifisha mifugo. Katika eneo hili Mkurugenzi wa Mashtaka ameahidi kukutana na watu hao na kuhakikisha kwamba rufaa zao zinasikilizwa mapema ili kuhakikisha kwamba wakishinda na kama ye ye hatakuwa na sababu ya kukata rufaa mifugo hiyo pia iachiwe. Kesi hizo moja itatajwa kesho tarehe 23/5 na nyngine tarehe 30 Mei.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naamini kabisa tarehe 23/5 na 30/5 kesi hizi nne za rufaa zitakuwa zimepatiwa ufumbuzi ambao ama unaweza ukaelekea mifugo hiyo kuachiwa kama wale wenyewe kesi wataelewana kwamba rufaa hiyo isiendelee na Mkurugenzi wa Mashtaka akiona hana sababu ya ye ye pia kukata rufaa. Kwa hiyo, ningesihi tu tusubiri hiyo kesho na tarehe 30 Mei tuone hizo rufaa nyngine nne zimekwendaje.

Mheshimiwa Spika, pia zipo jumla ya kesi 23 kati ya 27 ambazo watuhumiwa walilipa faini bila kupelekwa mahakamani na wakarejeshewa mifugo yao. Pamoja na kulipa faini ambayo ni kati ya shilingi 10,000 mpaka 300,000 lakini hata katika kesi hizo kumekuwa na malalamiko. Malalamiko hayo hatukuyapuuza na moja ya kesi iliyolalamikiwa ambayo ilielezwa kwamba mke wa mfugaji huyo alipigwa risasi na askari pori kisa alikuwa anafuatilia maeneo ya malisho na kwamba hakuna hatua iliyochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchunguzi uliofanyika na kupata majibu jana, taarifa hizi si za kweli kwani mama huyu alipigwa risasi na mtu ambaye sitaki kumtaja jina ambaye si askari na amefunguliwa kesi ya mauaji namba 27 ya mwaka 2017. Natoa huu mfano tu kuonesha kwamba ni lazima tufanye uhakiki wa kina ili tusimuonee mtu, lakini pia tusilee uzembe ambao unaweza kuwepo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa hatua nyingine ambayo kwa kuzingatia unyeti wa jambo hili ambalo tumeona kama Serikali tulichukue ni kuhakikisha kwamba tunakutanisha wadau wote, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Mifugo na Uvuu, Ofisi ya Mashtaka ya Taifa na Ofisi ya Rais TAMISEMI ili kuandaa mwongozo maalum ambao utakaotumika katika masuala yote yanayohusu mifugo inayoingia ndani ya hifadhi. Ni jinsi gani ukamataji ufanywe, ni jinsi gani mifugo hao watunzwe na jinsi gani ya kuharakisha kesi na baada ya kesi nini kitokee.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tumebaini kwamba mara nyingi mambo haya yanapofanywa kwa mtindo wa *operation* yanapokosa mwongozo wakati mwingine hutokeaa hitilafu, na hitilafu hizo ili tuzitatue basi vyombo vyote hivi vitakutana kwa pamoja na baada ya hapo tutakuwa na *standard operating procedure* na *standard operating manual* ambayo itaongoza shughuli zote zinazohusu mifugo kuingia ndani ya hifadhi na kulisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ushahidi, kwa sababu moja ya sababu ambazo zimekuwa zinapelekea mifugo hii kukamatwa na kubakizwa ni ili zitumike kama ushahidi mahakamani. Naomba niliahidi Bunge lako kwamba nitatafuta mimi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuonana na Jaji Mkuu ili tuone utaratibu mwingine unaoweza kutumika katika ukusanyaji wa ushahidi na utunzaji wa ushahidi ili baadaye uweze kutumika Mahakamani bila kuvunja sheria za nchi ili tusilazimike labda wakati wote kuwa na mifugo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mkurugenzi wa Mashtaka anasema alipeleka shauri hili Mahakama ya Rufaa kuiomba Mahakama ya Rufaa iruhusu mifugo ikikamatwa na kama kesi itachukua muda mrefu iuzwe, ile fedha itunzwe ili wafugaji wakishinda warudishiwe fedha lakini wale wafugaji waliohusika walipinga utaratibu huo kwamba wangependa wabaki na wale ng'ombe wao wenyewe na sio fedha, lakini hilo nalo pia tutalijadili na mamlaka husika.

Mheshimiwa Spika, ni kweli mifugo inapobaki kwa muda mrefu ili itumike kama ushahidi, mingi inakuwa na hata kesi inaposikilizwa, mifugo hiyo inakuwa imekufa na ikishinda, Serikali yenye we inakuwa haina mifugo na wale wafugaji wanakuwa hawana mifugo. Lakini kwa sababu ni suala la Mahakama, mniruhusu tu ili mimi na Mwanasheria Mkoo wa Serikali tukae tumwombe Jaji Mkoo aone ni utaratibu gani mpya unaoweza kutumika katika kutunza ushahidi bila kuwashikilia ng'ombe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni jambo ambalo lipi mikononi mwa Jaji Mkoo, siwezi kulisemea. Ninachowea kusema ni kwamba tutakwenda kushauriana naye halafu ye ye atoe maamuzi ili ikiwezekana pasiwe na ulazima wa ng'ombe kukaa hata miaka miwili wakati wanasubiri kesi ili njia nyine nyingine itumike. Pia huwa kuna mtindo wa kuhakikisha iwapo mfugaji atashindwa ni jinsi gani Serikali ina-recoverna iwapo mfugaji atashinda ni namna gani anarudishiwa fedha.

Mheshimiwa Spika, nimechukua muda mrefu kidogo kulieleza hili kwa sababu ni suala ambalo linagusa maisha ya watu, *livelihood* yao na ustawi wao na Serikali haiwezi kulifumbia macho, lakini kwa mujibu wa sheria ilivyo, hivi ndivyo inavyotakiwa kuwa lakini tutachukua hatua zinazostahili ili kuzikamilisha. Mara kila kesi tukayoshindwa Serikali na ambapo hatutakata rufaa, mifugo hiyo itaachiwa mara moja na pale tutakapolazimika kukata rufaa, basi tutajiridhisha kwamba zipo sababu *compelling* za sisi kukata rufaa ili kuhakikisha tunafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa wafugaji, ningerudia tena kuwasihhi wafugaji wasiingize mifugo katika maeneo ya hifadhi na wanapolazimika kufanya hivyo kwa sababu ya ukame uliopitiliza, basi watumie utaratibu wa sheria wa kuomba kibali na wakipata kibali hicho na masharti maalum wanaweza kulisha mifugo yao mpaka hali hiyo ya ukame inapoweza kuwa imebadilika.

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe natoka kwenye kundi la wafugaji na labda ndiyo maana naweza kuonekana

naongea hivi, lakini Watanzania waelewe kwamba sifanyi hivyo kwa sababu pia natoka kwenye jamii inayofuga, lakini tunajua kwamba mifugo ni muhimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi kama wewe ni wahifadhi, maana yake pia tunajali hifadhi zilizopo kwa sababu na zenyewe ni sehemu ya maendeleo yetu. Kwa hiyo, ni lazima tuwe na uwiano kati ya uhifadhi ambao ni muhimu sana lakini pia kuendeleza sekta ya ufugaji. Nawasihi sana wafugaji kwa kiasi kikubwa kabisa *wa-comply* na sheria. Na sisi upande wa Serikali tutajitahidi kabisa kuhakikisha kwamba sheria iliyopo haitumiki kwa namna ambayo inaleta madhara yasiyostahili na pale kwenye vitendo vya rushwa au uzembe, tutachukua hatua haraka na tuwaombe watu watoe taarifa ili *PCCB* na mamlaka nyingine zichukue hatua inayostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria. Tunakushukuru sana kwa kutupatia maelezo kwa urefu kuhusu suala hilo ambalo kwa kweli linagusa mioyo ya watu wengi.

Tunakushukuru sana na kwa kweli tunawaombea mwende mkaliangalie. Kwa sababu kama mpaka game *controlled areas* ziko *covered* kwamba ni hifadhi, kwa hiyo, ng'ombe wakiingia wanabanwa na sheria hiyo, maana yake ni kwamba kutoka *Lake Natron* mpaka mpaka wa Serengeti ile ni *game controlled area* yote. Maana yake ng'ombe wowote waliopo Loliondo, yaani wanatakiwa wataifishwe *in a way*, wauzwe. Kuanzia Simanjiro yote mpaka Arusha ni *game controlled area*. Kwa hiyo, maana yake ng'ombe wote wa maeneo hayo wakamatwe. Tuangalie vizuri eneo hilo. (*Makofi*)

Tunawashukuru sana kwa kweli kwa mwanga uliotupatia Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria. Mheshimiwa Naibu Waziri, dakika 20, Mheshimiwa Hasunga, tafadhalii. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ufanuzi mbele ya Bunge lako tukufu kuhusu baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa kujadili hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema ya kuwa hapa kwenye Bunge lako tukufu kujadili bajeti ya Serikali. Aidha, nachukua fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kunitfea kuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vilevile namshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo wanayoitoa katika kuendeleza na kuboresha uhifadhi nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe mwenyewe na Naibu Spika kwa kuliongoza vyema Bunge letu la Kumi na Moja katika Awamu ya Tano ya uongozi wa nchi yetu.

Aidha, kwa namna ya pekee napenda kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Nape Moses Nnauye na Makamu wake Mheshimiwa Kemilembe Julius Lwota na Waheshimiwa Wajumbe wote kwa namna ambavyo wameendelea kuishauri Wizara yetu ili kuimarisha sekta ya maliasili na utalii ifikie dira na dhima yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia naomba kuchukua nafasi hii kuishukuru sana familia yangu na watoto wangu ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakinombea, wakinishauri na kunipa faraja katika kipindi chote ambacho nimekuwa nikifanya kazi hii kama Naibu Waziri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kukishukuru chama changu, Chama cha Mapinduzi, Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Mbozi kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakinisaidia katika kutekeleza majukumu yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawashukuru sana wapiga kura wa Jimbo la Vwawa kwa muda mrefu wamenikosa na wamekuwa hawana muda wa kutosha wa kukaa na mimi, lakini naomba niwaambie kwamba nipo pamoja nao na ninaendelea kutekeleza majukumu ya kitaifa na wao waendelee kutekeleza majukumu yale mpaka hapo Mungu atakapopenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kutoa ufanuzi wa baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamechangia katika kuboresha bajeti yetu hii. Kwa kweli niseme Waheshimiwa Wabunge wametoa michango mizuri sana. Michango yao inafaa sana na kwa kweli kama tutaweza kuitumia michango yote hii ni imani yangu kabisa tutaboresha uhifadhi na tutaboresha utalii wetu katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu muda ni kidogo sana, hatutaweza kutoa ufanuzi wa hoja zote zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Naomba nichukue nafasi hii kutoa ufanuzi wa hoja chache ambazo Waheshimiwa Wabunge wamechangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ufanuzi mzuri ambao ameutoa juu ya migongano, sheria na kama sheria zilivunjwa na kadhalika. Pamoja na Waziri wa Katiba na Sheria kwa jinsi ambavyo wamefafanua hoja mbalimbali, kwa kweli tunawashukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nianze na sekta ya uwindaji wa kitalii; kumekuwepo na hoja nydingi sana zinazohusu juu ya uwindaji wa kitalii. Wapo Waheshimiwa Wabunge ambao kwa undani kabisa na kwa dhati wamechangia vizuri sana na wengine wakasema hii biashara sasa imedorora ni kwa

sababu labda hatua ambazo zimechukuliwa hazikuzingatia sheria. Naomba niseme kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, biashara ya uwindaji wa kitalii inaongozwa na sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ambayo Serikali imeiweka na hiyo ndiyo inayotu-*guide* namna ya kuendesha uwindaji wa kitalii nchini. Katika Sheria Namba 5 ya mwaka 2009 na Kanuni zake za mwaka 2015 zinatoa namna ya uwindaji wa kitalu utakavyoendeshwa kwenye nchi hii, namna vitalu vitakavyogawanywa na vitalu vingapi vitakuwa ni vya wenyehi, labda ni makampuni mangapi ya nje yatakuwepo? Kwa hiyo, sheria ile inafafanua vizuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na hoja kwamba Serikali ilifuta vibali...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumsikilize Mheshimiwa Naibu Waziri anapotujibu hoja zetu. Tunaleta hoja, halafu wakati wa kujibiwa hatusikilizi na hata kama unaongea na mwenzako, punguza sauti. Turudie hili jambo mara ngapi Waheshimiwa Wabunge?

Mheshimiwa Naibu Waziri endelea.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na hoja kwamba mnamo mwezi Oktoba, 2017 Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii ilibadili utaratibu wa kugawa vitalu kutoka kwenye ule utaratibu wa zamani wa kiutawala (*administrative allocation*) kuelekea kwenye mfumo mpya wa mnada. Kwa nini wakasema kwamba kumekuwa na ukiukaji wa sheria?

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kusema kwamba kwanza ni kweli kabisa makampuni ya uwindaji yalipewa kibali cha kufanya uwindaji kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2018 mpaka mwaka 2022. Wakati wanapewa hiyo mikataba ya miaka mitano, kwenye barua kulikuwa na maelekezo mazuri kabisa ambayo yalisema kwamba kufuatia mageuzi yanaoendelea ndani ya Wizara

katika kuimarisha Sekta ya Uwindaji wa Kitalii, Waziri mwenye dhamana ya Maliasili na Utalii anaweza kubadilisha wakati wowote na imeandikwa na kufafanuliwa vizuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutafakari namna sekta ya utalii ambavyo imekuwa ikiendeshwa nchini, tuliridhika kabisa kwamba bado kuna upungufu ambaeo upo ambaeo ni lazima tuurekebishe ili uendane na hali halisi iliyopo kwa sasa. Moja ya sababu iliyowekwa katika ile barua ya mkataba wa awali, ilikuwa ni kwamba kwa sasa hivi vitalu vya uwindaji viko chini ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (*TAWA*), lakini *TAWA* ndiyo inaanizishwa na kwa sababu ndiyo inaanizishwa, itakuja sasa na utaratibu mpya wa namna ya kusimamia hivyo vitalu, ndiyo maana kulikuwa na hicho kigezo kwenye ile barua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kuangalia kile kigezo ndiyo maana tukaamua kwamba sasa hebu tusitishe ili tuje na utaratibu mzuri kabisa ambaeo utakuwa na manufaa makubwa mawili; kwanza utaongeza mapato ya Serikali kwa sababu sasa tutafanya kwa mnada. Kwa hiyo, badala ya vile vitalu vingine kuuzwa labda dola 5,000, dola 15,000 na dola 30,000; vile vya daraja la kwanza kuuzwa dola 60,000, sasa unaweza ukakuta baadhi ya vitalu vikauzwa mpaka hata dola 300,000. Kwa hiyo, tukaona Serikali itapata mapato makubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tukasema sasa lazima hili tulifanyie marekebisho ili liendane na kwanza na tamko ambalo lilikuwepo kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi kwamba vitalu vya uwindaji vitaendeshwa kwa njia ya uwazi na kwa njia ya mnada ili kusudi kusiwe na milolongo ya rushwa na nini, watu waamue wenyewe na wapange bei wenyewe. Basi tukaona kwamba hili ni la msingi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusitisha, wadau wa uwindaji walitoa malalamiko yao wakatuambia hii sasa *frustrate industry*, na sisi tukaa tukakubaliana, tukasema kweli kuna hoja. Walipotueleza tukaelewa na ndiyo maana

tukasema sasa wakati tunakwenda badala ya kwamba tusitishe mwezi wa kumi ule halafu mwezi wa kwanza tuwe tumetoa, tutashindwa. Ndiyo maana tukaamua kufanya *extension* ya ule muda wa kwanza, tukaongeza miaka miwili wakati haya mabadiliko sasa yanaendelea kufanyika. Ndiyo maana wamepewa tena wameongezewa miaka miwili. Wameongezewa katika ile baada mitano baada ya kumalizika, wameongezewa miwili. Katika kipindi hiki, Serikali sasa itakuja na utaratibu mpya wa namna ya tutakavyoendeshwa kwa minada.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na hoja kwamba baada ya kutangaza hivi, kuna matatizo yamejitokeza; wakasema vitalu vingi vimerudishwa. Naomba nilitaarifu Bunge lako tukufu kwamba sekta ya uwindaji wa kitalii sasa hivi inakabiliwa na changamoto nydingi sana hapa, siyo tu kwa Tanzania bali kwa dunia nzima. Kuna mambo mengi yanaendelea katika hili. Kwanza wawindaji wa kitalii ni kweli kabisa ni wale wale ambao wapo nchi zote, ukiwa-*frustrate* hapa watahamia kwingine. Kwa hiyo, ni kweli lazima tuwalinde vizuri.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna kampeni zinaendelea duniani, kuna watu wanaosema wanalinda haki za wanyamapori. Hawa wamekuwa wakifanya kampeni kila mahali kwamba kuwinda wanyama ni dhambi kubwa. Hizo kampeni za *anti-hunting* zinaendelea. Makampuni mengi duniani sasa hivi yanafanya kampeni. Kwa hiyo, hiyo kwa kiwango fulani imeathiri kushuka kwa biashara ya uwindaji wa kitalii. Hiyo ni sababu ya kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sababu ya pili, baadhi ya nchi ambazo ndiyo wadau wakubwa wa uwindaji wa kitalii zimepiga marufuku baadhi ya *trophy* ambazo zilikuwa zinaenda ikiwemo Marekani na nchi za Ulaya (*European Union*) zimepiga marufuku na baadhi ya nchi juzi juzi tumesikia hata China wamepiga marufuku. Kupiga marufuku kule kutaathiri moja kwa moja biashara ya uwindaji wa kitalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sababu ya tatu, sheria yetu ile ilikuwa inasema asilimia 85 lazima ziwe ni kampuni za wazawa na lengo ilikuwa ni kuwasaidia wazawa ili waweze kumiliki hizi kampuni na wapate mapato makubwa kusudi wageni wawe na asilimia 15 tu ya makampuni. Ni kweli ilikuwa ni sheria nzuri na wazawa wengi walichukua, walipata hii, lakini kutokana na changamoto za biashara hii, kampuni nyingi za kizawa zimeshindwa kufanya hii biashara, ndiyo maana zikafikia hatua ya kuanza kuzirudisha.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa mpaka sasa hivi ni vitalu 81 vimesharudishwa, vimekosa wawekezaji. Huko nyuma baadhi ya makampuni yalikuwa yanunue hivi vitalu halafu tena yanavikodisha kwa Wazungu. Sasa hivi hiyo biashara haipo. Na sisi tunataka kwamba wale wale wanaokodi, wenyewe wazingatie sheria, sera unaendesha wewe mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hilo, ndiyo maana sasa kumekuwa na kushuka kwa hii biashara ya wenzetu. Kwa hiyo, ndiyo maana vitalu vingi vimerudishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tulichokifanya, sasa hivi tunaendelea kuuandaa utaratibu, mojawapo, vitalu hivi 81 vilivyorudishwa navyo pia tutaviingiza kwenye huu mnada ambao utakuja ambao tutautumia kusudi watu waweze kufanya hivyo. Pia katika hilo lazima tuendane na sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na hoja kwamba baada ya wale wawekezaji waliokuwa kwenye vile vitalu walipoondoka kuna changamoto zimejitokeza. Watu wakasema vitalu vimebaki bila ulinzi, bila nini.

Mheshimiwa Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba wale wawekezaji wakati wanaendesha au wanamiliki vile vitalu na Serikali pia tulikuwa bado tuna watumishi wetu wanaoshirikiana na zile kampuni za ulinzi. Baada ya wale kuondoka, sasa hivi tunabaki sisi wenyewe tunaendelea kulinda.

Mheshimiwa Spika, pia katika kile kikosi maalum cha Kitaifa ambacho kilianzishwa, yaani kile ambacho tumekuwa tukizunguka nchi nzima, wamekuwa wakipambana na uwindaji haramu, basi kampeni hiyo imefanyika vizuri na ulinzi umefanywa vizuri hasa kwa kutumia intelijensia. Sasa hivi matukio ya ujangili yamepungua kwa kiwango kikubwa sana. Kwa hiyo, vile vitalu vingi vipo salama na Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba inavilinda hivyo vyote ili viwe na manufaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunadhani hata baadhi ya yale mapori ya akiba, Mheshimiwa Waziri atayasemea, tunafikiria yapandishwe hadhi kama baadhi ya Waheshimiwa walivyosema, yaende kufikiwa kuwa ni Hifadhi za Taifa, yakifika hapo tutakuwa tumefikia hatua nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine kutokana na changamoto hizi ambazo zinaendelea duniani, tunataka tuanze kuipunguza hii biashara ya uwindaji wa kitalii, tuanze kwenda kwenye utalii wa picha zaidi. Utalii wa picha zaidi utaleta manufaa makubwa na utalinda hata hizo haki za wanyamapori kama ambavyo watu wengine wamekuwa wakisema.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana katika baadhi ya maeneo na katika mradi ambao tunakuja nao ule wa kuinua utalii wa Kusini (*Regrow*) ambao unahusu mbuga ya Selous, Mikumi, Udzungwa na Ruaha ambao tunaanza nao, kwa asilimia kubwa tunataka tuhakikishe hata kule Selous, Kanda ya Kaskazini tulete utalii wa picha badala ya utalii wa uwindaji kusudi tuweze kupata mapato makubwa. Ninaamini kabisa hiyo itasaidia sana katika kuleta hayo manufaa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitaka tu nitoe ufanuzi huo kwamba yale ambayo tuliya fanya, tuliya fanya kwa mujibu wa sheria na kwa sababu barua, au mkataba wenyewe ulikuwa una-*provide* ndiyo maana hayo yalifanyika.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo ningependa kutoa ufanuzi kidogo ni kuhusu sekta ndogo ya misitu. Waheshimiwa Wabunge, wamezungumzia mambo mengi sana kuhusiana na sekta ya misitu na mambo mengi. Kwa kweli nawashukuru sana na niwapongeze. Ni ukweli usiofichika kwamba sekta ya misitu ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi hii. Misitu inachangia asilimia nne.

Mheshimiwa Spika, hebu tuangalie jinsi misitu yetu inavyosimamiwa, kuna Serikali Kuu; Serikali Kuu ina hifadhi 455, lakini kuna nyingine ziko chini ya Halmashauri kama 167; lakini Serikali za Vijiji zina hifadhi 1,200. Sasa unapokuwa na hifadhi ambazo ziko *scattered*, zina mamlaka tofauti, lazima kuwe na changamoto. Ndiyo maana tukaamua sasa kupitia upya sera ya misitu ili hii sera ikipitiwa upya, ikihuishwa, tulete sasa sheria ambayo itahakikisha kwamba hii sekta ya misitu inatoa mchango mkubwa sana katika uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo basi, ndiyo maana kuna mapendekezo, hata Kamati nafikiri imependekenza kwamba tuwe na mamlaka moja. Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa hiyo hoja. Tuwe na mamlaka ya kusimamia misitu yote Tanzania. Hii itatusaidia sana. Misitu ndiyo uhai, bila misitu hakuna maji, bila misitu hakuna maisha na kwenye sekta hiyo ndiyo tuna nyuki, tuna asali, tuna vitu vingine vingi tu.

Mheshimiwa Spika, naomba niliambie Bunge, sasa hivi kwenye sekta ya nyuki hatujaiendeleza, lakini tunaamini tutaiendeleza vizuri sana. Mkitupa fedha tutaiendeleza sekta hii vizuri. Kwa sababu kwenye nyuki pale, najua hata baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hawajui, nyuki wanatoa maziwa ambayo ni mazuri sana. Pia kwenye nyuki pale tutapata nta, asali na mambo mengi sana, soko ni kubwa. Uzalishaji wa asali ukiongezeka, nta ikiongezeka, maziwa yakiongezeka na baadhi ya kemikali ambazo zinatokana na mazao haya, kutasaidia sana katika kuleta fedha kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine liliilojitokeza katika upande wa misitu ni matumizi ya mkaa. Waheshimiwa

Wabunge wengi wamelalamika kwamba kweli sijui kuna sehemu wanakamatwa, mikaa inazuiwa, mikaa imefanya nini; naomba nilitaarifu Bunge lako tukufu kwamba sisi tulichokifanya, hatujazuia matumizi ya mkaa. Tunasema kwa sababu asilimia kubwa ya Watanzania wanatumia mkaa, basi lazima tuwe na utaratibu mzuri wa maeneo ya upatikanaji wa mkaa. Tukiruhusu kila mahali kila mtu anauza mkaa, kila mtu anavuna, basi hiyo inakuwa ni changamoto katika uhifadhi wa misitu yetu.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana sasa tunasema kwamba tunataka wananchi wapewe elimu, wawe na meko yanayotumia mkaa kidogo. Pia tuwe na *centres ambazo* zina vibali wamelipia tozo zinazostahili, tuwe tunajua kwamba wanaauza mkaa. Tatu, tuje na elimu. Sasa hivi tumefanya utafiti tumegundua kuna baadhi ya miti ambayo tutahamasisha ipandwe kila mahali ambayo inachukua kati ya miaka mitatu na minne, inafaa sana kwenye kuni na inafaa sana katika uzalishaji wa mikaa. Kwa hiyo, hiyo misitu nayo tutaisambaza, elimu hiyo tutaitoa ili wananchi wa nchi hii wahamashishe namna ya matumizi bora ya hizo kuni na mikaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala ambalo limejitokeza kwamba boda boda wanakamatwa kila mahali wakiwa wamebeba mkaa, magari yanakamatwa; nataka niseme hivi, kwa mujibu wa Sheria ya Usalama Barabarani, bodaboda hawaruhusiwi kubeba mkaa. Hawaruhusiwi kwa mujibu wa sheria, yale hawaruhusiwi kabisa! Kwa hiyo, tunachosema, magari yaliyoruhusiwa yenye vibali ndiyo hayo yaweze kuruhusiwa kusambaza mkaa katika vituo mbalimbali na wananchi waelekezwe wapi mkaa halali unapatikana ili wale wanaochukua kwa rejareja wachukue katika hayo maeneo.

Mheshimiwa Spika, naamini kwamba hilo litapunguza changamoto ambazo zipo katika suala hili la matumizi ya mkaa. Ni muhimu sana wananchi wakael mishwa matumizi ya mkaa vizuri, tuwe na majiko mazuri, tuwe na namna ya kuendeleza hii sekta, itatusaidia sana katika maisha yetu na itatoa mchango mkubwa katika uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, viwanda vingi vinavyotokana na misitu; sasa hivi tuna viwanda vingi vinatokana na mazao ya misitu. Ni imani yangu kabisa kwamba hii Sekta Ndogo ya Misitu lazima tuiimarishe ili vile viwanda vyote vitoe mchango mkubwa kwa sababu Sera yetu ya Taifa inataka tuwe ni nchi ya viwanda. Sasa viwanda vinavyotokana na mazao ya misitu lazima viimarishwe na vihakikishe kwamba kwa kweli vinatoa mchango ule unaohitajika.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba baadhi ya watumishi katika maeneo ya hifadhi wamekuwa wakitoa rushwa...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, nashukuru sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Hasunga, tunakushukuru sana kwa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. (*Makofii*)

Sasa nimwite mtoa hoja, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, Waziri wa Maliasili na Utalii, karibu sana. Mheshimiwa Waziri una nusu saa. (*Makofii*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii niweze kuhitimisha hoja yetu ya Wizara ya Maliasili na Utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutumia fursa hii kukushukuru wewe mwenyewe pamoja na Mheshimiwa Mtemi John Chenge, Mbunge na Mwenyekiti wa Bunge kwa kutuongoza vyema kwenye mjadala huu toka tulipoweka mezani mapema jana. Pia nitumie fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa kujadili hotuba ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, nitumie pia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Mbunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhii, Maliasili na Utalii pamoja na Kamati yake yote kwa kuchambua, kujadili na kutoa maoni na ushauri kwenye maeneo mbalimbali yaliyohusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara yetu kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na pia kutoa maoni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango ya maandishi lakini pia kwa michango ya kusema hapa Bungeni moja kwa moja. Kimsingi Wizara yetu imepokea uchambuzi, maoni na ushauri wao. Niwahakikishie tu kwamba tutauzingatia kwa kina na kwa uzito wake katika utekelezaji wa majukumu yetu katika siku zinazokuja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia binafsi niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwa kwa kweli siku mbili za kukaa hapa mbele zimekuwa ni somo kubwa sana kwangu kwenye kazi hii ya dhamana ya Wizara ya kuwa kama Waziri kwenye Wizara ambayo nimepewa na Mheshimiwa Rais niweze kuwatumikia Watanzania wenzangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, japokuwa michango mingine nikiri ilikuwa mikali kweli kweli, lakini nilifarrijika kwamba michango hii imenipika vizuri zaidi na ninaamini baada ya leo nitakuwa Waziri mzuri zaidi kuliko ilivyokuwa juzi kabla sijasimama mbele ya Bunge lako tukufu na kutoa hoja ya Wizara yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninaamini michango ya Waheshimiwa Wabunge imenipitisha kwenye tanuru ambalo linazidi kuongeza uwezo na umahiri wangu wa kukabiliana na changamoto zilizopo kwenye sekta hii nyeti, kwenye uchumi na maendeleo ya Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo wahenga waliwahi kusema kwamba ili dhahabu iweze kung'ara vizuri ni lazima ipite kwenye tanuru lenye moto mkali na mimi

ninashukuru sana kwa fursa ya kupita mbele ya tanuru la Bunge lako tukufu ambapo nimepikwa na kuiva vizuri zaidi tayari kukabili ana na changamoto mbalimbali zilizopo kwenye seka hii nyeti. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Wabunge waliochangia kwenye Wizara yetu jumla walifika 99 kati yao waliochangia kwa kuongea moja kwa moja hapa Bungeni ni 42 na 57 walichangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, naomba niwahakikishie tu kwamba maoni yao tumeyapokea na pamoja na hoja ambazo zimetolewa ufanuzi na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria na Mheshimiwa Naibu Waziri na nyingine ambazo nitazifafanua mimi mwenyewe hapa, naomba kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba hoja nyingine tutawasilisha majibu yake kwa maandishi kwa sababu hatutaweza kufafanua maeneo yote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyoguswa na Kamati yetu ni pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo, migogoro ya mipaka na ushirikishaji katika zoezi la uwekaji vizingi, ukokotoaji wa takwimu za idadi ya watalii wanaotembelea Tanzania, utozaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*), uwindaji wa kitalii, biashara ya wanyamapori hai, utangazaji wa utalii, ukusanyaji wa mapato, mgongano wa Sheria za Uhifadhi na sheria nyingine, hali ya jumuiya za hifadhi za wanyamapori, uingizaji mifugo kwenye maeneo ya hifadhi, uharibifu wa misitu na matumizi mseto ya eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia baadhi ya hoja ambazo zimewasilishwa na Waheshimiwa Wabunge ziligusa maeneo ya biashara ya wanyamapori hai, mradi wa umeme wa Rufiji, kurejesha Wizara ya Maliasili na Utalii sehemu ya uvuvi ili kuendeleza utalii wa fukwe, migogoro ya mipaka na ushirikishaji katika zoezi la uwekaji vizingi, mgogoro wa Pori Tengefu la Loliondo, kuendeleza utalii Kusini mwa Tanzania, wanyamapori wakali na waharibifu, uwindaji wa wenyeji,

ulinzi wa maeneo ya mapito, mtawanyiko na mazalia ya wanyamapori, tozo ya pango kwenye hoteli zilizopo kwenye maeneo ya hifadhi na kodi na tozo mbalimbali kwenye sekta ya utalii.

Mheshimiwa Spika, nyingine ni kubaini na kuendeleza vivutio vya utalii, ushirikishaji kwenye uhifadhi wa maliasili, malikale na utalii, biashara ya mazao ya misitu, uwezo wa kusimamia uhifadhi wa maliasili, malikale na utalii, matumizi ya nishati ya kuni na mkaa, utangazaji utalii, maeneo ya hifadhi yaliyopoteza sifa kwa mfano Pori Tengefu la Wembele, uingizaji mifugo kwenye maeneo ya hifadhi, uendelezaji wa maeneo ya malikale na historia ya utamaduni wa makabila mbalimbali, kuimarisha mikakati ya uhifadhi wa vyanzo vikuu vya maji kwenye Mto Ruaha na mito mingine, matumizi mseto eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na changamoto ya utawala bora.

Mheshimiwa Spika, nitaomba nitumie fursa hii sasa kutoa ufanuzi kwenye baadhi ya maeneo mahususi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, rafiki yangu na mtani wangu alinipiga sana hapa jana. Napenda kutumia sehemu moja kuanza kufafanua kwenye hoja yangu kwamba mimi ni kiongozi kijana, ningepaswa kuwa *visionary* zaidi, lakini yeye alikuwa anasema mpaka jana alikuwa hajaona chochote kipyा ambacho kimeletwa na Waziri huyu kijana. Kwanza mimi sio kijana, labda nina sura tu ya ujana, lakini nilishavuka ujana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuleta kwenye *attention* ya Mheshimiwa Msigwa pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote mambo machache kadhaa ambayo katika kipindi hiki cha miezi nane tumeweza kuyabuni ya kuyaanzisha na mengi yapo katika hatua mbalimbali. Pengine ndiyo maana watu wengi sana wamekuwa wakishangaa hata Mawaziri wenzangu kwamba mbona Wizara ya Maliasili safari hii inapita taratibu fulani hivi ukilinganisha na miaka takribani mitatu mfululizo iliopita?

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba tumebadilisha sana namna ambavyo tuna-*approach* mambo kwenye Wizara hii toka tulipoteuliwa na zaidi tunatumia mbinu ya ku-*engage* wadau. Mbinu ya kushirikisha wadau pamoja na waathirika wa maamuzi mbalimbali ambayo tumekuwa tukiyafanya (*multisectoral stakeholders engagement*). Tunafanya sana mambo yetu kwa kushirikisha wadau.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mambo ambayo tumeanza kuyafanya ni pamoja na kubuni Tamasha la Urithi wa Mtanzania ambalo litafanyika kila mwaka hapa nchini na kwenye maeneo yote yale ambapo Watanzania ama marafiki zetu wanaweza kupenda kufanya ambapo litafanyika mwezi Septemba wa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Tamasha hilo tumelipa jina la *Urithi Festival*. Tuliteua Kamati ya wadau mbalimbali wa *media*, tasnia za utamaduni, mambo ya urithi na utalii na kuwashirikisha kubuni wazo la kuwa na tamasha ambalo litautambulisha utamaduni wetu sisi kama Watanzania kwamba tuna lugha yetu ya Kiswahili, lugha zetu za asili za makabila zaidi ya 120 tuliyonayo, mila na desturi zetu, historia yetu kama Taifa na Muungano wetu wa kipekee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengi ambayo tunaweza tukaelezea kuhusu Tanzania zaidi ya kuwa na aina moja tu ya urithi ambao ni urithi wa asilia, kibailojia (*natural heritage*) ambayo ni ya wanyamapori, uoto na uwanda, tunaweza tukazungumza pia kuhusu utamaduni wetu kuhusu mila na desturi, historia yetu na mambo kama hayo. Kwa hiyo, tumeamua ku-*designate* na kuutambua mwezi Septemba kama Mwezi wa Urithi wa Mtanzania na kilele chake itakuwa ni Tamasha la *Urithi Festival* ambalo litafanyika kila mwaka na tutaanza kulitekeleza mwaka huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika mwezi huu, mambo mengi yatafanyika ikiwemo matamasha ya ngoma za jadi, michezo ya kuigiza, matamasha ya muziki wa kizazi kipyaa, matamasha ya muziki wa dansi, matamasha ya filamu, matamasha ya

hotuba, ngonjera na vitu vingine mbalimbali ambavyo tumekuwa tukivifanya kama Watanzania.

Mheshimiwa Spika, pia katika mwezi huu kutapikwa vyakula nya Kitanzania, *menu* maalum ya vyakula nya asili nya Mtanzania kwenye mahotelii yote ya kitalii. Kwa hiyo, ndiyo maana tumesema tuna-*engage*wadau wa sekta hii ili waweze ku-*absorb* na kukubaliana na mawazo haya, waweze kushiriki kwenye tamasha hili kikamilifu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia katika mwezi huu mavazi yatakuwa ni ya Kitanzania, kama utapenda kuvalaa vazi la asili ya kimwambao, vazi la Kiswahili kama alivyopendeza Mheshimiwa Mtalea na Mheshimiwa Masoud, basi utavaa hivyo na kwenye mahotelii wanaweza wakavaa hivyo. Kama utapenda kuvalaa vazi la Kimasai, utavaa hilo; kama utapenda kuvalaa vazi la vitenge (*African prints*) utavaa vitenge ama khanga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, basi kwenye mahotelii yote ya kitalii, Balozi zetu, Ofisi za Serikali kutakuwa kuna mavazi ya aina hiyo kuanzia tarehe moja Septemba na lengo ni kuutambulisha utamaduni wetu, lakini pia tutapamba maeneo mbalimbali ya nchi na taswira mbalimbali za Utanzania wetu. Lengo ni kusherehekeea Urithi wa Mtanzania na mwezi Septemba tumeamua kufanya hivyo. Hili ni katika mojawapo ya mawazo tuliyokujanayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia lengo letu kufanya hivi, ni kuhakikisha tunaweka fungamanisho (*linkage*) la utalii wa wanyamapori (*wildlife*), maeneo asilia na utalii wa utamaduni. Lengo ni kuongeza mazao ya utalii ili watalii wawe na shughuli nyingi wanazoweza kuja kuzishuhudia Tanzania. Matamasha ya namna hii yanafanyika *South Africa* na Brazil.

Mheshimiwa Spika, kuna watu wanafahamu Tamasha la Samba huko kwenye nchi za kule Amerika ya Kusini, ni maarufu sana duniani na watu wanakwenda kule kipindi hicho cha tamasha hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kusudio la kuwa na tamasha hili ni kitu kama hicho ambacho kinafanyika nchi kama za Brazil na Mexico ambapo kuna mwezi wa urithi wa nchi zao kama huu tunaozungumza hapa. Hili ni katika mojawapo ya mawazo tuliyonayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili, tumekuja na wazo la kuhuisha mifumo ya kukusanya mapato na mifumo ya taarifa katika Wizara ya Maliasili. Tunatengeneza mfumo mmoja unaojulikana kama *MNRT Portal* ambapo ifikapo Julai Mosi mfumo huu utaanza kutumika. Malengo ni kukidhi matakwa ya llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi lakini pia kukidhi matakwa ya maagizo mbalimbali ya viongozi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais hapa alipokuwa anazindua Bunge hili alisema ni lazima tubuni mbinu ya kukusanya mapato kisasa ili kuhakikisha mapato hayavuji katika sekta ya utalii. Pia ni kukidhi matakwa ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano tulioupitisha hapa mwaka 2016 kwamba tutumie mifumo ya kielektroniki kukusanya mapato ili kuongeza tija katika ukusanyaji, lakini pia ili kuongeza urahisi wa mtu kufanya malipo ndani ya Serikali hususan sisi kwenye sekta yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumetengeneza mfumo mmoja ambao ndiyo walikuwa wanauzungumza Waheshimiwa Wabunge hapa, hata leo alizungumza Mheshimiwa dada yangu na shemeji yangu, Mheshimiwa Lucy Owenya kwamba kuwe kuna dirisha moja. Sasa dirisha tunalolitengeneza ndiyo huu mfumo wa kielektroniki. Kwa hiyo, ukitaka kulipa chochote kile kwenye sekta ya utalii, kila Idara ya Serikali tutakuwa tumetengeneza fungamanisho ambapo unaweza ukalipa kupitia kwetu na wao wakapata pesa zao ili kuongeza urahisi wa kufanya biashara kwenye sekta ya utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia kumekuwa kuna malalamiko mengi kwamba watalii wanalipa kwa mawakala huko nje ya nchi na sisi hapa pesa haziingii, lakini mtalii anakuja,

alishalipia kule, hapa anahudumiwa na pesa inabaki kule nje. Ili kuondoa hiyo, tuliona tukitengeneza mfumo mmoja wa malipo wa kielektroniki ambao pia utakuwa una *applications* mbalimbali zikiwemo za kwenye simu, zikiwemo za kwenye mtandao tunaweza ku-*capture* malipo yanayofanyika nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, pia tutaweza ku-*capture* taarifa, Kamati yetu ilizungumzia suala la taarifa, tutaweza ku-*capture* taarifa kwa sababu mfumo huu tutaufungamanisha na mifumo ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, nafikiri kila mtu anafahamu jitihada zinazoendelea kule Wizara ya Mambo ya Ndani kutengeneza *e-visa* na *e-migration systems* ambazo zitakuwa zimefungwa kule, lakini sisi tutazifungamanisha na mfumo wetu ili tuweze kukusanya taarifa sahihi na kwa wakati katika sekta ya utalii. Kwa hiyo, tunakoenda, changamoto kama hizi za takwimu kutokuwa sahihi hazitakuwepo tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo tumefanya na tunaendelea kulishughulikia ni suala la kuhuisha maeneo ya makumbusho pamoja na maeneo ya mambo ya kale kwani yamekuwa katika hali duni. Tumeona mfano mzuri wa utekelezaji wa mpango huu kwenye eneo la Oldivai Gorge ambapo Mamlaka ya Hifadhi ya eneo la Ngorongoro imeingia ubia na Idara ya Mambo ya Kale, pamoja Taasisi ya Makumbusho, wamejenga kituo kizuri sana cha makumbusho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *model* hii tumeona tu-*amplify* kwa sababu Idara ya Mambo ya Kale inapata bajeti ndogo, lakini ina maeneo nyeti yenye thamani kubwa sana kidunia ya kiutalii, tumeona tuwaunganishe na taasisi zetu nytingine ambazo zinafanya shughuli mbalimbali na zinaingiza kipato kikubwa ili waweze kuyaboresha yale maeneo ya mambo ya kale na maeneo ya makumbusho kwa ubia na hatimaye tuweze kuyatangaza kwa pamoja ukilinganisha na maeneo ya Hifadhi za Taifa za maeneo ya Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu ili tuweze kupata wageni wengi zaidi

watakaokuwa wanatembelea maeneo ya mambo ya kale na maeneo ya makumbusho.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri mkakati huu uko vizuri na tumeingiza kwenye bajeti hii. Kwa hiyo, kuanzia mwezi wa Saba, taasisi hizi ambazo zinauwezo mkubwa wa kipesa, zitaanza kufanya uendelezaji kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, eneo la makumbusho pia litaboreka na lengo ni kuongeza *productza* utalii (*tourism products*), mazao ya utalii, kwa sababu sasa hivi utalii kwa zaidi ya asilimia 80 umejikita zaidi kwenye utalii wa mambo ya wanyamapori. Sasa tunavyotanua wigo kufanya matamasha, lakini pia kuongeza makumbusho na kuboresha maeneo ya mambo ya kale, maana yake tunaongeza mazao ya utalii. Lengo letu tunapoongeza mazao ya utalii ni kumtaka mtalii anapoingia nchini akae muda mrefu zaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi wastani wa mtalii kukaa hapa nchini ni katи ya siku tisa mpaka kumi. Tunataka tunavyoongeza hizi *tourism products* mtalii a-spend muda zaidi. Kadri anavyozidi kukaa hapa nchini ndivyo anavyozidi kutumia zaidi dola zake na ndivyo anavyozidi kuacha pesa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaongeza mazao haya ili kuongeza kipato cha Serikali. Pia kadri maeneo ya vivutio yanavyoongezeka, wananchi pia wanaoishi jirani na maeneo haya nao wanapata shughuli za kufanya, watauza baadhi ya vifaa, watauza *souvenirs* wataweza na wenyewe kushiriki katika uchumi mpana wa utalii.

Mheshimiwa Spika, kwenye Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano tulioupitisha mwaka 2016 palizungumzwa kutokuwepo kwa *linkage* kati ya sekta ya utalii na maendeleo ya watu; na ndiyo maana pengine malalamiko yanakuwa mengi dhidi ya sekta hii kwa sababu pengine kuna baadhi ya jamii zinazozunguka maeneo yaliyohifadhiwa hazioni faida ya moja kwa moja ya uwepo wa maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kadri tunavyozidi kufungamanisha sekta ya utalii na maendeleo ya watu ndivyo ambavyo hata hii migogoro ambayo inajitokeza sasa tunarajia itazidi kupungua. Pamoja na mambo mengine mengi ambayo ningeweza kuyasema, lakini kwa faida ya muda nisiyaeleze yote kwa upana, naona muda nao unanitupa mkono, inatosha tu kutaja maeneo ya misitu ya asili ambayo ilipoteza hadhi kwenye Halmashauri, kwenye vijiji tumeiwekea mkakati wa kuifufua, mkakati wa kuitengea maeneo kwa ajili ya mkaa, Mheshimiwa Naibu Waziri amefafanua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia tumeanzisha utaratibu mpya wa kutengeza utambulisho wa Mtanzania (*destination branding*) ambapo tumetengeneza *slogan* ya *Tanzania Unforgettable* kwa kutumia wadau mbalimbali waliobobea katika eneo hili la kufanya *branding*. Billa shaka mmeona hata kwenye mabegi tumewapa ndio tunaanza hivyo kuitangaza *brand* yetu. Pia tutatoa *print materials* mbalimbali, tutatumia mitandao kuitangaza *brand* yetu kuanzia sasa na Tanzania kwa kweli kwa jinsi ilivyo na vivutio ambavyo ni *unmatched au unparalleled*, kwa hakika mtu akija hapa ataondoka na *unforgettable experience*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunakusudia kuanzisha Mamlaka ya Utalii wa Fukwe, limezungumzwa hapa suala la fukwe, ni katika mambo mapya ambayo tunakusudia kuyafanya na hivyo tuta- *harmonize* mahusiano yetu kwenye *ku-manage* hizi fukwe pamoja na zile *marine parks* ambazo kwa sasa ziko chini ya Idara ya *Fisheries* iliyopo Wizara ya Mifugo ili iwe *package* moja kwenye hiyo sheria mpya ambayo pengine tutaitleta hapa Bunge siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, pia tuanzishe Jeshi Usu ili kuimarishe ulinzi wa maliasili zetu, lakini pia kuhuishia sheria za *TAWA*, *TFS* na kutunga kanuni mbalimbali kama kanuni za shoroba, kanuni za *buffer zone*, kanuni za maeneo ya mtawanyiko wa wanyamapori, lakini pia kufanya mabadiliko makubwa kwenye Kanuni za Jumuiya za Hifadhi ya Wanyama

Pori (*WMAs*). Yote haya ni mambo ambayo tunayafanya kazi; na tunayafanya kazi kwa *speed* kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo tunalifanya kwa sasa ni kufungua *corridor* ya Kusini. Tunakusudia kwa kweli kufungua *corridor* ya Kusini na mikakati mwezangu ameigusia kidogo, nisiirudie kuelezea jambo hili.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba nitumie nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuridhia maombi yetu kadhaa ambayo tumempelekea ya kutaka kupandisha hadhi baadhi ya maeneo ili tukae kimkakati zaidi katika kufungua *corridor* nyingine kiutalii. Alizungumza Mheshimiwa Mbatia hapa. Kwa sababu tunakusudia kufikia hao watalii 8,000,000 katika miaka takribani saba iliyobakia ili tuweze kufikia malengo ya kukusanya mapato ya dola za Marekani billioni 16 kufikia mwaka 2025, ni lazima pia tufungue maeneo mapya ya utalii. Kwa sababu maeneo ya Kaskazini yameanza kuwa *exhausted*, watalii wamekuwa wengi sana kiasi kwamba hata *maintenance* ya barabara inakuwa ngumu, kila baada ya mwezi inabidi mfanye *repairy* ya barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wakati tuna vivutio vingi na vyote vina wanyama wale wale, kwa hiyo, tunafungua maeneo mengine. Hapa nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kukubali kupandisha hadhi mapori ya akiba ya Burigi. Biharamulo, Kimisi, Ibanda na Chifu Rumanyika badala ya kuwa na Mapori ya Akiba, sasa tunaanzisha mchakato raskmi wa kuyapandisha hadhi ili yaende yakawe *National Parks*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, watu wa Kanda ya Kaskazini Magharibi, mama yangu Mheshimiwa Profesa Tibaijuka na mdogo wangu Mheshimiwa Innocent Bashungwa, wakae mkao wa kula, utalii unakuja Ukanda wao. Tuna-*take advantage* ya kiwanja cha ndege cha Chato, lakini pia kwenye bajeti hii tumeweka mkakati wa kuchonga barabara zinazoingia kwenye mapori haya ya akiba ambayo sasa tunaanzisha mchakato wa kuyapandisha

hadhi yaende yakawe *National Parks* ili tuifungue *corridor* hii ya Kaskazini Magharibi kiutalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia tunasubiri majibu mengine kama Mheshimiwa Rais ataridhia kupandisha hadhi baadhi ya mapori yaliyopo Ukanda wa Kati na Magharibi ili tuifungue *corridor* ya kati Magharibi kwa maana ya kutokea hapa Dodoma kwenda Tabora kupita Katavi tuunganishe na Kigoma iwe nayo ni *circuit* nyingine ya kiutatalii. Mapori ninayoyazungumzia ni mapori kama Swagaswaga, Mkungunero, Rungwa, Mhesi lakini pia mapori ya Ugala kwenda mpaka mapori ya Kigosi Moyomosi ili nayo tuchague baadhi yake tuyapandishe hadhi yawe *National Parks* ili tuyajengee miundombinu na yenyewe yaweze kuanza kutumika kwa kasi zaidi kwa shughuli mbalimbali za utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nachukua fursa hii adhimu kwa kweli kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutujibu maombi yetu hayo na bahati nzuri majibu yamekuja kwa wakati muafaka, barua nimeipokea jana kwamba Mheshimiwa Rais ameridhia tuanze mchako wa kuyapandisha hadhi mapori hayo ya akiba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo llingine jipya ambalo tumekuja nalo ni kushirikisha jamii. Sisi tuna falsafa kwenye Wizara yetu kwa sasa kwamba uhifadhi endelevu ni uhifadhi shirikishi jamii na hapa tunamaanisha kwamba kwenye kila changamoto ni lazima tuzungumze na jamii na ndiyo maana nilikuwa tayari kuzungumza na wananchi wa Momela kwa mdogo wangu, rafiki yangu Mheshimiwa Joshua Nassari, lakini pia nilizungumza na Mheshimiwa John Heche.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya sana, Waheshimiwa Wabunge hata ukiwatendea wema namna gani, wakija hapa ndani wanakupiga tu. Hawazungumzi yale mema dhidi ya watu wao. Kwa mfano, Mheshimiwa Heche juzi tu hapa watu wake zaidi ya 100 walikuwa wamekamatwa wamewekwa ndani kwenye *operation* ambayo ilikuwa inaendelea kule. Sisemi *operation* ilikuwa haramu, hapana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, operesheni ilikuwa halali, imefanyika vizuri, wananchi wameshirikishwa, ushahidi upo, kuna ushahidi wa picha, kuna ushahidi wa video, kuna ushahidi wa miutasari ya mikutano ya kushirikisha wananchi. Katika vizingi ambavyo vilifikia idadi ya 147 kwa *plan* iliyokuwepo, siku wananchi wake wanafanya mgomo zoezi lisiendelee pale Kegonga, kulikuwa kumeshawekwa *beacons* zaidi ya asilimia 90.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, zilibaki *beacons* 13 tu katika *beacons* 147. Kama kweli zoezi halikuwa shirikishi toka mwanzo, vijiji vingine vyote zaidi ya kumi vingekataa. Kilikataa kijiji kimoja tu cha Kegonga kwenye Kata hiyo ya Nyandugu ambapo wao walitaka kufanya vurugu na walidhani kwamba kulikuwa hakuna ushirikishwaji na kuna mtu mmoja pale alihamasisha vurugu hizo kutokea.

Mheshimiwa Spika, mimi pamoja na kufuatilia na kupata ukweli wa jambo lenyewe, nikatumia busara, nikasema kwamba ni vema hawa watu nitumie busara ya kuzungumza na....

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

SPIKA: Tumpe nafasi Mheshimiwa Waziri. Nimekuona, nitakupa nafasi baadae kidogo.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, nikasema nitumie busara ya kuzungumza na Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, wewe kiongozi mzoefu unafahamu changamoto ninayoweza kuipata katika mazingira kama hayo, wakati Mkuu wa Wilaya na Kamati yake ya Ulinzi na Usalama inaendesha *operation*, Mkuu wa Mkoa amefanya ziara, amebariki *operation* iendelee, kuna

timu nzima pale ya vyombo vya Ulinzi na Usalama vipo pale vinaendesha *operation*, halafu mimi Waziri ambaye ninashikiria sheria ambao inasimamiwa sasa na Serikali yetu kule kwenye *Local Government*, ninapofanya uamuzi wa kumwambia Mkuu wa Wilaya sitisha hiyo *operationyako*, siyo katika maslahi ya umma, na mimi Waziri mwenye sheria, naona kwa sasa haiendi sawa. Hebu sitisha mpaka nije mimi mwenyewe. Ni mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Spika, nilikwenda *extra mile* kwa sababu ya urafiki wangu mimi na Mheshimiwa John Heche kwamba amenieleza hili jambo kwa hisia kali, na mimi ni Waziri, na mimi ni Mbunge mwenzake, hebu ngoja *intervene* kusimamisha hiyo *operation* na hatimaye tutatafuta suluhu mimi mwenyewe nikienda *site*. Nikasitisha zoezi lile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikamwomba zaidi Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ambapo tayari *charge sheets* zilikuwa zimeandikwa kwa watu wale zaidi ya 100 na wako ndani kwamba Mheshimiwa naomba hao watu hebu watoe ili nijenge mahusiano mema na hao watu, nitakapokuja niweze kuzungumza nao vizuri wakiwa hawana kesi. Nikamshawishi Mkuu wa Wilaya na akaacha kufungua hizo kesi na waendesha mashitaka walikuwa njiani wanatoka Mkoani kwenda pale na wako kambi pale wanaendelea kuandika hayo mashtaka ili wawapeleke Mahakamani, lakini nikasitisha na zoezi la kwenda Mahakamani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, bado ukiwa Waziri wa Wizara hii, utapata lawama sana. Watu watasema *beacon* imechimbiwa chini ya uvungu, *beacon* imechimbiwa kanisani, imechimbiwa msikitini. Mambo mengi haya yanayosemwa kwa kweli nimekuwa nikiyafuatalia toka nimekaa kwenye kiti hiki, mengi nimekuwa nikiona siyo ya kweli.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, *beacon* yenye urefu wa kunishinda mimi, zaidi *6.4 feet* haiwezi kukaa kwenye uvungu wa kitanda. Hizo ni *beacon* ndefu, lakini pia ziko *beacon* fupi ambazo zinanifika mimi hapa. Kwenye picha

zilizokuwa zinarushwa hapa nafikiri mliona, *beacons* zote nilizozitembelea zinanifika hapa. Haiwezi kukaa chini ya uvungu wa kitanda. Hicho kitanda labla ni *double decker* ambacho chini hakina kitanda. Kwa vitanda vya ndugu zetu huko vijijini tunakotoka, ni vifupi chini. Kwa hiyo, maneno mengi yanasemwa ili kujenga hoja kwamba Wizara ya Maliasili na Askari ambao ni *barbaric* kweli kweli, ambao hawajali masilahi ya watu.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza niseme falsafa hiyo sasa tumeifuta kwenye Wizara hii. Tunashirikiana vizuri na wananchi, na mimi kama kiongozi mkuu kwenye Wizara hii napenda kushirikisha wananchi, napenda kuwa-*engage* wadau. Hata Mheshimiwa Heche huna haja ya kusema hapa kwa sababu kwanza nimeshakuhakikishia kwamba tutakwenda kule kwenye Jimbo lako tukaone hali halisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia wewe umesema maneno mazito hapa kwamba Gibaso, *boundary* ile ni *hard line*, wananchi hapa, hifadhi hapa. Huwezi kuweka *buffer zone* kwenye eneo la wananchi, ni *simple logic!* Nikienda nikikuta hali iko hivyo, niko radhi kumshawishi Mheshimiwa Rais tufanye *variation* ya mipaka, niko radhi kufanya hivyo.

Kwa hiyo, mambo ya namna hiyo hayapaswi kuzua mjadala hapa kwa sababu mimi mwenyewe nitayafanya kwa mikono yangu. Nitafika maeneo husika na nitahakikisha tunaweka sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia tumeanzisha pale *TTB studio* ya TEHAMA ambayo itaenda kutumika kwa ajili ya ku-*monitor* mawasiliano kila mahali kwenye mtandao neno Tanzania litakapotokea kwenye mjadala. Lengo letu ni kukusanya takwimu na kuwajua watu wanaozungumzia kuhusu Tanzania wanapatikana wapi, ni wa umri gani na tufanye nini ili kuweza kuwavutia kuja kitalii katika nchi yetu.

(hana kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Muda umeisha?

SPIKA: Tayari. Malizia tu Mheshimiwa Waziri, dakika moja.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze la vizingi dakika mbili tu. Naomba sana Bunge lako tukufu lisitishe zoezi hili. Nasema kwa sababu ifuatayo kubwa moja.

Mheshimiwa Spika, tunaweka vizingi ili tujue nani na nani wameingia ndani ya eneo la hifadhi. Kama ni hifadhi imeingia ndani ya eneo la wananchi tujue. Halafu mahali palipo na mgogoro tunatatua. Kwa mfano nilikwenda Kimotorok kwa ndugu yangu Mheshimiwa Milly, nikafika pale, nikajionea, kweli kuna vizingi, kuna makanisa yako ndani ya hifadhi na kituo cha afya kimo ndani ya hifadhi. Katika maeneo kama haya, mimi binafsi niko radhi kumshawishi Mheshimiwa Rais turekebishe mipaka, vitu kama hivi vitoke. Kwa sababu ni eneo ukakuta labla ni la kilometra moja, ni eneo dogo tu ambalo tunaweza tuka-*coincide* tukasema hili tulirudishe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mchakato wake utaanza, lakini ni lazima Waziri uanzishe huo mchakato. Kama mipaka hajjawekwa au vizingi havijawekwa nitajua kipi na kipi kimeingia na kipi kipo ndani na kipi kipo nje? Kwa hiyo, zoezi liendele, Waheshimiwa Wabunge mtupe ushirikiano na wananchi wenzetu watupe ushirikiano tukamilishe zoezi la kuweka vizingi, lakini tukijua kwamba hiyo siyo *final*, hiyo siyo hatua ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, askari wanaolinda hizi hifadhi wasisumbue wananchi wala wasitumie nguvu kulazimisha vizingi kuwekwa ama kuwaondoa katika hatua hii ya kwanza. Wananchi wabaki katika maeneo hayo, tutatatua mgogoro mmoja baada ya mwingine kwa kufuata harama za vizingi ambazo zitakuwa zimeshawekwa. Naomba hili pia niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge wenzangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo bila kuchukua sana muda wako, nitakwenda Arumeru mimi mwenyewe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja IItolewa lamuliwe*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa ufanuzi wa hoja mbalimbali.

Nakushuruku sana Mheshimiwa Waziri, kama tulivyosema, matumaini yetu ni kwamba watumishi wa Wizara yako nao watakuwa na *vision* hii uliyonayo ya Uhifadhi Shirikishi. Kwa sababu tukishakuwa na uhifadhi shirikishi mambo ya kuuzia ng'ombe wote kwa mpigo yatapungua sana na migogoro mingi itapungua sana. (*Makof*)

Vilevile Mheshimiwa Waziri amezungumza jambo moja zuri sana, sijui kama mlikuwa mnasikiliza Waheshimiwa, maana yake muda mwangi mnaongea sana. Alipoambiwa na Mheshimiwa Msigwa Waziri kijana, akasema ye ye siyo kijana. Kwa kweli wako Wabunge wengi humu wanafikiri wao ni vijana, kumbe wala siyo vijana. (*Makof/Kicheko*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Kigwangalla nakushukuru bwana, wewe unatambua hilo. (*Kicheko/Makof*)

Mimi siku moja niliwaambia watu wangu ofisini hapa, hebu nifanyieni utafiti wa umri wa Waheshimiwa Wabunge. Sitatoa matokeo ya utafiti, lakini vijana humu ndani ni wachache sana. (*Kicheko/Makof*)

Katibu.

NDG. PAMELA PALLANGYO - KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MWENYEKITI: Waheshimiwa naomba tukae. Tunaendelea. Katibu.

NDG. PAMELA PALLANGYO - KATIBU MEZANI:

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii

Kif.1001 - *Administration and HR Management*.....Sh. 5,346,504,496/=

MWENYEKITI: Haya, orodha ninayo. Mshahara wa Waziri, masuala ya sera. Mheshimiwa Innocent Bashungwa kwa kifupi.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utumiaji wa mkaa ni suala ambalo linawagusa Watanzania walio wengi zaidi ya asilimia 80. Watanzania hawa wanalahisimika kutumia mkaa siyo kwamba wanapenda kuona misitu ikipotea, bali wanakosa nishati mbadala ya mkaa iliyo nafuu na inayopatikana kirahisi.

Sasa napenda kupata *commitment* ya Mheshimiwa Waziri kwamba yeye kama Waziri mwenye dhamana ya misitu atashirikiana na Wizara nydingine hususani Ofisi ya Makamu wa Rais, Wizara ya Viwanda na Biashara kuhakikisha kunakuwepo na mpango mkakati kuhakikisha Watanzania wanapata nishati mbadala ya mkaa badala ya kutoa matamko ya kukataza utuamiaji wa mkaa. Kwa hiyo, nisipopata maelezo ya kutosha nakusudia kushika shilingi. Ahsante. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, ufanuzi tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MALIASLI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue nafasi hii kutoa maelezo kwamba kama tulivyosema kwenye maelezo yetu, mkaa ni nishati muhimu sana kwa matumizi ya wananchi na wananchi kwa asilimia kubwa wanatumia kuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema ni kwamba tutashirikiana na Wizara hizo kama anavyosema, lazima tukae Wizara zote; Wizara ya Mazingira na Wizara nyingine na wadau wengine wote ili tuje na nishati mbadala. Pale tutakapokuwa tumefikia katika hatua nzuri, basi kutakuwa hakuna tatizo. Tunachosema ni kwamba sasa hivi watu wataendelea kutumia, lakini kwa kufuata utaratibu ambaao utakuwa umewekwa katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo hayo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Mheshimiwa Goodluck Mlinga. Aah, Mheshimiwa Bashungwa ulisimama tena? Haya nakupa nafasi.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini sijasikia ile *serious commitment* ya Serikali na hajasema ni lini huu mpango mkakati mbadala wa utumiaji mkaa tutaupata hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu jambo huili linawagusa Watanzania walio wengi, naomba nitoe hoja kwamba Waheshimiwa Wabunge, tulijadili na naomba mniunge mkono.

MWENYEKITI: Sasa Waheshimiwa, kaomba sana kwamba wataaka tena *multi-sectoral*, sasa anaweza ye ye tena akasema ni lini kweli sasa hivi tu hapa hapa? Naona kama maelezo aliyotoa, tumpe muda. Nawashukuruni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza naunga mkono utekelezaji wa mradi wa *Stiegler's Gorge* kwa sababu utaleta ufumbuzi mkubwa wa tatizo la umeme, lakini utekelezaji wa mradi huu utaathiri watu wengi sana. Watu wengi watapisha hasa kutoka Bonde la Mto Kilombero hasa wakulima na wafugaji kutoka Wilaya za Malinyi, Ulanga na Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba *commitment* ya Serikali, kwa kuwa mradi utakapoisha utakuwa na utekelezaji wa mradi wa umwagiliaji wa zaidi ya hekta 85,000 kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali iji-*commit* kuwa wale watu ambao watapisha mradi huo wa *Stiegler's Gorge* wawe kipaumbele katika mradi wa umwagiliaji ambao utatokana na Bonde la Mto Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba *commitment* ya Serikali. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri, ufanuzi tafadhali.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza ni ngumu sana kuja kubaini kwamba hawa ndio wanapaswa tu kufaidika na *project* ya umwagiliaji katika hatua hii ya sasa. Vile vile ni ngumu kusema moja kwa moja kwamba kuna wananchi ambao watatolewa ili kupisha mradi wa *Stiegler's Gorge* kwa sababu hilo halipo. Mradi wa *Stiegler's Gorge* unatekelezwa katikati ya Pori la Akiba la Selous, hautekelezwi huku *upstream* ambako kuna Wilaya za Malinyi, Ulanga na Kilombero. Huku kinachofanyika ni kitu kingine kabisa. Kinachofanyika huku, tunachora mipaka ya ardhi oevu ya Bonde la Kilombero. Hiki ni kitu kingine, *Kilombero Ramsar Site* ambayo ina hadhi ya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunachora mipaka upya ya *Kilombero Game Controlled Area*. Napenda nitumie fursa hii kulieleza Bunge lako tukufu, tumeachia eneo kubwa sana kwenye vijiji kwa sababu mwanzoni *Kilombero Game Controlled Area* ilikuwa ina ukubwa wa kilometra za mraba

7,500 lakini leo hii ninavyozungumza hapa, tumepunguza kutoka 7,500 mpaka 2,200. Kwa hiyo, kuna eneo kubwa sana la *Game Controlled Area* tumeliacha kwa ajili ya matumizi ya wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hivyo, tunatengeneza miradi hii ya *schemes* za umwagiliaji ili wananchi waweze kutumia maji hayo *sustainably* ili Mto Kilombero na Mto Luegu na Mito mingine kama Ruaha isiharibike. Kwa hiyo, maji yapatikane kwa ajili ya kwenda kwenye hiyo *Stiegler's Gorge*. Kwa hiyo, ni vitu viwili tofauti wala haviungani, sema tu vinagusana kwa sababu ya *geographical location* yake.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mlinga nakushukuru au bado una neno?

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyoongea Jimboni hakukaliki na siyo Ulanga tu, Malinyi, Kilombero na Mlimba. Sasa Mheshimiwa Waziri naona anachukulia sijui kama masihara au sijui nisemeje? Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu mniunge mkono tujadili suala hili.

MBUNGE FULANI: Toa hoja.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba natoa hoja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Goodluck hukusema mwanzo nia yako hiyo, lakini nimekuelewa. Naamini kabisa Mheshimiwa Waziri amekuelewa na linaweza lisiwe lake sana kwa sasa hivi, zaidi ni la watu wa nishati. Mheshimiwa Waziri wa Nishati, kwenye hii hoja inayosemwa kwamba sijui miti milioni ngapi itakatwa *Stiegler's Gorge* na athari ambazo zitatokea *upstream* na kadhalika, *TANESCO* hawajishughulishi na miradi ya kimazingira.

Ni lazima wafike mahali waseme hii miti milioni ngapi sisi katika bajeti zetu tutajishughulisha na kuwezesha kuotesha

miti, kufanya hivi ambayo itapandwa Tanzania nzima, yaani kama unafidia hivi kile kitu. (*Makofii*)

Huwezi tu kukata miti na wewe *Director of Forest* unasi mamia mamilioni halafu hata husemi habari ya kwamba baadaye huko una mpango fulani, haiwezekani. Kwa sababu ile *dam* itaingiza pesa. Katika pesa zile, basi mtakuwa mnaweka sehemu fulani ya ku-*remedy* hizo athari za *upstream* na kadhalika. Yaani *TANESCO* badala ya kujishughulisha na kuzalisha umeme peke yake, lazima wajue kwamba wanawajibika na wenyewe kiasi fulani ndiyo ujumbe wa Mheshimiwa Mlinga. Mheshimiwa Marwa Ryoba. Mheshimiwa Waziri umesimama? Ahsante, karibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mlinga kwa kuuliza swali hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo mawili hapa, kwanza labda nisahihishe kidogo takwimu za Mheshimiwa Mbunge ambazo ni nzuri kwamba lile bwawa litakalojengwa litawenza kuhifadhi maji yatakayoweza kuhudumia heka za umwagiliaji zaidi ya 250,000. Kwa hiyo, wala siyo heka 80,000. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi maji hayo yatasaidia sana pamoja na shughuli nyingine za umwagiliaji, lakini hasa maeneo ambayo yanapakana na mradi ikiwemo pamoja na maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge anayetaja. Leo asubuhi nimesikiliza vizuri kwa Mheshimiwa Mbunge Susan kwamba siyo kwamba yataathiri, badala yake ndiyo itakuwa manufaa sana kwa vijiji vinavyopakana na mradi huo. Niliona niliweke vizuri jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi haujaanza kutekelezwa. Utakapofika hatua za kuanza utekelezaji kwa maana ya *physical work*, taratibu zote hizo zitazingatiwa na wananchi wataelekezwa manufaa yao na maoni yao yatafanyiwa kazi. Kwa hiyo, siyo kwamba mradi utaanza tu na kusukuma na ma-*bulldozer*, hatua zote za utekelezaji wa mradi zitazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukataji miti vile vile; hapa tunapoongea kwanza kabisa hakuna mti hata mmoja uliokatwa kwa sasa. Kwa hiyo, tunaamini wakati wa utekelezaji wa mradi, taratibu kabisa husika zitazingatiwa kabla ya ukataji wa miti. Kwa hiyo, niwaondoe wasiwasi wananchi, utaratibu wa kuzingatia mazingira utakuwepo na uzalishaji wa mradi umuhimu wake utabaki pale pale. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa utakuwa wa mwisho. Waziri wa Maji ultaka kusema kitu? Tafadhalii nakupa dakika moja.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Mlinga, lakini nimhakikishie kwamba, ile *scheme* ya umwagiliaji tutakapokuwa tumeikamilisha kujenga, watu watakaopewa nafasi ya kwanza ni watu wanaoishi katika yale maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hakuna wasiwasi wowote. Wananchi wako pamoja na wa Halmashauri nyingine zinazozunguka Bwawa la *Stiegler's Gorge* ndio watakuwa wa kwanza kupewa yale maeneo ya umwagiliaji yatakayotokana na Bwawa la *Stiegler's Gorge*.

Katika mwaka ujao wa fedha, Mheshimiwa Mlinga tayari na wewe tumekuvekea bajeti...

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MBUNGE FULANI: Haa!

MWENYEKITI: Nawaomba tumwache Mheshimiwa Waziri akimaliza tu, nanyi mtapewa nafasi. Ndiyo Mheshimiwa Waziri, malizia.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari katika mwaka ujao wa fedha, *scheme* ya Lupilo ambayo iko kwenye eneo lako Mheshimiwa Mlinga, tumeweka fedha kwa ajili ya kujenga *scheme* ya umwagiliaji. Kwa hiyo, wananchi wako hawatakuwa na wasiwasi wowote kuhusu eneo la kulima. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Zitto ulisimama kuhusu nini? Dakika moja tu.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka tu niseme, ni vizuri sana tunapojadili mambo ya kitaifa tuwe wakweli, kwa sababu kuna mifano ambayo tumeshaiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni Mbunge wa Mkoa wa Dodoma, Mtera wana Bwawa, kuna umwagiliaji? Kidatu wana bwawa, kuna umwagiliaji? Kihansi wana bwawa, kuna umwagiliaji? *Where is that design?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hoja ya msingi hapa ni ile ambayo umeisema kwamba kuna ukataji wa miti, shirika ambalo linafaidika na mradi lazima lije na mpango mbadala wa *ku-mitigate*. Hayo ndiyo maelekezo yachukuliwe na Serikali na siyo blah blah tunazopewa, maelekezo yako ya Kiti ndiyo yachukuliwe. Hizi nyingine zote zifutwe kwenye *Hansard*. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nishati, japo hukusema, mimi najua ulisha-note hilo kwa hiyo, hakuna shida.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo tu.

MWENYEKITI: Haya, dakika moja.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mradi una *design* yake. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, mradi tunaotekeleza sasa, niwasihi kwa mambo mawili; Ethiopia ambayo ina jumla ya megawati 4,228 inatekeleza mradi mwingine mkubwa wa zaidi ya megawati 6,450 wa aina hii, la kwanza. Isipokuwa kwa *design* hii ya mradi, *design* ya Mtera, *design* ya Kihansi ni tofauti na *design* ya Mto Rufiji. (*Makofi*)

Mheshiwa Mwenyekiti, Mtera hakuna hifadhi kama ya Selous, Kihansi hakuna hifadhi kama ya Selous, kwa vyovyothe vile lazima *design* zitofautiane. Manufaa mengine ambayo tunayazungumzia katika suala la umwagiliaji, kwa sababu mradi huu unatekelezwa katika hifadhi, kwa hiyo, ipo mikakati ya kuhakikisha kwamba *bioanuai* haiathiriki tofauti na maeneo mengine na ndiyo maana ya kujenga mradi huu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Sasa naamini Mheshimiwa Waziri hujatuelewa kabisa, yaani suala letu ni dogo sana, labda sijui Mheshimiwa Kangi Lugola, suala letu ni dogo sana.

Katika mambo ya mazingira kuna kitu kinaitwa *Polluters Pay Principle*. Kuna hiyo miti itakayokatwa, hilo ni lazima lifanyike, wala hatulaumu. Unanielewa?

Sasa huyu anayekuwa kuwa *beneficiary* wa huo mradi, bwana *TANESCO* katika mipango yake anapaswa kuwa na mawazo ya kimazingira pia baadae huko. Mradi umeshajengwa, ameanza *ku-operate*, akumbuke kwamba alikotoka aliwahi kufanya moja, mbili, tatu; anakuwa na *programs* za kimazingira za kuwezesha masuala ya uoteshaji wa miti nchini kote tu, yaani badala ya *TANESCO* ya sasa ambayo hajihusishi na masuala ya mazingira. Hoja ni hiyo, wala siyo mbaya. (*Makofi/Kicheko*)

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Maliasili, tumalize Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unipe fursa nimalizie.

MWENYEKITI: Hapana, hapana inatosha, Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri wa Maliasili. (*Kicheko*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ambalo ninapenda kusema ni kwamba tunakubaliana na mapendekezo yako na mapendekezo yako *actually* ndio mapendekezo ya Wizara yetu. Kuna Kamati ya Uongozi ndani ya Serikali ya utekelezaji wa mradi wa ufuaji umeme wa Mto Rufiji. Kwenye ile Kamati sisi tumepeleka mapendekezo yetu mapya ambapo tunataka tutumie hiyo Kanuni ya *PPP* (*Polluters Pay Principle*) ili kutaka kutengenezwe tozo kidogo ambayo itarudi kuja kufanya uhifadhi wa mazingira. Hilo ni la kwanza katika mapendekezo tuliyoweka sisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, katika uvunaji wa miti utakaofanyika katika eneo hili, kuna matarajio ya kuuza miti hiyo kibishara badala ya kuivuruga na *bulldozer* tutaivuna. Katika uvunaji, kuna mauzo yatafanyika na mauzo yake yana thamani ya kati ya shilingi bilioni 400 mpaka 600. Hizi pesa pia zitatumika kwenye uhifadhi wa eneo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa tatu wa kimazingira ambao tunautekeleza katika eneo hilo, mpaka sasa kuna timu ya Wizara takribani nane za wataalam na taasisi za Serikali zipo pale Selous kwenye aneo ambalo mradi utatekelezwa ikichukua *species* mbalimbali na kufanya utafiti wa *ku-identify species* zipi ni *endemic* na *species* zipi ni *exotic* ambazo zimehamia, kuzichukua za miti, nyasi, wanyama wanaotambaa, wanyama wanaoogelea, samaki, ndege na kuzihifadhi kwenye eneo lingine ili baadae tuweze kuzirudisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tunachimba pia mabwawa matatu sambamba na huu mradi ambayo yatatumika kuhifadhi *species* hizi katika kipindi cha *transition* wakati wanyama wakijaribu kufanya *adaptation* kwenye mazingira mapya baada ya mradi kutekelezwa. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Majibu kama haya yanatusaidia sana kwenye kujibu ile athari ya mazingira, yanatuweka mahali pazuri sana tukijua kuna *plan* kama hiyo.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira. Kwa kifupi sana.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuwaondolea wasiwasi Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote juu ya mradi wa umeme wa *Stiegler's Gorge*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaondolea wasiwasi kwa sababu wangekuwa wamesoma ripoti ya Profesa Raphael Mwalyosi ambayo aliifanya mwaka 2001mpaka 2002 ambaye ni mtalaamu wa Ikolojia, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *Institute of Resource Assessment*. Katika *study* yake ile aliwaondolea wasiwasi Watanzania juu ya mradi huu utakapotekelezwa pale *Rufiji Basin*.

Pili, tayari *TANESCO* pamoja na *NEMC* wamekwishamaliza tathmini ya athari kwa mazingira juu ya mradi wa umeme wa megawati 2100 pale *Stiegler's Gorge*. Hiyo ripoti ndiyo tunayoitwa *Environment Impact Assessment Report*. Katika ripoti hiyo ya kitaalamu, Waheshimiwa Wabunge inazaa kitu kinaitwa *Environment Management Plan...*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS
(MUUNGANO NA MAZINGIRA: Sikilizeni niwape shule. Sikilizeni niwape shule...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS
(MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, shule hii ninayoitoa kwenye darasa la *MEMKWA* ambao wameikosa elimu hii, ripoti ile inazaa kitu cha kitaalamu kinachoitwa *Environmental Management Plan*. Sasa katika ile *plan* ndimo ambapo maeneo yote yale yatakayoathirika, nitaonesha namna gani maeneo yote yale yatavyokuwa *mitigated* kwa maana ya kitaalam.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS
(MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mtake msitake mradi huu Serikali tutaujenga....

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MBUNGE FULANI: Kaa chini!

SPIKA: Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU YA RAIS
(MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, yeoyote atakayeleta kipingamizi wakati sio mtalaam, tutakuwa tayari kumfunga.

MBUNGE FULANI: Taarifa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Labda kwa kumalizia tu Mheshimiwa Waziri wa Nishati sisi *point* yetu ilikuwa kwa *TANESCO*. Mradi wa Kidatu, mradi wa Mtera, *TANESCO* mimi sijui kama wanatoa hata shilingi moja kwa ajili ya uhifadhi wa milima ile yote ambayo ndiyo inaleta maji mpaka kwenye mabwawa, yaani *TANESCO* wanamwachia Waziri wa Mazingira peke yake, wakati na wao wanawajibika kwa sababu wao ndio wanaofaidika na hayo maji. Tunachotaka sisi, *TANESCO* naye asaidiane na Waziri wa Mazingira kwenye kuhifadhi mazingira. (*Makofi*)

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Anabishana na Kiti Mheshimiwa Spika. Anabishana na Kiti huyo!

SPIKA: Mheshimiwa Marwa Ryoba.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilimsikiliza Mheshimiwa Naibu akijibu swalii la vizingi, sasa nahisi pengine haelewi vizuri, naomba nieleze. Naomba niseme kwamba kama hakutoa maelezo mazuri nitakamata shillingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko hivi, hizi hifadhi; mapori ya akiba and *whatever* *mean* *zishwa* kwa *GN*. Haya mapori ya zamani, *National Parks* hizi, zamani *GN* ilivyozi tangaza ilikuwa inatamka mipaka ile wazi wazi, ipo kwenye *GN* imeandikwa kwamba mlima fulani, mwamba fulani, mto fulani, kigongo fulani, imeandikwa, hii mipaka inajulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi ya nchi, naomba nikueleze, hiki ambacho ameeleza ndiyo utaratibu umefanyika, mapori mengi, wamepanua *National Parks* nyingi, wameingiza viji vingi kinyemela kwa mtindo huo. Tukikubaliana na maelezo yake kwamba tuachie hilli zoezi

liendelee, hiyo biashara imetoka nakwambia. Hebu angalia kwa mfano, *Ruaha National Park* ilikuwa na *square meter* 10,300, lakini tunavyoongea ina *square meter* 20,226, Tarangire na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyokuwa naeleza hapa niliwaambia, sisi Serengeti tumeenda Mahakamani kwa hicho walichokifanya, tumewashinda. Kwa sababu kwanza waling'oa zile *beacon* ambazo zilikuwa zinapita kwenye maeneo yenye *GN*, wakang'oa kwa makusudi ili wajiongezee maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba maelezo, mipaka inajulikana, imeandikwa kwenye *GN*, hifadhi zenyewe hazina ramani mpaka leo. Mheshimiwa Waziri Lukuvi yuko hapa anafahamu, hizi hifadhi hazina ramani. Serengeti haina ramani. Sasa tueleze hapa, hii mipaka hamulioni? Hamna *GN*? Hebu naomba utupe maelezo ya kutushawishi kwamba *GN*..., yaani sielewi; mnakuja kwenye maeneo ya wananchi mnachukua ardhi, maeneo ambayo walikuwa wanachunga ng'ombe, mnakamata ng'ombe, ng'ombe wanakufa. Hamwatendei haki.

Kwa hiyo, naomba maelezo ya kuelewaka. Kama hayaeleweki, mimi nitatoa shilingi ili Waheshimiwa Wabunge tujadili. Ni jambo la Kitaifa, nchi nzima watu wetu wana-suffer.

SPIKA: Mheshimiwa Marwa Ryoba, kwa nusu dakika, *issue* yako hasa ni nini ambayo Waziri anapaswa ajibu sasa baada ya maelezo yako yote hayo.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* yangu ni kwamba *GN*ipo kwa mujibu wa sheria, mipaka inatambulika. Wanavuka ile mipaka, wanakuja vijijini kuchukua yale maeneo kuweka vizingi vijijini, katika ya miji. Sasa nataka kwanza zoezi lisimamishwe, lakini pia atueleze ni kwamba hawajui mipaka na wanapoweka hivyo vizingi mbona hawashirikishi wananchi wa maeneo hayo hivyo wala Halmashauri za maeneo hayo? Kwa nini yeye Mheshimiwa

Kigwangalla na *TANAPA* yake aende achukue Mkoo wa Mkoa, Mkoo wa Wilaya, Kamati ya Ulinzi na Usalama ana-*ignore* wananchi wa maeneo husika, kwa nini?

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri natumaini umemwelewa pamoja na maelezo mengi. Ahsante, karibu kwa ufanuzi.

WAZIRI WA MALIASILI UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Tata Chacha Marwa Ryoba kwa hoja yake ambayo ameiwasilisha kwa hisia sana. Hoja za namna hii siku zote zinazua hisia kali sana mionganoni mwetu Waheshimiwa Wabunge lakini pia mionganoni mwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema wakati na-*wind up* hoja yangu nilisema dhana yetu katika zama hizi ni kushirikisha wananchi, hiyo ndiyo *guiding principle* yetu. Namuomba sana avute subira, ukanda wa Serengeti kuanzia Magharibi mpaka Kaskazini bado sijafanya ziara, nafikiri ndiyo maana changamoto nyingi katika Bunge lako hili la safari hii zimetoka katika ukanda ule, kwa sababu sijafika katika eneo hilo na kutatua changamoto ambazo zimekuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya vagingi kwamba vilikuwepo hapa vimeletwa hapa, hiyo pengine siyo hoja yetu pengine kujibu sisi, kwa sababu ni hoja ambayo ingepaswa kujibisha na wenzetu wa Wizara ya Ardhi kwa sababu ndio wenyewe Mamlaka ya kuweka alama na wanatuonesha kwamba wekeni kigingi chenu hapa. Sio sisi, hatujiwekei wenywewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja ambalo sote kama Waheshimiwa Wabunge tunapaswa kulitambua na kulikubali ni kwamba miaka ile ya 1959 huko wakati hizi hifadhi zinaanzishwa miaka ya 1970 kulikuwa hakuna teknolojia ya GPS ambayo leo hii inatumika. Kwa hiyo, *GN*nyingi ambazo zilitolewa katika zama hizo zilikuwa ni *descriptive*, zilikuwa ni *GN* zinazolezea alama mbalimbali zisizohamishika. Sasa miaka 50 au 60 baadaye, leo hii tunaambiwa mlima huu ndiyo unaitwa labda Mlima Kigwangalla, mwingine anasema

hapana, huu siyo Mlima Kigwagalla, huu ni Mlima Chacha; Mlima Kigwangalla ni huu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, milima inabadilika majina, mito inabadilika majina na mabonde yanabadilika majina. Kwa hiyo, alama hasa kubainika kwa baadhi ya maeneo zinakuwa ngumu. Mfano halisi ni mgogoro wa Kimotorok pale Mkungunero na Tarangire. Milima imebadilika majina, kwa hiyo, inakuwa hata ngumu kujua alama hasa iko wapi? Kwa hiyo, kwa kuwa miaka ile ya nyuma hakukufanyika uhakiki wa mipaka na uhakiki umeanza miaka ya 2000 ndiyo maana leo hii tunapata hii migogoro. Ndiyo maana sasa hii *approach* tuliyoelekezwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba tuweke alama zinazoonekana, baada ya kuziweka alama zinazoonekana, sasa tutaanza kutatua mgogoro mmoja baada ya mwingine, *case by case*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yenyе migogoro siyo mengi kama ambavyo inajulikana huko zamani. Migogoro hii inajitokeza kwa wingi sana pale ambapo hifadhi imeingia kwenye kijiji, lakini pale ambapo hifadhi inaachia eneo la hifadhi ambalo lilikuwa linajulikana kama eneo la hifadhi na kulipeleka kwenye kijiji, wananchi hawalalamiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba tupate muda, nimeahidi nitafanya ziara ukanda wa Serengeti Magharibi mpaka Kaskazini kwa Mheshimiwa Heche, wanipe nafasi, tukimaliza Bunge hili mimi mwenyewe nitaongozana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu tutapitia hizo kesi na kama wameshinda kesi tutawarudishia hilo eneo, hakuna shida, hakuna mtu anayetaka kumnyanyasa mwananchi. Tunahifadhi kwa ajili ya wananchi. (*Makofii*)

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti,...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Marwa.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala siyo la Serengeti peke yake, ni suala la hifadhi nyngi. Ukimsikiliza hapo Mheshimiwa Waziri anasema wanaishirikisha

Wizara ya Ardhi. Hawajawahi kuishirikisha, wanaenda wenyewe. Labda kama wanaenda wanabaka mtu kule Wizarani wanakuja naye bila ridhaa ya Wizara, atuambie.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Marwa, lugha kidogo iwe ya Kibunge. (*Kicheko*)

MHE. MARWA R. CHACHA: Sawa. Ni lugha yetu, nadhani nimeeleweka. Naomba kutoa hoja ili tulijadili, jambo hili siyo la Serengeti peke yake, ni jambo la kitaifa, linagusa watu...

MWENYEKITI: Sasa Mheshimiwa Marwa kijadiliwe nini hasa?

MBUNGE FULANI: Vizingi.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizingi. Zoezi la vizingi lisimame kwa sababu siyo shirikishi. Wewe unaendaje kuweka mpaka kwenye eneo la mtu bila kumshirikisha? Vijiji vimepimwa, Serikali za Mitaa, vijiji vimepimwa vina *GN*, wewe unaenda kuiwekea mipaka yako; wewe sio Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja...

MWENYEKITI: Ngoja kwanza! Ngojeni kwanza. Mheshimiwa Marwa kaa tu. Kaa Mzee wa Serengeti. Kama najaribu kuwaelewa, mnachobishania, Mheshimiwa Waziri anasema kubalini kwanza vizingi viwekwe, halafu mtayazungumza haya mambo baadae. Unachosema wewe...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bilia kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Nakosea? Anachosema Mheshimiwa Marwa, zoezi lisimame kwanza, vizingi vitawekwa baadae. Yaani hapo ndipo penye tofauti. Hapo tu. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Hilo la kujadiliwa kweli?

WABUNGE FULANI: Ndiyo!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lukuvi, hebu tusaidie bwana.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu mazoezi haya Wizara ya Ardhi kama kuna uhakiki wa mpaka, inapaswa kushirikishwa na inashirikishwa, lakini wakati wa kutayarisha *GN* ni kazi ya sekta yenye we inayopeleka huo muswada na kuandika *GN*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumegundua hivi karibuni kuna matatizo ya namna ya kuainisha zile alama zinazotumika kuandika zile *GN*. Wizara yangu sasa hivi inapendekeza wote wanaondika upya, hao wanaofufua mipaka, sasa tutatumia nukta badala ya kutumia alama za maumbo. Kwa sababu zile alama zinahama na zinabadilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata juzi nimetoka Kiteto na Kilindi tumeamua kuandika upya zile *GN* kwa kutumia nukta ambazo mtu ye yote hata akiwa Marekani akifungua vipimo vyake anaweza kujua mipaka ya Serengeti iko wapi. Tunapitia upya namna hiyo. Nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, alilosema Mheshimiwa Kigwangalla, tutashirikiana. Na mimi niko tayari kumpa sasa hata Mkurugenzi wa Upimaji wa Taifa atembee naye ambaye ndiye mwenye mamlaka ya kufanya shughuli hiyo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Badala ya kuwa...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri tunakushukuru.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Eeh!

MWENYEKITI: Jambo letu halikuwa kubwa sana, nakushukuru. Naomba tu ukae. Nimeona kwenye kitabu cha Kamati jambo hili wamelizungumzia. Kwenye Kamati ukurasa wa 10 na Kamati inasema, Serikali isitishe mara moja zoezi la kuweka vizingi katika mipaka ya hifadhi. Ndiyo ushauri tunapewa na Kamati. (*Makof*)

Kwa kweli tuseme tu, ile wanasema msema kweli ni mpenzi wa Mungu, si ndiyo! Yaani hawa jamaa waweke vizingi kwanza, halafu siku moja waje mrekebishe? Hiyo jamani naomba tuokoe muda. Naomba tuokoe muda. *TANAPA* ndugu zangu nawafahamu, mimi mhifadhi mwenzenu. Nilimwambia hata Naibu siku ile, hawa jamaa yaani wanatamani ardhi hata watu wote sijui waondoke wabakie wao, yaani hawawezi, waweke kigingi wakarekebishe? Waliwahi kurekebisha wapi? Wakishaweka kigingi, wameweka. (*Kicheko/Makof*)

Hivyo vizingi vyenyewe kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, yeye mwenyewe karibu awe mfupi, hiyo mipaka hiyo. Kwa kweli kinachotakiwa hapa ni nia njema tu kwamba wanakutana wanazungumza wanaelewana wanaweka kigingi. Wanakutana, wanaelewana, wanaweka kigingi. Kwa kawaida huwa kigingi kinawekwa mahali ambapo watu wameshaelewana. Kwa sababu wote ni Watanzania, hifadhi ni zetu, wanakijiji ni wetu, Wizara ya Ardhi ipo, Serikali itafute tu namna bora ya kuliangalia jambo hili. Hatuamui sisi, tunatoa ushauri tu, hatuamui; tunatoa ushauri tu kwamba ni vizuri mkaona namna bora zaidi. Kwa hawa jamaa, mnaweza mkaufuna bure, mimi nawajua. Mmh! Kweli, sio utani. (*Kicheko*)

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maneno uliyoyasema, nakubaliana na wewe asilimia 100. Namrudishia shilingi, nakubaliana na wewe na Kamati. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Karibu tunafika mwisho. Mheshimiwa Waziri, ngoja kwa nusu dakika nikupe mchap. Safari moja nikifanya hizo kazi za maliasili kuna kijiji kimoja

kiko juu ya Tarime kule kwa huyu Bwana; kiko mpaka wa Kenya huu, Serengeti hapa, huku Tarime, kijiji cha mwisho hapo. Tulikuwa tumeenda huko kwa ajili ya kukutana na kijiji, mambo ya uhifadhi, maeneo ya Kengonga kule.

Tukakuta siku hiyo, usiku huo walikuwa wamevamiwa na Wakenya, kuja kuiba mifugo na wakawa wameuawa watu kama wanne au watano, usiku huo kuamkia asubuhi hiyo ambayo sisi tumefika. Wale watu wanne au watano wakawa ndani ya Ofisi ya Kijiji, zile maiti, asubuhi ile.

Kwa hiyo, tukakuta watu wamekusanyana, wako wengi na silaha za jadi na kadhalika. Sasa tumefika pale tukawaambia jamani, aah, poleni sana kwa msiba. Kwa kuwa tulikuja kwa ajili ya mkutano tu, sisi tutapanga siku nyingine kuja. Wakatuambia ninyi namna gani? Siku nyingine maana yake nini? Sema kilichokuleta! Wewe zungumza, baada ya hapa, sisi tunatengeneza mambo yetu, tunaenda vita kule Kenya, tunarudisha wale ng'ombe kesho. (*Kicheko*)

Nilishangaa sijawahi kuona watu wa namna hiyo. Maiti ziko ndani, tunaambiwa sema kilichokuleta. Ila ni watu wazuri sana, ni watu wema sana. Simaanishi wabaya. (*Makofii*)

Tuko mwisho, kabisa kabisa kama mnavyoona, lakini kwa dakika chache sana Mheshimiwa Mtolea.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu nchi jirani kama Kenya wananaufaika sana na fukwe za Mombasa. Sisi hapa kwetu fukwe zetu zimekuwa ni chafu, zimekuwa zikitoa harufu mbaya, hatunufaiki na utalii kwenye fukwe zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maelezo yake Mheshimiwa Waziri alikuwa anasema kwamba anampango wa *ku-strengthen* hiyo *beach tourism*, lakini nikakimbilia kwenye randama nione kama kuna chochote kimepangwa

kama kazi ambazo zitakwenda kutekelezwa kwa ajili ya kuimarisha huu utalii wa kwenye fukwe zetu, sijaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka maelezo ya Serikali nione ni kwa namna gani wamejipanga katika kuhakikisha kwamba na sisi tutanufaika na utalii wa kwenye fukwe zetu? Sasa kama sijaridhishwa, nitafikiria kutoa shilingi. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Muda haupo upande wako. Mheshimiwa Waziri, tafadhalii ufanuzi.

WAZIRI WA MALIASILI UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanuzi wetu ni kwamba na sisi tunaiona thamani kubwa tuliyonayo ya urithi wa utajiri wa fukwe ambayo ni ndefu zaidi, nzuri kuliko nchi nyingi ambazo tunapakana nazo katika bahari ya Hindi. Urefu wa fukwe zetu ni karibu kilometra 1,400, ni ndefu sana ukillinganisha na majirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Mch. Msigwa alisema Waziri kijana, nimeingia na nimeiona hii, nikaangalia na wenzetu wanavyotumia vizuri pale Mombasa na kule Thailand, Maldives na sehemu nyingine kama Cuba nikaona na sisi tutafute *model* ambayo itahuisha, itatia chachu ya ukuaji wa utalii wa fukwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika kuanzisha kukuza utalii wa fukwe ni lazima tuanzishe na *legal framework*, tutengeneze muundo wa kisheria wa namna ya *ku-manage beaches* zetu. Kwa hiyo, tutatunga sheria ambayo itaananza Mamlaya ya Usimamizi wa Fukwe Tanzania ambapo kuanzia pale sasa mamlaka itaanza kufanya kazi kama *TANAPA* wanavyofanya kwenye wanyamapor, ama Ngorongoro ama *TAWA* *ku-manage* fukwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wenzetu wa Wizara ya Ardhi nao wanafanya mabadiliko ili kuongeza eneo la hifadhi ya fukwe ili mamlaka itakapoundwa iwe rahisi kufanya uwekezaji katika fukwe zetu. Kwa hiyo, tuna mkakati mahususi

mzuri sana wa kuanzisha chachu ya ukuaji wa utalii wa fukwe katika nchi yetu.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Katibu

NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaingia kwenye *guillotine*.

MWENYEKITI: Sasa tunaingia kwenye *guillotine*. Katibu, haraka haraka.

Kif. 1001 – <i>Admin. and HR. Mgt</i>	Sh. 5,346,496/=
Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts</i>	Sh.1,494,670,000/=
Kif. 1003 – <i>Policy and Planning</i>	Sh.1,558,878,048/=
Kif. 1004 – <i>Government Commun. Unit</i>	Sh. 368,895,861/=
Kif. 1005 – <i>Internal Audit Unit</i>	Sh. 478,477,837/=
Kif. 1006 – <i>Procurement Mgn't Unit</i>	Sh. 628,179,361/=
Kif. 1007 – <i>Legal Services Unit</i>	Sh. 409,524,000/=
Kif. 1008 – <i>Mg'nt Information Systems</i>	Sh. 642,210,451/=
Kif. 2001 – <i>Wildlife</i>	Sh. 21,200,925,000/=
Kif. 3001 – <i>Forestry and Beekeeping</i>	Sh. 42,176,508,147/=
Kif. 4001 – <i>Tourism</i>	Sh. 7,359,006,404/=
Kif. 4002 – <i>Antiquities Unit</i>	Sh. 4,152,878,395/=

(Vifungu vilivyo tajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii

Kif. 1003 – <i>Policy and Planning</i>	Sh. 3,251,120,000/=
Kif. 2001 – <i>Wildlife</i>	Sh. 14,463,599,007/=
Kif. 3001 – <i>Forestry and Beekeeping</i>	Sh. 11,263,362,993/=
Kif. 4001 – <i>Tourism</i>	Sh. 1,000,000,000/=

(Vifungu vilivyo tajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae. Mheshimiwa Waziri, mtoa hoja, tafadhali. (*Makofii*)

T A A R I F A

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia mapendekezo ya bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii na kuyapitisha. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru tena Mheshimiwa Waziri kwa mara ya pili, sasa Waheshimiwa Wabunge kama ilivyoa ada ninaomba niwahoji kwamba Bunge hili sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

(*Hoja IItolewa lamuliwe*)
(*Hoja IIamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 – Wizara ya Maliasili na Utalii yalipitishwa na Bunge*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watumishi wote wa Wizara hii, tunawataktakia kila heri katika utekelezaji wa bajeti hii. Tunaamini kabisa katika baadhi ya watumishi wanaofanya kazi katika mazingira magumu sana ni watumishi wa Maliasili. Ukitikilia mazingira magumu, huko ndiko yalipo hasa. Kule maporini, kwenye misitu ya hifadhi, kwenye mapori ya akiba, kwenye hifadhi zenyewe kwa maana ya TANAPA, Ngorogoro na kadhalika. Tunawapa moyo sana, mnafanya kazi iliyoitukuka. (*Makofii*)

Baadhi ya mambo yetu hapa Bungeni yasiwasikitishé sana, ndiyo kawaida yetu. Hata hili la mwisho lisiwape shida sana, ni kurekebisha tu. Naona wengine wamenuna kidogo, yaani kama vile mna shamba watu wawili na mwenzako mnagombea mpaka, anasema hapa, wewe hapa. Sasa anakwambia tulia, ngoja mimi niweke mpaka kwanza kwenye shamba lako huku halafu baadae tutakuja kuzungumza. Yaani ndiyo maana tukasema mmh! Kwa kawaida watu huwa wanazungumza kwanza halafu wanakubaliana tuweke hapa, baada ya kuzungumza. Kwa hiyo, msikasirike sana jamani. Ni jambo la kawaida tu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa shughuli za leo zimekamilika, kulikuwa na futari fulani, Mheshimiwa Jenista, bado ipo? Ile futari nitangaze? Hamna neno, palikuwa na futari fulani lakini tutaisogeza mbele kidogo, Mheshimiwa Jenista anafahamu. Kwa hiyo, katika siku zijazo tutaweza kukutana hapa kwenye eneo letu kwa ajilli ya futari ya pamoja.

Basi naomba nichukue fursa hii kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 12.00 jioni Bunge lilahirishwa hadi siku ya Jumatano,
Tarehe 23 Mei, 2018 Saa Tatu Asubuhi)*